# TANZANIA OSAKA ALUMNI

# Kitabu cha

# Mbinu Bora

Ofisi ya Waziri Mkuu
Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
P.O. Box 1923,
Dodoma.

Novemba, 2012

# KITABU CHA MBINU BORA (2012)

**Kimeandaliwa na Tanzania Osaka Alumni (TOA):**
**Paulo Faty,**
**Mhadhiri, Chuo Kikuu Mzumbe;**
**Judicate Mwanga,**
**Mhadhiri, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo;**
**na**
**Michiyuki Shimoda,**
**Mshauri Mwandamizi, OWM-TAMISEMI**

**na kuhaririwa na**

**Stella Paschal;**
**Afisa Serikali za Mitaa Mkuu – OWM-TAMISEMI**
**Paulo Faty;**
**Mhadhiri – Chuo Kikuu Mzumbe**
**Honorina Ng'omba;**
**Mshauri wa Serikali za Mitaa – JICA-TANZANIA**
**Elias Magere;**
**Katibu wa Mikutano – Manispaa ya Dodoma**

# Yaliyomo


| Yaliyomo | Ukurasa |
| --- | --- |
| Dibaji | 4 |
| Utangulizi (TOA) | 5 |
| Utangulizi (JICA) | 6 |
| Vifupisho | 7 |
| Sura ya Kwanza:Masuala Yaliyoigwa Kutokana na Uzoefu wa Japani | 9 |
| Sura ya Pili: Utawala na Usimamizi wa Raslimali Watu katika Serikali za Mitaa | 23 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga: Uwajibikaji wa madiwani katika miradi ya Maendeleo | 25 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda: Uboreshaji wa Miundombinu kwa Ajili ya Kuvutia na Kubakiza Watumishi | 38 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe: Kuvutia na Kubakiza Watumishi kwa Kuboresha Mazingira ya Kazi na Makazi | 48 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Chunya: Kutafuta, Kuvutia na Kubakiza Watumishi kwenye Halmashauri zenye Mazingira Magumu | 58 |
| Sura ya Tatu: Ugatuaji wa Masuala ya Fedha na Uboreshaji wa Mapato | 71 |
| Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani: Uboreshaji wa mapato Kutumia Mfumo wa Digitali wa Upimaji Ardhi na Uthamini Majengo | 73 |
| Halmashauri ya Jiji la Mbeya:Uboreshaji wa Mapato kwa njia ya Ujasiriamali | 86 |
| Sura ya Nne:Ushirikishwaji wa Jamii katika Utoaji wa Huduma | 93 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Ileje: Ujenzi wa Madaraja ya Mawe yenye Gharama nafuu | 95 |
| Halmashauri ya Jiji la Mwanza: Ukusanyaji na Udhibiti Bora wa Taka Ngumu | 103 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Nzega: Mradi wa Afya na Usafi wa Mazingira; Kata ya Mambali | 115 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Igunga:Utekelezaji Bora wa Mfuko wa Afya ya Jamii | 121 |

| | |
|---|---|
| *Sura ya Tano: Maendeleo ya Jamii Kiuchumi* | ***133*** |
| *Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro: Uendelezaji wa Mazao Yasiyothaminiwa* | ***136*** |
| *Halmashauri ya Wilaya Ya Same :Uzalishaji wa Tangawizi na Mnyororo wa Ongezeko la Thamani* | ***147*** |
| *Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino:Uendelezaji wa Kilimo cha Zabibu* | ***156*** |
| *Halmashauri ya Wilaya ya Iramba DC:Uzalishaji wa Alizeti na Mnyororo wa Ongezeko la Thamani* | ***165*** |
| *Marejeo* | ***176*** |

# Dibaji

Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania yamelenga katika utoaji bora wa huduma wa Serikali za Mitaa kwa kuzingatia sera za kitaifa za Serikali Kuu. Maboresho yamekaribisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, washirika wa maendeleo na wadau wengine tangu awamu ya kwanza hadi sasa. Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D) iliwekwa dhahiri mwaka 1998 na utekelezaji wake wa maboresho ya Serikali za Mitaa ulianza mwaka 2000. Kupitia ushirikiano huu maboresho ya Serikali za Mitaa hapa Tanzania yamefanikiwa kuleta Serikali za Mitaa za kidemokrasia, matumizi bora ya raslimali watu, kuongozeka kwa ruzuku toka hazina, kuimarika kwa utawala bora katika Serikali za Mitaa, kuongezeka kwa ushiriki wa wananchi, na kwa ujumla kuongezeka kwa uhuru wa serikali za mitaa katika utoaji huduma.

Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania yametekelezwa kwa mkakati wa jumla ambao umejumuisha kujifunza jitihada za maboresho na utekelezaji wake katika nchi nyingine, Afrika na nje, na kuunda mkakati sahihi wa utekelezaji wake na mbinu mbadala kwa Tanzania. Tangu mwaka 2002 Serikali ya Tanzania kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM – TAMISEMI) na Serikali ya Japani kupitia Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japani (JICA) kwa pamoja wameendesha mafunzo kuhusu Ugatuaji nchini Japani kupitia mafunzo ya Osaka. Mafunzo haya yamehudhuriwa na Wakurugenzi na Watumishi wengine toka OWM – TAMISEMI, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri na wadau wengine wa maboresho ya Serikali za Mitaa. Mafunzo haya pia yalitolewa kwa Makatibu Tawala Wasaidizi, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya na wakuu wa idara kupita mafunzo ya mikoa baada ya mafunzo ya Osaka (Reginal Post Osaka Training).

Mafunzo ya Osaka na yale ya Mikoa yametoa fursa kwa watumishi wa serikali kuu na serikali za mitaa kujifunza uzoefu wa ugatuaji madaraka wa kijapani, kuchagua mbinu bora za ugatuaji wa kijapani na kutekeleza mbinu hizo katika Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hili limeibua umuhimu wa kutoa taarifa za utekelezaji wa mbinu hizi bora kupitia kitabu, ili kuzifanya Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri kuona na kujifunza utekelezaji na siri zake humuhumu nchini.

Kitabu hiki ni mwendelezo wa juhudi za pamoja kati ya OWM – TAMISEMI na JICA kuimarisha sera ya ugatuahi wa madaraka Tanzania. Kitabu hiki kinaanza kwa kuonyesha historia ya mafunzo ya Osaka na mbinu bora kama ifuatavyo; Sura ya Kwanza inaonyesha kwa ufupi Masuala mazuri yaliyoigwa toka Japani, Sura ya Pili inahusu utawala katika Serikali za Mitaa na Usimamizi wa Raslimali Watu ikiwasilisha mbinu bora toka halmashauri za wilaya za Mbinga, Mpanda, Ukerewe na Chunya; Sura ya Tatu inahusu Ugatuaji wa Masuala ya Fedha na uboreshaji wa mapato ikiwasilisha Mbinu Bora kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara – Makindani na Halmashauri ya Jiji la Mbeya; Sura ya Nne inahusu Ushirikishwaji wa jamii katika Utoaji Huduma ambayo inawasilisha Mbinu bora kutoka Halmashauri za Ileje, Mwanza, Nzega

na Igunga; na Sura ya Mwisho inayohusu Maendeleo ya jamii Kiuchumi ikiwaisilisha kesi toka Halmashauri za Morogoro, Same, Chamwino na Iramba.

OWM – TAMISEMI inashauri watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na wa Halmashauri na wadau wote wa maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania kusoma kitabu hiki, kufahamu jitihada za ndani, kujifunza siri za mafanikio na kutumia fursa zilizopo kwenye maeneo yao kuonyesha utendaji mzuri katika mazingira ya ugatuaji wa madaraka.

**Jumanne Sagini**

**KATIBU MKUU - OWM-TAMISEMI**

# Utangulizi (TOA)

Kitabu cha mbinu bora cha TOA ni matokeo ya jitihada za pamoja za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia OWM – TAMISEMI na Serikali ya Japani kupitia JICA tangu mwaka 2002 kwa kuendesha mafunzo huko Osaka na mafunzo baada ya Osaka katika kila mkoa juu ya uzoefu wa Ugatuaji Madaraka huko Japani. Mafunzo haya yalitoa fursa kwa watumishi wa Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri na wadau mbalimbali wa maboresho hapa Tanzania kujifunza uzoefu wa kijapani kuhusu Ugatuaji katika maeneo ya Utawala katika Serikali za Mitaa na Usimamizi wa Raslimali Watu, Ugatuaji wa Masuala ya Fedha na Uboreshaji wa Mapato, Upangaji na Utoaji Huduma Shirikishi na Maendeleo ya Kiuchumi katika Halmashauri hasa kupitia wimbi la OVOP. Masuala mazuri yaliyoigwa yametekelezwa katika Sekretariati za Mikoa na Halmashauri nyingi kwa lengo la kuboresha utoaji huduma kwa jamii ndani ya sera ya ugatuaji, yaani "D by D". Kesi nyingi za utekelezaji zimeonyesha mafanikio na matokeo chanya kwa jamii. Hata hivyo kwa sababu za uandishi na urahisi wa kusoma Kamati ya Utendaji ya TOA iliamua kuanza na kesi nzuri 14 ambazo zimewasilishwa kwenye toleo hili la kwanza la kitabu. TOA inatarajia kutoa matoleo mengine ya kitabu hiki siku za mbele sambamba na utekelezaji unaondelea wa Masuala mazuri yaliyoigwa kwenye mafunzo ya Osaka na yale ya Mikoa.

Kukamilika kwa kitabu hiki cha Mbinu Bora kumetokana na misaada kutoka taasisi na watu binafsi mbalimbali. TOA inapenda kutambua na kutoa shukrani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kufikia makubaliano na Serikali ya Japani, kufadhili na kuruhusu watumishi wa Tanzania kuhudhuria mafunzo ya Ugatuaji nchini Japani toka mwaka 2002 mpaka sasa. Pili TOA inaelekeza shukrani za dhati kwa serikali ya Japani na JICA kwa kuandaa, kusaidia na kufadhili mafunzo ya Osaka na Mafunzo ya Mkoa na uzalishaji wa kitabu hiki. TOA pia inapenda kutambua na kushukuru juhudi za utekelezaji wa yale yaliyojifunzwa za Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri na utayari wao wa kuandika kesi kamilifu ambazo zinaonekana kwenye kitabu hiki.

Uchambuzi na uunganishi wa Mbinu Bora zilizopo kwenye kitabu hiki ulifanywa na Bwana Paulo F. Faty (Mhadhiri - Chuo Kikuu Mzumbe) na Bwana Judicate Mwanga (Mhadhiri - Chuo cha Serikali za Mitaa – Hombolo), pia Masuala yaliyoigwa Japani yamechambuliwa na Bwana Michiyuki Shimoda (Mshauri Mwandamizi, OWM – TAMISEMI). TOA kwa dhati kabisa inapongeza mchango wao na inawashukuru sana. Mwisho TOA inapenda kuwashukuru watumishi wote wa OWM – TAMISEMI, JICA na TOA kwa kushiriki katika mikutano mbalimbali iliyoboresha na kuunda kitabu hiki. Siyo rahisi kutaja wote waliochangia katika kazi hii, hata hivyo TOA inaheshimu michango yote iliyotolewa na Taasisi na Watu mbalimabali. Mwisho kabisa, ingawa Watu na Taasisi nyingi zimechangia katika kitabu hiki, TOA na timu ya uchambuaji wanawajibika kwa makosa na mapungufu yanayoweza kuhisiwa na wasomaji wa kitabu hiki.

**Jane Mutagurwa**

**MWENYEKITI - TOA**

# Utangulizi (JICA)

Wasomaji Wapendwa!

Utekelezaji wa sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D) umechukua zaidi ya miaka 10 sasa ukiwa na lengo la kuboresha huduma kwa kugatua shughuli, majukumu na raslimali toka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa.

Kutokana na ukweli huu hapo juu Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japani (JICA) limejikita katika kusaidia utekelezaji wa sera hii hasa katika kuimarisha utoaji huduma katika ngazi za chini kwa kujenga uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na maendeleo ya sekta za afya, kilimo, maji na barabara.

Toka mwaka 2002, JICA kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM – TAMISEMI) imekuwa ikiendesha mafunzo kuhusu maboresho katika Serikali za Mitaa yanayoitwa "Osaka Training". Mafunzo haya yalilenga Maofisa wa juu wa Menejimenti katika maboresho ya Serikali za Mitaa, yaani Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri, Maofisa wa OWM – TAMISEMI na Vyuo vya Elimu ya Juu kwa malengo ya kujifunza uzoefu wa Kijapani katika maboresho ya Serikali za Mitaa. Katika kurudi kwao, waliwasilisha na kujadiliana uelewa na uzoefu walioupata kwenye warsha za mafunzo za mikoa (2003 – 2007). Matokeo yake Umoja wa Makatibu Tawala na Wakurugenzi wa Halmashauri (TOA) ulianzishwa ili kuwa na jukwaa ambalo wajumbe wa TOA wanapata fursa ya kubadilishana uzoefu, mbinu bora na changamoto zilizopo. JICA imekuwa ikisaidia uimarishaji wa taasisi ya TOA.

Kutokana na utekelezaji wa Masuala yaliyoigwa kwenye mafunzo ya Osaka, mbinu bora nyingi ziliwasilishwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika warsha za Mikoa zilizofanyika katika kanda sita mwaka 2011/12. Baada ya uhakiki na uchambuzi wa mbinu hizi bora, toleo hili la kwanza la "kitabu cha mbinu bora" hatimaye limetoka. Kitabu hiki kinathibitisha kuwa ***"tunatakiwa kujifunza siyo tu kutoka nchi nyingine bali katika jitihada nyingi zilizopo ndani ya nchi".***

Nitafurahi kama mtajifunza vipengele muhimu kutoka kitabu hiki na kuchukua hatua ndogo lakini za uhakika ili kuboresha utendaji katika eneo husika.

JICA ina mpango wa kuisaidia TOA kuendesha mafunzo ya Watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na Wakuu wa Idara katika Mikoa yote kwa kutumia kitabu hiki. Tungependa kufuatilia na kujua mbinu bora zitakazofuata zilizotokana na kitabu hiki na mafunzo yake. Tunatarajia kuanzisha jukwaa la kujifunza wenyewe kwa wenyewe (Horizontal Learning) katika ngazi za chini.

**Yukihide KATSUTA**
***Mwakilishi Mkuu – Ofisi ya JICA Tanzania***

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| AMCOs | Agricultural Marketing Cooperatives |
| ALAT | Association of Local Authorities In Tanzania |
| ASDP | Agriculture Sector Development Programme |
| AMSDP | Agricultural Marketing Systems Development Programme |
| BA | Bachelor of Arts Degree |
| CAG | Controller and Auditor General |
| CAMA | Computer Assisted Mass Appraisal |
| CBD | Central business District |
| CCTV camera | Surveillance cameras |
| CDC | Chunya District Council |
| CCBRT | Community Based Rehabilitation in Tanzania |
| CHUDET | Chunya Development Trust |
| CHMT | Council Health Management Team |
| CHF | Community Health Fund |
| CHSB | Council Health Service Board |
| CMT | Council Management Team |
| CG | Special Grant for Remote Districts |
| CRB | Contractors Registration Board |
| CRDB | Cooperative and Rural Development Bank |
| CM | Council Management |
| DANIDA | Danish International Development Agency |
| DADPs | District Agricultural Development Plans |
| DALDO | District Agricultural and Livestock Development Officer |
| DCDO | District Community Development Officer |
| DED | District Development Director |
| DRC | Democratic Republic of Congo |
| FBO | Faith Based Organization |
| FCDS | Fiscal Cadastre Digital System |
| FFS | Farmers Field School |
| FTC | Full Technician Certificate |
| GPS | Geographical Positioning System |
| GTZ/ GIZ | Germany International Development Agency |
| HQ | Headquarters |
| IDC | Ileje District Council |

| | |
|---|---|
| ICT | Information Communication Technology |
| KCMC | Kilimanjaro Christian Medical Centre |
| LGA | Local Government Authority |
| LAs | Local Authorities |
| LGCBG | Local Government Capacity Building Grant |
| LGLB | Local Government Loans Board |
| MCC | Mbeya Municipal Council |
| MDC | Mbinga District Council |
| MDC | Morogoro District Council |
| MVIWATA | Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (A Network of Farmer Groups in Tanzania) |
| MVI ARF | Multivitamin - Agricultural Research Fund |
| MPB | Mbinga Peoples' Bank |
| MEOs | Mtaa Executive Officers |
| MoUs | Memorandum of Understanding |
| OVOP | One Village One Product movement |
| POT | Post Osaka Trainings |
| PPP | Public –Private- Partnership |
| PRA | Participatory Rural Appraisal |
| RCC | Regional Coordination Committee |
| RLDC | Rural Livelihood Development Company |
| RUBADA | Rufiji Basin Development Authority |
| SACCOs | Savings and Credit Cooperative Societies |
| SARI | Selian Agricultural Research Institute |
| SDC | Same District Council |
| SEDP | Secondary Education Development Programme |
| SGR | Strategic Grain Reserve |
| SHERRIF | Mwanza City patrol agency for waste management |
| SIDO | Small Industries Development Organization |
| SMEs | Small and medium Enterprises |
| SUA | Sokoine University of Agriculture |
| TANZAM | Tanzania Zambia highway |
| TANROAD | Tanzania Road Agency |
| TASAF | Tanzania Social Action Fund |
| TAZARA | Tanzania Zambia Railways |
| TOA | Tanzania Osaka Alumni |
| TSCP | Tanzania Strategic City Project |
| TZS | Tanzania Shilling |

| | |
|---|---|
| UCC | University Computing Centre |
| VAEOs | Village Agricultural Extension officer |
| VETA | Vocational Training Authority |
| WAEO | Ward Agricultural Extension Officer |
| WEO | Ward Executive Officer |
| WDC | Ward Development Committee |
| WHC | Ward Health Committees |
| WHCs, | Ward Health Committees |
| WPs | Ward Patrons |

# Sura ya Kwanza: Utangulizi; Masuala Yaliyoigwa Kutokana na Uzoefu wa Japani

## 1.0 MAFUNZO YA OSAKA

Kitabu hiki kimeandaliwa na Umoja wa Washiriki wa Mafunzo ya Osaka kuhusu Serikali za Mitaa wanatoka Tanzania (TOA). TOA ni Umoja wa washiriki wa kozi inayotolewa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA). Mafunzo yenyewe yanaitwa "Mafunzo yenye Mrengo wa Nchi – Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania", lakini yajulikanayo sana kama "Mafunzo ya Osaka". Umoja una wanachama ambao ni Makatibu Tawala wote wa Sekretarieti za Mikoa na Wakurugenzi wote wa Halmashauri nchini.

Mafunzo ya Osaka yalianza mwaka 2002. Kipindi cha miaka mitano ya mwanzo, Makatibu Tawala wote kutoka Mikoa 21 (kipindi hicho) pamoja na Wakurugenzi wa Halmahauri wawili kutoka kila mkoa walihudhuria. Pia maofisa wa juu toka OWM – TAMISEMI (wakurugenzi na wakurugenzi wasaidizi)[1], Katibu Mkuu wa ALAT na baadhi ya wanataaluma mashuhuri walihudhuria kozi hii.

Kutokana na mafanikio na matokeo dhahiri, JICA iliamua kuendelea na mpango huu, kwa kupanua wigo wake kwa kuongeza nchi nyingine tatu za kiafrika ambazo zilikuwa zikipanga maboresho ya ugatuaji, yaani Kenya, Uganda na Zambia, pamoja na Tanzania. Mpaka leo zaidi ya viongozi 100 wa maboresho wanaojumuisha Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri wamefaidika moja kwa moja na mafunzo ya Osaka. Pia washiriki hawa waliporudi katika mikoa yao waliendesha warsha za ndani zijulikanazo kama "mafunzo ya Post Osaka" ili kubadilishana uzoefu na uelewa walioupata Osaka kwa kuwaalika Wakurugenzi waliobaki pamoja na wakuu wa idara. Hivyo wafaidika wa mafunzo haya waliongezeka mpaka kufikia zaidi ya 1,500, ingawa uanachama wa TOA ulibakia kuwa wa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri.

Kutoka katika Masuala mbalimbali yaliyoigwa Osaka na mafunzo ya Post Osaka, Halmashauri zilizohudhuria ziliandaa mipango kazi ya kuboresha utendaji wao. Kukiwa na zaidi ya miaka 10 ya utendaji, imethibitishwa kuwa kuna idadi kubwa ya mbinu bora zinajitokeza katika Halmashauri nyingi kwa kutekeleza ile mipango kazi ambayo ni vyema kuwashirikisha wengine. Kwa hiyo TOA iliamua kuhakiki na kuchambua kesi hizo za mbinu bora na kutengeneza kitabu hiki, ili viongozi wa Halmashauri waweze kuzirejea kesi hizi na kuzitumia pale wanapoona zinafaa na zina tija, katika kuboresha kazi zao.

[1] Pamoja na Makatibu wakuu wawili wa Zamani wa OWM-TAMISEMI, yaani, MS. Tarishi M.K. na Bwana H.A. Katanga

Kabla ya kuingia kwenye kesi zenyewe za mbinu bora, ni vyema katika sura hii tukaangalia kwa nini JICA iliamua kutoa mafunzo haya kwa viongozi wa maboresho wa kitanzania, nini ilikuwa maana ya mafunzo ya Osaka kwa Tanzania na Masuala gani yalijadiliwa kwenye mafunzo haya.

## 2.0 HISTORIA YA MAFUNZO YA OSAKA

Kwa nini JICA iliamua kutoa mafunzo haya? Na yalikuwa na maana gani kwa Tanzania?

### 2.1 Maoni ya JICA Kuhusu Msaada kwenye Ugatuaji

JICA ina maoni ya kipekee kuhusu misaada kwenye utawala ambayo yanaweza kutofautiana na maoni ya washirika wengine wa maendeleo. JICA imeshuhudia programu kubwa kubwa za maboresho zikifanywa katika nchi zinazoendelea na washirika wa maendeleo kama Programu wa kurekibisha Miundo ya Uchumi (SAPs) na maboresho ya utawala ikiwa ni pamoja na Ugatuaji wa madaraka. Inaweza kusemwa kuwa programu hizi na maboresho haya yaliyofanywa katika nchi zinazoendelea ni sawa kabisa na yale yanayojaribiwa sasa katika nchi zilizoendelea bila kujali tofauti iliyopo ya kihistoria na mazingira kati ya nchi hizi. Pia mara kwa mara inajidhihirisha kuwa maboresho haya yanatekelezwa kwa msukumo mkubwa toka kwa wafadhili, bila kuzingatia asili ya mchakato wa maendeleo na umiliki wa nchi husika.

Kutokana na machungu ya kushindwa kufikia malengo katika ushirikiano wa kimataifa wa aina hii, JICA imekuwa na msimamo ufuatazo katika kusaidia ugatuaji.

(i) Hakuna mfumo wowote unaoweza kutumika katika nchi zote.
(ii) Ugatuaji wenyewe siyo lengo bali ni njia ya kufikia lengo fulani.
(iii) Kuasilisha na kukuza mfumo ndani ya nchi kupitia majadiliano ya kitaifa ni muhimu.
(iv) Jinsi gani ya kuhakikisha viwango vya chini vya kitaifa vya huduma[2] vinafikiwa ni muhimu katika kuandaa maboresho ya Ugatuaji.
(v) Maboresho ya Ugatuaji ni mchakato mrefu, ambao hautakiwi kuchukuliwa kama Mradi au Programu tu.
(vi) Maboresho ya Ugatuaji ya haraka haraka yanaweza kuleta fujo. Katika kila maboresho ya Ugatuaji (d by d), ni lazima kuhakikisha kuna mazingira sahihi kwa upande wa Halmashauri na wanajamii kupokea majukumu makubwa yanayogatuliwa.

## 2.0 Changamoto Kubwa Iliyogunduliwa katika Programu ya Tanzania ya Maboresho ya Serikali za Mitaa na Ujumbe wa Maandalizi ya Mafunzo wa Mwaka 2002

Baada ya maombi ya Serikali ya Tanzania kuhusu kuwepo kwa Mpango wa mafunzo wa maboresho katika serikali za mitaa mwaka 2001, JICA iliamua kutuma ujumbe kwenda kuchambua hali ilivyo ili kuunda kozi ya mafunzo yenye maudhui ya kumaliza Masuala muhimu.

[2] Viwango vya chini vya kitaifa vya huduma ni nadharia kuwa kiwango fulani cha huduma lazima kifikiwe hata kama ni katika jamii maskini vijijini sawa na kwenye miji mikubwa.

Ujumbe ule ulipofika Tanzania, Novemba mwaka 2002, uligundua kuwa Programu ya maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania ilikuwa na changamoto zifuatazo;

(i) Jedwali kubwa na lenye hatua nyingi za utekelezaji (Zaidi ya kurasa 80)

(ii) Programu ya maboresho ilikuwa ukitekelezwa kwa jedwali zuri sana lakini halikuruhusu maboresho/mabadiliko zaidi. Ujumbe uliona kulikuwa na nafasi ndogo sana iliyoachwa ya kuweza kubadili lolote ili kuruhusu majaribio ya suala ambalo ni muhimu. Ujumbe uliona kuwa kila kitu kimeshadhamiriwa, na Serikali ya Tanzania ililazimika kufuata reli hiyo bila kwenda pembeni au kurudi vyuma.

(iii) Programu iliandaliwa kwa msaada mkubwa kutoka kundi la wafadhili.

(iv) Wafadhili wa kawaida waliopo kwenye mfuko "Basket funding" waliunda kamati ya msukumo pamoja na serikali. Kuandikwa kwa Programu yenyewe kulifanywa na wataalamu washauri wa nje na hata utekelezaji wenyewe. Ujumbe ulihofia kuwa Programu ya maboresho iliandaliwa bila kupitia mchakato stahiki wa kujenga uelewa ndani ya nchi na kupata makubaliano yanayohusu mahitaji ya mabadiliko.

(v) Hatari ya kukimbilia kwa haraka Ugatuaji wa Madaraka (D by D).

Sera ya ugatuaji (D by D) iliyokuwa ikihamasishwa na Serikali ilidhihirika kwenye ujumbe huo kuwa ni kama vile Tanzania ilikuwa inatekeleza ugatuaji wa madaraka sawa na ule wa nchi zilizoendelea. Swali likawa; Je ni kweli uwezo na mtazamo wa Halmashauri na Wizara zote ulikuwa tayari kwa mabadiliko haya ya haraka? Ujumbe huu uliaona changamoto zifuatazo katika hili;

- Upinzani kutoka Wizara za kisekta
- Ukosefu wa majadiliano ya kina kuhusu ugatuaji katika jamii
- Hakukuwa na uwezo kamilifu kwa upande wa Halmashauri kuchukua majukumu yote yaliyogatuliwa

### 2.3 Uwezekano wa Umuhimu wa Uzoefu toka Japani katika Ujenzi wa Taifa na Maboresho ya Ugatuaji - Ujumbe kutoka Japan kwenda Tanzania kupitia Mafunzo ya Osaka.

Baada ya kuona hali halisi ya Tanzania iliyoelezewa hapo juu, JICA iliamua kuwa uzoefu wa Japani kwenye ujenzi wa Taifa na Maboresho yaliyokuwa na mchakato wa muda mrefu ya Ugatuaji ungeweza kuwa unastahili na muhimu kwa viongozi wa maboresho wa Tanzania kujifunza na kupitia upya maboresho yao.

Japani ni nchi ndogo huko Bara la Asia isiyo na ustaarabu wa Magharibi, ambayo ilianza ujenzi wa taifa kama nchi iliyo nyuma kabisa lakini ikafikia maendeleo ya ajabu. Japani ina uzoefu mwingi wa aina yake wa kutumia mifano (models) ya nje (mfano wa Magharibi) ambayo wafadhili wengine hawana. (Mataifa ya Ulaya yamekuwa mara zote mstari wa mbele na katikati ya dunia na hujiona hayana sababu ya kujifunza toka nje). Kwa kweli, Japani ilianza Ujenzi wa taifa na maendeleo, kwa kujaribu kuiga mifano ya Magharibi lakini ikashindikana

mwanzoni kabisa. Tokea hapo ikawa ni mchakato mrefu wa kujaribu na kushindwa mpaka hatimaye ilipofikia Japani ikaunda mfumo wake wa kipekee unaoitwa “Nusu kijapani nusu Magharibi”. Japani inaamini kuwa aina hii ya uanzishaji wa mfumo, pamoja na umiliki wake thabiti kupitia kujaribu na kushindwa mara nyingi ni muhimu sana kwa maendeleo endelevu ya nchi.

Mchakato huu ambao Japan ilitumia ili kuanzisha mfumo wake wa serikali za mitaa na maboresho ya Ugatuaji ni tofauti kabisa na mifano ya Ulaya ambayo nchi zinazoendelea zinajaribu kuanzisha kwa sasa. JICA ilifikiri kuwa kuwasilisha “mfumo huu tofauti” unaweza kuwa muhimu, kwani kuwa na mfano mmoja tu, inaonekana kama vile “ndio njia pekee” hakuna nyingine. Lakini kukiwa na mifano zaidi ya miwili, wanaweza wakaanza kulinganisha na kuona ni mfano upi unafaa zaidi katika mazingira yao, na ni hatua ipi iwe ya kwanza katika kuandaa mfumo wao wenyewe.

Ifuatayo ni mifano tu ya kuvutia ya vigezo vinavyoweza kuigwa toka mfumo wa kijapani kati ya mengi yaliyopo;

**(1) Mchakato wa Maboresho wa Polepole Sana Lakini wa Uhakika**

Japani ilitumia miaka 110 toka ilipoanza kuunda mfumo wa Serikali za Mitaa na Ugatuaji; ingawa tunahesabu miaka 55 ya Maboresho Makuu baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia hadi kufika ugatuaji halisi (D by D) mwaka 2000. Serikali ilijaribu kuhakikisha kuwa Halmashauri zimeshajengewa uwezo wa kutosha kabla ya kugatua majukumu, na siyo kukimbilia kurekebisha taasisi za Ugatuaji (D by D). Uzoefu huu wa Japani unaipa Tanzania fursa ya kufikiria mara mbili kama mwendo wa maboresho siyo kasi sana, na kama nchi inataka kuendelea na mwendo kasi uliopo, basi haina budi kuhakikisha kuna ujenzi wa uwezo stahiki kwa upande wa Serikali za Mitaa.

**(2) Ukasimishaji wa Shughuli/Majukumu kwa Wakala (Agency Delegated Functions)**

Katika kipindi tajwa cha miaka 55, serikali ilichagua mfumo wa “kukasimu” unaoitwa ADF kama hatua ya mpito, badala ya kurukia Ugatuaji moja kwa moja. Kwa sababu ya mfumo huu Japani ilipingwa sana na nchi za Magharibi kwa kipindi kirefu kuwa haijafanya Ugatuaji sahihi, na mwishoni kabisa Serikali ikaamua kuingia katika Ugatuaji halisi mwaka 2000 na kuondokana na mfumo wa kukasimu (ADF). Hata hivyo sasa hivi imethibitika kuwa ADF ilichangia kwa kiasi kikubwa kukua kwa mfumo mzuri wa Serikali za Mitaa na kupelekea kufikiwa kwa ugatuaji halisi (D by D) nchini Japani; hasa katika vipengele vifuatavyo;

- Shukrani kwa ADF, Halmashauri zilifanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na Wizara husika, na zikaweza kujenga uwezo wao kupitia mafunzo kazini (on the job training) kukiwa na usaidizi wa kitaalamu wa karibu toka wizarani. Kila walipopata changamoto, maofisa wa Serikali za Mitaa waliweza kuwasiliana na maofisa wa wizara husika kwa simu na maofisa wa wizara waliweza kusaidia kwa wema na kumaliza changamoto hizo pamoja. Haya yote yaliwezekana kwa sababu kimsingi shughuli zote zilikuwa ni wajibu wa Wizara na zilikasimishwa tu kwa Halmashauri. Hivyo hakukuwa na upinzani wowote

toka wizarani, zaidi ya ushirikiano ilipofikia Ugatuaji wa shughuli; kinyume kabisa na yanayotokea katika nchi zinzoendelea zinapotekeleza ugatuaji.

- Hoja ya msingi ilikuwa ni kuhakikisha kuwa raslimali ambazo ni chache zilizopo ndani ya nchi zinaweza kutumika vizuri zaidi kuelekea upande mmoja yaani maendeleo ya nchi, badala ya kuzigawa na kutengeneza tofauti kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.
- Ilikuwa ni muhimu sana katika hatua za mwanzo ambapo Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikuwa na uwezo dhaifu. Bila mfumo wa kukasimu (ADF) kipindi hicho Halmashauri zisingeweza kufanya vizuri shughuli zao za kuhudumia watu wala uwezo wao usingejengeka.
- Sababu nyingine muhimu ilikuwa mafunzo kazini (OJT). Shukrani kwa mchakato wa mafunzo kazini (OJT), kwa miaka 55, watumishi wote wa Serikali za Mitaa pamoja na muundo wao kwa ujumla walijenga uwezo thabiti, kwa kupokea ufahamu na utaalamu kutoka wizarani, na kuwa tayari Serikali Kuu ilipoamua kugatua madaraka (D by D).

Uzoefu huu wa Japan unaleta swali moja la msingi kwa Tanzania juu ya namna gani nchi inaweza kujithibitishia uhakika na ubora wa mchakato wa kuzijengea uwezo Halmashauri ilihali Ugatuaji (D by D) ukiendelea; kuhakikisha matumizi mazuri ya raslimali chache zilizopo nchini na kukwepa kabisa upinzani toka Wizara za kisekta.

**(3) Mfumo wa Kubadilishana Watumishi kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa**

Nchini Japani, kipindi cha hatua za mwanzo za maboresho, mtindo wa kubadilishana watumishi kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ulitumika sana kama mbinu bora kabisa ya (a) kujaza upungufu wa watumishi hasa wenye sifa katika Halmashauri za pembezoni na (b) kuhakikisha uhamishaji wa ujuzi na utaalamu kutoka kwa wasomi wa Wizara kwenda kwa watumishi wa Halmashauri waliokuwa na ujuzi na uzoefu mdogo ili kujenga uwezo wa Halmshauri hizo.

Serikali iliunda jopo kubwa la maofisa wataalamu katika wizara ya Serikali za Mitaa na kuwapeleka kwenda kwenye Halmashauri zilizokuwa na uwezo mdogo huko pembezoni ili kuzisaidia. Hatua hii ya uhamisho wa muda ilidumu kwa muda wa miaka 4 - 5 na baadaya watumishi hawa walirudishwa kwenye nafasi zao za kawaida kwenye wizara zao. Kadri walivyokuwa na uwezo wa kitaalamu kuwezesha wengine ndivyo walivyopelekwa kwenye Halmashauri za mbali na zenye udhaifu mkubwa. Pale walipofaulu na kutenda vizuri katika vituo hivi vipya, waliahidiwa kupanda vyeo zaidi wanaporudi, ambayo iliwapa motisha wataalamu hawa waliobobea kwenda kwenye sehemu zisizovutia kwa hamasa ya juu kabisa. Pia Halmashauri nyingi zilipeleka watumishi wao kwenye wizara mbalimbali kufanya kazi, katika misingi ya mafunzo kazini kwenye maeneo ambayo Halmashauri husika ilihitaji.

Baada ya kurudia mizunguko kadhaa ya kubadilishana watumishi, ujuzi na utaalamu wa kutosha ulihamishwa kikamilifu toka Wizara kwenda Halmashauri, kitu ambacho kilisaidia sana kujenga uwezo wa Halmshauri nchini Japanni. Sasa Halmashauri zinajitegemea katika raslimali watu bila kuitegemea Serikali Kuu tena.

Nidhahiri kuwa ugatuaji wa raslimali watu ukifanyika kwa ukamilifu wake bila kuwa na mbinu za kutatua matatizo, hupelekea upungufu mkubwa wa watumishi kwenye Halmashauri ambazo zipo katika maeneo maskini na pembezoni. Ni kwa sababu hii Tanzania iliamua kurudisha Masuala ya raslimali watu kwa sehemu kubwa Serikali Kuu. Hata hivyo haina mantiki kuendeleza Ugatuaji wa madaraka (D by D) bila Ugatuaji halisi wa raslimali watu. Badala ya "0 au 100", serikali inatakiwa kutafuta mkakati wa namna ya kugatua raslimali watu na wakati huohuo kukwepa kutengeneza upungufu katika maeneo ya vijijini, na kujiridhisha kuwa kuna mchakato wa kujenga uwezo wa baadaye wa Halmashauri.

## 3.0 MASUALA YALIYOJITOKEZA NA KUJADILIWA WAKATI WA MAFUNZO YA OSAKA

Kutokana na upungufu wa nafasi Masuala machache tu ya msingi yameweza kuwasilishwa kwenye sehemu hiyo hapo juu, kati ya mambo mengi yanayotokana na uzoefu wa Japani ambayo Tanzania imepewa. Hapa vipengele vingine vitatajwa na kuelezewa kwa kifupi.

### 3.1 Masuala ya Jumla

Masuala na Maswali yafuatayo yalijitokeza na kujadiliwa wakati wa mafunzo ya Osaka:

**(1) Umuhimu wa kukuza uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kama kigezo cha mafanikio ya Ugatuaji wenyewe**

- Je hakuna hatari ya kudidimiza utoaji huduma, kugatua wajibu mkubwa kiasi hiki ndani ya muda mfupi?
- Ni namna gani ya kukabiliana na hali halisi kuwa Halmashauri zinahitaji uwezo zaidi ili kutekeleza shughuli zilizogatuliwa?
    - Vipi kuhusu ajira? Namna gani itawezekana kupata watumishi wenye sifa katika Halmashauri zilizopo kwenye maeneo maskini na pembezoni?
    - Ni jinsi gani ya kuziba pengo kati ya ujuzi na utaalamu katika Serikali za Mitaa na kuziendeleza? Je siyo muhimu kwanza kuweka mbinu za kuhamisha ujuzi na utaalamu, pamoja na usaidizi wa kitaalamu kutoka serikali kuu kwenda Halmshauri? Siyo muhimu kwanza kuimarisha mahusiano ya ushirikiano kati ya Serikali Kuu na Halmashauri badala ya kutegemea misaada toka nje?

**(2) Ugatuaji na Maendeleo**

- Ili kuweza kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi na kwa raslimali chache zilizopo, ni muhimu kutafuta mbinu mkakati ya kuzitumia raslimali hizi (hivi ndivyo ambavyo Japani imekuwa ikifanya kujiletea maendeleo yake)
- Namna gani unaweza kusimamia maendeleo ya nchi na ugatuaji kwa pamoja wakati mara kadhaa hupingana? Unawezaje kujiridhisha kuwa hakutakuwa na utengano wa

raslimali na tofauti (kutokuelewana) kati ya Serikali Kuu na Halmashauri au kati ya Halmashauri zenyewe?

**(3) Ugatuaji na Viwango vya chini vya kitaifa**

- Jinsi gani ya kusimamia ugatuaji na kuzingatia viwango vya chini vya kitaifa? Ni jinsi gani itahakikishwa kuwa Halmshauri zilizopo vijijini zitakuwa na uwezo wa kutosha kama zilivyo zile tajiri katika kigezo cha utoaji huduma kwa watu? (uwezo wa watumishi na fedha).

**(4) Ukweli Kuhusu Uwezo wa Halmashauri kuweza Kutoa Huduma**

- Swali liliulizwa; Ni Maofisa Ugani wangapi waliopo katika Halmashauri ukijumuisha na wale ambao wanatumikia katika kata na vijiji? Swali hili liliulizwa kwa washiriki ili kuwafanya waelewe hali ilivyo mbaya ambayo Halmashauri za Tanzania zinatakiwa kukabiliana nayo. Ukichukua Mkoa mmoja kama mfano, Mkoa wa Nagano nchini Japani, ni mkoa mdogo kabisa ulioko maeneo ya vijijini lakini una maofisa ugani wa kilimo wapatao 1500. Pia kuna Halmshauri 77 za ngazi za chini katika Mkoa huu ambazo kila moja inaajiri maofisa ugani kati ya 20 – 30. Maana yake kuwa wakulima katika Mkoa (prefecture)[3] wa Nagano wanafurahia huduma zinazotolewa na zaidi ya maofisa ugani 3,000 wa Halmshauri ikilinganishwa na wakulima wa Tanzania ambao wana maofisa ugani wasiozidi 100[4]. Pia nchini Japani kuna mashirika mengi ya binafsi yanayouza mashine za kilimo, mbolea, madawa, mbegu n.k pamoja na taasisi za ushirika zilizo imara; zote hizi hutoa huduma mbalimbali za ugani na ushauri wa kitaalamu.
- Ni vyema kutambua hali ngumu iliyoelezewa hapo juu na kuanzisha mkakati mpya. Hatutakiwi kuota ndoto kwamba Tanzania inaweza kufikia kutoa huduma nzuri kama za nchi zilizoendelea kwa idadi ndogo hivi ya watumishi kwenye eneo lote hata kama Serikali Kuu itaamuwa kufanya kila kitu peke yake.

**(5) Umuhimu wa Juhudi za Wananchi na Ushirikiano kati ya Halmashauri na Jamii**

- Kutokana na Ukweli ulioongelewa hapo juu, haikwepeki kutumia kwa kiasi kikubwa Uwezo wa watu na Juhudi za kujitegemea ili kutoa huduma zilizo bora.

---

[3] Mkoa (prefecture) huko Japani ni karibu sawa na wilaya za Tanzania kwa ukubwa wa eneo. (Ingawa Wilaya nyingine za Tanzania ni kubwa sana kuliko Mikoa ya Kijapani).

[4] Pia si kwamba Japani ina hali nzuri katika maana hii. Kinyume chake, Japani ni nchi ambayo ina idadi ndogo kabisa ya watumishi kwa idadi ya watu waliopo ikilinganishwa na nchi zilizoendelea. Maana yake ni kuwa Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Italia n.k wana watumishi wengi zaidi wa serikali.

- Ni imani ya JICA kuwa kama watu wataongozwa na kuwezeshwa vizuri, wana uwezo wa kufanya mambo mengi wenyewe, kama kujenga shule za msingi, zahanati, barabara zao na kuzitunza.
- Kwa Japani pia, kipindi cha hatua za mwanzo za Maendeleo, Serikali haikuwa na uwezo wa kujenga shule za msingi. Kwa mfano, ilikuwa ni watu katika jamii zao waliochangia kutoka mifukoni mwao na wakafanya kazi pamoja kujenga na zaidi wakatafuta watu wanaoweza kufundisha na wakawalipa mishahara yao. Ndiyo maana shule nyingi za kipindi hicho hazikuwa za "umma" bali "binafsi", kwa maana ya "shule zinazomilikiwa na jamii; ilikuwa ni baada ya miongo kadhaa, serikali ilipotajirika na ikaanza kuzimiliki na hatimaye kuwa shule za umma.
- Inahitaji mabadiliko ya mtazamo wa Serikali na Watu, kutoka fikra kuwa ni jukumu la Serikali kutoa huduma zote kwa watu kuelekea mtazamo kuwa watu wanaweza kufanya mengi sana kwa juhudi zao wenyewe na serikali ikawezesha tu mchakato huo badala ya Serikali kutekeleza peke yake.

**(6) Umuhimu wa Kuainisha Ukubwa Sahihi wa Sehemu za Serikali za Mitaa; na Kuunda Mbinu Mpya za Kuzifikia Jamii kutoka makao makuu ya Halmashauri**

- Kutokana na vigezo hivyo hapo juu ni lazima kuunda mbinu imara sana za Halmashauri kuzifikia jamii. Hapa Tanzania, Halmashauri za Wilaya ni kubwa mno, hivyo ni muhimu kufikiria jinsi ya kujenga daraja kati ya Halmashauri na jamii.
- Kutoka kwenye wazo la kukuza mtazamo wa watu kuwa na uhuru wao, eneo la Halmashauri linatakiwa kuwa dogo sana ili watu waweze kuona kuwa sehemu hiyo kweli ni yao. Kwa upande mwingine sehemu hii ndogo ya Serikali za Mitaa inatakiwa iwe na uimara wa kutosha kutoa huduma za kutosha ambayo inahitaji kiasi cha raslimali fedha na watu. Haya ni mahitaji muhimu mawili yanayopingana.
- Kuweza kutoa majibu kwa swali hili hapa juu linalojipanga lenyewe, sahihisho lililopo ni kuwa na mfumo wenye ngazi nyingi kutoka Halmashauri hadi jamii. Kwa Japani mfumo huu wa ngazi nyingi unafanya kazi vizuri. Lakini Tanzania pia ina mfumo mzuri wenye wilaya – kata – kijiji – kitongoji. Hii inasaidia sana kukuza uhuru wa jamii na jitihada shirikishi za maendeleo kati ya Halmashauri na jamii. Zaidi ya hayo, Mfumo wa Upangaji Mipango Shirikishi Jamii (O&OD) unaweza kuwa jukwaa zuri zaidi la kuboresha mfumo huu na kuuwezesha kufanya kazi vizuri zaidi.

### 3.2 Usimamizi na Ugatuaji wa Raslimali Watu

Kama ilivyo kwenye sehemu iliyotangulia, mafunzo ya Osaka yalitoa tahadhari kwa Viongozi wa Tanzania katika miaka michache ya mwanzo kuwa waangalifu kuhusu kutoharakisha kugatua na kupeleka madaraka maarufu kama *D-by-D*. Hata hivyo, kuhusu ugatuaji wa masuala ya rasilimali

watu, ujumbe ulikuwa tofauti kidogo kwa vile ilionekana kwamba madaraka haya yalikwisha anza kurudishwa Serikal Kuu; kwani uteuzi wa Wakurugenzi wa Halmasahuri na Wakuu wa Idara unafanywa na Wizara pamoja na kuanzishwa kwa Sekretarieti ya Ajira ili kuendesha mchakato wa ajira kwa kada nyingine za watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Nchi ya Japani haikugatua madaraka na kuyapeleka Halamashauri kwa haraka, bali Serikali Kuu ilendelea kuhodhi baadhi ya shughuli. Kwa mantiki hii, ugatuaji nchini Japani haukuwa umekamilika kwa miaka mingi mpaka ilipofika mwaka 2000. Hata hivyo, kuhusiana na kugatua masuala ya usimamizi wa rasilimali watu, Japan ilihakikisha kwamba madaraka haya yamegatuliwa na kupelekwa Halmashauri kikamilifu tangu mwanzo kabisa wa maboresho.

Hii ni kwa sababu kugatua masuala ya usimamizi wa rasilimali watu ndiyo jambo la muhimu sana na msingi wa ugatuaji. Kulingana na mfumo wa Serikali za Mitaa Japani, masuala yote huamuliwa na kutekelezwa ndani ya Mamlaka za Serikali Mitaa husika bila kuingiliwa na Serikali Kuu, yaani kuajiri na kufukuza, kuendesha mafunzo, kupanga ngazi za mishahara, kufanya uhamisho, kupandisha vyeo , mpaka kustaafu. Mamlaka za Serikali za Mitaa Japani huajiri wahitimu wapya kutoka vyuo vikuu kila inapofika mwezi Aprili kulingana na mahitaji yao. Wahitimu walioajiriwa na Mamlaka fulani ya Serikali za Mitaa, wataitumikia Mamlaka husika kwa maisha yao yote mpaka watakapostaafu. Hakuna kanuni ya uhamisho kutoka Mamlaka moja ya Serikali za Mitaa kwenda mamlaka nyingine.

Zaidi ya hayo, Wenyeviti au Mameya ni wanasiasa na huchaguliwa na wananchi kwa njia ya kura, na ndio wakuu wa Tawi la Utawala/Utendaji sambamba na Tawi la Baraza la Madiwani la Halmashauri husika. Watendaji wanawajibika kwa Meya/Mwenyekiti na siyo kwa Madiwani, kwa hiyo masuala ya watendaji hulindwa na huwakilishwa na Meya/Mwenyekiti katika Baraza la Madiwani.

Kwenye mafunzo ya Osaka, mambo matatu yafuatayo yalitiliwa mkazo kwamba ndivyo vitu muhimu katika kufikia uwezo wa juu wa rasilimali watu katika Halmashauri:

1) Kuajiri
   Kuajiri watumishi wenye sifa kuliko wote na wanaofaa katika kufikia dhima/malengo ya mamlaka husika; na
2) Mafunzo
   Baada ya kuajiri, kuwapa mafunzo yanayolenga na kuwezesha kufikiwa kwa dhima/malengo ya mamlaka husika (siyo malengo ya mtu binafsi); na
3) Kujipanga
   Kuhakikisha kuwa uwezo wote wa Raslimali watu katika Halmashauri unatumika kikamilifu ili kutimiza malengo ya mamlaka husika

Kwa minajili hiyo, Japani iliona kuwa ni jambo lisilokwepeka kutangulia kugatua madaraka yahusuyo usimamizi wa rasilimali watu ili kila Halmashauri iweze kuchambua hali halisi, kupanga mipango, kuajiri, kutoa mafunzo, kupanga majukumu na kudhibiti watumishi. Mtumishi wa Halmashauri lazima awe mtu anayelipenda eneo husika na watu waliopo,

anayefanya kazi kwa bidii kwa ajili ya watu, anayeelewa vizuri kuhusu hali ya eneo husika, anayewafahamu watu vizuri na kuwa na uwezo wa kufanya kazi kwa karibu na wakazi wa eneo husika; hii ndiyo mantiki ya ugatuaji. Ni uzoefu wa nchi ya Japani kwamba, kwenye Halmashauri zenye mafanikio ya kuridhisha, kuna maofisa na watendaji wanaofanya kazi kwa kujituma hasa katika kuwahudumia watu, na kushirikiana na wakazi; na walio wengi wao ni wale watendaji waliozaliwa na kukulia katika maeneo hayo na wanayapenda makazi hayo, pamoja na uongozi thabiti wa Meya/Mwenyekiti ambaye naye ni mzawa.


Jambo jingine muhimu linalozifanya Halmashauri za Japani ziwe na nguvu ni juhudi waliyonayo katika kuwapa watumishi wao mafunzo. Halmashauri za Japani zinawekeza sana kwa watumishi kwa kuwapeleka kwenye mafunzo pamoja na mpango wa mafunzo kazini ambao uko kimkakati kulingana na mahitaji ya kitaasisi (siyo mahitaji binafsi) na kwa mtazamo wa mbali.

Hili linawezekana kule Japani kwa sababu hakuna uhamisho wa watumishi toka Halmashauri moja kwenda nyingine ya na kiwango cha kubakiza/kushikilia watumishi kazini ni kikubwa sana, hivyo Halmashauri huwekeza bila hofu kwamba baada ya kuwasomesha watakimbia.

Kinyume chake, Tanzania kuna uhamisho wa mara kwa mara wa watumishi muhimu kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine na hivyo ni vigumu sana kuwabakiza/kuwashikilia watumishi kwenye Halmashauri moja. Katika hali kama hii, changamoto kubwa ni jinsi ya kuhakikisha kwamba matokeo yatokanayo na mafunzo ya watumishi yanabaki ili yalete maboresho katika utendaji kazi wa mamlaka husika, na kuzifanya Halmashauri ziwe na bidii katika kujenga uwezo wa watumishi licha ya uwezekano mkubwa wa kuwapoteza baada ya kuwasomesha. Swali moja liliulizwa kwenye mafunzo ya Osaka kama Tanzania inaweza kuandaa na kutekeleza mpango mkakati na thabiti wa muda mrefu wa mafunzo ya kuwajengea watumishi wake uwezo katika hali hii.

Kwa upande mwingine, mafunzo ya Osaka yaliibua suala la "kufanya kazi kama timu" ili kuweza kutumia asilimia 120 ya uwezo wa nguvu kazi iliyopo na kuyafikia malengo ya kitaasisi. Kule Japani, kuna mambo kadhaa kuhusu mfumo wa usimamizi wa rasilimali watu ambayo yamefafanuliwa kwa uangalifu mkubwa kwa ajili hiyo, kama vile:

1) Ngazi za mishahara zimewekwa makusudi kwa lengo la kuondokana na rushwa na kuchochea watumishi wafanye kazi kwa bidii hadi watakapostaafu;
2) Mfumo wa kipekee wa Japani "kuchelewesha upandishaji vyeo" ili kumfanya kila mtu afanye kazi kwa bidii kwa miaka mingi kabla ya kupandishwa cheo (kukamua asilimia 120 ya uwezo wa kila mmoja);
3) Watumishi kufanya kazi kwa kuzunguka kila idara ya Halmashauri husika na mtindo wa kuweka kumbukumbu za kila mwaka za utendaji wa kila mtumishi ili kufanya za tathimini kwa haki na kwa malengo na kuchagua wale wenye uwezo mkubwa na wanaostahili kupandishwa vyeo kuwa Wakurugenzi;
4) Shughuli zote zinazohusu rasilimali watu ziko chini ya Idara ya Uendelezaji Rasilimali Watu ili iwezeshe namba 3) hapo juu;
5) Mazingira ya kipekee ya Japani yanawezesha "utendaji kazi kama timu", usimamizi unaofanywa na wakuu/viongozi, na mafunzo kazini yanayoendeshwa na wasimamizi, mtindo unaojulikana kama mtindo wa "chumba kikubwa" yaani ofisi ya wazi mithili ya ofisi za benki.




Mchoro (1): Uwiano wa matumuzi ya SK na SM kwa kila sekta
Chanzo: White Paper on Local Public Finance, 2010
(Ministry of Home Affairs of Government of Japan)

Yote yaliyoelezwa kwenye sehemu hiyo hapo juu yamewekwa na kanuni zinazotawala Mamlaka za SM za Japani ili kuhakikisha mambo matatu yahusuyo usimamizi wa rasilimali watu yanazingatiwa mfano 1) Kuajiri; 2) Mafunzo; na 3) Kushughulika kwa bidii. Swali liliulizwa, katika mazingira ya sasa ya Halmashauri za Tanzania, ni kwa jinsi gani zinaweza kutekeleza mambo haya matatu.

### 3.3 Fedha za Serikali za Mitaa na Ugatuaji wa Masuala ya Fedha

**a) <u>Misingi ya kifedha katika Halmashauri</u>**


Michoro (1) na (2) inaonyesha japo kwa ufupi hali ya Halmashauri za Japani kuhusu masuala ya fedha.

Mchoro (1) unaonyesha ukubwa wa majukumu ya Halmashauri katika matumizi ya kutoa huduma ndani ya kila sekta. Ukiangalia sekta ya afya, Halmashauri hutumia 94% ya fedha iliyotengwa kwenye bajeti ya afya ya taifa na Serikali Kuu hutumia 6% tu. Kwenye elimu uwiano kati ya Halmashauri na Serikali Kuu ni 85% kwa 15%. Ukizingatia uhusiano wa karibu uliopo kati ya uzito wa majukumu na matumizi, Halmashauri za Japani zinafanya sehemu kubwa zaidi ya majukumu ya Serikali ya kutoa Huduma. Kwa upande mwingine, ni muhimu kutambua kwamba kiasi kikubwa cha bajeti <u>hutengwa</u> kwa ajili ya kuziwezesha Halmashauri kutekeleza majukumu mazito yaliyogatuliwa na kupelekwa kwao.


Je hali ikoje Tanzania? Ukweli ni huu, ukiangalia majukumu yote yaliyogatuliwa na kupelekwa kwenye ngazi za msingi katika Halmashauri Tanzania, ukubwa wa majukumu ni sawa tu yale ya Halmashauri za Japani. Lakini, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Halmashauri Tanzania,
ilikuwa pungufu ya TZS trilioni 3 ya bajeti ya taifa ya zaidi ya TZS trilioni 11 ya mwaka 2011/12.

Ulinganisho unaofanywa, ni ule unaohusu bajeti za Halmashauri zenye kuwa na masharti au uhuru wa matumizi. Mchoro (2) unaonyesha viwango na vyanzo mbalimbali vya mapato ya Halmashauri za Japani. Kama ilivyothibitishwa na takwimu hizi, 51% ya mapato hutokana na vyanzo vya ndani ( kodi ushuru na malipo mbalimbali). Pia kuna <u>ruzuku ambazo hazina masharti yoyote ya matumizi</u> zinazoitwa “ruzuku toka SK kwenda SM ” (ruzuku za LAT). Ruzuku ya LAT ni <u>fedha nyingi inayotoka SK kwa mara moja</u> kwenda SM na serikali za mikoa. Fedha hii inahamishwa toka Wizara ya Fedha kwenda kwenye akaunti kuu ya kila Halmashauri <u>siku ya kwanza ya kila robo mwaka</u>. Ukijumlisha mapato ya ndani na ruzuku za LAT toka SK, Halmashauri za Japani zina aslimia 75% ya bajeti yao isiyo na masharti na wanaweza kutumia kama wanavyoamua wenyewe. Mchanganuo huu ni wa muhimu sana kwa Halmashauri SM za

Japani katika kufikia malengo ya mipango yao ya maendeleo, kwani wana bajeti ya kutosha na ya uhakika kila mwaka. Washiriki toka Tanzania walipochunguza hali za Halmashauri za kwao, walithibitisha kwamba zina hali mbaya ya kifedha pia fedha nyingi wanayopokea ina masharti ya matumizi kama ilivyo kwenye Mchoro, (3).




Mchoro(2): Vyanzo na viwango vya mapato ya SM za Japani
Chanzo: White Paper on Local Public Finance, 2010
(Ministry of Home Affairs of Government of Japan)




Mchoro (3): Muundo wa vyanzo mapato ya SM za Tanzania
Chanzo: Ni hesabu zilizofanywa na mwandishi toka


Ama kwa hakika, hata kwa hali hii ingelikuwa jambo la maana kama 94% ya ruzuku wanayopokea isingelikuwa na masharti ili Halmashauri ziwe na uhuru wa kuzitumia. Bahati mbaya, kuna ruzuku mbalimbali zinazokuja zikiambatana na masharti katika matumizi. Hivyo basi, hata kama Halmashauri itaanda mipango mizuri ya maendeleo, ni vigumu sana kutekeleza miradi yao ya vipaumbele kwa sababu ya ruzuku zenye masharti, ambazo husababisha mipango ya maendeleo isitekelezeke kirahisi.

Ikumbukwe kwamba kiasi cha fedha inayotengwa kwenye bajeti za Halmashauri ni kidogo mno cha Shilingi trilioni 3 kati ya trilioni 11 za bajeti ya taifa (2011/12). Hizi Shilingi trillioni 3 ni sawa na 94% ya bajeti nzima ya Halmashauri, na hii inathibitisha jinsi ambavyo hawana vyanzo vya ndani vya kutosha.

Mafunzo ya Osaka yaliwataka viongozi wa Serikali ya Tanzania kutenga kiasi cha kutosha cha bajeti kutekeleza wingi wa majukumu ya Halmashauri yaliyogatuliwa na kupelekwa kwao kama kweli wameazimia kufikia ugatuaji wa madaraka. Fedha hii inaweza kuwa zile kutoka vyanzo vya ndani au katika ruzuku isiyo na masharti[5]. Kama hakuna bajeti ya kutosha inayotengwa, basi

[5] Kwa hatua zilipofikia kwa sasa, bado haishauriwi kugatua madaraka ya kifedha na kuwapa SM mamlaka makubwa ya kutoza kodi. Hii ni kwa sababu hali hii itaziumiza zile SM zilizo kwenye maeneo yenye ufukara ya vijijini, kwa vile hazina vyanzo vya uhakika vya kodi, huku zile SM tajiri za mijini zitakuwa na mapato mengi

hakuna sababu ya kugatua majukumu kwenda ngazi za Halmashauri. Vinginevyo, shughuli hizo hazitatekelezwa na mwishowe jamii itateseka kwa kukosa huduma. Kama tulivyoona kwa Halmashauri za Japani, ikitokea kwamba 85% ya majukumu ya kutoa huduma za elimu yamegatuliwa na kupelekwa ngazi za Halmashauri, basi kiasi cha kutosha cha bajeti ya kutekeleza majukumu hayo hugatuliwa na kupelekwa Halmashauri ili kufikia malengo. Vinginevyo si haki hata kidogo kwa Halmashauri na hasa kwa watu wanaotegemea huduma.




Mchoro (4): Aina za Kodi kwenye Majiji/Miji
Chanzo: White Paper on Local Public Finance, 2010 (Ministry of Home Affairs of Government of Japan)

## b) Kodi za Ndani kwa ajili ya Uendelevu na ushamiri wa Serikali za Mitaa

Kule Japani, kuna sababu zilizo wazi kabisa kuhusu aina zote za kodi zinazotengwa kwenye ngazi zote mbili za SM. Prefectures(SM za Wilaya ndiyo ngazi ya juu za SM) na Municipalities(Miji na Majiji) ndiyo ngazi za chini za SM[6]). Japokuwa Wilaya (Prefecture) ndiyo ngazi ya juu ya SM ya Japani, zinaweza kulinganishwa na Halmashauri za Tanzania kwa ukubwa wa eneo. Kuhusu majukumu, ngazi za chini za SM Japani (Municipalities) ndizo zinalinganishwa na ngazi za Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa/Jiji kwa Tanzania. Hata hivyo kule Japani, huduma zote za muhimu kwa jamii hutolewa na Majiji/Miji (Municipalities) kwa sababu ndizo ngazi za msingi zilizo karibu na watu, huku Prefecture/Wilaya wanahusika hasahasa na maendeleo ya kiuchumi kwa vile majukumu haya yanahitaji eneo kubwa kwa ajili ya mipango na kuyatekeleza kimkakati.

Kulingana na majukumu yalivyo na wajibu wa Majiji/Miji, zifuatazo ni kodi ambazo zinaweza kutozwa na Majiji :

Kama inavyoonekana katika mchoro (4), kodi za nyumba na mali zisizo hamishika ni sawa na 45.3% ya mapato yatokayo na kodi, ambayo ni karibu na nusu ya mapato yote yatokanayo na kodi. Ukijumlisha na "Kodi ya mkazi"(kodi ya Kichwa) pamoja na "kodi ya mipango miji", inakuwa ni zaidi ya 80% ya mapato yatokanayo na kodi. Kodi za nyumba na kodi ya mipango miji hutozwa kwenye ardhi na majengo na hizi ni kodi ambazo hakuna awezaye kuzikwepa. Kama ardhi yote na majengo yote yamesajiliwa na kuthaminiwa vizuri, basi hivi ni vyanzo vya uhakika kwa serikali za Mitaa.

---

kutoka vyanzo vyao vya ndani . Kwa hiyo ni busara zaidi kuendelea kutoa ruzuku kutoka chanzo kimoja, lakini SM ziwe na uhuru na maamuzi wa kuzitumia kulingana na vipaumbele vyao kwa sasa.

[6] Kuna Prefecture/Wilaya 47 na (Munispaa) 1,742 hadi kufikia Octoba 2012. Manispaa za Japani zinajumuisha **Majiji, Miji na Vijiji**, na tofauti na mgawanyiko wa ngazi za SM za Tanzania.

“Kodi ya kila mkazi wa Halmashauri za Japani” ni “kodi ya kichwa” iliyofutwa hapa Tanzania ambayo ni “kodi ya maendeleo”[7]. Chanzo hiki cha kodi pia huwa ni chanzo cha kuaminika kwa sababu wakazi wote wameandikishwa na Halmashauri inajua wanapoishi. Tukiangalia hali ya Tanzania, vyanzo vingi vya mapato ni vile vinavyohusiana na shughuli za kiuchumi, mfano ushuru wa mazao (23%), ushuru wa huduma (18%), ushuru wa nyumba za kulala wageni(3%), leseni (10%), karo na malipo mbalimbali (17%), ambazo hubadilika kulingana na mabadiliko ya hali ya uchumi wa eneo husika, na cha kushangaza ni kwamba kodi ya majengo ni 8% tu ya mapato yatokanayo na kodi.

Mafunzo ya Osaka yaliwapa viongozi wa Tanzania changamoto kwamba ili Halmashauri ziweze kutoa huduma endelevu zinazohitajika kwa wakati na viwango vinavyotegemewa, ni lazima kujenga wigo mpana na mfumo wa uhakika wa kukusanya kodi ndani ya Halmasahuri zenyewe. Uzoefu wa Japani unaonyesha kwamba bila kuweka msisitizo kwenye vyanzo vyenye uhakika vya kodi/ushuru kama vile kodi za majengo, kodi ya kichwa/kodi ya maendeleo, siyo rahisi hata kidogo kwa Halmashauri kutekeleza majukumu yake. Kwa mazingira haya, ni muhimu kuwa na mfumo wa daftari la kuandikisha ardhi na mali zisizo hamishika pamoja na daftari la wakazi wote kwa kila Halmashauri, hii itasaidia nchi nzima siyo tu kwenye masuala ya kukusanya mapato, bali kwa matumizi mengine mengi.

Kuhusu utaratibu huu, inafaa kusema kwamba tayari Tanzania kuna mifano ya kufurahisha na inayotia moyo ya Halmashauri zinazotekeleza kile kinachopendekezwa hapa, rejea kisa mkasa cha Manispaa ya Mtwara Mikindani kwenye Sura ya Tatu.

### 3.4 Maendeleo ya Kiuchumi ya Serikali za Mitaa – Uzoefu wa kufurahisha wa dhana ya ki-Japani ya “Kijiji kimoja zao moja” au (OVOP)”

Hitaji la maendeleo ya kiuchumi ya Halmashauri limekuwa likisumbua vichwa vya Wakurugenzi wengi wa Tanzania. Kuhusiana na hili, kuna uzoefu maarufu nchini Japani wa dhana ijulikanayo kama “zao moja kwa kijiji kimoja” maarufu kama OVOP, iliyoanzia kwenye wilaya/ Prefecture ya Oita ambayo hapo awali ilikuwa moja ya wilaya fukara kuliko zote nchini humo. Uzoefu unaotokana na dhana hii unaweza kuwa muafaka kwa Tanzania kama utatafsiriwa na kutumika inavyostahili kulingana na mazingira ya Tanzania.

#### (a) Zao moja kwa kijiji kimoja (OVOP) ni nini?

Vuguvugu la “zao moja kwa kijiji kimoja” au OVOP ni mkusanyiko wa ubunifu wa shughuli za maendeleo ya jamii zilizobuniwa na kupata msukumo wa viongozi kutoka jamii husika katika Wilaya (Prefecture) ya Oita, ambao waliipenda jamii yao na wakahuzunishwa kutokana na hali ya ufukara uliokuwa umekithiri huko miaka ya nyuma. Japokuwa juhudi kama hizo za mtu mmoja mmoja zilikuwepo hapa na pale kwenye Wilaya (Prefecture)ya Oita tangu miaka ya

[7] Tofauti pekee ni kwamba kodi ya kichwaTanzania hutozwa kwa kiwango sawa kwa kila mtu, kwa Japani kodi ya mkazi hutozwa kulingana na viwango vya kipato cha kaya. Kama hakuna kipato cha kiasi fulani kinachokubalika, basi wanakaya wa kaya hiyo hawana sababu ya kulipa kodi ya mkazi.

1960, dhana yenyewe ya “zao moja kwa kijiji kimoja” au OVOP ilianzishwa rasmi mwaka 1979 na Dr. Morihiko HIRAMATSU, akiwa Gavana[8] wa Wilaya hiyo kwa kuanza kuzitambua baadhi ya juhudi za jamii zilizokwisha anza na kuziendeleza.

Dr. HIRAMATSU, alikuwa ni msomi mwenye mafanikio makubwa akiwa mtumishi wa cheo cha juu kwenye Wizara ya Biashara za kimataifa na Viwanda yaani “Ministry of International Trade and Industry (MITI)”. Hii ilikuwa Wizara yenye nguvu sana, lakini aliamua kuacha kazi hiyo na kurudi kwenye Wilaya ya Oita yaani nyumbani kwao. Kilichomsukuma ni kwa sababu alihofia sana kuwa Wilaya ya nyumbani kwake iliendelea kubaki nyuma kimaendeleo na kuwa miongoni mwa Wilaya fukara kuliko zote nchini Japani kwa wakati huo.

Baada ya kurudi kwao, aligombea na kushinda cheo cha Ugavana wa Wilaya ya Oita. Alipoanza kazi hii jambo la kwanza alilolifanya ni kutembelea vijiji vyote kwenye Wilaya hiyo. Wakati akifanya matembezi haya, alikuta kuna miradi ya maendeleo na jitihada mbalimbali za watu wenyewe kujaribu kujinasua huko vijijini. Aliguswa sana na jitihada hizo za wananchi wakiongozwa na viongozi wao wenye mapenzi mema na juhudi hizi zilikuwa hazijulikani kwa serikali. Alithamini sana juhudi za jamii, na akawatia moyo waendelee na jitihada za kujikwamua. Kwa wanavijiji, wengi wao walikuwa hawajawahi kutoka nje ya vijiji vyao, kwa hiyo kwao ilikuwa ni faraja kubwa kutembelewa na mtu mkubwa kama Gavana na kusifiwa kwa kile walichokuwa wanakifanya!. Hawakuwahi kuwaza kwamba kile walichokuwa wanakifanya kilikuwa ni kitu cha kipekee na cha thamani machoni pa wengine. Tangu Gavana wao Dr. HIRAMATSU alipofanya matembezi haya, juhudi hizo za jamii zilipewa msukumo mkubwa na watu wakahamasika zaidi na kujisikia fahari wenyewe.

Kwa upande wake, Dr. HIRAMATSU alifikiri ni jukumu muhimu kwa Serikali ngazi ya Wilaya kuunga mkono na kuendeleza juhudi za thamani kubwa zilizoanzishwa na wananchi kutaka kuboresha maisha yao wenyewe, kuzieneza zaidi na kubadilisha uzoefu huu mzuri na viongozi wa vijiji vingine ndani ya Wilaya yao.

Vuguvugu la “zao moja kwa kijiji kimoja” yaani OVOP ina mambo muhimu yanayolitofautisha na dhana nyingine kwani Vuguvugu hili hupelekea kuzalisha bidhaa za kipekee (ikijumuisha utalii), ili kupata maendeleo kwa kutumia rasilimali zilizopo ndani ya jamii husika. Hata hivyo, jambo jingine la tofauti kwenye vuguvugu la “zao moja kwa kijiji kimoja” ni kwamba: kuna uzoefu dhabiti wa jamii unaopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi midogo ya maendeleo ya shughuli za kiuchumi ngazi za msingi. Wananchi husika huunganisha uwezo wao wa kujipanga na kutekeleza mustakabali wa maisha yao; jamii zimejijengea uwezo, zimeamka na zina ujasiri; Jamii zimeimarika na zimefikia uwezo wa kujitawala na kujiendesha wenyewe kama kijiji. Ukweli uliopo hapa ni kwamba wananchi wana uzoefu wa kufanikiwa na wakati mwingine kushindwa (lakini wamejijengea uwezo na tabia ya kujikwamua katika kushindwa huko), siyo tu kwamba jamii inategemea kupata mafanikio ya kiuchumi pekee, bali pia jamii inatarajia kujijengea uwezo, uzoefu na ujasiri na kupata nguvu zaidi katika mchakato huo. Ukweli huu ni

[8] Cheo cha Gavana wa Prefecture ni cheo cha juu zaidi kwenye SM za juu Japani ikilinganishwa na Meya wa kwenye SM za Tanzania (Ona “3.2. Usimamizi wa Rasilimali Watu na Ugatuzi wa madaraka” kwa Meya.)

muhimu ufahamike ili kulielewa vizuri vuguvugu la “zao moja kwa kijiji kimoja”. Ikumbukwe kwamba ni rahisi sana kupata mafanikio au faida ya mara moja katika biashara au mradi fulani kutokana na msaada wa mara moja kutoka nje ya jamii, lakini kama jamii hiyo itakumbana na vikwazo fulani fulani baadaye, hawataweza kuvishinda kama watakuwa hawajajijengea uwezo kupitia michakato iliyotangulia ya kutatua matatizo yao kwa nguvu na jitihada zao wenyewe.

Kwa mantiki hii, ni vyema kutambua kwamba nyingi kati ya juhudi zilizojitokeza kwenye Vuguvugu la “zao moja kwa kijiji kimoja” kule Oita, zilipitia mchakato ufuatao:

- Kabla ya vuguvugu la “zao moja kwa kijiji kimoja”au OVOP, wanavijiji wa Oita walikuwa fukara sana, walikuwa wamekata tamaa kuhusu mabadiliko, wenye kijicho na kuoneana wivu wao kwa wao, kutokana na hali hii haikuwezekana kushirikiana baina yao ili kuboresha maisha kwa pamoja. Hata hivyo, kupitia Vuguvugu la “zao moja kwa kijiji kimoja” walianza kujitambua kwamba “Ndiyo, tunaweza kama tunataka!” Haya ni mafanikio makubwa katika mchakato wa kubadili fikra.
- Katika badiliko la fikra hapo juu, wanavijiji walianza kujijengea uzoefu wa kushirikiana kwenye shughuli mbalimbali ndani ya jamii, wakizikabili changamoto wanazokutana nazo na kuzishinda kwa pamoja. Mchakato huu uliwafanya waweze kujipanga vizuri na vizuri zaidi.
- Kupitia mchakato huo huo, waliimarisha mahusiano na taasisi za nje zenye usaidizi ikijumuisha Halmashauri na Asasi za kiraia na mashirika yasiyo ya kiserikali.
- Pamoja na ujenzi wa uwezo wa jamii ulioelezwa hapo juu, jamii husika zilifanikiwa kupata matokeo dhahiri ya maendeleo ya kiuchumi.

**(b) Dr. HIRAMATSU alifanya nini akiwa Gavana wa Wilaya?**

Kwanza kabisa, ieleweke vizuri kwamba vuguvugu la “zao moja kwa kijiji kimoja” halikuwa ni programu ya lazima(“maamrisho ya kutoka juu kwenda ngazi za msingi”) iliyoandaliwa na Dr. HIRAMATSU na kwamba watu hawakuambiwa cha kufanya. Kwa bahati mbaya, baadhi ya nchi zinazoendelea ambazo zilivutiwa na Vuguvugu la “zao moja kwa kijiji kimoja”, waliuelewa vibaya ukweli huu. Walizingatia tuu zile faida za kiuchumi zinazotokana na OVOP na kujaribu kuendeleza vuguvugu la “zao moja kwa kijiji kimoja” kama sera ya taifa na kutoa maamrisho kutoka juu kwamba kila kijiji kizalishe kitu ambacho kinaweza kuuzwa hapa nchini au nje ya nchi. Kinyume chake sasa, alichokifanya Dr. HIRAMATSU kwenye Wilaya ya Oita ilikuwa ni, kwanza, kutembelea vijiji vyote, kuzitambua juhudi za wananchi za thamani ambazo zilikwishaanza, akawasifia na kuwatia moyo.

Pili, alivishirikisha vijiji vingine na viongozi wao kuhusu mambo mema yanayofaa kuigwa ili habari hii iwe kichocheo, waanze na wao kufikiri kuhusu maendeleo yao wenyewe kwa kutumia rasilimali zilizopo kwenye maeneo husika, badala ya kulalamika eti hawana chochote kwenye vijiji vyao na kukata tamaa.

Tatu, alipotambua bidhaa fulani za kipekee kwenye baadhi ya vijiji, alisaidia kutafuta soko la ndani na nje ya Wilaya ya Oita. Alitumia maarifa yake, uzoefu na mitandao ambayo alikwisha

jijengea alipokuwa afisa wa ngazi za juu Wizara ya Biashara ya Kimataifa na Viwanda. Alizitangaza bidhaa hizi nchi nzima.

Nne, aliwezesha suala zima la kubadilishana uzoefu baina ya viongozi wa vijiji mbalimbali ili wajifunze na kuhamasika kutokana na kujifunza kwa watu walio kwenye ngazi moja na siyo kujifunza kwa ngazi tofauti ya maendeleo. Alianzisha shule ya kuendeleza rasilimali watu[9]" iliyoitwa "*Toyonokuni*[10]. Juhudi hizi za Gavana, zilisaidia kuchochea ari ya viongozi na hii ikapelekea kuibuka kwa miradi mingi yenye sura ya "zao moja kwa kijiji kimoja" yaani OVOP.

Kama inavyoonekana hapo juu, dhamira ya vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" au OVOP ilikuwa ni Halmashauri kuzitambua, kuzisifia, kutia moyo juhudi za kimaendeleo zinazojitokeza kwa jamii. Jukumu la Halmashauri ni "uwezeshaji" na siyo "utekelezaji" au "uelekezaji". Dr. HIRAMATSU hakuwaambia wanavijiji jambo la kufanya katika kuendeleza vuguvugu hili, bali aliheshimu juhudi zao na umiliki wao, pamoja na nguvu zao. Mafunzo ya Osaka yanasisitiza vuguvugu la"zao moja kwa kijiji kimoja", kwani ni dhana muafaka kwa mazingira ya Tanzania, na inaaminika kwamba tayari zipo juhudi za namna hiyo kwenye Vijiji na wapo viongozi wazuri wanaojali maendelo ya nyumbani kwao. Ingelikuwa ni jambo la manufaa makubwa kwa Tanzania kuunga mkono vuguvugu hili na kutoa fursa ya wazalishaji kujifunza kwa wenzao walio ngazi moja. Mafunzo ya Osaka yaliwataka viongozi wa Tanzania kudhani kwamba eti hakuna chochote kwenye vijiji vyao. Kuna mambo mengi mazuri yanayostahili kuigwa lakini pengine wao ndio hawajayatambua. Ni wajibu wa viongozi wa Halmashauri kuanza kuzitambua juhudi za jamii zilizopo, kuzitia moyo, na kubadilishana uzoefu na wengine. Ingekuwa ni njia yenye tija zaidi ya wazalishaji kujifunza kutoka kwa wenzao walio kwenye ngazi moja kuliko kujifunza watu wa ngazi tofauti au kutoka kwenye vitabu. Ni kutokana na mtizamo huu ndipo kitabu hiki kikaandaliwa.

### 3.5 Masuala Mengine

Kuna mengi ambayo hatukugusia hapo juu kutokana na kukosa nafasi. Lakini, yapo ambayo ni ya muhimu kugusia ambayo yanafaa kwa Tanzania kama vile kisamkasa cha Minamata na uzoefu unaotokana na "Ugonjwa wa Minamata"(Minamata Disease) na jinsi walivyoweza kuhuisha jamii kutokana na mkasa huo; Upangaji mipango shirikishi jamii; mipango miji; mipango ya matumizi bora ya ardhi na marekebisho ya ardhi, uzoefu wa Japani kuhusu maendeleo ya kiuchumi na mchango wa Halmashauri katika mkasa huo, n.k.

Kuhusu kisamkasa cha Minamata, mafunzo ya Osaka yanaweka msistizo kwenye umuhimu wake, na inaaminika kwamba nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania zina mengi ya kujifunza kutokana na kisa mkasa hiki. Masuala ya kisa hiki yatagusiwa kwa undani kwenye kitabu kinachofuata.

---

[9] Inaitwa "shule" lakini hakuna majengo. Huwa ni aina fulani ya mafunzo kwanjia ya warsha kwa ajili ya viongozi ili kuwakutanisha pamoja.

[10] "Toyonokuni" jina la kienyeji la eneo hili la Wilaya ya Oita

## 4.0 MAENDELEO BAADA YA MAFUNZO YA OSAKA YALIYOSABABISHA KUCHAPWA KWA KITABU HIKI

Kama ilivyoelezwa kwenye sehemu ya 1 hapo juu, mafunzo ya Osaka yalikuwa yameandaliwa mahsusi kwa nchi ya Tanzania kwenye miaka mitano ya mwanzo(2002 – 2007), yaliendelea kwa miaka mingine sita lakini wigo wake ukapanuliwa na kuingiza nchi nyingine tatu (2008 – 2012). Mafanikio makubwa katika miaka hii 11 hapa Tanzania ni kule kuanzishwa kwa Umoja wa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi waliosoma Osaka, kwa kifupi TOA. Huu ni mfano wa pekee Duniani kuwa na Umoja wa Wahitimu wa kozi ya aina moja ukijumuisha Wadau Maarufu ambao ni viongozi wa maboresho kama vile Makatibu Tawala wa Mikoa (RAS) na Wakurugenzi wa Halmashauri pamoja na wakuu wengine kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI). Japokuwa haikutegemewa, lakini ni jambo la kupendeza hata kwa JICA ambao wanaendesha maelfu ya kozi za mafunzo duniani kote.

Kwa nyongeza, TOA wameshaanza kuendesha semina mbalimbali na warsha za mafunzo kama vile Mafunzo baada ya Osaka na Warsha za Mafunzo za Kanda kwa ajili ya kubadilishana uzoefu baina ya Halmaushauri wanachama. Fursa hizi, siyo tu kwamba zina saidia kubadilishana maoni baina ya Halmashauri wanachama, bali yametoa uwanja ambao ni nadra kuupata wa majadiliano na kuhusu uhalisia wa Ugatuaji wa Madaraka, hususan changamoto wanazokutana nazo katika kutekeleza maboresho ya Serikali za Mitaa.

Mpaka sasa, hakuna asasi ya namna hii hapa Tanzania, inayowahusisha Watendaji wa Serikali za Mitaa na wale wa Sekretarieti za Mkoa. Jumuia ya Serikali za Mitaa (ALAT) ipo, lakini wahusika wake wakuu ni Wenyeviti wa Halmashauri, Mameya na Wabunge. Vikao vya Jumuiya hii haviwapi fursa Wakurugenzi wa Halmashauri kushiriki kikamilifu na kutoa ushauri wa kitaalamu ingawa wao pia ni wajumbe. Kwa mantiki hii, TOA ina uwezekano mkubwa wa kukua hadi kuwa Umoja wa Watendaji Wakuu wa Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa yaani Wakurugenzi wa Halmashauri na Makatibu Tawala wa Sekretarieti za Mikoa ambao ni wataalamu na watekelezaji wa ugatuaji wa madaraka na maboresho nchini. Hawa ndio wanaoshughulika kila siku kwenye mstari wa mbele wa maboresho. Maoni na mapendekezo yao ya pamoja yanaweza kuwa ni ya maana sana na ya kuongeza ufanisi kwenye kutekeleza maboresho.

Kuhusu mambo mema yanayofaa kuigwa, tayari Tanzania imekwishajijengea uzoefu kwa zaidi ya muongo mmoja wa utekelezaji Ugatuaji wa Madaraka kwenda ngazi za msingi katika kila Mamlaka ya Serikali za Mtaa. Lazima kutakuwepo na idadi kubwa ya mambo ya kufurahisha na uzoefu mzuri kwenye Halmashauri nyingi kote nchini ambao unafaa kushirikisha Halmashauri nyingine. Japani inaamini kwamba aina hii ya kujifunza kwa taasisi zilizo kwenye ngazi zinazofanana inaweza kuwa muafaka zaidi kuliko kujifunza kutoka nje ya nchi yaani kutoka kwenye ngazi tofauti au ya juu sana. Tanzania inaweza kujifunza vizuri kutokana na uzoefu ulioko ndani mfano shughuli za OVOP kama zilivyoelezwa kwenye 3.4. hapo juu. Kitabu hiki cha rejea kiliandaliwa kwa kuzingatia maelezo na msingi huo ulioelezwa hapo juu. Ni matumaini ya TOA na mafunzo ya Osaka kwamba yatachangia kuboresha utendaji ndani ya Mamlaka nyingi za Serikali za Mitaa, kila moja ikimchochea mwenzie, na kuendeleza mambo mema

yanayojitokeza, ambayo yatapelekea kwenye ufanisi na mafanikio ya ugatuaji wa madaraka katika nchi hii.

Mwishowe, inastahili kusema kwamba kutokana na matokeo ya kufurahisha yaliyotokana na mafunzo ya Osaka kwa nchi ya Tanzania, ambayo yameelezwa kwenye sura hii, Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japani (JICA) limeaamua kuendelea kutoa mafunzo ya Osaka kwa miaka mingine mitano, yakilenga Tanzania kwa mara nyingine tena na litatoa msisitizo maalumu katika kuwezesha shughuli za wanaumoja wa TOA na juhudi zake za ujenzi wa kitaasisi. Hii ina maana kwamba, viongozi wengine wengi wa maboresho Tanzania watafaidika kutokana na mafunzo ya Osaka ili waweze kuchangia utekelezaji mzuri zaidi wa maboresho ya ugatuaji wa madaraka kwenda ngazi za msingi nchini.

# Sura ya Pili:
# Utawala na Usimamizi wa Raslimali Watu Katika Serikali za Mitaa

Sura ya Pili inaelezea Utawala na Usimamizi wa Raslimali Watu katika Serikali za Mitaa. Ni vyema ikumbukwe kuwa lengo kuu la Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI) ni kuzipatia Serikali za Mitaa Uhuru wa kufanya maamuzi hadi ngazi za chini kabisa. Utawala ni mchakato wa kuipa jamii mwongozo ambapo msisistizo upo kwenye mahusiano kati ya Dola na washiriki wengine pamoja na taasisi za biashara. Utawala katika Serikali za Mitaa haumaanishi nafasi na majukumu tu, bali mahusiano mbalimbali kati ya Serikali za Mitaa na makundi mengine. Mahusiano haya huleta mambo muhimu ya maendeleo endelevu kama utoaji huduma, maendeleo ya miundombinu na Mipango. Msisitizo katika mahusiano ya Utawala Bora, siyo tu kwenye nafasi ya taasisi za serikali, bali pia yameegamia kwenye sera ya kuongeza ushiriki wa wananchi na wadau katika kufanya maamuzi na mipango (Hamann et al 2005). Utawala Bora katika Serikali za Mitaa ni ile nafasi ya kujikita katika kuhamasisha ushiriki katika ngazi za chini (ugatuaji ) na kutambua umuhimu wa jamii katika kuleta matokeo kwa jamii. (klinken, 2003).

Katika mazingira ya Ugatuaji (D by D) hapa Tanzania, Utawala katika Serikali za Mitaa ni ile namna ambayo Mamlaka ya Halmashauri hutimiza majukumu yake kwa wananchi waliopo kwenye eneo lake. Inajumuisha mahusiano kati ya viongozi wa Mamlaka na wananchi, pamoja na vyama vya siasa, mashirika yasiyo ya kiserikali, na Serikali Kuu katika maeneo yote ya kutunga na kutekeleza sera zinazogusa watu katika maeneo yao. Dalili muhimu na za kuonekana za kiutawala katika kesi zilizopo hapa chini ni (i) Uhuru wa Serikali za Mitaa (ii) Mahusiano ya sekta mbalimbali (iii) upangaji mipango toka chini kwenda juu na (iv) mahusiano ya kiuaminifu kati ya watumishi na madiwani na kati ya wananchi na Halmashauri (breathn,et al 2005).

Katika Sura hii kesi nne zimewasilishwa; zote zinahusiana na Mbinu Bora za Utawala Bora na Usimamizi bora wa Raslimali Watu. Kesi ya kwanza inatoka Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga na inaelezea ugunduzi wa mbinu ya Uwajibikaji wa Madiwani ambayo hujulikana kama Mbinu ya Katanga (Katanga model). Kesi hii ni ya kuvutia sana na imehamasisha wadau wengi wa Utawala katika Serikali za Mitaa na inaonyesha uhalisia wa nafasi ya Diwani kwa wapiga kura na Halmashauri kwa Ujumla. Kesi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda inaongelea Maboresho ya mazingira katika sehemu za kazi ili kuongeza utendaji katika ngazi zote za Halmashauri. Imejikita zaidi katika kujenga ofisi za kisasa, kuweka samani, na kujenga nyumba za watumishi katika kata na vijiji na kuwapatia watumishi usafiri. Kesi ya Halmashauri ya Ukerewe imeegemea zaidi kwenye kubakiza watumishi katika Halmashauri kupitia uboreshaji wa mazingira ya kazi na makazi. Kesi hii inasisitiza Uongozi wa kibinadamu kwa watumishi wa Halmashauri. Neno “Kibinadamu“ linamaanisha wema, huruma, au upendo kwa watumishi. Kesi hii inasisitiza juu ya

sifa na mwelekeo wa kibinadamu na unaoonyeshwa na Menejimenti. Kesi ya Halmashauri ya wilaya ya Chunya inahusu Kutafuta, Kumotisha na Kubakiza watumishi katika mazingira magumu na ya pembezoni. Katika kesi hii mbinu bunifu za kuvutia na kubakiza watumishi katika mazingira magumu na ya pembezoni zimeainishwa. Kesi hii inapendekeza kuwa Serikali inatakiwa kuwa na tengo la kipekee kwenye bajeti kwa ajili ya ajira na posho ya mazingira magumu kwa watumishi wa umma wanaoishi kwenye mazingira magumu sana.
Kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweza kujiendesha katika misingi ya utawala bora, zinahitaji watumishi wenye uwezo na usimamizi bora wa Raslimali Watu. Raslimali watu ni kujaza nafasi za watumishi na kuendesha taasisi. Usimamizi wa raslimali watu ni shughuli ya taasisi inayohusiana na Masuala ya watumishi kama ajira, utendaji, mafunzo, motisha na mwelekeo wa watu wanaofanyakazi kwenye taasisi. Usimamizi wa raslimali watu wa kisasa unajumuisha kushughulikia motisha, mafunzo, maisha ya kazini na maendeleo kazini ya mfanyakazi binafsi. Usimamizi bora wa raslimali watu huimarisha utendaji wa taasisi kwa kuongeza fursa za watumishi katika ubora na uzalishaji. Hii inahusisha matumizi ya watumishi kiuzalishaji katika kufikia malengo ya taasisi pamoja na kuridhisha mahitaji ya mtumishi binafsi.

Katika Ugatuaji hapa Tanzania usimamizi wa Rasilimali Watu umekuwa eneo muhimu la Maboresho na Maendeleo. Ukiacha kutangaza ajira na kuchagua watumishi wenye sifa, eneo la usimamizi wa raslimaliwatu katika maboresho limeshughulika zaidi na Masuala ya mafunzo, motisha, upunguzaji kuacha kazi na utendaji wa watumishi pamoja na kujenga uwezo. Mamlaka za serikali za mitaa hapa Tanzania chini ya uongozi wa Wakurugenzi wa Halmashauri zinatarajiwa kuwa na watumishi wenye sifa, motisha na dhamira kuanzia Halmashauri, Kata na Vijiji kwa lengo la kutoa huduma bora kwa jamii zilizopo kwenye maeneo yao.

Mambo muhimu yanayojitokeza katika kesi zilizopo kwenye sura hii yanaonyesha kuwa utendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa hapa Tanzania unategemea zaidi sifa za viongozi wa kuteuliwa na kuchaguliwa;

- Kama mchakato wa kutafuta uongozi wa Halmashauri hautasisitiza sifa kama vipaji, uwezo, uzoefu uliojikusanya, mtazamo, uwakilishi, ushawishi na uhamasishaji jamii; na uelewa sahihi, hatuwezi kutarajia mengi katika mantiki ya maendeleo kijamii na kiuchumi. Ni dhahiri sasa kinachohitajika zaidi katika uongozi wa Halmashauri ni mbali kabisa na sifa za vyeti au uwezo tu wa kusoma na kuandika.
- Suala la pili ni umoja kati ya uongozi wa kuchaguliwa na ule wa kuteuliwa. Kunatakiwa kuwa na mshikamano thabiti na ushirikiano kati ya, na ndani ya hizi ngazi mbili ili kutatua changamoto za Halmashauri kwa pamoja kama timu.
- Motisha wa watumishi ni suala jingine linalohitajika katika utoaji huduma bora hasa katika maeneo yaliyo pembezoni, yaliyojitenga na magumu kuishi. Maeneo haya yanahitaji kuainishwa na kupewa kipaumbele.
- Raslimali fedha, watu na nyinginezo ni muhimu. Raslimali watu wana umuhimu wa pekee kwani ndio huratibu raslimali nyingine kwa maendeleo ya watu.

- Upatikanaji wa taarifa pia ni muhimu na kila mtu kwenye Halmashauri anahitajika kujijengea tabia ya kujisomea ili kujua yanayoendelea katika mchakato wa maendeleo. Kesi zifuatazo zitachambua kwa kina masuala haya kwa kutumia mifano rahisi ya uzoefu wa kazini.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MBINGA

## UWAJIBIKAJI WA MADIWANI KATIKA MIRADI YA MAENDELEO






Mbinga: Baraza Likiendelea

## 1.0 UTANGULIZI

Uwajibikaji jamii ni mfumo ambao huruhusu wananchi kudai uwajibikaji wa watoa huduma na viongonzi wa umma kwa kushiriki moja kwa moja au kwa uwakilishi. Uwajibikaji jamii hujumuisha taarifa juu ya haki na utoaji huduma pamoja na uwajibikaji wa pamoja katika kuleta mabadiliko.

Taasisi za Serikali, watoa huduma na wawakilishi wa wananchi katika nchi zinazoendelea mara nyingi huwaangusha maskini. Mapungufu ni mengi na mabaya; rushwa, kutokuwajibika, huduma zenye ubora duni, na wakati mwingine kukosekana kabisa kwa huduma. Matokeo ya haya yote ni uendelevu wa kuwanyonya wananchi, kubomoka kwa madarasa, vituo vya afya visivyo na umeme au madawa, ofisi za umma zisizo na samani na vitendea kazi, kutokuwepo kwa walimu na wauguzi, mabomba yasiyo na maji, ubovu wa barabara, kukosekana kwa masoko ya bidhaa za ndani na ukosekanaji wa sauti ya wananchi katika maamuzi muhimu.

Kesi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ni mfano mzuri wa jinsi ambavyo madiwani na watendaji wanaweza kuwajibika vizuri kwa wapiga kura na walipa kodi kwa lengo la upatikanaji wa huduma bora. Pia kesi hii inaonyesha jinsi wapiga kura na walipa kodi wanavyoweza kuwajibika kuchukua hatua kwa pamoja katika kuondoa matatizo ya kijamii na kiuchumi na kufikia maisha bora. Kutokana na mfumo huu na uwajibikaji jamii toka mwaka 1999, Halmashauri ya Mbinga haijawahi kupata hati chafu au yenye mashaka katika ukaguzi wa hesabu za Halmashauri. Kutokana na hili; TOA iliamua kesi ya Mbinga yaani “Katanga model” ichukuliwe kama kesi ya mfano ya utendaji uliotukuka katika Utawala Bora hasa kwa eneo la Uwajibikaji wa Madiwani hapa Tanzania. Kesi hii inajulikana kama Katanga Model kwa sababu ya uongozi thabiti na udiriki wa Mkurugenzi Mtendaji aliyekuwepo Bwana Hussein Katanga. Ni vyema pia ikumbukwe kuwa Bwana Hussein Katanga alikuwa mmoja wa Wakuruguenzi wa mwanzo kabisa waliohudhuria mafunzo ya Utawala Bora huko Osaka Japan. Baadhi ya mifano ya utendaji iliyopo humu inatokana na mafunzo ya Osaka na ambayo ina thamani kwa Halmashauri nyingine hapa Tanzania.

## 2.0 HISTORIA

Halmashauri ya Wilaya Mbinga ni mojawapo ya Halmashauri tano za Mkoa wa Ruvuma iliyo kusini mwa Tanzania takribani 1,000km kutoka Dar – es – salaam. Mbinga ipo upande wa kusini mashariki mwa Mkoa wa Ruvuma, ikipakana na Halmashauri ya Wilaya ya Songea kwa upande wa Mashariki, Jamhuri ya Msumbiji kwa upande wa Kusini na Ziwa Nyasa na Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kwa upande wa Kaskazini. Halmashauri hii ina km za mraba 11,396, kata 49, na vijiji 233, ikiwa na millima na eneo jembamba la ardhi ya chini kwenye mwambao wa Ziwa Nyasa. Mbinga ina mwinuko wa ardhi wa kati ya mita 900 hadi mita 1300 juu ya usawa wa bahari na maeneo machache ya tambarare za matengo ambazo zipo mita 2000 juu ya usawa wa bahari.

Eneo bora la uzalishaji linakaliwa na Wamatengo ambao hulima mazao ya chakula na biashara kwenye milima yenye miteremko mikali ipatayo kipimo cha 40%. Wamatengo wana mfumo wa

kipekee wa kilimo ambapo huchanganya kilimo cha kahawa kama zao la biashara na mfumo wa "ngoro," kulima mahindi na maharage ambayo ni mazao muhimu ya chakula. Mbinga hutegemea kwa kiasi kikubwa uzalishaji wa kahawa bora inayolimwa kwenye ardhi ya volcano yenye ubora wa hali ya juu.

## 3.0 MATATIZO YALIYOKUWEPO KABLA YA MBINU YA KATANGA

Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ilikuwa na vigingi vingi vilivyozuia kupatikana kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika sekta mbalimbali. Baadhi ya matatizo haya yalikuwa;

(i) Ushiriki hafifu wa Madiwani katika utekelezaji wa miradi. Ilichukuliwa ni jukumu la watendaji kuhamasisha na kushirikisha jamii katika maendeleo. Madiwani walijihusisha na uchaguzi tu na sio maendeleo ya watu.

(ii) Uwajibikaji hafifu wa Madiwani kuhusu shughuli za maendeleo ya jamii. Ni mara chache sana madiwani waliwajibika kuhusu shughuli za maendeleo. Watendaji kata na maofisa wengine wa Halmashauri ndio waliokuwa wakilaumiwa mara kwa mara kuhusu utekelezaji duni wa miradi.

(iii) Upashanaji habari duni kati ya Madiwani, Watumishi na Wadau wengine wa Halmashauri. Kulikuwa hakuna jukwaa la kupashana habari kuhusu miradi na maendeleo ya jamii. Pia hakukuwa na utaratibu wa kutoa taarifa kwa jamii kuhusu mipango na bajeti za Halmashauri.

(iv) Mahusiano mabaya kati ya Madiwani, Watumishi wa Halmashauri na jamii. Hakukuwa na maelewano kati ya makundi haya matatu. Hata lugha iliyotumika kati ya makundi haya haikuwa ya kuridhisha. Hii ni kwa sababu matarajio ya kila kundi hayakufikiwa na kundi jingine, pia kulikuwa na kulaumiana kwingi kulikotokana na ukosefu wa ushirkiano kati yao.

(v) Ushiriki mdogo wa jamii katika shughuli za maendeleo. Jamii ilishiriki shughuli za maendeleo bila maandalizi wakati madiwani hawakuwa na ari ya kuhamasisha na kushirikisha jamii kwenye shughuli za maendeleo kwa kuhofia kupoteza umaarufu. Hatimaye mchango wa Halmashauri kwenye miradi ya maendeleo haukuwa ukifikiwa na kama ulifikiwa basi siyo kwa wakati.

## 4.0 MALENGO

Ili kukabiliana na matatizo haya Halmashauri ilidhamiria kufikia malengo yafuatayo;

(i) Kuboresha Ushiriki, Kujituma na Uwajibikaji kwenye utekelezaji wa miradi.

(ii) Kuimarisha hali ya kuaminiana kati ya Watendaji, Madiwani na jamii ili kuboresha upashanaji habari.

(iii) Kuimarisha mahusiano bora kati ya Madiwani, Watendaji na jamii.

(iv) Kusisitiza uelewa wa jamii kwa kuwa na maandalizi jamii ili kushiriki kikamilifu kwenye uibuaji na utekelezajji wa miradi.
(v) Kuboresha nidhamu katika usimamizi na matumizi ya fedha za miradi.

**5.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga iliazimia kwa msisitizo kuondoa tatizo la uwajibikaji kwa kutumia mfumo wa uwajibikaji jamii. Mwaka 1998 mfumo wa Uwajibikaji wa Madiwani kuhusu miradi ya jamii (Katanga Model) ulianzishwa na aliyekuuwa Mkurugenzi Mtendaji Bwana Hussein Katanga kwa ushirikiano thabiti na Mwenyekiti wa Halmashauri kipindi hicho hayati Luteni Kanali Jackob Likopesi Kulemba. Mfumo huu ulianza kufanya kazi rasmi mwaka 2006/2007.

**6.0 MBINU YA KATANGA**

"Katanga Model" ni mfumo ambao una lengo la kuanzisha na kuingiza tabia ya uwajibikaji kwa Madiwani hasa katika vipaumbele vya jamii wanazoziwakilisha kwenye Halmashauri. Madiwani, Watendaji wa Kata na walezi wa Kata katika mfumo huu hushiriki kikamilifu kwa pamoja kuitumikia jamii tena kwa utambuzi na ufahamu wa hali ya juu. Madiwanni wamepewa jukumu la lazima la kutoa taarifa na kuwajibika kwa shughuli zote za maendeleo zinazofanyika katika maeneo yao ya uwakilishi. Vipengele muhimu vya Katanga Model ni;

(i) Kwa kushirikiana na jamii, Madiwani, Maafisa tarafa, walezi wa kata kuendesha mikutano ya kisheria katika Vitongoji, Vijiji na Kata (WDC). Kwa njia hii madiwani hupata uelewa na taarifa za shughuli za maendeleo zinazofanyika katika ngazi za msingi za jamii na kupata umiliki wa miradi. Madiwani hushiriki kwenye vikao vya Vitongoji na Vijiji kama daraja kati ya Halmashauri na jamii.
(ii) Taarifa kutoka ngazi ya Kitongoji zinaunganishwa kupata taarifa ya Kijiji. Taarifa za Vijiji zinaunganishwa kupata taarifa za Kata. Taafira ya Kata hujadiliwa kwa kina na kuandikwa katika mtiririko uliokubalika kabla ya kusomwa kwenye kikao cha Halmashauri.
(iii) Ili kudhibiti tofauti katika uwasilishaji wa taarifa za madiwani, mtiririko maalumu wa uandishi wa uwasilishaji wa taarifa umeandaliwa na Halmashauiri ili kupata taarifa zote muhimu za ngazi za msingi. Mtiririko huu hujumuisha utekelezaji wa miradi na utendaji katika utawala bora. Taarifa hizi huwasilishwa na Madiwani na kujadiliwa siku ya kwanza ya Baraza la Madiwani.
(iv) Kwa kawaida Baraza la Madiwani nchini Tanzania hufanyika kwa siku moja, lakini kwa Halmashauri ya Mbinga huchukua siku mbili. Kwa kuzingatia sheria na taratibu za Serikali za Mitaa, Halmashauri ilipitisha siku moja zaidi ya Baraza kwa kurejea kanuni za kudumu na kupata ruhusa (kibali) kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za

Mitaa. Siku ya kwanza ya baraza ni maalum kwa uwasilishaji wa Taarifa za maendeleo za Kata na huitwa kikao cha kazi. Taarifa hizi huwasilishwa na Madiwani wa kila Kata. Siku ya pili ndio siku maalum ya kikao cha Baraza la Madiwani.

(v) Kikao cha baraza la madiwani pia huhudhuriwa na Maafisa Watendaji wa Kata. Kwa siku ya kwanza ya kikao, Maafisa Watendaji wa Kata ndio huwasilisha taarifa za maendeleo za Kata, kwa niaba ya madiwani. Taarifa hizi hujadiliwa kwa kina na Madiwani wote, wakiomba maelezo kutoka kwa Diwani wa Kata husika na kukemea utendaji usioridhisha.

(vi) Siku ya pili ya kikao cha Baraza Idara ya Uchumi na Mipango huwasilisha taarifa ya utekelezaji iliyoboreshwa na picha kuongeza ushahidi wa taarifa za Kata zilizowasilishwa siku ya kwanza.

(vii) Maamuzi ya Baraza na Bajeti zilizopitishwa kwa ajili ya miradi katika jamii hutolewa taarifa kwa jamii na kwa miradi ambayo haitapata fedha, jamii zinahamasishwa kuchangia kwa hali na mali ili kupunguza uwezekano wa jamii kukosa hamasa na kukata tamaa.

### 6.1 Utekelezaji wa Mbinu ya Katanga

Ili kuweza kutumia mfumo huu kuna vitu vya msingi na maandalizi yanayohitajika. Kwa Halmashauri ya Mbinga ilibidi Madiwani washiriki mafunzo ya siku mbili juu ya utawala bora ili kupata stadi za uwajibikaji kwa jamii. Viongozi wa Kata na Vijiji sambamba na Madiwani pia walipata mafunzo ya stadi za uongozi na maadili.

Kila Kata ilipatiwa Mlezi kutoka watumishi wa Halmashauri ambao ni Wakuu wa Idara. Mlezi hachukui nafasi ya Afisa Mtendaji wa Kata bali anajazia utendaji na utekelezaji wa majukumu ya Afisa Mtendaji wa Kata. Mlezi ni kiungo muhimu kati ya jamii na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri. Mlezi anatakiwa kujishughulisha na mambo ya maendeleo kwenye Kata na anatakiwa kuwa na taarifa zote muhimu pale zinapohitajika au kuingilia utendaji kabla mambo hayajaharibika. Walezi wana ari ya utendaji na kila mwezi hushirikiana na jamii katika kampeni ya usafi wa mazingira.

**Motisha kwa watumishi.** Kila mwezi Mkurugenzi Mtendaji Bwana Katanga alijiwekea utaratibu wa kukutana na Watendaji Kata na kujadili mambo muhimu yanayohusu utekelezaji wa haraka. Kwa Mkurugenzi kukutana na Maafisa Watendaji wa Kata ni njia mojawapo ya kuunda na kuboresha mfumo wa timu. Inawajengea imani na ukweli kuwa Watendaji wa Kata ni muhimu katika Halmashauri na kuwa kuna mtu anayewajali kwa yale wanayoyatekeleza. Kila uwezo wa bajeti unaporuhusu watendaji wote wa Kata na Vijiji hupewa samani za ofisi na vitendea kazi.

Kutokana na hali ya milima ya Mbinga usafiri kwa Maafisa Watendaji na Wakuu wa Idara ni muhimu kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za maendeleo. Maafisa Watendaji wa Kata wote 49 na walezi wote walipatiwa usafiri wa pikipiki kwa gharama nafuu. Ili kuwatia motisha,

wanatakiwa kulipa asilimia 50 tu ya gharama za kununulia pikipiki kidogo kidogo kwa miaka mitano. Hili liliwezekana kwa sababu Halmashauri ina mfuko endelevu wa kusaidia watumishi. Utaratibu huu wa mfuko endelevu ulianzishwa katika Halmashauri. Lengo kuu la mfuko ni kuhakikisha watumishi wote wanapata usafiri stahiki kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zao.

Mfuko huu endelevu na maalum ulioanzishwa na kuimarishwa katika Makao Makuu ya Halmashauri. Lengo kuu la mfuko ni kuhakikisha watumishi wote watapata usafiri wa uhakika kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zao. Fedha za kuanzisha mfuko huu zilitolewa na Halmashauri na watumishi kuendelea kuchangia kila mwezi. Mfuko ukishakuwa na fedha za kutosha, kikundi cha wakopaji huruhusiwa kukopa. Angalia picha hapo chini.



**Pikipiki zinazomilikiwa na watumishi kupitia Mfuko wa Usafiri**

Mwaka 2004/2005 Halmashauri iliwezesha umiliki wa viwanja vya makazi kwa watumishi. Hii ilifanyika pamoja na mikopo ya vifaa vya ujenzi kama simenti, mabati na mabomba. Matokeo yake ni kuwa watumishi wengi wanaishi kwenye nyumba zoa binafsi na wengi wameamua kutokuhama Mbinga.

**Uboreshaji wa miundo mbinu,** Halmashauri inamiliki na kutunza mitambo ya ujenzi kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu. Mitambo hii inajumuisha greda, kijiko, mashine ya kushindilia, matrekta mawili na lori kubwa. Kwa kutumia mitambo hii matengenezo ya barabara hufanyika kwa muda uliopangwa na thamani ya pesa huonekana. Endapo jamii yoyote ndani ya Halmashauri inataka kutumia mitambo hii kwa kusawazisha viwanja au ardhi hupewa bure kwa sharti la kuweka mafuta (dizeli) tu.



Mitambo ya Ujenzi wa Miundombinu



**Uboreshaji wa Taasisi,** huduma za kifedha ni muhimu sana kwa miradi ya maendeleo. Kwa kujua hili, Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ilianzisha Benki ya watu wa Mbinga (MCB) ambayo inakidhi mahitaji yote ya kifedha ya vikundi vya wakulima na ushirika (Saccos).

**Maendeleo ya Kiuchumi,** watu wa Mbinga na makampuni binafsi ya kahawa wametumia jitihada za ziada kuhakikisha kahawa ya Mbinga ina ubora wa hali ya juu na inapata bei za juu kwenye Soko. Walianzisha Makaushio bora 13 ya kahawa na mpaka sasa yamefikia 100, ili kuhakikisha maandalizi bora ya kahawa. Pia siyo kahawa yote inauzwa nje, karibu 10% husindikwa Mbinga na kupatikana kwa Kahawa ya Mbinga yenye ladha ya pekee.



**Kaushio la Kahawa**

## 7.0 RASLIMALI ZILIZOTUMIKA

Rasilimali zilizotumika kwenye Katanga model zinajumuisha raslimali watu, fedha, mali nyingine na muda. Raslimali watu zilijumuisha watendaji wa Halmashauri (walezi wa kata), madiwani, Wenyeviti wa Vijiji, Watendaji wa Kata na Vijiji na wanavijiji. Mtiririko wa matumizi ya fedha unaoneshwa kwenye jedwali 2.1.

**Jedwali 2.1: Mtiririko wa Matumizi Kabla na Baada ya Mbinu ya Katanga**

| No | Aina Ya Mkutano | Mwaka | Kiasi Kilichotumika kwa Mkutano TZS | Kiasi Kilichotumika kwa Mwaka in TZS |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Baraza la Madiwani | 2004 | 19.650,000.00 | 78,600,000.00 |
| 2 | Baraza la Madiwani | 2005 | 19.650,000.00 | 78,600,000.00 |
| 3 | Baraza la Madiwani | 2006 | 19,900,000.00 | 79,600,000.00 |
| 4 | Baraza la Madiwani | 2007 | 21,500,800.00 | 86,003,200.00 |
| 5 | Baraza la Madiwani | 2008 | 21,500,800.00 | 86,003,200.00 |
| 6 | Baraza la Madiwani | 2009 | 28,745,000.00 | 114,980,000.00 |
| 7 | Baraza la Madiwani | 2010 | 38,842,000.00 | 155,368,000.00 |
| 8 | Baraza la Madiwani | 2011 | 38,842,000.00 | 155,368,000.00 |

Chanzo: Mbinga DC, 2011

Raslimali nyingine zilizotumika ni pikipiki 49 kwa ajili ya Maafisa waliokuwa mstari wa mbele kwenye utekelezaji, mashine 49 za uchapaji, shajara (stationary) n.k. Hizi zote zilipelekwa kwenye ngazi za msingi za utekelezaji.

Kwa upande wa raslimali muda walezi wa Kata (49) hutumia wastani wa siku mbili kwa robo mwaka kuzitembelea Kata kwa ajili ya usimamizi na ushauri. Hii ni sawa na siku nane kwa mwaka. Karibu siku 10 kwa robo mwaka hutumiwa na Madiwani na Timu ya Menejementi ya Halmashauri kukagua utekelezaji wa miradi. Vikao vya kawaida vya Madiwani hufanyika kwa siku mbili kila robo mwaka. Mikutano ya Kitongoji hufanyika kila mwezi, wakati vikao vya Kijiji na Kamati ya Maendeleo ya Kata hufanyika kila robo mwaka.

## 8.0 MAFANIKIO NA MATOKEO

**Kubadilika Tabia na Mtazamo.** Kupitia utekelezaji wa Katanga Model (mfumo wa uwajibikaji wa Madiwani) kumekuwa na matokeo mazuri ya mahusiano kati ya jamii na Halmashauri. Kumekuwa na hali ya juu ya uwajibikaji kwa pande zote mbili. Mfumo huu una ufanisi wa hali ya juu katika kuhakikisha uwajibikaji kwa jamii. Madiwani wamekuwa na uelewa zaidi wa wajibu na majukumu yao kuliko zamani. Madiwani pia wanafurahia utendaji wa watumishi wa Halmashauri. Kumekuwa na ushirikiano mzuri kati ya viongozi wa kisiasa na watumishi ikilinganishwa na hapo awali. Watu wa Mbinga wamehamasika zaidi kuelekea mageuzi wamekuwa tayari zaidi kwa mambo mapya ya maendeleo kuliko hapo mwanzo.

**Boksi 2.1. Maoni ya Mdau**
Makamu Mwenyekiti wa Halamashauri Mh. Prisca Haule anasema…..
" ..Mfumo huu mpya umeimarisha uwajibikaji jamii kwa pande zote mbili, wapokeaji na watoaji. Watu wanawajibika kwa maendeleo yao na watoaji (Halmashauri) wana dhamira ya kusaidia mchakato wa maendeleo ya watu. Kuhitajika kwa taarifa za Kata imewaweka wadau wote wa Kata kuwa tayari muda wote kuainisha changamoto na mafanikio, kila Diwani anatakiwa kutoa mrejesho kwa watu wake, na zaidi kumekuwa na uwazi wa hali ya juu…"

**Mawasiliwano Bora.** Mfumo huu umeboresha mawasiliano kati ya Madiwani na Watendaji wa Kata, hakuna tena kutoelewana kati ya wanasiasa na watumishi. Wote wanafanya kazi kama timu moja kwa lengo la kutoa huduma bora. Imekuwa kawaida kwa Madiwani kuwaita wataalam kutembelea Kata na kutoa maelekezo bila urasimu uliokuwepo kabla.

**Boksi 2.2: Afisa Mtendaji Kata ya Mkako, Edwin Kiulu:**
**"…Kupitia mfumo huu mpya,kumekuwa na kuaminiana zaidi kati ya Watendaji na Madiwani; kwa sasa tunashauriana pamoja. Wote viongozi wa kuchaguliwa na watumishi wataalam wanafanya kazi pamoja kutafuta michango ya jamii kwa ajili ya miradi ya maendeleo, haikuwa hivi siku za nyuma!! Lugha ya mawasiliano kati yetu ni kindugu zaidi kuliko huko nyuma…"**

**Ushiriki wa kweli wa jamii.** Ushiriki jamii wa kweli ni mfumo ambao wadau wote hushiriki kwenye miradi ya maendeleo kwa uelewa, uhuru, haki, uchangamfu na bila kubagua baadhi ya makundi katika jamii. Kwa sasa Mbinga kuna ushiriki wa kweli wa wananchi katika kupanga, kuweka vipaumbele, kuchagua, kutekeleza na kupima shughuli za maendeleo. Wanatumia mfumo wa upangaji mipango unaoanzia chini kikamilifu.

**Mazingira mazuri ya Kazi.** Watumishi wote waliohojiwa hakuna hata mmoja yuko tayari kuhama Mbinga; ikidhihirisha kuwa Mbinu ya Katanga haina uhusiano wowote na motisha unaotokana na mshahara. Mfumo huu umeimarisha watumishi kubakia Mbinga. Afisa Utumishi wa Halmashauri aliwahi kusema "watumishi wengi wanaopangiwa Mbinga huwa hawapendi lakini wakishafika na kukaa kidogo hakuna hata mmoja anayetaka kuhamishwa".

**Utoaji bora wa huduma za jamii**. Kila Kata ina Sekondari moja au mbili. Kati ya Vijiji 233, Vijiji 79 vimeshajenga zahanati, kati ya Kata 49, kata 10 zina vituo vya afya vinavyofanya kazi vizuri

na Kata nyingine zinaendelea na ujenzi katika hatua mbalimbali. Katika shule za Msingi na Sekondari, jamii imeweza kujenga idadi tosha ya madarasa, matundu ya choo na nyumba za Walimu. Jamii pia imeweza kujenga ofisi za Vijiji kila Kijiji. Halmashauri imejenga jengo la kisasa la kuhifadhia maiti na wadi ya daraja la kwanza kwa ajili ya wagonjwa wa ndani katika Hospitali ya Wilaya. Zaidi ya haya Halmashauri ya Mbinga inaendesha Mfuko wa Afya ya Jamii ambao unasaidia wagonjwa 10,000 wa nje na 20,000 waliolazwa.



**Muuguzi akiwa katika Moja ya Vituo vya Afya**



**Nyumba za Watumishi**

**Umeme,** Kidimba ni kijiji kilichopo kwenye mteremko wa Ziwa Nyasa na kina kituo chake cha kuzalisha umeme kwa njia ya maji. Wanaofaidika na mradi huu ni pamoja na vijiji viwili na kituo cha afya kilichopo Kidimba Chini na Mbamba Bay.

**Mafanikio katika ujenzi wa barabara**, karibu 70% ya barabara zote za Halmashauri zinapitika mwaka mzima na 4.15 km za lami zilijengwa kwa kutumia mapato ya ndani. Haya ni mafanikio makubwa. Jedwali 2.2. linaonyesha.

**Table 2.2: Ujenzi wa Barabara Mbinga DC**

| Aina ya Barabara | km | Mhusika | Hali Halisi |
|---|---|---|---|
| Barabara Kuu | 122 | TANROADS | |
| Barabara za mkoa | 371 | TANROADS | |
| Barabara za Halmashauri | 1393.7 | Mbinga DC | 70% zinapitika mwaka mzima |
| Barabara za jamii | 800 | Vijiji, halmashauri huchangia makalveti, madaraja na Usimamizi | |
| Barabara za Mjini | 53.1 | Mbinga DC, Mfuko wa barabara, Mapato ya ndani, LGCOG | 4.15 barabara ya lami kwa fedha za halmashauri |

**Chanzo: Mbinga DC 2012**

**Matumizi ya mafundi wenyeji.** Kati ya mabadiliko katika Halmashauri ya Mbinga mojawapo ni la matumizi ya mafundi wenyeji badala ya wakandarasi kwa shughuli ndogondogo. Utaratibu huu umefanikisha kupunguza gharama. Matokeo yake ni kuwa Vijiji vingi vimeweza kuboresha miundo mbinu kwa gharama nafuu kabisa. Pia Halmashauri ya Mbinga inatumia uzoefu wa

waastaafu katika kuamsha na kuhamasisha jamii. Kwa mfano katika kijiji cha Utiri, Diwani ni Afisa Elimu Mkoa mstaafu.

**Kuimarika kwa Utawala Bora.** Wananchi katika ngazi za msingi kwa hiari wanashiriki vikao vya kisheria. Matumizi ya mbao za matangazo yameongezeka kwa ajili ya upashanaji habari katika jamii. Zaidi ya hiyo, kuna kiasi kikubwa cha mwamko katika jamii wa kufuatilia majadiliano ya Baraza la Madiwani ikilinganishwa na zamani. La msingi zaidi hapa ni ongezeko la ushiriki wa jamii katika kupanga, kutekeleza na umiliki wa miradi yao.



**Matumizi ya Mbao za Matangazo Kuweka wazi Taarifa Muhimu**

**Utunzaji wa mazingira**. Kwa upande wa utunzaji wa mazingira Halmashauri ya Mbinga imeanzisha vitalu katika ngazi ya jamii katika shule zote za msingi zipatazo 915. Jitihada hii ina lengo la kuimarisha kilimo cha miti kwa kuchanganya miti na mazao ya chakula. Pia kuna jitihada za makusudi za kuilinda misitu ya jamii na janga la moto katika vijiji. Katika Mji wa Mbinga, Halmashauri imejenga sehemu za kukusanyia taka na mfumo wa maji taka. Pia kuna kampeni ya kuelimisha jamii juu ya usafi wa mazingira kwa kudhibiti utupaji ovyo taka katika kila Kata.



**Mfumo wa Kimatengo wa kilimo (ngoro)**



**Shamba la kahawa kwenye mteremko mkali**

**Uhamasishaji wa shughuli za kiuchumi.** Halmashauri ya Mbinga inahamasisha shughuli za kiuchumi, mazao ya biashara na chakula (korosho, kahawa,ndizi,mihogo na mpunga) pamoja na kilimo maji. Halmashauri ya Mbinga ni mfano kwenye kusaidia biashara ndogo na za kati (SMEs). Kila panapotokea jitihada za wananchi Halmashauri huitikia kwa haraka na kuwasaidia. Halmashauri hugawa mbegu, matawi na miche ya aina zilizoboreshwa bila malipo ili kuongeza uzalishaji. Halmashauri pia inahamasisha uanzishwaji wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo. Kwa mfano kuna zaidi ya makaushio 100 ya kahawa yaliyoko katikati ya maeneo ya uzalishaji. Ili kusaidia biashara zote hizi Halmashauri imeanzisha taasisi za fedha.






**Benki ya wananchi wa Kata ya Utiri** **Ofisi za Muungano SACCOs na ya Kimuli AMCOs**

Kama ilivyoelezwa hapo juu, Benki ya Watu wa Mbinga inahudumia vikundi vya wakulima wa ushirika (SACCOS). Kuna jitihada za kuanzisha Benki Kata katika kila Kata. Kwa mfano katika kata ya Utiri, chama cha ushirika cha Muungano (Saccos) kilibadilika na kuwa Benki kata.

Matokeo ya jitihada zote hizi, mfumo Katanga umechangia sana kuboresha mapato ya ndani ya Halmashauri (angalia jedwali 2.3.). Mfumo huu pia umepelekea kuongezeka kwa matumizi yenye nidhamu ya mapato ya Halmashauri. Toka mwaka 1999 Halmashauri ya Mbinga haijawahi kupata hati yenye mashaka au chafu. Huu ni ushahidi tosha wa ufanisi na ubora wa matumizi ya fedha za umma.

**Table 2.3: Mtiririko wa mapato ya ndani**

| Mwaka | Makisio | Makusanyo halisi | % |
|---|---:|---:|---:|
| 2002/3 | 575,713,000.00 | 618,598,369.35 | 107.45 |
| 2000/4 | 261,988,961.00 | 150,449,953.39 | 57.43 |
| 2005/06 | 740,902,800.00 | 835,844,720.00 | 116 |
| 2006/07 | 752,000,000.00 | 1,042,445,687.19 | 138.62 |
| 2007/08 | 934,000,000.00 | 1,190,610,229.87 | 127 |
| 2008/09 | 1,184,660,720.00 | 1,428,065,019.19 | 121 |
| 2009/10 | 1,074,750,000.00 | 609,887,799.97 | 56.75 |
| 2010/11 | 1,289,700,000.00 | 2,133,966,435.00 | 165 |

**Chanzo: Mbinga DC 2011**

**Matokeo ya ziada.** Halmashauri kama tano hivi zimeshafika Mbinga kwa lengo la mafunzo. Hizi ni Halmashauri za wilaya za Songea, Namtumbo, Siha, Kilolo na Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga. Katika kipindi cha kuchapa kitabu hiki halmashauri ya wilaya ya Tandahimba walikuwa wanasubiri kutembelea Mbinga. Ni mahali ambapo kuna thamani kupatembelea kwa lengo la kukuza uwajibikaji.

**9.0 CHANGAMOTO ZILIZOKUWEPO**

Kutokana na ufanisi na ubora wa mfumo huu jamii imehamasika na kuchangamkia sana fursa kiasi cha kuzidi uwezo wa Halmashauri kusaidia miradi yote ya jamii. Matokeo yake kumejitokeza miradi ambayo haijakamilika kwa muda wake. Pia kumekuwa na ongezeko la gharama za vikao vya baraza kutokana na ongezeko la siku moja kwa kila Mkutano wa Baraza.

**10.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Ili kukabiliana na matatizo yaliyoambatana na mfumo Katanga, Halmashauri iliandikisha miradi yote ambayo haikuwa imekamilika. Kipaumbele kikawa ni kumaliza miradi yote kabla ya kuanzisha mipya. Halmashauri inajaribu kuongeza bajeti ya vikao vya baraza kutoka kwenye mapato yake ya ndani. Ili kuendeleza maboresho, Halmashauri imekuwa ikihamasisha uanzishaji wa miradi ambayo inabuniwa na jamii na kutekelezwa na jamii kutumia raslimali asilia. Katika msingi huu jamii huendelea na utekelezaji wa miradi hata kama Halmashauri itachelewa kuchangia. Hii pia husaidia jamii kutokuchoka kushiriki. Halmashauri imekuwa pia ikitumia mafundi wenyeji kama mafundi bomba na waashi kwa ile miradi ambayo haihitaji wakandarasi.

**11.0 SIRI ZA MAFANIKIO NA MASUALA YA KUJIFUNZA**

Mafanikio yaliyotajwa humu yanatokana na kufanya kazi kama timu, utashi wa kisiasa kuhusu maendeleo na uongozi wenye kipaji na kujitoa. Hayati Mwenyekiti Luteni Kanali Jacob Likoperi Kulemba na Mkurugenzi Mtendaji Hussein Katanga walikuwa viongozi wenye mrengo wa maendeleo. Waliweka nguvu nyingi katika kujenga daraja kati ya Madiwani, Watendaji na wananchi. Kutoka kwa Watendaji Kata waliohojiwa, Mkurugenzi aliyekuwepo Bw. Hussein Katanga alikuwa imara, kiongozi mbunifu, afuataye sheria na taratibu na anayechukua nafasi ya "Mmaliza Maumivu" kwa matatizo ya Halmashauri. Alikuwa mzuri katika kukasimu na kutia motisha watumishi wote kuwa wawajibikaji. Kupitia utaratibu wa kukasimu madaraka alianzisha mfumo thabiti wa walezi wa Kata. Haitoshi kuwa na mlezi wa Kata bali pia ana ufanisi gani na maono gani kuhusu Kata.

Nguvu ya kiuchumi inayotokana na mapato ya kahawa huchangia kiasi kikubwa kwenye shughuli za maendeleo. Wakulima wa Mbinga wamepigania mabadiliko ya sera juu ya uzalishaji wa kahawa, mazingira jamii na ya kawaida huku wakitumia vizuri uzoefu wanaoupata kutoka kwenye soko huria jipya.Tatizo la soko huria ni udhibiti wa ubora. Wakati kahawa inapungua sehemu nyingine za Tanzania, kahawa ya Mbinga inaendelea kutamba na sababu kubwa ni

udhibiti wa ubora. Kuna mfumo wa udhibiti wa ubora kuanzia sehemu za uzalishaji hadi kwenye hatua za kuongeza thamani. Matokeo yake ni kuwa kahawa ya Mbinga ni ya aina ya pekee. Kupitia ushuru wa mazao, Halmashauri imeweza kujenga barabara za lami km 4.15 kutoka kwenye mapato ya ndani.

Halmashauri inamiliki na kutunza vizuri mitambo ya kuboresha miundombinu. Hiki ni kipengele moja wapo ambacho Halmashauri nyingine zinaweza kuiga. Kuwa na seti ya mitambo ina ufanisi katika kuboresha barabara za Vijijini na Jamii, ingawa utunzaji na matengenezo ni kikwazo kikubwa. Kwa sababu ya uwajibikaji wa hali ya juu Halmashauri ya Mbinga imefanikiwa katika hili.

Wakazi wa Mbinga ni wa pekee kitabia. Kupitia mipango ya kusaidiana wanatimiza miradi ya maendeleo kwa wakati. Katika miongo miwili iliyopita ya uchumi huria wakulima wameachana na mfumo hodhi wa Serikali, wamekuwa wakijitegemea kiuchumi na wameboresha mfumo mzima wa uchumi Vijijini. Pia jamii imekubali kushiriki kwenye shughuli za maendeleo.

Watu wa Mbinga wanatabia ya kurithisha kwa kizazi kingine uzalishaji wa kahawa na stadi za kilimo cha “ngoro” cha Wamatengo (pit cultivation skills). Katika aina hii ya elimu jamii, mtoto wa kimatengo hupewa kipande cha ardhi katika umri mdogo. Watoto hushiriki katika shughuli za kiuchumi katika umri mdogo na wanapokuwa watu wazima inawawia rahisi kukabiliana cha changamoto za maendeleo. Pia Wamatengo ni wavumbuzi ambao wako tayari kujaribu mawazo mapya ya maendeleo. Kwa mfano kila kaya inajitahidi kupata maji ya bomba kwa kutumia ujuzi wao huku wakitumia fursa ya miteremko mikali, maji yanashuka yenyewe kufuata mgandamizo wa ardhi “gravity”na hivyo gharama kuwa ndogo. Kila kaya imetengeneza njia ya kuhakikisha magari yanaweza kufika kwa urahisi na kukimbizwa hospitali na mazao kupelekwa sokoni kwa usafiri wa uhakika kuliko kubebwa kwa kichwa hasa na wanawake. Kila kitongoji kina mashine binafsi za kusaga nafaka ambazo zinapunguza mzigo wa kazi kwa watoto wa kike na akina mama. Kila Kitongoji kina walau pikipiki 10 ambazo zinatoa huduma ya usafiri kwa wakazi. Haya ni mambo ya pekee ikilinganishwa na sehemu nyingine za Vijijini hapa Tanzania.

Halmashauri ya Mbinga ina vituo viwili vya Kata vya kujifunzia ambapo jamii zinaweza kupata stadi, taarifa na teknologia. Baadhi ya teknologia zilizopo ni kilimo cha Maksai, trekta za mikono (power tillers), utunzaji wa nyuki, ufugaji wa ng’ombe chotara pamoja na matumizi ya mbegu bora. Ni rahisi kutawala wanajamii wenye uelewa kuliko wasio na uelewa. Zaidi ya hayo, Halmashauri ya Mbinga inatumia utaalam, ujuzi na stadi za asili zilizopo. Hutumia mafundi mchundo waliopo kwenye shughuli za ujenzi na maofisa waliostaafu kwenye masuala mbalimbali ya Maendeleo ya Jamii. Maendeleo ya Jamii hutokea ndani ya jamii husika hivyo Halmashauri lazima zitumie rasilimali zilizopo kwenye jamii.


Mfuko endelevu (revolving fund) wa Mbinga ni mbinu sahihi ya kuhakikisha watumishi wanapata usafiri kwa mikopo ya gharama nafuu. Mfuko huu unaweza pia kutumika kwenye kutoa mikopo kwa watumishi wa Serikali kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za kuishi. Mtumishi

akishapata mkopo, licha ya kuhamasika, analazimika kubakia ndani ya Halmashauri mpaka atakapomaliza mkopo; na hivyo, ni mbinu ya kubakiza watumishi. Mfuko huu endelevu huhitaji menejimenti thabiti na nidhamu ya fedha. Kwa mfano, hairuhusiwi kutumia fedha za mfuko kwa matumizi ambayo hayakudhamiriwa kwa sababu hukatisha tamaa wanaosubiri zamu ya kupata mkopo.

Kutokana na uwazi uliopo katika modeli ya Katanga, kumekuwa na ushiriki wa kweli na wa kujitoa wa jamii katika miradi ya maendeleo. Watu wako tayari kuchangia kwa hali na mali kwa sababu wanaona jinsi rasilimali zao zinavyotumika. Hii inatokana na matumizi sahihi ya mbinu za uhamasishaji jamii zinazotumiwa na viongozi wa kuchaguliwa na wa kuteuliwa.

# HAMSHAURI YA WILAYA YA MPANDA

## UBORESHAJI WA MIUNDOMBINU KWA AJILI YA KUVUTIA NA KUBAKIZA WATUMISHI




*OFISI MPYA YA KATA YA NSIMBO – MPANDA*

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda ipo katika Mkoa mpya wa Katavi. Halmashauri hii ni kati ya Halmashauri za zamani sana nchini Tanzania kwa sababu ilianzishwa mwaka 1947 na utawalawa kikoloni wa Kiingereza. Halmashauri ina eneo la Km za Mraba 47,527 na ipo kwenye usawa wa bahari kuanzia 1000m hadi 2500m, latitudo 5’15” Kusini na 7’03” Kaskazini pamoja na Longitude 3 mpaka 31 Mashariki. Inapakana na Mkoa wa Rukwa na nchi ya DRC kwa upande wa Magharibi. Pia Halmashauri hii inapakana na Wilaya ya Nkasi kwa upande wa Kusini-Mashariki, Wilaya ya Chunya kwa upande wa Mashariki na Wilaya za Urambo na Sikonge kwa upande wa Kaskazini.

Halmashauri hii ina Tarafa nane ambazo ni Nsimbo, Inyonga, Mpimbwe, Mamba, Karema, Mwese, Kabungu na Ndurumo. Halmashauri ina jumla ya Kata 33, Vijiji 119 na Vitongoji 553. Kutokana na sensa ya mwaka 2002 Halmashauri ilikuwa na watu 412,683 kati ya 202,466 ni Wanaume na 210,217 ni Wanawake. Ongezeko la wastani la watu kwa mwaka linakadiriwa kuwa ni 3.6. Mapato ya ndani kwa ujumla kwa mwaka 2011/2012 yalikuwa Sh. 1,876,432,000. Katika hali ya kawaida shughuli za kiuchumi katika Halmashauri hii hutegemea zaidi kilimo cha Tumbaku kama zao kuu la biashara, uzalishaji wa mahindi, ufugaji wa nyuki na ufugaji wa ng’ombe. Pia shughuli za uvuvi kwenye ziwa Tanganyika na shughuli za utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Katavi. Shughuli zote hizi huchangia kwenye mapato ya ndani ya Halmashauri.




Ramani ya Mpanda – Chanzo: Mpanda DC 2011

## 2.0 TATIZO LILILOKUWEPO KABLA YA UBORESHAJI WA MIUNDOMBINU

Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda kama zilivyo Halmashauri nyingine Tanzania ni kubwa kwa eneo na makazi yametawanyika mno. Tabia za kijiografia za Wilaya hii ni ngumu kwani kuna mabonde, tambarare za savana, vilima na milima. Kufikika kwa baadhi ya Kata na Vijiji ni vigumu kutokana na miundombinu, misitu mizito na wanyama pori. Barabara za vijijini hupitika wakati wa kiangazi tu. Baadhi ya Vijiji vimetenganishwa na misitu kwa zaidi ya km 50 kukuta Kijiji kingine. Hii hufanya utoaji wa huduma na usimamizi wake kuwa mgumu sana. Jedwali 2.4 linaonyesha umbali toka Makao Makuu ya Wilaya kwenda kwenye baadhi ya Kata.

**Jedwali 2.4: Umbali toka Kata-Mpanda**

| Makao Makuu ya Kata | Umbali kutoka Mpanda Town |
|---|---|
| Usevya | Km 125 |
| Mamba | Km 145 |
| Inyonga | Km 120 |
| Ilunde | Km 170 |
| Mwese | Km 118 |
| Karema | Km 120 |
| Nsimbo | Km 20 |
| Mishamo | Km 160 |
| Ugala | Km 70 |

**Chanzo: Mpanda DC 2011**

Jukumu kuu la Halmashauri ya Wilaya ni kutoa huduma katika sekta zote. Wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda hupambana na matatizo mengi ikiwemo uhaba wa maji na makazi duni. Kusafiri kwenda Makao Makuu ya Wilaya ni gharama mno na ni hatari. Kata na Vijiji hivi pia havikuwavutia watumishi wa Halmashauri kama Maafisa Watendaji, Walimu na Maafisa Kilimo kuishi maeneo haya kutokana na ukosefu wa huduma muhimu kama maji na nyumba. Hii ilipelekea kuporomoka kwa huduma Vijijini na kuongezeka kwa umaskini.

## 3.0 LENGO

Mwaka 1996 Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda ilibuni mpango wa kuboresha utoaji wa huduma katika Kata na Vijiji vyote. Kwenye warsha ya “Post Osaka” ya Mkoa wa Rukwa iliyofanyika mwaka 2006, Sumbawanga Mjini, Halmashauri iliingiza kipengele kwenye mpango kazi kilichosomeka “kuboresha mazingira ya kazi kwa kujenga ofisi na kuhakikisha ni safi na yana vifaa.” Azimio hili baadaye liliboreshwa na kuwa lengo mahsusi la kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa ngazi za chini hasa Watendaji wa Kata. Lengo la pili la Halmashauri likawa kuwavutia watanzania kufanya kazi Halmashauri ya Mpanda na kuwabakiza wale ambao wamepangiwa Halmashauri ya Mpanda kwa kuwajengea nyumba na ofisi, kuwapatia usafiri na kuwawekea mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Ni vyema kukumbuka kuwa maeneo magumu ya Mpanda yalipelekea Watendaji wa Kata na Vijiji, Walimu na watumishi wengine kukataa kuishi na kufanya kazi Mpanda.

## 4.0 MKAKATI WA KUVUTIA NA KUBAKIZA WATUMISHI

**Uboreshaji wa ofisi na makazi**

Kufikia lengo la kubakiza watumishi katika maeneo magumu, Halmashauri ilianza kujenga ofisi za Kata za kisasa katika kata zote za pembezoni. Ofisi hizi zilijengwa zikiwa na Ofisi ya Mtendaji, ukumbi wa mikutano, Ofisi ya Diwani na chumba cha Maafisa Ugani. Ofisi hizi zilitiwa samani na vifaa vingine. Halmashauri pia ilijenga nyumba za kisasa kwa ajili ya Maafisa Watendaji wa Kata ili kuwafanya waishi kwa furaha na familia zao na kuwatia motisha wa kutoa huduma bila kikomo. Haya yamepelekea nidhamu bora kazini, matumizi bora ya muda wa ofisi, kupungua kwa gharama za kupanga nyumba na ubora unaonekana katika utoaji huduma.



OFISI YA KATA YA KAREMA



NYUMBA YA MTENDAJI KATA - KAREMA

### Usafiri

Halmashauri ilinunua pikipiki ambazo walipewa Maafisa Watendaji wa Kata ili waweze kuhudumia wananchi wanaozunguka makao makuu ya Kata bila kuchelewa. Usafiri ni mojawapo ya motisha bora kwa watumishi wa Tanzania. Usafiri pia huboresha hadhi ya mtumishi. Maafisa Watendaji wa Kata wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda wana motisha wa juu kabisa na mwitiko wao kwa mahitaji ya wananchi umeongezeka sana kutokana na kupewa pikipiki na Halmashauri.

### Huduma za Mikopo kwa Watumishi

Watumishi katika Halmashauri ya Mpanda wana chama cha ushirika (SACCOS) ambacho huwasaidia kuweka akiba na kupata mikopo midogo ambayo hutumika kuanzisha biashara ndogondogo na za kati kujiongezea kipato juu ya mishahara yake. Mikopo hii midogo pia hutolewa kwa mahitaji mengine kama ada za shule, samani za nyumba na matukio mengine ya kijamii. Ili kuwezesha watumishi wengi kupata mikopo hii na kuhakikisha SACCOS hii ina fedha mwaka mzima, Halmashauri huchangia kiasi cha fedha. Mkakati huu huwatia motisha watumishi kwani wana uhakika wa kupata mikopo.

### Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Halmashauri pia ilianzisha na kuboresha kituo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ambacho hutumiwa na watumishi kupata taarifa za ulimwengu juu ya maendeleo katika utoaji huduma, na kupata fursa ya kuweza kuwasiliana na Halmashauri na taasisi nyingine. Kituo hiki kimewahakikishia watumishi kupatikana kwa taarifa na haki ya kuwasiliana na ulimwengu wa nje.

**Dawati la Malalamiko**
Ili kujiridhisha kuwa Halmashauri inapata taarifa kwa wakati za mahitaji na matatizo ya wananchi, Halmashauri ilianzisha dawati la malalamiko katika kila Kata ambalo husaidia kufuatilia matatizo yanayowakabili watumishi na wananchi. Dawati hili pia husaidia kutoa mrejesho wa haraka kwa Halmashauri kuhusu huduma zinazotolewa na miradi inayotekelezwa na ubora wa utendaji wa watumishi katika kata na Halmashauri kwa ujumla.

**Vifaa vya Ofisi**
Halmashauri hutenga fungu la bajeti la kutosha kwa ajili ya manunuzi ya vifaa vya ofisi na vitendea kazi. Hii ina lengo la kuhakikisha kuwa ofisi za Kata na Vijiji hazipati upungufu wa karatasi, kalamu na mafaili ili kupelekea utendaji bora na ufanisi. Matokeo ya utaratibu huu yameonekana katika utendaji bora wa watumishi.

**Mafunzo**
Mwisho, Halmashauri hutenga fungu katika bajeti kila mwaka kwa ajili ya mafunzo na uendelezaji wa watumishi. Baadhi ya watumishi hupewa fursa ya kuhudhuria mafunzo mafupi juu ya mambo mapya katika taaluma zao, wakati watumishi wa kada za chini hupewa fursa ya kujiunga na elimu ya juu na Halmashauri huwasaidia kwa kuwalipia ada na gharama zingine za chuoni.

**5.0 RASLIMALI ZA UTEKELEZAJI**

Mkakati wa kuvutia na kubakiza watumishi katika Halmashauri si jambo rahisi. Halmashauri nyingi nchini Tanzania zimejaribu kuwapa motisha watumishi ili wabakie katika Halmashauri husika bila mafanikio, kutokana na kukosekana kwa dhamira ya dhati na mipango duni ya raslimali zinazohitajika. Katika kutekeleza mkakati wa kubakiza watumishi katika Halmashauri, Wilaya ya Mpanda ilitumia raslimali zifuatazo;

(i) Ujenzi wa Nyumba 9 za Maafisa Watendaji wa Kata na nyumba 2 za Wakuu wa Idara kwa sh. 205,000,000/= mwaka 2010/2011.
(ii) Mwaka 2011/2012 Halmashauri ilitenga sh. 120,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Maafisa Watendaji wa Kata.
(iii) Mwaka 2012/2013 Halmashauri ilitenga sh. 170,000,000/= kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa nyumba za Watendaji wa Kata katika kata zilizosalia.
(iv) Ujenzi wa ofisi za Kata pia uligharimu fedha zifuatazo sh. 300,000,000/= mwaka 2010/20122, sh. 40,000,000/= mwaka 2011/2012 na sh 300,000,000/= mwaka 2012/2013.
(v) Pamoja na fedha hizi, kila mwaka wananchi katika kata zao walichangia kiasi cha 20% ya gharama zote za ujenzi kwa kufyatua matofali, kukusanya mawe na mchanga na kushiriki kwenye ujenzi.
(vi) Ununuzi wa vyombo vya usafiri hasa pikipiki na mitumbwi ulitumia fedha zifuatanzo; sh. 74,000,000/= kuwa ununuzi wa mitumbwi na sh. 40,000,000/= kwa ununuzi wa pikipiki mwaka 2010/2011, sh. 40,000,000/= kwa ununuzi wa pikipiki mwaka 2011/2012 na sh. 40,000,000/= kwa ununuzi wa pikipiki mwaka 2012/2013.

(vii) Uboreshaji wa kituo cha Technolojia ya Habari na Mawasiliano uliigharimu Halmashauri sh. 2,500,000/= kwa kila chapisho la jarida la "Mpanda leo". Halmashauri pia hutumia sh. 1,000,000/= kila mwezi kwa kuunganishwa na mtandao (internet) kutoka TTCL.

(viii) Tangu 2010/2011 Halmashauri husaidia chama cha akiba na mikopo (SACCOS) cha watumishi kwa kuchangia sh. 30,000,500/= kila mwaka.

## 6.0 MAFANIKIO

Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda imefanikiwa sana katika mkakati wake wa kubakiza watumishi na kuwapa motisha. Siyo rahisi kusimulia mafanikio yote, lakini ukitembelea Kata za Halmashauri hii kila kitu kiko wazi. Mpaka kufika mwezi Mei 2012 Halmashauri ilikuwa imeshajenga ofisi za Kata na nyumba za watumishi katika Kata 25 kati ya Kata 33. Ofisi na nyumba hizi zinazoonekana katika picha hapa chini zimeboresha utendaji wa Maafisa Watendaji wa Kata, ufanisi wa kuendesha mikutano na ukaaji ofisini kwa muda mrefu kutatua matatizo ya wananchi.

Maafisa Watendaji wa Kata na famila zao wanafuraha na heshima kutokana na kuishi kwenye nyumba za kisasa katika maeneo ya Vijijini. Hapa chini Afisa mtendaji wa kata ya Nsimbo anathibitisha kuhusu maboresho yaliyofanyika katika mazingiraya kazi na ubora wa maisha.

*"….naweza kukwambia….. nilikuwa naishi kwenye nyumba ya nyasi na nilitakiwa kulipa kila mwezi… watoto na mke wangu walikuwa na matatizo ya kila aina kutokana na wadudu na hasa msimu wa mvua ambapo nyumba ilikuwa inavuja na kufanya magodoro kulowa… lakini sasa tunafuraha…. halmashauri na wananchi wamefanya kazi nzuri sana…. kujenga ofisi na nyumba ya kuishi ni motisha… mke wangu na watoto wanafuraha pia… napenda kuishi kwenye kata hii… naweza kuishi milele hapa…. ofisi ina nafasi ya kutosha tunafanyia mikutano….. pia ina chumba cha mahabusu.*



OFISI YA KATA YA KABUNGU




*PIKIPIKI ZA WATUMISHI*

Kupitia mpango endelevu wa kuwapatia watumishi usafiri Halmashauri imeweza kuwa na magari 32 mitumbwi 2 inayotumika kufanya doria katika mipaka ya Ziwa Tanganyika, pikipiki 90 na baiskeli 68. Halmashauri iligawa pikipiki na baiskeli kwa vigezo vya umiliki kwa Maafisa Watendaji wa Kata. (kuchangia gharama na au kuwakopesha watumishi na madiwani). Jedwali 2.5 linaonyesha watumishi na madiwani waliopata pikipiki na baiskeli kwa njia ya mikopo.

**Jedwali 2.5: Mgawanyo wa Pikipiki na Baiskeli**

| Mtumishi | Aina ya Usafiri | Idadi |
|---|---|---|
| Madiwani | pikipiki | 40 |
| Maafisa watendaji wa kata | Pikipiki | 30 |
| Maafisa watendaji wa vijiji | Baiskeli | 68 |
| Maafisa Ugani | Pikipiki | 8 |
| Karani wa Braza | Pikipiki | 1 |
| Maofisa wa maendelo ya jamii | Pikipiki | 3 |
| Afisa Utumishi | Pikipiki | 1 |
| Maafisa Mipango | Pikipiki | 2 |
| Whasibu | Pikipiki | 3 |
| Maafisa Ununuzi | Pikipiki | 2 |

**Chanzo: Mpanda DC 2011**

Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda ina kituo cha Technolojia ya Habari na Mawasiliano kinachofanya kazi vizuri. Kituo hiki pia hutumika kama maktaba kwani kuna vitabu, magazeti na majarida ambapo watumishi hushauriwa kwenda mara kawa mara kujijengea uwezo. Kupitia tovuti ya Halmashauri www.mpanda.go.tz, kituo hiki pamoja na watumishi wanaweza kwa urahisi kabisa kupata taarifa za ndani, za kitaifa na kimataifa kuhusu kilimo, kuongeza thamani mazao ya kilimo na mambo mengine ya maendeleo. Pamoja na kituo hiki cha Technolojia ya Habari na Mawasiliano, Halmashauri imezindua jarida liitwalo ***"Mpanda leo"*** ambalo limeongeza usambazaji wa habari za Halmashauri kwenda kwenye jamii, wadau mbalimbali na Tanzania kwa ujumla kuhusu maliasili za Mpanda, vivutio vya utalii na shughuli mbalimbali za maendeleo na mafanikio yake.

Watumishi katika Halmashauri ya Mpanda wana ari ya juu ikilinganishwa na miaka ya nyuma kabla ya mpango huu. Ongezeko la nyumba za Maafisa Watendaji, watumishi wa Afya, Walimu na maafisa ugani wengine ni sababu moja kubwa ya ongezeko la ari. Sababu nyingine za ongezeko la ari na dhamira ya utendaji ni pamoja na kuwepo kwa usafiri kwa ajili ya watumishi na Madiwani kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali 2.6, mpango wa Halmashauri wa kuchangia kila mwaka chama cha ushirika cha kuweka na kukopa (SACCOS) cha Walimu, watumishi wa Afya na wa Utawala na kuwaruhusu watumishi kuishi kwenye nyumba za Halmashauri bila malipo ya pango.

**Jedwali 2.6: Idadi ya SACCOS**

| SACCOS | IDADI YA WANACHAMA |
|---|---|
| SACCOS YA WALIMU | 215 |
| SACCOS YA WATUMISHI WA AFYA | 155 |
| SACCOS YA HALMASHAURI YA MPANDA | 94 |
| JUMLA | 464 |

**Chanzo: Mpanda DC 2011**

Kukubali kwa watumishi kubakia Mpanda, kuishi na kufanya kazi kumeongezeka sana. Hii imetokana na uboreshaji wa miundo mbinu, ujenzi wa nyumba, utoaji wa usafiri na utawala na uongozi unaomjali binadamu (utu). Mfano mzuri wa uongozi unaojali binadamu ni utoaji wa mikopo kwa waajiriwa wapya ili waweze kuanza maisha kwa kununua vitu vya msingi vya kuanzia maisha. Angalia jedwali 2.7.

**Table 2.7: Takwimu za Watumishi Kubakia Kazini**

| Kesi | 2009/10 | 2010/11 | 2011/12 |
|---|---|---|---|
| Watumishi walioondoka Mpanda | 36 | 21 | 8 |
| Watumishi walioingia Mpanda | 7 | 12 | 21 |
| Watumishi waliojiuzulu | 14 | 9 | 4 |

**Chanzo: Mpanda DC 2011**

Kuanzishwa kwa Dawati la Maoni (malalamiko) Desemba 14 mwaka 2009 lenye watumishi watano wa kada mbalimbali limesaidia sana Halmashauri kujua kwa wakati mahitaji na matatizo ya wananchi Vijijini na kuyamaliza . Watumishi wa dawati hili hutakiwa kutembelea Kata na Vijiji na kukusanya maoni na malalamiko yanayohitaji kushughulikiwa na kutoa majibu ya haraka. Maoni na Malalamiko yote yaliyokusanywa hufikishwa kwenye Timu ya Menejimeti ya Wilaya na kufanyiwa kazi. Hii imepelekea kuwepo kwa mahusiano mazuri kati ya Halmashauri na wakazi wa Halmashauri ya Mpanda. Wajumbe wa dawati la malalamiko wanaonyeshwa kwenye jedwali 2.8 hapa chini.

**Jedwali 2.8: Wajumbe wa Dawati la Malalamiko**

| JINA | CHEO | IDARA | NAFASI KATIKA DAWATI |
|---|---|---|---|
| **Patrick Mwakyusa** | Mwanasheria | Kitengo cha Sheria | Mratibu |
| **Samson Medola** | Afisa Utumishi | Utawala na Utumishi | Mwenyekiti wa Dawati |
| **Onesmo Gadau** | Mchumi | Mipango | Katibu wa Dawati |
| **Marcus Nazi** | Afisa Elimu – Elimu ya Ufundi | Elimu | Mjumbe |
| **Oscar Mkende** | Afisa Maendelo ya Jamii | Afya | Mjumbe |

**Chanzo: Mpanda DC 2011**

**7.0 CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI**

Kwa ujumla Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda imefanikiwa kuwatia motisha na kuwafanya watumishi kubakia Mpanda tangu mwaka 2009 kutokana na dhamira thabiti ya kuboresha mazingira ya kazi katika Kata, shule, zahanati na sekta zingine. Hata hivyo mafanikio haya yalikumbana na matatizo mengi moja likiwa upungufu wa fedha. Lengo la Halmashauri lilikuwa kuhakikisha mpaka mwaka 2012 kila mtumishi ana nyumba na ofisi bora lakini fedha hazikutosha kufikisha lengo hili kikamilifu.

Pili, juhudi zote za kuwafanya watumishi kupenda na kuishi mpanda na hasa vijijini hazikutegemea tu raslimali kutokea makao makuu ya Halmashauri, bali michango ya jamii nayo ilikuwa muhimu. Kwa bahati mbaya katika baadhi ya Kata na Vijiji michango ya wananchi kwenye ujenzi wa nyumba za watumishi na ofisi haikuwa ya kutosha na hivyo kupunguza kasi ya kuwatia motisha watumishi kubaki na kuishi mpanda. Halmashauri pia imekumbana na malalamiko mengi kutoka kwa jamii na watumishi ambayo hayawezi kumalizwa kwa urahisi. Baadhi yanahitaji mipango mikakati na mbinu za muda mrefu.

Mwisho, ni kukiri kuwa kujiografia ya Halmashauri ya Mpanda ni kubwa mno, inayochanganya na ngumu. Hili limeongeza ugumu katika utekelezaji na usimamizi wa miradi ikiwa ni pamoja na mradi huu wa kuboresha mazingira ya kazi ili watumishi waipende Mpanda.

**8.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Halmashauri ya Mpanda imetumia mikakati mbalimbali kukabiliana na matatizo katika mpango huu. Kupambana na tatizo la upungufu wa fedha, Halmashauri iliwashirikisha wadau wa maendeleo kuchangia fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi na ofisi katika Kata. Kwa mfano ofisi ya Kata ya Ugala na nyumba ya Afisa Mtendaji ilijengwa kupitia mpango wa MASITO – UGALA uliofadhiliwa na Taasisi ya Jane Goodall.

Katika kushawishi ushiriki wa jamii kwenye ujenzi wa nyumba na ofisi, Halmashauri iliendesha kampeni kadhaa za uhamasishaji ili kuongeza utambuzi kwa jamii na umuhimu wa ushiriki katika jitihada za Halmashauri. Pia dawati la malalamiko na mfumo wa mlezi wa Kata vyote viliimarisha ushiriki wa jamii na usimamizi wa miradi katika ngazi ya Kata.

Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda pia imejiwekea mikakati kadhaa ili kujihakikishia uendelevu wa mazingira mazuri ya kufanyia kazi hii ni pamoja na;

(i) Kutenga fungu kwenye bajeti kila mwaka kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi na ofisi katika Kata na Vijiji. Kwa mfano kwenye bajeti ya 2012/2013 sh. 190,000,000/= zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa ofisi za Kata na Vijiji, sh. 160,000,000/= kwa ajili ya ujenzi nyumba za Wakuu wa Idara na Tshs. 20,000,000/= kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za watumishi. Halmashauri inadhamiria kutoa usafiri kwa watumishi wake, na kwa mwaka 2012/2013 imetenga kwenye bajeti Tshs. 40,000,000/= kwa ajili ya ununuzi wa pikipiki zitakazokopeshwa kwa watumishi.

(ii) Kuendelea kuwapa motisha watumishi na kuwafanya wabakie Mpanda. Halmashauri ina mpango wa kuongeza uwezo wa chama cha kuweka na kukopa (SACCOS) ili chama kiweze kuwakopesha watumishi mikopo ya riba nafuu ikilinganishwa na ya benki na taasisi nyingine za mikopo midogo. Kwa kuanzia, mwaka 2012/2013 Halmashauri imetenga kwenye bajeti sh. 30,000,000/= kuchangia vyama vitatu vya wafanyakazi (SACCOS).

(iii) Halmashauri imedhamiria kujenga uwezo wa watumishi wote kupitia mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa kutumia mapato ya ndani.

(iv) Mwisho, Halmashauri imedhamiria pia kujaza nafasi zote za watumishi zilizo wazi kila mwaka hasa kwenye sekta za kilimo, afya na elimu, kuboresha mawasiliano vijijini kwa kushirikisha na makampuni ya simu za mkononi na kujenga nyumba za walimu katika shule zote za Sekondari za Kata.

**9.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Alipoteuliwa (Eng. Kalobelo) kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda, Halmashauri ilikuwa na udhaifu mwingi wa uendeshaji. Kwa mfano watumishi wengi hawakuwa wakifanya kazi kwa jitihada zote, baadhi walizoea kupoteza muda wa masaa ya kazi; wakiambiwa waendelee na kazi baada ya muda wa kazi au siku za mwisho wa wiki walizoea kulalamika kuwa wanalazimishwa kufanya kazi bila malipo ya ziada. Kazi zilikuwa zikifanywa na watumishi wachache ambao walizidiwa na majukumu ilihali wengine hawakuwa na kazi za kufanya kabisa. Kwa ujumla utendaji katika Halmashauri ya Mpanda ulikuwa wa kawaida sana usiokuwa na mabadiliko chanya wala umoja.

Katika mazingira haya Eng. Kalobelo aliweka malengo yafuatayo;

- Kila mtumishi afanye kazi kwa uwezo wake wote.
- Kila mtumishi aonyeshe Upeombele (proactive) katika kazi yake, na sio ukawaida tu.
- Kila mtumishi aitawale nafasi yake vizuri, kwa mgawanyo wa haki wa kazi, kuwepo na kusaidiana.
- Kujenga umoja kama timu kati ya Halmashauri na katika kila Idara.
- Kuelewa ukweli kuhusu wananchi katika Halmashauri na kubuni miradi na shughuli ambazo zinakidhi mahitaji ya wananchi kiuhalisia.

Mkurugenzi alitumia mbinu mbalimbali kuzikabili changamoto alizozikuta ili kufikia malengo haya. Mbinu hizi ni pamoja na;

- Kuanzisha Daftari kwa kila Afisa. Kila Afisa alilazimishwa kuandika muda alioingia ofisini, kazi alizofanya, na muda aliotoka. Hii ilionyesha kiasi cha utendaji. Baada ya kuanzisha utaratibu huu, watumishi waliona aibu ya kudai malipo ya muda wa ziada, kwani daftari lilionyesha utendaji halisi na hawakuhitaji kulipwa zaidi.
- Pia utaratibu huu uliwafanya watumishi kutambua jinsi walivyokuwa wakifanya kazi (au kutokufanya kazi) na wakaanza kubadilika kimtazamo. Wakaanza kuwa makini kwenye kazi zao na matumizi ya muda.
- Mkuruguenzi pia alianzisha mfumo wa kazi ambapo kila idara ilitakiwa kutengeneza mpango kazi ambao unaonyesha muda wa utekelezaji na ofisi husika. Wakuu wa Idara walielekezwa kugawa majukumu kwa kila Afisa katika idara kwa haki na usawa. Hii ililenga ugawaji sawa wa majukumu kwa kila mtumishi na kuongeza umoja na ushirikiano kati ya watumishi (Majukumu hayakuachwa kwa Afisa husika tu). Mkuu wa Idara aliachiwa jukumu la kubuni njia nzuri zaidi za utekelezaji na utendaji hata kama Afisa husika si mtendaji mzuri.

Mkurugenzi pia alianzisha mahusiano sahihi na wanasiasa ambao ndio wafanya maamuzi katika Halmashauri. Hili lilifanyika kupitia mikutano ambako madiwani walikumbushwa mara kwa

mara kuhusu mahusiano bora na ya kitaalamu, yenye tija kwa maendeleo ya Halmashauri, Kata na Vijiji.

Kuanzishwa kwa Dawati la Malalamiko katika Halmashauri ambapo wananchi wa Mpanda hupitishia madai, mahitaji na malalamiko ilisaidia sana Halmashauri kujua kwa ufanisi shida za watumishi na kuzitatua. Pamoja na utaratibu wa Mlezi wa Kata anayefanya kazi kwa karibu na watumishi wa Kata, ugunduzi wa matatizo, upatikanaji wa raslimali na utekelezaji wa miradi ulirahisishwa sana. Uwazi katika matumizi ya raslimali, kupitia taarifa shirikishi katika manunuzi ya bidhaa, malipo ya mafundi na gharama nyingine ilisaidia jamii kushiriki kikamilifu kwenye miradi ya ujenzi bila migomo baridi. Lengo kuu la kuvutia na kubakiza watumishi katika Halmashauri ya Mpanda likawa limefikiwa na kuimarika.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE


## KUVUTIA NA KUBAKIZA WATUMISHI KWA KUBORESHA MAZINGIRA YA KAZI NA MAKAZI



*UKUMBI WA HALMASHAURI NA OFISI ZILIZOKARABATIWA*

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe ni moja wapo ya Halmashauri za Mkoa wa Mwanza ambayo ni kisiwa kimoja kikubwa, Nansio, na visiwa vingine vidogo 38 katika Ziwa Viktoria. Kati ya visiwa 38, 15 vina makazi ya kudumu na vilivyobaki 23 hutumiwa kwa muda na wavuvi. Halmashauri ina Tarafa 4 za Mumbuga, Munlambo, Ilangala na Ukara, Kata 24 na Vijiji 73. Kutokana na sensa ya mwaka 2002 Halmashauri ina jumla ya wakazi 260,831, kati ya hao, 128,842 ni wanaume na 131,989 ni wanawake.




**Chanzo: Ukerewe DC, 2011**

## 2.0 TATIZO LILILOKUWEPO KABLA YA KUBORESHA MAZINGIRA YA KAZI NA MAKAZI

Tangu Kuanzishwa toka enzi za ukoloni Halmashauri ya Ukerewe imekuwa ikikumbwa na matatizo mengi yaliyopelekea watumishi wanaopangwa na serikali kufanya kazi Ukerewe kutofika kabisa, Kujiuzulu au kuomba uhamisho kwenda sehemu zingine za Mkoa wa Mwanza au Tanzania. Mapungufu yaliyokuwepo hadi mwaka 2006 yalikuwa haya yafuatayo:-

(i) Majengo ya ofisi yaliyochakaa sana na upungufu mkubwa wa nafasi za ofisi kwa watumishi hasa katika Makao Makuu ya Halmashauri. Kwa mfano jengo kuu la Halmashauri ambalo lilijengwa mwaka 1957 lilikuwa halijawahi kufanyiwa matengenezo

kabla ya mwaka 2007. Majengo mengine kama yale ya Idara za Maji, Ujenzi, Ardhi na Maliasili yalikuwa yametawanyika karibu mji mzima wa Nansio kwa kipenyo cha takribani kilometa moja na yalionekana machakavu sana kiasi cha kuwatisha watumishi kuyatumia.



**Hali halisi ya Jengo la Makao Makuu ya Halmashauri lililojengwa toka mwaka 1957 likiwa na paa la Asbestos kabla ya kukarabatiwa mwaka 2007.**

(ii) Nyumba za watumishi pia zilikuwa tatizo kuu katika kuwabakiza watumishi. Mkurugenzi, Wakuu wa Idara na watumishi wengine walikuwa wakipanga nyumba mbaya na zisizo tunzwa vizuri katika mji mdogo wa Nansio. Hali hii ilitishia uwepo wa afya bora kwa familia za watumishi. Watendaji wa Kata na Vijiji na wataalamu wengine huko vijijini hawakuwa na nyumba za kuishi na waliishi na familia zao katika mazingira ya kimaskini sana.

(iii) Jiografia ya kisiwa cha Nansio ambako ndio Makao Makuu ya Halmashauri ni ngumu kwa kufika na usafiri. Utoaji wa huduma na usimamizi wa miradi kwenye visiwa 38 vilivyotawanyika ni mgumu pia. Watumishi pia hawakupenda kuishi na kufanya kazi kwenye visiwa hivi ambavyo vilikuwa vinafikika kwa ngalawa ndogo, kitu ambacho kilikuwa ni hatari sana kwa maisha ya watumishi kwani Ziwa mara nyingi lina upepo mkali, mvua nyingi na mawimbi makubwa.

(iv) Sehemu kubwa ya visiwa vyenye makazi ya watu hakukuwa na huduma bora za jamii kama maji salama, huduma za afya na ulinzi na usalama (Polisi). Kwa waajiriwa wapya huduma hizi ni muhimu kwa ujumla. Ukosefu uliokithiri wa huduma za jamii ulichangia sana watumishi kujiuzulu na wengine kuomba kuhama Halmashauri ya Ukerewe.

(v) Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe ina visiwa vidogo 38 vilivyotawanyika hovyo na vilikuwa vikishambuliwa sana na uvamizi, wizi na ujambazi. Jamii hizi za visiwa pamoja na watumishi walikuwa wakivamiwa ovyo na majambazi na vibaka na kulazimishwa kukabidhi mali zao. Kuzuia hali hii ilikuwa vigumu kutokana na hali ngumu ya Ziwa na upungufu wa vifaa vya Halmashauri vya kufanyia doria, hasa mitumbwi iendeyo kasi.

(vi) Mtazamo hasi wa watanzania kuhusu Ukerewe unaotokana na imani kuwa jamii za Ukerewe huendekeza na kutenda uchawi na kwamba ni rahisi sana kwa wageni kuuawa kwa uchawi wa Mamba. Imani hii ilitia hofu kwa watumishi wapya waliopangwa kazi Halmashauri ya Ukerewe.

Kwa ujumla, matatizo yaliyotajwa hapo juu yalifanya Halmashauri kuwa na upungufu mkubwa wa watumishi kwani takribani asilimia 20 ya watumishi wote waliopangwa kufanya kazi Ukerewe hawakuwa wanafika kabisa, wakati asilimia 40 ya wale wanaofika na kuajiriwa waliomba uhamisho au waliachana kabisa na Utumishi wa Serikali za Mitaa. Sekta ambazo ziliathirika sana na upungufu huu wa watumishi ni Afya, Elimu ya msingi na Sekondari na Mipango.

**3.0 LENGO LA PROGRAMU**

Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe iligundua ongezeko la watumishi kuondoka na kupungua kwa ari ya kufanyakazi na kupelekea utoaji duni wa huduma kwa jamii ya Ukerewe. Mwaka 2007 katika Warsha ya Post Osaka ya Mkoa wa Mwanza, Halmashauri ilijiwekea lengo la kuboresha motisha kwa wafanyakazi kupitia maboresho ya mazingira ya kazi na makazi. Lengo hili baadaye lilifanywa mahsusi ili kuhakikisha kuwa 90% ya watumishi wanaopangwa kazi Ukerewe wanabakia Ukerewe na wanawezeshwa kufikia utendaji ulio bora ifikapo Juni 2012.

**4.0 SHUGHULI ZA UTEKELEZAJI**

Dhamira ya Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe ya kuwatia motisha watumishi waliopo na wapya ilitekelezwa kwa shughuli zilizoelezewa hapa chini.

(i) Kukusanya takwimu sahihi za watumishi wanaoondoka (kuacha kazi) Ukerewe na kuandaa Andiko la mradi kwa ajili ya maombi maalum ya bajeti toka Serikali Kuu na washirika wa maendeleo.

(ii) Kuandaa hoja za uhakika za kulishawishi Baraza la Madiwani kuweka kipaumbele kwenye suala la motisha kwa wafanyakazi na mpango wa kuwabakiza watumishi Ukerewe kwa kuboresha ofisi na makazi.

(iii) Kubuni na kutekeleza mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa mapato na mbinu za kujenga uwezo wa kifedha ili kutekeleza mpango wa kubakiza watumishi kwa kutumia mapato ya ndani na kupunguza utegemezi kutoka Serikali Kuu na wafadhili.

(iv) Kukarabati na kupanua jengo kuu la Halmashauri ili kuwa na ukumbi wa kisasa, ofisi zenye nafasi na samani bora na kumbi za wageni kwa kila kitengo.

(v) Ujenzi wa nyumba 14 za wakuu wa idara na nyumba moja ya kupumzikia wageni kwa gharama za chini zikitumia raslimali asilia kama matofali ya kuchoma na wajenzi wenyeji. Pia Halmashauri ilijenga ofisi na nyumba mpya kwa ajili ya watumishi ngazi za Kata na Vijiji.

(vi) Ununuzi wa vitendea kazi vya kisasa kama vile kompyuta, printa, mashine ya kudurufu na samani za ofisi. Halmashauri pia ilinunua gari la Mkurugenzi ambaye alikuwa akitumia gari bovu lililozeeka.

(vii) Ununuzi wa mitumbwi mitatu ya kisasa na iendayo kasi kwa ajili ya kukusanya mapato toka visiwa 38 vilivyotawanyika na kufanya doria ziwani kupambana na uvamizi, ujambazi na unyang'anyi kwa jamii za visiwa.

(viii) Kuwapatia dhamana za mikopo watumishi wa Halmashauri na Madiwani waliohitaji kuwa na usafiri binafsi. Watumishi na Madiwani kadhaa walinunua magari kwa kutumia mikopo toka benki ya NMB.

(ix) Malipo ya deni la LAPF ambalo lililolimbikizwa toka mwaka 2006 hadi kufikia Tshs. 329,882,449.40. Deni hilo lilitishia haki za watumishi wakati wa kustaafu na hivyo kupunguza motisha.

(x) Ukarabati wa Hospitali ya Wilaya na uwekekaji wa samani na vifaa vya hospitali vilivyo bora. Uboreshaji wa hospitali ulijumuisha ujenzi wa nyumba 3 za watumishi, chumba cha kuhifadhia maiti, na ukarabati wa jengo la "Mama Ngojea" uliofadhiliwa na Rotary Club – ya Uingereza.

(xi) Halmashauri iliwezesha ujenzi wa Vituo vya Polisi na majengo ya Mahakama ya Mwanzo katika kisiwa cha Irugwa lengo likiwa kuboresha hali ya amani, usalama na huduma za utoaji haki ndani ya Halmashauri ili kuongeza motisha kwa watumishi wataalam kubaki katika Halmashauri ya Ukerewe.

## 5.0 RASILIMALI ZILIZOTUMIKA

Jitihada za kufanya watumishi wasiondoke au kuhama siyo rahisi. Licha ya raslimali fedha, Halmashauri ilitumia zaidi raslimali watu kwenye ubunifu, uongozi bora, subira na dhamira. Jedwali 2.9 linaonyesha uhalisia wa raslimali fedha zilizotumika kwenye jitihada ya kuvutia na kubakiza watumishi katika Halmashauri ya Ukerewe.

## 6.0 MAFANIKIO NA MATOKEO

Katika kutekeleza mradi, lengo la kuvutia na kubakiza watumishi lilifikiwa kupitia shughuli na raslimali zilizotumika kama ilivyoonyeshwa kwenye sehemu 4 na 5 ya kesi hii. Haya yote yamepelekea mafanikio yafuatayo ambayo yamejadiliwa hapa chini:-





*Nyumba 14 za wakuu wa Idara*

*Nyumba ya Mkurugenzi*


**Mapato ya Halmashauri,** yamekuwa yakiongezeka toka mwaka 2007. Ongezeka hili limwezesha Halmashauri kuwa na mazingira mazuri ya ofisi na makazi ya watumishi kutoka 65% mwaka 2007 hadi 85% mwaka 2011. Ongezeko la mapato pia limejenga uwezo wa Halmashauri kuweza kutoa mikopo ya mishahara kwa waajiriwa wapya ili kuwabakiza Ukerewe kipindi ambapo mishahara yao bado inashughulikiwa. Ongezeko la mapato lenyewe ni matokeo ya uboreshaji wa motisha kwa watumishi kuifanyia kazi Halmashauri. Hili limewezesha ulipaji wa Posho mbalimbali za Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji na watumishi wengine bila kuchelewa na kupelekea kuongezeka kwa motisha na dhamira katika kazi.

**Ukarabati na upanuaji wa jengo kuu la Halmashauri** (angalia picha kwenye kichwa cha habari ) pamoja na uwekaji wa vifaa na samani za kisasa za ofisi vimeongeza ari ya watumishhi wa Makao Makuu ya Halmashauri na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji mapato, utatuzi wa matatizo, ufanyaji wa maamuzi na mawasiliano na wahitaji wa huduma. Ukumbi ulioboreshwa umewavutia wananchi kutembelea Makao Makuu ya Halmashauri hasa wakati wa vikao vya Baraza la Madiwani na kusikiliza majadiliano na maamuzi, kuongezeka kwa uelewa na elimu jamii unaonekana Ukerewe ni matokeo ya ziada ya mpango wa motisha kwa watumishi.

**Nyumba 14 za Wakuu wa Idara** zilizojengwa kuzunguka jengo kuu la Halmashauri ni mojawapo ya mafanikio makuu. Wakuu wa Idara sasa wanaishi kwa furaha na familia zao kwenye nyumba za kisasa na umbali ulio chini ya mita 500 kutoka Ofisi Kuu. Wakuu wa Idara sasa wanaweza kuitwa kwa haraka na kuweza kutatua matatizo ya Halmashauri hata siku za mwisho wa wiki. Mradi wa ujenzi wa nyumba hizi umeondoa matatizo yote ya kuchelewa kazini, uzembe na maombi ya ruhusa kushughulikia matatizo ya familia.

**Uwepo wa nyumba ya wageni** (picha chini) imechangia sana kuwapa motisha watumishi na kubakia Ukerewe. Waajiriwa wapya huwekwa kwenye nyumba hii na kuishi kwa starehe mpaka wanapopelekwa kwenye vituo vyao vya kazi. Nyumba hii ya mapumziko hutumiwa na Halmashauri kuwahifadhi wageni mbalimbali kitendo ambacho hupunguza gharama ambazo zingetumika kuwapangishia hoteli au nyumba za kulala wageni.





*Nyumba ya Wageni Ukerewe* *Ofisi yenye Samani na Vifaa vyote*

Halmashauri imefanikiwa kuwa na mazingira mazuri ya kufanyia kazi kwa watumishi wote wa makao makuu kwa sababu ofisi zote zina vifaa na samani za kisasa. Maofisa wote wanaweza kutumia kompyuta, printa, mashine za kudurufu na makabati ya kisasa. Ofisa mmoja alisema ***"tulizoea kunyang'anyana kompyuta mbaya, karatasi…. hata nafasi za kukaa…. sasa hivi tuna kompyuta katika kila dawati, printa katika kila chumba tunaandika barua na kuzichapa haraka…. hapa hapa ofisini"***

Jitihada ya Halmashauri kudhamini mikopo ya watumishi kutoka benki ya NMB imepelekea matumizi bora ya muda kwa Madiwani wa Maafisa.






***Gari la Mtumishi*** ***Pikipiki ya Mtumishi***

Magari, pikipiki na baiskeli zimerahisisha mwendo toka eneo moja hadi jingine kuliko zamani. Matokeo ya usafiri mzuri ni utoaji wa huduma bora na fanisi wa Halmashauri ambayo imepelekea jamii kuridhika na kushiriki zaidi katika shughuli za maendeleo. Jitihada na shughuli zote hizi mwishoni zimesababisha kuongezeka kwa kiwango cha kubakiza watumishi toka 60% mwaka 2006 hadi 85% mwaka 2012. Kwa maneno mengine matatizo ya watumishi kuacha kuwasili ukerewe, kujiuzulu na maombi ya kuhamia Halmashauri nyingine yamemalizwa kwa kiasi kikubwa.

## 7.0 CHANGAMOTO NA SULUHISHO

Changamoto kubwa ambayo Halmashauri ilikumbana nayo ni ukosefu wa makandarasi waliofuzu na kusajiliwa. Kisiwa cha Ukerewe ni kidogo na kimejitenga hivyo kina hali ngumu ya kusafirisha mitambo mikubwa ya ujenzi kutoka bandari ya Mwanza na kusababisha upungufu wa huduma za ujenzi. Kukabiliana na changamoto hii na kuendelea na miradi ya ujenzi Halmashauri ilitumia wakandarasi na wajenzi wenyeji katika Vijiji. Utaratibu huu ulipunguza gharama za ujenzi na kukuza uwezo wa wajenzi wenyeji. Pili Halmashauri iliamua kununua mashine za kutengeneza matofali (hydroform machine) ambazo ni bora na rahisi kutumia kwa ujenzi wa ofisi na nyumba za watumishi.

Ili kujihakikishia kuwa juhudi za Timu ya Menejimenti ya Halmashauri haipingwi na Madiwani na Jamii, Halmashauri huwasilisha mapendekezo ya miradi kwenye kamati za kudumu ambako hujadiliwa na kueleweka kwa wajumbe kabla ya kufikishwa kwenye Baraza la Madiwani, Baraza la Wafanyakazi na Kamati ya Ushauri ya Wilaya.

## 8.0 MIKAKATI YA UENDELEVU

Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe imelenga kuondoa tatizo la watumishi kuikwepa Ukerewe kwa 100% kupitia mpango huu wa kuwapa motisha watumishi. Mikakati iliyowekwa ili kujihakikishia uendelevu wa kubakiza watumishi ni kama ifuatavyo;-

(i) Kuwashauri watumishi kutumia kituo cha Technolojia ya Habari na Mawasiliano kwa ajili ya kukuza taaluma zao na kujijengea stadi za kutumia kompyuta, tovuti na maktaba.
(ii) Kujenga jengo ambalo zitakuwemo idara za ujenzi, maji na kilimo ambazo kwa sasa zipo kwenye jengo chakavu.
(iii) Kukamilisha ujenzi wa ofisi na nyumba za watumishi katika Kata na Vijiji
(iv) Kuboresha huduma za afya katika kisiwa cha Ukara kwa kujenga jengo la upasuaji
(v) Kujenga bweni kwa ajili wauguzi katika Hospitali ya Wilaya
(vi) Kuunganisha umeme kwenye nyumba zote za watumishi hadi ngazi ya Kijiji
(vii) Kufunga vifaa vya kuvuna maji katika nyumba zote za watumishi hadi ngazi ya Kijiji
(viii) Kuendelea kuwawekea dhamana watumishi ili wapate mikopo.

## 9.0 SIRI ZA MAFANIKIO

Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe ni mojawapo ya Halmashauri nyingi Tanzania zenye fursa na changamoto zinazofanana. Kwa Halmashauri ya Ukerewe kuweza kupunguza tatizo la watumishi kuacha kazi ni mafanikio ambayo Halmashauri nyingi zimeshindwa kufikia. Swali moja kubwa ni sababu zipi za msingi zilizopelekea ushindi huu? Majadiliano na Mkurugenzi na Wakuu wa Idara yalionyesha siri moja kuu; yaani Menejimenti Shirikishi. Menejimenti Shirikishi katika Halmashauri ya Ukerewe inajidhihirisha katika mbinu zifuatazo;

(i) Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya Dr. Leonard Mosses Massale alifikiri sana kwa kina juu ya namna ya kuboresha mazingira ya kazi na ya kuishi katika Halmashauri ya Ukerewe.

Ikawa dhahiri kuwa kupata fedha kwa kutumia njia za kawaida za mahusiano ya kifedha kati ya Halmashauri na Serikali Kuu haingetosheleza haja ya kuwa na watumishi wenye motisha na dhamira ya ndani kwa muda mfupi. Mkurugenzi na Timu yake waliamua kuandaa andiko la mradi na kulinadi Wizara ya Fedha. Wizara ilikubali kulipia mradi wa ukarabati na ujenzi wa nyumba za watumishi. Siri kubwa ya kufanikiwa ni kuishawishi Wizara kusaidia mradi na hasa kwa hatua zilizofuatia; ni ule mpango wa Mkurugenzi wa Halmashauri kuwaalika watumishi wa Wizara kutembelea Halmashauri. Mkurugenzi aliwaalika maafisa wa Wizara ya Fedha kufika Ukerewe na kujionea maboresho yaliyofanyika kupitia fedha za Wizara. Thamani ya fedha kwenye mradi huu ilikuwa wazi kabisa, maafisa wa Wizara waliridhika na jitihada za Mkurugenzi na kusababisha Wizara kuendelea kulipia ukarabati na ujenzi wa nyumba za watumishi sio tu Makao Makuu ya Halmashauri bali pia Hospitali ya Wilaya.

(ii) Mikutano mifupi kila siku asubuhi ya Mkurugenzi na Wakuu wa Idara kuhusu utendaji wa kila siku wa shughuli na matukio ya kila siku ya kila Afisa.

(iii) Mkutano wa mwezi wa kamati ya Kata ya wataalamu inayowashirkisha Watendaji wa Kata na Vijiji pamoja na Maafisa Ugani. Mkutano huu hujadili na kuazimia juu ya utendaji wa sekta mbalimbali na wa mtumishi mmoja mmoja.

(iv) Mikutano ya robo mwaka ya Tarafa ambayo wajumbe wake ni Maafisa Ugani wote na Watendaji wa Kata na Vijiji kwenye Tarafa husika. Mkutano huu una msingi wake katika kuhamashisha jitihada za maendeleo ya jamii.

(v) Ukaguzi wa kila robo mwaka wa utekelezaji wa miradi unaofanywa na kamati ya ukaguzi ya Halmashauri. Shughuli hii hufanywa ili kuboresha majadiliano ya kamati za kudumu za Halmashauri.

(vi) Kuanzisha kwa Timu ya uboreshaji na ukusanyaji mapato ambayo hukutana na wadau wa mapato pamoja na walipa kodi ili kushughulikia changamoto za ukusanyaji mapato.

(vii) Mikutano kuandaliwa kati ya mawakala wa kukusanya mapato na Kamati ya Fedha ya Halmashauri ili kuboresha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

(viii) Jukumu la Halmashauri za Vijiji kujadili na kuamua kuhusu mapato yanayokusanywa katika ngazi za Vijiji linatekelezwa kikamilifu.

(ix) Wakuu wa Idara waliochaguliwa na kupewa nafasi ya kuwa Mlezi wa Kata, majukumu yao ni kuhamasisha jamii katika Kata kuanzisha miradi ya maendeleo na kufuatilia shughuli zote zinazohusiana na utekelezaji wa miradi katika Kata na Vijiji.

**Jedwali 2.9: Fedha zilizotumika kuboresha ofisi na ujenzi wa nyumba za watumishi**

| Mradi | 2006 | | 2012 | | Chanzo cha Fedha |
|---|---|---|---|---|---|
| | *Number* | *costs* | *Number* | *Costs* | |
| Ukarabati wa jingo kuuu la halmashauri | 1 | 0 | 1 | 276,000,000 | Serikali Kuu |
| Kupanua jingo la makao makuu | 0 | 0 | 1 | 453,000,000 | Serikali Kuu |
| Ujenzi wa nyumba za wakuu wa idara | 0 | 0 | 14 | 490,000,000 | Serikali Kuu |
| Ujenzi wa nyumba ya wageni | 0 | 0 | 1 | 95,000,000 | Serikali Kuu |
| Ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi | 0 | 0 | 1 | 167,000,000 | Serikali Kuu |
| Ujenzi wa nyumba za maafisa Tarafa | 0 | 0 | 4 | 140,000,000 | Mapato ya Ndani (CDG) |
| Ujenzi wa Ofisi za Kata | 0 | 0 | 5 | 120,000,000 | Mapato ya Ndani (CDG) |
| Kompyuta ndogo | 1 | 2,000,000 | 13 | 26,000,000 | Mapato ya Ndani (CDG) |
| Kompyuta za mezani | 4 | 6,400,000 | 16 | 256,000,000 | Mapato ya Ndani (CDG) |
| Printa | 3 | 1,200,000 | 11 | 4,950,000 | Mapato ya Ndani (CDG) |
| Ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya | 0 | 0 | 3 | 105,000,000 | MMAM |
| Ujenzi wa wadi ya wanawake | 0 | 0 | 2 | 199,000,00 | Mapato ya Ndani (CDG) |
| Ukarabati wa wadi | 0 | 0 | 1 | 33,000,000 | SIDA |
| Ujenzi wa idara ya meno | 0 | 0 | 1 | 59,000,000 | Mapato ya Ndani (CDG) |
| Ujenzi wa jingo la Utawala Hospitali | 0 | 0 | 1 | 141,000,000 | Mapato ya Ndani (CDG) |
| Ujenzi wa nyumba za watumishi wa zahanati | 0 | 0 | 4 | 100,000,000 | Serikali Kuu |
| Ujenzi wa nyumba za walimu | 0 | 0 | 43 | 602,000,000 | Serikali Kuu |
| Ujenzi wa mahakama ya mwanzo - Irugwa | 0 | 0 | 1 | 76,000,000 | Serikali Kuu |
| Ujenzi wa kituo cha polisi - Irugwa | 0 | 0 | 1 | 71,400,000 | Serikali Kuu |
| Ujenzi wa nyumba za polisi - Irugwa | 0 | 0 | 1 | 86,600,000 | Serikali Kuu |

**Chanzo: Halmashauri ya Ukerewe 2011**

# HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA

## KUTAFUTA, KUVUTIA NA KUBAKIZA WATUMISHI KWENYE HALMASHAURI ZENYE MAZINGIRA MAGUMU










*CHUNYA : Nyumba za Watumishi*

## 1.0 UTANGULIZI

Tanzania ina maeneo yenye mazingira magumu (korofi) ambayo huathirika kwa ukosefu wa watumishi. Kufanya kazi katika maeneo hayo magumu inahitaji uvumbuzi wa mameneja na waajiri kutafuta, kuvutia na kubakiza watumishi katika baadhi ya sekta za utoaji huduma. Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ni moja ya maeneo hayo yenye mazingira magumu ya kufanyia kazi na kubakiza watumishi wa umma. Afya, elimu na kilimo ni baadhi ya sekta ambazo zimeathirika sana kutokana na watumishi kukimbia maeneo haya. Makao Makuu ya Wilaya ya Chunya yako mbali sana na wakazi (wapokea huduma) waliotawanyika kwa uchache katika eneo lote Halmashauri.

Kuwasimamia watumishi katika maeneo yao imekuwa ni changamoto siku zote. Hata hivyo ni muhimu kutafuta na kuainisha utendaji wa watumishi kipindi chote cha mahusiano ya ajira. Watumishi ni raslimali, waajiri wote wanatakiwa kutafuta na kuajiri watumishi bora zaidi kutoka vyuoni. Kufuatilia mahudhurio, utendaji, malipo, ongezeko la utendaji, muda na uzalishaji wa mtumishi ni kitu muhimu kwa afya ya Halmashauri. Ufuatiliaji wa Mtumishi ni muhimu pia kwa maslahi ya mtumishi kwenye nyanja za ubora, usalama, ulinzi na kuridhika kwake ambavyo kwa ujumla huboresha kubakia kwake kazini.

Kuwatia motisha watumishi huelezewa kama ni mchakato ambao huanzisha, kuongeza na kuendeleza tabia zenye kufikia malengo. Motisha humaanisha hitaji, hamu, shida au msukumo ndani ya mtu kutaka kufanya kitu. Kutia motisha ni mchakato wa kuchochea watu kutenda ili kufikia malengo. Moja ya kazi muhimu za Menejimenti ni kutengeneza uhiari kati ya watumishi wa kufanya kazi kwa uwezo wao wote. Kwa hiyo nafasi ya kiongozi ni kuchochea hamu ya watumishi kufanya kazi zao. Utiaji motisha wa watumishi na utoaji wa zawadi huamsha motisha chanya. Hata hivyo kuna ongezeko la hoja kuwa watumishi wa umma hasa walimu, madaktari, wauguzi na watumishi wa ugani hapa Tanzania, kama ilivyo kwenye nchi zingine zinazoendelea wanaendelea kukosa motisha, na hii inajionesha kwenye kuporomoka kwa utendaji kazi na matokeo yake.

Kubakiza wafanyakazi (retention) ni ule uwezo wa taasisi kuwafanya watumishi wake wasiache kazi kwa sababu yoyote ile. Kubakiza wafanyazi kunaweza kuelezewa kwa hesabu rahisi. Kwa mfano ubakizaji wa watumishi wa 80% ina maana taasisi ilibaki na watumishi wake kwa 80% bila kuondoka kwa muda fulani. Hata hivyo, wengi huchukulia kubakiza watumishi inahusu juhudi zinazofanywa na mwajiri kujaribu kuwabakiza watumishi katika nguvukazi yao. Lengo la waajiri kwa kawaida ni kupunguza uachaji kazi wa watumishi na hivyo kupunguza gharama za mafunzo, ajira na upoteaji wa vipaji pamoja na elimu ya taasisi iliyopatikana kwa mda mrefu.

Katika maeneo yote hayo hapo juu, Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ni moja ya mifano mizuri tuliyo nayo hapa Tanzania kiasi cha TOA kuamua kuichukua kama mwakilishi wa mbinu bora katika kuboresha mazingira ya kazi, kuwavutia na kuwabakiza watumishi katika mazingira magumu na yaliyo pembezoni.

## 2.0 HISTORIA

Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ni moja wapo ya Halmashauri saba za Mkoa wa Mbeya na ina eneo la kilometa za mraba 29,219 (ambayo ni 46% ya eneo la Mkoa wa Mbeya). Kwa kutumia sensa ya mwaka 2002 Halmashauri ya Chunya ilikuwa na watu wapatao 206,615. Kwa sasa inakadiriwa kuna wakazi 273,236. Ikilinganishwa na Halmashauri nyingine za Mkoa wa Mbeya, Halmashauri ya Chunya ndiyo yenye wakazi wachache zaidi na mgandamizo wake wa idadi ya watu ni sita kwa kila kilometa ya mraba. Halmashauri ina majimbo mawili ya uchaguzi yaani Songwe na Lupa.

Halmashauri ina Tarafa 4, Kata 30, Vijiji vilivyoandikishwa 73 na Mji mdogo wa Makongolosi. Watumishi wamegawanywa katika kata 30 kulingana na taaluma zao. Halmashauri ina Shule za Msingi 108, Sekondari 30, Zahanati 38 na Maafisa ugani wa Kilimo na Maafisa wa Maliasili wapatao 26 ambao wanahudumia wananchi katika maeneo ya Vijijini. Ili kuweza kutoa huduma katika taasisi zote hizi ni muhimu kuwa na idadi ya kutosha ya wafanyakazi wenye motisha. Ramani hii hapa chini inaonyesha Makao Makuu ya Halmashauri ambayo yako mbali sana na wananchi wanaohitaji huduma za mamlaka hii.




**Mchoro 2.3 Ramani ya Wilaya ya Chunya**

N.B. Ramani hii inaonesha yalipo mako makuu ya Halmashauri katika kona ya Kusini Mashariki kabisa ikimaanisha kuna gharama kubwa za kutoa huduma kutoka kati kwenda Kata na Vijiji vya pembezoni

## 3.0 TATIZO LILILOKUWEPO KABLA YA JITIHADA ZA KUTAFUTA, KUVUTIA NA KUBAKIZA WATUMISHI

Iligundulika kuwa kwa miaka kumi iliyopita watumishi hawakuwa tayari kwenda na kufanyakazi katika Wilaya ya Chunya kwa sababu Wilaya ni kubwa mno, imesahaulika na mazingira yake ya kazi kwa wakati huo yalikuwa ya kukatisha tamaa. Pia watumishi waliojizatiti kwenda na kufanya kazi Chunya, walikaa kwa muda mfupi sana na kuondoka. Kwa mfano mwaka 2009 kati ya Maafisa Maendeleo ya Jamii 10 waliofika kwenye Halmashauri na kupangiwa vituo, sita walikata tamaa na baada ya muda mfupi kuondoka na kuwaacha wane tu. Mwaka huo huo Waalimu wote sita wa Sekondari walioajiriwa katika Sekondari ya Kapalala waliamua kuondoka baada ya miezi michache. Kwa kweli kulikuwa na changamoto nyingi zinazohusiana na mazingira ya kazi ya Halmashauri ya Chunya . Baadhi ya changamoto hizo ni;

(i) Ukosefu wa nyumba za watumishi hasa Vijijini.
(ii) Umbali mrefu kutoka makao makuu ya Halmashauri kwenda Vijijini na kutoka Kijiji kimoja hadi kingine.
(iii) Huduma za jamii zisizoridhisha katika vituo vya kazi (maeneo ya Vijijini).
(iv) Uhaba wa raslimali watu. Idadi hitajika ya watumishi ilikuwa 1,691 lakini waliokuwepo ni 1304 tu, hivyo kulikuwa na upungufu wa watumishi 386.
(v) Usafiri wa umma duni kutokana na barabara mbaya za Halmashauri na pia kutoka Chunya kwenda makao makuu ya Mkoa, Mbeya.

Box 2.3: Maelezo ya Bwana **Maurice Sapanjo – Mkurugenzi Mtendaji - Chunya**



"Kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya siyo kazi rahisi! Kuna changamoto nyingi sana katika Wilaya hii kwa sababu makazi yametawanyika (Vijiji) na wakazi wachache lakini waliotawanyika sana hata ndani ya Kijiji au Kata moja na kuna misitu minene na wanyama wengi wa porini ambao wanatishia usalama wa watumishi katika maeneo hayo. Katika Mazingira kama haya, gharama za uendeshaji ni kubwa mno kwa sababu eneo la pembezoni kabisa ni km 225 (Kijiji cha KambiKatoto) kutoka Makao Makuu ya Halmashauri na eneo la karibu ni km 24 tu (Kijiji cha Chalangwa). Halmashauri imeanzisha jitihada za kuwafanya watumishi walioko maeneo ya pembezoni wawe na furaha kwa kuwajengea nyumba na kuwapatia usafiri na wakati mwingine posho kwa watumishi wapya. Kuna haja ya Serikali Kuu kuliona hili na kuongeza fedha za matumizi ya kawaida kwa Halmashauri zote zenye mazingira kama ya Chunya.

## 4.0 MALENGO

Ili kukabiliana na changamoto hizo hapo juu Halmashauri ya Chunya ilidhamiria;

(i) Kutumia vyema stadi na elimu za watumishi kufikia malengo ya taasisi.

(ii) Kupunguza muda wa siku wa walizokuwa wakitumia watumishi kutoka maeneo yao ya Vijijini kuja Makao Makuu ya Halmashauri kuchukua mshahara kila mwezi.

(iii) Kuvutia na kubakiza watumishi wafanye kazi katika Halmashauri.

(iv) Kuhakikisha uwepo wa watumishi wa kutosha wenye stadi stahiki ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

### 5.0 MIKAKATI NA SHUGHULI ZA UTEKELEZAJI

**Mkakati wa kwanza** ulikuwa kuanisha idadi ya watumishi waliopo maeneo ya Vijijini mbali na Makao Makuu ya Halmashauri. Hii iliambatana na uainishaji wa umbali uliopo kati ya Makao Makuu ya Halmashauri na vituo mahsusi ambako watumishi wanafanyia kazi. Ilihali watumishi wengine hutembea nusu kilometa tu kwenda Makao Makuu ya Halmashauri, wengine husafiri kwa usafiri wa umma usio na uhakika kwa zaidi ya kilometa 225 kwenda kuchukua mishahara yao ya mwezi.

**Mkakati wa pili** ulikuwa kutoa usafiri na ulinzi kwa watumishi wanaoishi mbali na Makao Makuu ya Halmashauri kwenda kuchukua mishahara na kurudi. Mwanzoni, kila mwezi, gari la wagonjwa la kituo cha afya cha Mtanila lilitumika kusafirisha watumishi toka kata za Mtanila, Kambikatoto na Mafyeko kwenda kuchukua mishahara yao. Hata hivyo gari la wagonjwa siyo la kuchukulia mishahara. Wakati gari hili halipo, dharura za wagonjwa zilikuwa zinajitokeza.

**Mkakati wa tatu,** Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ilianzisha utaratibu wa kuwapa makazi, posho za kujilkimu na vyombo vya nyumbani watumishi wapya. Katika hili, Halmashauri ilikodi nyumba kwa ajili ya wahasibu sita na kuwapa magodoro na posho za kujikimu ili wasiondoke. Angalia jedwali namba 4.

**Mkakati wa nne** ulikuwa kutafuta watumishi wa afya kutoka vyuoni (Jedwali 5). Katika hili Mkuu wa Wilaya binafsi na Afisa Utumishi walitembelea Chuo cha Afya cha Sumbawanga kinachoandaa waganga wasaidizi na Chuo cha Wauguzi cha Namenyere Wilayani Nkasi kuwashawishi watumishi watarajiwa kufanya kazi katika Halmashauri ya Chunya.

**Mkakati wa tano** ulikuwa kutoa usafiri (pikipiki na baiskeli) kwa watumishi walioko vituoni (Jedwali 2 na 3). Ili kufanikisha mkakati huu mfuko maalum kwa ajili ya maeneo yaliyojitenga ulianzishwa (Serikali kuu). Pia wadau na programu mbalimbali zilialikwa kushiriki katika hili. Hii inajumuisha Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (SEDP), Programu ya Maendeleo ya Kilimo Wilaya (DADPS), Ruzuku ya Maendeleo (CDG), na Taasisi ya Maendeleo Chunya (CHUDET). Pamoja waliweza kujenga nyumba za watumishi 35 zilizogharimu shilingi Bilioni Moja. Angalia jedwali 2.10.

## 6.0 RASLIMALI ZILIZOTUMIKA

Takribani shs. 1,420,000/= zilitumika kwa ajili ya usafiri na ulinzi kwa mwezi, kwa watumishi wa maeneo yaliyojitenga kuwapeleka kuchukua mishahara kila mwezi, magari manne yanayotumia lita 2000 yalitumika katika njia nne, madereva wanne na polisi wanne pia walihusika na zoezi hili. Zoezi hili lilikuwa likichukua takribani siku mbili na watumishi wote wa pembezoni mwa Halmashauri walifurahi sana na kurudi salama kwenye vituo vyao vya kazi bila usmbufu mkubwa katika ratiba zao za kazi.

Raslimali nyingine ni pamoja na shilingi billion moja za kujenga nyumba za watumishi 35, manunuzi ya pikipiki 23 zenye thamani ya shs 12.5 million na baiskeli 15 zenye thamani ya shs 1,695,000/= kila moja kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali 2.12, 2.14. Takribani shs 826,000/= zilitumika kununulia vitanda, magodoro na chandarua. Pia kulikuwa na michango mbalimbali toka taasisi kadhaa.

## 7.0 MATOKEO YA JITIHADA HII

**Tukio kubwa kabisa kwa Halmashauri ya Chunya ni kuwa tatizo la kuondoka kwa wafanyakazi lilikwisha.** Badala yake watumishi wamevutiwa kufanya kazi kwenye Halmashauri hii. Wauguzi watano na Waganga sita wameajiriwa. Watumishi wa umma katika maeneo ya pembezoni mwa Halmashauri wameendelea kubaki kazini kutokana na motisha hizi na siyo mshahara. Ukweli kuwa Mkurugenzi anajali maslahi na usalama wao kwa kuwapa usafiri kwenda kuchukua mshahara imepelekea badiliko kubwa la kitabia.

**Utoaji wa huduma za Bweni** (vitanda, magodoro na vyandarua) kwa Shule za Sekondari umekuwa na faida kubwa kwa shule za bweni hasa kwa wasichana (Jedwali2.10). Wanafunzi wanaweza kujikita zaidi katika masomo yao kama wanalala vizuri na mwisho ni kufaulu mitihani yao. Bweni hili hapa chini hutumiwa na wanafunzi na wanafurahia. Halmashauri ilijenga Bweni hili ili kupunguza utoro uliokuwa unatokana na hofu ya wanyama pori. Kwa mfano nyumba mpya ya mtumishi (Angalia picha) ilijengwa kwa kutumia mfuko wa elimu (Chunya) ambako hupata michango kutoka kwa wakulima wa Tumbaku.



*Bweni katika Sekondari ya Lupa*

**Boksi 2.4: Dada Mary Chekwe, Mwalimu Sekondari ya Lupa, Chunya DC**




Dada Mary Chekwe ni mmoja wa Walimu wa shule ya Sekondari ya Lupa katika Halmashauri ya Chunya, ana Shahada ya Elimu; anafurahia kufanya kazi hapa na kuishi kwenye mojawapo ya nyumba za watumishi.

**Muda ambao ulikuwa ukitumika kwenda kufuata mishahara na kila mtumishi umepungua sana.** Muda sasa unapatikana kwa ajili ya utoaji huduma. Mahudhurio ya Walimu darasani

yameongezeka. Wagonjwa zaidi wanahudumiwa na Wauguzi na Waganga. Matokeo ni kuwa ufanisi na ubora wa kazi za watumishi umeongezeka ikilinganishwa na hapa mwanzo.

**Nyumba ya watumishi zimejengwa** ikimaanisha kuwa watumishi na familia zao wanaishi kwa furaha na wanaweza kujikita zaidi katika kazi na kuboresha utoaji wa huduma. Shughuli za ugani zimerahisishwa sana. Watao huduma sasa wanaweza kufika maeneo mengi zaidi kwa muda mfupi, na wanaweza kufika maeneo ya pembezoni ambako magari hayawezi kufika. Kwa taarifa zaidi angalia Jedwali 2.10.

**Boksi no 2.4: Patrick Mpemba ni Afisa Kilimo wa Kata ya Mafyeko**




Kata ya Mafyeko ipo Km 148 toka Makao Makuu ya Halmashauri. Patrick alipangwa kazi hapa toka mwaka 2009 kwa mara ya kwanza katika ajira yake. Anajihisi ana bahati kuliko Maafisa wenzake wengine kwa sababu Halmashauri ilimpatia pikipiki kuwezesha na kurahisisha kazi yake katika Kata kwa wananchi waliotawanyika sana kwenye Vijiji viwili.



*Nyumba ya Afisa Ugani yenye Kibanda cha kuku kwa ajili ya chakula bora*

**Jedwali No. 2.10: Jitihada Nyinginezo zilizofanywa na Halmashauri Kuboresha Maeneo yaliyojitenga**

| No | Jina la Mpokeaji/taasisi/kijiji /village | Vifaa | Km toka Makaomakuu | Kiasi | Chanzo cha Fedha |
|---|---|---|---|---|---|
| **1** | Kapalala shule ya Sekondari | 3 Vyandarua, | 152 | 30,000 | **Mkurugenzi Binafsi** |
| **2** | Kapalala shule ya Sekondari | 100 magodoro, | 152 | 1,700,000 | **Vyanzo vya ndani** |
| **3** | Isangawana shule ya Sekondari | 48 magodoro, | 113 | 816,000 | " |
| **4** | Totowe walimu wa sekondari | 3 magodoro, 3 vitanda | 131 | 600,000 | " |
| **5** | Namkukwe walimu wa sekondari | 4 magodoro, 4 vitanda | 171 | 800,000 | " |
| **6** | Kapalala walimu wa sekondari | 3 magrodoro, 3 vitanda | 152 | 600,000 | " |
| **7** | Chunya hospitali | 1 godoro, 1 kitanda, Fedha taslimu | | 412,000 | Matumizi Mengineyo - afya |
| 8 | Mbuyuni Kituo cha afya | 2 magodoro, 2 vitanda, Fedha taslim | 121 | 826,000 | Matumizi mengineyo - afya |

Chanzo: Chunya DC 2011

## 6. UTAFUTAJI WA WATUMISHI

Jedwali 2.11 linaonesha matokeo ya zoezi la kutafuta watumishi katika sekta ya Afya. Ingawa wanafunzi 15 wa Uuguzi na Uganga walikubali kufanya kazi Chunya baada ya ushawishi kufanywa na Mkuu wa Wilaya na Afisa Utumishi, mchakato wa ajira ulifanywa na Wizara ya Afya, kwa hiyo ilibidi Halmashauri ifanye ombi maalumu kwa Wizara na hata hivyo kati ya wahitimu 15 waliokubali kufanya kazi Chunya ni 11 tu walipelekwa Chunya na Wizara.

**Jedwali No. 2.11: Matokeo ya Utafutaji Watumishi (afya)**

| Kada | Idadi ya waliokubali | Idadi ya walioajiriwa |
|---|---|---|
| **Wauguzi na Wakunga** | 7 | **5** |
| **Waganga wasaidizi** | 8 | **6** |
| **Jumla** | **15** | **11** |

**Chanzo: Chunya DC 2011**

Siri ya mafanikio ya Halmashauri ya Chunya inajumuisha utashi wa kisiasa wa Madiwani ulioruhusu suala la kuvutia na kubakiza watumishi kuwa kipaumbele. Pia kuna dhamira ya dhati ya viongozi wa Halmashauri na Wilaya kuhusu suala hili.

## 7.0 CHANGAMOTO ZILIJITOKEZA WAKATI WA UTEKELEZAJI

Changamoto kuu ni miundombinu duni. Barabara zote kuu na ndogo ni mbovu hivyo ni vigumu kwa watoa huduma kufika katika baadhi ya Vijiji na Kata. Vijiji vingi vimetawanyika na hivyo gharama za uendeshaji ni kubwa. Pia kuna misitu minene yenye wanyama pori kati ya Vijiji na Kata ambayo huwazuia Maafisa Tarafa na Maafisa Ugani kusafiri kutoka Kata moja hadi nyingine au Kijiji kimoja hadi kingine. Mtiririko dhaifu wa raslimali fedha pia ni kikwazo kwa uendelevu wa zoezi la kutafuta watumishi vyuoni.



***Barabara mbaya kwenye msitu mnene hukwamisha utoaji wa huduma Chunya***

## 8.0 MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

Halmashauri ya Wilaya ya Chunya imeendelea na ukarabati wa barabara. Pia Halmashauri inaendelea kuomba fedha zaidi kutoka Serikali Kuu. Halmashauri inatarajia kuwapa magari Maafisa Tarafa wawili ili kuboresha utendaji wao hasa ikizingatiwa Jiografia ya Wilaya ya Chunya. Halmashauri inaendelea kuomba fedha kutoka Serikali Kuu ili kuweza kutoa vivutio kwa watumishi. Jitihada zaidi zinaandaliwa ili kuongeza uwepo wa watumishi wa Wilaya ya Chunya.

## 9.0 SIRI YA MAFANIKIO NA MIFANO YA KUIGWA

Katika kesi hii ya Chunya, mafanikio yametokana na sifa za uongozi (Mkurugenzi na Mwenyekiti) ambazo ni muhimu kwa maendeleo ya Chunya. Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri Bwana Maurice Sapanjo ana sifa binafsi zinazohitajika na kila kiongozi. Ni mtu mwenye vipaji, ujasiri, kujitoa na anayepania kuacha nyayo. Inahitaji watu wenye ujasiri na uvumbuzi kufanya maamuzi kama haya ya Chunya. Mkurugenzi aliwaita na kuwashirikisha wahusika wote kujenga hoja juu ya changamoto zinzoikabili Halmashauri kwa sababu alijua bila kushirikisha wadau ni vigumu kufikia malengo.

Ushiriki wa wadau ni kipengele kingine muhimu cha mafanikio ya Halmashauri ya Chunya. Bwana Sapanjo alikuwa mwalimu mzuri kwa Timu yake ya Menejimenti. Timu hiyo ilikuwa yenye nguvu katika utekelezaji wa maamuzi ya Halmashauri ya Chunya, walionesha stadi nzuri za ushawishi kuweza kuwashawishi Madiwani na kufanya maamuzi magumu yaliyolenga kuvutia watumishi na kuwabakiza ndani ya Halmashauri. Kati ya wadau muhimu, ni pamoja na Ushirika wa Wakulima wa Tumbaku na Mfuko wa Maendeleo Chunya.

Kipengele cha Tatu cha kuigwa ni mchakato wa kuweka Vipaumbele ulio bora. Katika Mchakato wao wa Mipango, Halmashauri ilitambua kuwa utafutaji wa Watumishi na Kuwapa motisha ilikuwa kipaumbele namba moja. Kwa hiyo raslimali zilitengwa kulingana na vipaumbele hivi.

**Kiambatisho Jedwali no. 2.12: Nyumba zilizojengwa,kiasi cha fedha na chanzo cha fedha**

| No | Jinala Kat/Kijiji | Idadi ya nyumba | Km toka makao Makuu | Gharama | Chanzo cha Fedha |
|---|---|---|---|---|---|
| **1** | Namkukwe Secondary School | 3 | 171 | 54,000,000 | **SEDP and Community** |
| **2** | Gua Village | 1 | 192 | 29,700,000 | **DADPS and Community** |
| **3** | Mafyeko Village | 1 | 160 | 29,700,000 | **DADPS and Community** |
| **4** | Lualaje Village | 2 | 128 | 59,400,000 | **DADPS and Community** |
| **5** | Kapalala Secondary School | 5 | 154 | 150,000,000 | **PEDP and Community(1)**<br>**CG* (1)**<br>**CDG (1)**<br>**Community (2)** |
| **6** | Mbangala Village | 1 | 80 | 30,000,000 | **CG* (1)** |
| **7** | Mwagala Secondary school | 3 | 120 | 81,000,000 | **Community** |
| **8** | Maweni Secondary school | 2 | 72 | 60,000,000 | **CG* (1)** |
| **9** | Makongolosi Township | 2 | 41 | 60,000,000 | **CDG (1)**<br>**CG* (1)** |
| **10** | Lupa Secondary School | 3 | 88 | 90,000,000 | **CHUDET** |
| **11** | Isangawana Secondary school | 3 | 113 | 90,000,000 | **Lake Rukwa project (2)**<br>**SEDP and Community (1)** |
| **12** | Chunya Town | 9 | 0 | 270,000,000 | **CG* (6)**<br>**CDG (3)** |
| Total | | 35 | | 1,003,800,000 | |

**Chanzo: Chunya DC 2011**

**CG* = Ruzuku maalumu kwa Halmashauri za pembezoni**

**Kiambatisho Jedwali No. 2.13: Idadi ya Pikipiki zilizogawanywa kwa Watumishi wa pembezoni**

| No | Jina la kata/kijiji | Cheo | **Idadi ya pikipiki** | Km toka makao makuu | gharama | Chanzo cha fedha |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **1** | Gua | Maafisa Ugani | 1 | 192 | 6,500,000 | **DADPS** |
| **2** | Ngwala | " | 1 | 189 | 6,500,000 | **DADPS** |
| **3** | Lualaje | " | 1 | 128 | 6,500,000 | **DADPS** |
| **4** | Sangambi | " | 1 | 30 | 6,500,000 | **DADPS** |
| **5** | Mbuyuni | " | 1 | 121 | 6,500,000 | **DADPS** |
| **6** | Matwiga | " | 1 | 121 | 5,000,000 | **DADPS** |
| **7** | Galula | " | 1 | 106 | 5,000,000 | **DADPS** |
| **8** | Chokaa | " | 1 | - | 5,000,000 | **DADPS** |
| **9** | Mkwajuni | " | 1 | 72 | 5,000,000 | **DADPS** |
| **10** | DALDO HQ | " | 1 | - | 5,000,000 | **DADPS** |
| **11** | Makongolosi | " | 1 | 41 | 5,000,000 | **VECO (Belgian Govt. support)** |
| **12** | Chalangwa | " | 1 | 24 | 5,000,000 | **VECO** |
| **13** | Kanga | " | 1 | 94 | 5,000,000 | **VECO** |
| **14** | Ifumbo | " | 1 | 114 | 5,000,000 | **VECO** |
| **15** | Mtanila | " | 1 | 103 | 5,000,000 | **VECO** |
| **16** | Makongolosi | Afisa Mtendaji kata | 1 | 41 | 5,000,000 | **VECO** |
| **17** | Chalangwa | " | 1 | 24 | 5,000,000 | **VECO** |
| **18** | Kanga | " | 1 | 94 | 5,000,000 | **VECO** |
| **19** | Ifumbo | " | 1 | 114 | 5,000,000 | **VECO** |
| **20** | Mtanila | " | 1 | 103 | 5,000,000 | **VECO** |
| **21** | Namkukwe | Mwalimu Mkuu | 1 | 171 | 5,000,000 | **Mapato ya ndani** |
| **22** | Ngwala | Mtendaji Kata | 1 | 189 | 5,000,000 | **Mapato ya ndani** |
| **23** | HQ | Afisa Ushirika | 1 | - | 5,000,000 | **VECO** |
| | TOTAL | | 23 | | 122,500,000 | |

**Chanzo: Chunya DC 2011**

**Kiambatisho Jedwali Table No. 2.14: Idadi ya Baiskeli zilizogawiwa vijijini**

| No | Kujiji | Walengwa | Idadi ya Baiskeli | Km toka Makao makuu | Gharama | Chanzo cha fedha |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **1** | Igagwe | Village Executive Officer | 1 | 99 | 113,000 | **Capacity Building Grant** |
| **2** | Kalangali | " | 1 | 93 | 113,000 | " |
| **3** | Lupa | " | 1 | 88 | 113,000 | " |
| **4** | Igundu | " | 1 | 18 | 113,000 | " |
| **5** | Sangambi | " | 1 | 30 | 113,000 | " |
| **6** | Isewe | " | 1 | 26 | 113,000 | " |
| **7** | Itindi | " | 1 | 112 | 113,000 | " |
| **8** | Ileya | " | 1 | 105 | 113,000 | " |
| **9** | Maleza | " | 1 | 84 | 113,000 | " |
| **10** | Mbala | " | 1 | 90 | 113,000 | " |
| **11** | Iseche | " | 1 | 82 | 113,000 | " |
| **12** | Patamela | " | 1 | 54 | 113,000 | " |
| **13** | Mbuyuni | " | 1 | 121 | 113,000 | " |
| **14** | Mpona | " | 1 | 155 | 113,000 | " |
| **15** | Namambo | " | 1 | 129 | 113,000 | " |
| Jumla | | | 15 | | 1,695,000 | |

**Chanzo: Chunya DC 2011**

# Sura ya Tatu: Ugatuajii wa Masuala ya Fedha na Uboreshaji wa Mapato

Ugatuaji wa Masuala ya Fedha humaanisha mamlaka ya kukusanya kodi na kutumia yanahamishwa toka ofisi za juu (Serikali kuu) kwenda ofisi za chini (Serikali za mitaa) kwa lengo la kutoa huduma za umma sahihi ili kuboresha ustawi wa wananchi. Wapo wanaoamini kuwa kuna uwiano unaotakiwa kati ya fedha za Serikali Kuu na fedha za Serikali za Mitaa, au kuwa Serikali za Mitaa zina nguvu ya kufanya maamuzi kwa ajili ya kuboresha masuala ya fedha. Ingawa kuna maoni mbalimbali kuhusu ugatuaji wa masuala ya fedha, kwa ujumla kiasi cha maamuzi kuhusu fedha na mamlaka iliyonayo Halmashauri, huongezeka kadri ugatuaji wa masuala fedha unavyoongezeka katika ngazi za chini. Mambo ya lazima katika ugatuaji wa masuala ya fedha ni Baraza la Madiwani, maafisa wakuu walioteliwa katika eneo husika, uwezo thabiti wa mapato ya Halmashauri, jukumu thabiti la matumizi ya Halmashauri, uhuru wa bajeti, uzingatiaji wa bajeti na uwazi. Mazingira yanayostahili ni pamoja na uhuru wa kutokuingiliwa na udhibiti wa Serikali Kuu, haki ya matumizi, fedha kutolewa bila masharti na uwezo kukopa.

Andiko la maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania (1998) linaonyesha kuwa ugatuaji wa masuala ya fedha maana yake ni kuzifanya Halmashauri ziwe na vyanzo vyao vya uhakika vya mapato, kuanzisha uhamishaji fanisi wa fedha toka Serikali Kuu, kuwepo kwa upatikanaji fanisi wa fedha za kutolea huduma zilizokasimishwa, kuboresha ongezeko la mapato, kuhakikisha uwepo wa uwazi na usawa katika mgawanyo wa fedha na kuhakikisha usawa katika utoaji wa huduma. Ugatuaji wa masuala ya fedha kwa Tanzania kimsingi unajumuisha ukweli ufuatao;

(i) Halmashauri hazitakiwi kukasimishwa wajibu wa majukumu ambayo hayatengewi fedha.
(ii) Mfumo wa ruzuku unatakiwa kuruhusu sera za kitaifa kutekelezwa kupitia Halmshauri ambazo zingelipiwa kupitia ruzuku zenye masharti na zinazozingatia viwango vya chini vya kitaifa.
(iii) Mfumo wa ruzuku unatakiwa kuzihamasisha Halmashauri kuamua vipaumbele vyao kwa kuanzisha ruzuku ya kawaida na ya maendeleo bila masharti.
(iv) Ruzuku ambazo hazina masharti lazima zitolewe kwa mtindo wa usawa ili kusaidia Halmashauri ambazo zina vyanzo dhaifu vya mapato.
(v) Ukokotoaji wa ruzuku lazima ufanyike kwa kufuata fomula yenye viwango vya kutegemewa, vya haki na visivyo na upendeleo
(vi) Ruzuku toka bajeti za Wizara za sekta zinatakiwa kuachwa kadri iwezekanavyo.

Uongezaji wa Mapato ya Ndani humaanisha matumizi ya uhuru uliotolewa na Serikali Kuu kwa Halmashauri kukusanya mapato na kutumia kulingana na vipaumbele vyao. Uongezaji wa

Mapato hujumuisha upanuaji wa wigo wa mapato, uhamasishaji shughuli za kiuchumi zinazoongeza vyanzo vya kodi na kutunga sheria ndogo za kuwezesha ukusanyaji na utumiaji wa mapato.

Katika sura hii Kesi mbili zimewasilishwa. Kesi ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani inahusu mfumo wa ukusanyaji mapato wa Digitali unaotumia kompyuta kuainisha Majengo, kupiga picha na kufanya tathmini ya haki na sawa ya thamani za majengo. Kesi ya Halmashauri ya Jiji la Mbeya inahusu jitihada za kijasiriamali za kuongeza mapato kupitia uwekezaji wa ndani. Kesi hii inaonyesha ujasiri na umakini unaotakiwa na Halmashauri kukopa fedha toka taasisi za fedha na kuziwekeza kwenye miradi inayolipa haraka. Ikizingatiwa kuwa mgawo wa fedha toka serikali kuu unaendelea kupungua na una masharti magumu, Halmashauri zinalazimika kuchangamka kutafuta mapato kutoka vyanzo vingine kama miradi ya kuongeza mapato. Uchambuzi wa kesi kwenye sura hii unaonyesha kuwa;

(i) Kodi ya majengo ni chanzo muhimu kwenye vyanzo vya ndani vya Halmashauri nyingi ambacho kinatumiwa chini ya uwezo wake. Sababu za kutumika chini ya uhalisia inajumuisha kutokutambuliwa kwa majengo, kutosajiliwa majengo, utunzaji hovyo wa takwimu, tathmini za thamani zisizo na haki, na kumbukumbu za thamani zilizopitwa na wakati. Ili kukabiliana na changamoto hizi mfumo huu wa Digitali unaweza kuwa msaada siyo tu katika kuongeza mapato bali pia kwa kupata takwimu muhimu kwa ajili ya kufanya maamuzi mengine.

(ii) Halmshauri ni taasisi zinazojiendesha zenyewe kisheria. Kwa mantiki hii na kwa kuzingatia upungufu wa raslimali toka Serikali Kuu, Halmashauri zinatakiwa kujiingiza kwenye uwekezaji mkubwa na shughuli za kijasiriamali zenye mwelekeo wa kuzalisha mapato ya kutosha. Halmashauri zinatakiwa kuwa na maamuzi na ubunifu wa kuingia kwenye mambo ya ardhi, uchimbaji madini, kuendesha shughuli za mafunzo na utalii. Ili kuweza kufanya hivi zinahitaji kuchukua hatua na kudiriki kukopa kutoka kwenye taasisi za fedha zilizopo kama Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB), benki ya uwekezaji, mfuko wa kijiji cha millennia, mfuko wa majiji wa millennia, Mpango wa mazingira wa Umoja wa Mataifa (UN Habitat) na nyingine nyingi.

(iii) Uendeshaji wa uwekezaji wa umma unahitaji umakini wa menejimenti, hivyo Halmashauri lazima zishirikiane na sekta binafsi kupitia mfumo wa ushirikiano kati ya taasisi za umma na binafsi yaani PPP.

# HALMASHAURI YA MANISPAAA YA MTWARA - MIKINDANI

## UBORESHAJI WA MAPATO KWA KUTUMIA MFUMO WA DIGITALI WA UPIMAJI ARDHI NA UTHAMINI WA MAJENGO




*MFANO WA NAMBA ZA UTAMBULISHO WA JENGO*

## 1.0 UTANGULIZI

Hapa Tanzania, sehemu kubwa ya vipande vya ardhi pamoja na majengo yaliyopo kwenye ardhi havijaainishwa na kusajiliwa. Kwa sababu majengo haya hayajaainishwa na kusajiliwa, haikuwa rahisi kukadiria kodi za kisheria kama kodi ya majengo. Hali hii inaleta ulazima wa kuainisha na kusajili kwa ujumla majengo yote. Kesi hii inaongelea uboreshaji wa mapato kupitia mfumo wa digitali wa upimaji Ardhi na Majengo (FCDS) katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara – Mikindani. Mfumo huu wa digitali hutumia kompyuta. Katika mfumo huu majengo yote ndani ya Halmashauri hupimwa, huainishwa na husajiliwa kwa njia za digitali na kodi stahiki za majengo hayo hukadiriwa kulingana na viwango vilivyopo kwenye soko. Kwa njia hii Halmashauri inatarajia kuongeza mapato kutokana na kodi ya majengo mara kumi. Hii ni kesi ya aina yake iliyochaguliwa na TOA kama mfano wa ugatuaji raslimali fedha hapa Tanzania. Kwa siku za karibuni Halmashauri hii imefanya maboresho dhahiri siyo tu kwenye ukusanyaji wa mapato bali pia katika matumizi fanisi ya fedha za umma. Kwa miaka miwili iliyopita mfululizo Halmashauri imepata hati safi katika hesabu zake kutoka kwa Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti wa Hesabu na Serikali. Ni Halmashauri ya kwanza kufanya utambuzi wa jumla wa majengo na ni mfano ambao unaweza ukaigwa mara kwa mara na Halmashauri zingine kwa marekebisho madogo tu.

Manispaa ya Mtwara-Mikindani ipo Mkoa wa Mtwara Kusini mwa Tanzania, imepakana na Msumbiji kwa Kusini, Mkoa wa Ruvuma kwa Magharibbi, Mkoa wa Lindi kwa Kaskazini na Bahari ya Hindi kwa Mashariki. Ndiyo Halmashauri ndogo kabisa kati ya Halmashauri sita za Mkoa wa Mtwara. Mtwara-Mikindani ina eneo la mjini lipatalo km 163 za mraba. Kiutawala Halmashauri hii ina Kata 13, na Vijiji viwili. Licha ya kuwa pembezoni mwa nchi na kuwa na uchumi mdogo Halmashauri hii imekuza uchumi kwa kiasi chake.

Mtwara-Mikindani, kama ilivyo katika maeneo mengine ya Tanzania ina uchumi unaotegemea Kilimo. Shughuli kuu ya kiuchumi ya wananchi ni kilimo. Karibu 92% ya wakazi hujishughulisha na kilimo pamoja na shughuli nyingine kama uvuvi, ufugaji nyuki, na viwanda vidogo vidogo. Katika siku za nyuma, ukanda wote wa Kusini na hasa Mtwara hakukuwa kunawavutia vijana wa kizazi kipya, hivyo waliondoka kwenda kutafuta maisha mazuri sehemu nyingine za Tanzania. Wimbi hili lilikuwa na madhara makubwa kwa maendeleo ya kichumi kwa Mtwara. Hata hivyo kuanzia mwaka 2005 kumekuwa na maboresho ya haraka ya barabara kutoka Mtwara kuelekea Kaskazini na Magharibi ambayo yameufungua Mkoa kwenye masoko ya nje. Matokeo yake ni kuwa makazi katika Halmashauri ya Mtwara-Mikindani yameongezeka kwa haraka, umiliki wa ardhi na majengo umeongezeka pia kwa kasi na kuwa chanzo muhimu tarajiwa cha mapato ya Halmashauri. Siku za nyuma Halmashauri ilitoza kodi inayofanana kwa majengo yote ya makazi na ya biashara yaani shs 10,000/= kwa majengo ya makazi na shs 20,000/= kwa majengo ya biashara. Jumla ya mapato ya mwaka toka chanzo hiki yakawa Tshs 20 milioni tu. Lakini mfumo huu mpya utakapo kamilika na kufanya kazi vilivyo chanzo hiki kitazalisha zaidi ya shs 200 millioni kwa mwaka.

Mfumo huu wa Digitali hutumika kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa kutumia Upimaji na Ramani za Cadastrali. Pia mfumo huu una Rejesta kamilifu ya Ardhi na Majengo katika Nchi. Upimaji Ramani na taarifa za Cadastrali kawaida hujumuisha taarifa za umiliki, mtumiaji wa jengo, eneo jengo lilipo, vipimo na thamani ya kipande cha ardhi/jengo husika. Mfumo huu wa Cadastrali hutumika katika nchi nyingi duniani kuhusiana na taarifa za hati na rejesta za ardhi/majengo. Katika nchi nyingi mifumo ya kisheria imejengeka juu ya mifumo ya kiutawala na hutumia taarifa za Cadastrali kuelezea vipimo na mahali ardhi ilipo inayohusika kwenye hati za kisheria. Cadastrali ni chanzo cha msingi cha taarifa katika migogoro na kesi kati ya wamiliki ardhi. Hata hivyo bado ni mfumo mpya kwa hapa Tanzania na Manispaa ya Mtwara-Mikindani ni mwanzilishi wa mfumo huu.

## 2.0 TATIZO LILILOKUWEPO KABLA YA KUANZISHWA KWA MFUMO WA CADASTRALI

Mwaka 2002/2003 kulitokea marekebisho ya kodi za Serikali za Mitaa na hasa kufutwa kwa Kodi ya Maendeleo ambayo iliathiri Halmashauri nyingi na ikaonekana kwa muda mfupi kuwa mapato ya ndani ya Halmashauri yangepungua kwa kati ya asilimia 40 – 50. Suala hili liliamsha angalizo kati ya wadau wa pande zote za Serikali za Mitaa na Serikali Kuu kuwa Uhuru wa Kifedha wa Halmashauri unaingiliwa kupitia marekebisho ya kodi za Serikali za Mitaa. Pia ukwepaji kodi ulikuwa mkubwa hasa ikijionyesha kuwa wananchi wengi kupinga kulipa kodi. Hali hii ilipelekea kupungua kwa kasi kwa mapato ya ndani ya Serikali za Mitaa na ikalazimu kupitia upya mchakato wa kodi za Serikali za Mitaa.

Pitio hili lililenga kuzitia hamasa Serikali za Mitaa kupanua wigo wa vyanzo vyao vya kodi. Kwa Manispaa ya Mtwara-Mikindani eneo la marekebisho likawa uboreshaji wa Kodi ya Majengo. Mfumo wa Cadastrali ukawa njia mojawapo ya kuongeza mapato. Wazo hili lilijadiliwa kwenye Baraza la Madiwani mwaka 2003/2004 na kuamuliwa kuwa yafanyike mapitio katika vyanzo vilivyopo na tarajiwa vya mapato. Katika pitio hili iligundulika kuwa;

(i) Manispaa ilikuwa inatumia thamani za Majengo za mwaka 1992 zikiwa zimepitwa na wakati katika vipengele vya thamani halisi na idadi kamili ya majengo katika eneo husika.

(ii) Ingawa haikwepeki zoezi la kuthamini majengo lilikuwa aghali sana.

(iii) Tozo linalofanana kwa majengo yote katika mtaa halikuwa la haki na lilipelekea walipakodi kutoridhika na hivyo kupunguza ari ya ulipaji. Mfumo huu wa tozo linalofanana haukuangalia tofauti za thamani wala ukubwa ardhi/jengo.

(iv) Utunzaji duni wa kumbukumbu za malipo ulipunguza kasi ya kuwashughulikia wasiolipa kodi. Ni rahisi sana katika mfumo wa utunzaji kumbukumbu wa kienyeji kupoteza, kukosea na kusahau kumbukumbu.

(v) Ukosefu wa vituo mbalimbali vya kulipia ulipelekea kupungua kwa ari ya kulipa kodi. Walipaji wote wa kodi ya majengo walilazimika kufika Makao Makuu ya Manispaa kulipa kodi zao. Hii haikuwa haki kwa walipaji waliopo pembezoni mwa Manispaa. Kwa

kuruhusu malipo kufanyika ngazi za Kata na Mitaa ingeweza kupunguza ukwepaji wa kulipa kodi.

(vi) Ufuatiliaji dhaifu wa ukusanyaji kodi Manispaa. Manispaa ilikuwa na watumishi wachache sana wa kufuatilia walipa kodi kwa Halmashauri nzima. Zoezi hili likawa gumu zaidi kutokana na ugumu wa kuyatambua majengo.

(vii) Uelewa mdogo juu ya kodi ya majengo. Walipakodi hawakuwa wameelimishwa; kulikuwa na uelewa mdogo sana kuhusu kodi za Serikali za Mitaa na hivyo hakukuwa na hamasa ya kulipa.

(viii) Tofauti kati ya makisio na makusanyo halisi ya kodi ya majengo. Makusanyo ya mwaka hayakuwa yakilingana na makisio (kati ya Majengo zaidi ya 10,000) kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini. Hali hii inamaanisha Halmashauri haikuwa na taarifa za uhakika za walipakodi za majengo.

Table 3.1: Tofauti ya Kodi ya Majengo 2005-2010

| Mwaka | Makisio (TAS) | Makusanyo (TAS) |
|---|---|---|
| 2005/2006 | 26,000,000.00 | 39,234,325.00 |
| 2009/2010 | 65,000,000.00 | 49,203,004.85 |

**Chanzo: Mtwara Mikindani MC 2011**

## 3.0 LENGO

Ili kuondokana na matatizo hayo hapo juu Manispaa ya Mtwara-Mikindani iliamua kuboresha ukusanyaji wa mapato. Malengo mahususi yalikuwa;

(i) Kuwa na taarifa mpya za majengo yote katika eneo la Manispaa.
(ii) Kuwa na mgawanyo haki na fanisi wa mzigo wa kodi kwa wakazi wa Manispaa.
(iii) Kuwa na taratibu fanisi na rahisi.
(iv) Kuongeza makusanyo ya kodi ya majengo.
(v) Kuboresha utoaji wa huduma za kijamii na za kiuchumi.

## 4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

Manispaa ya Mtwara-Mikindani ni eneo la majaribbio la mfumo huu wa Cadastrali. Mfumo huu unatekelezwa kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo ambao ni pamoja na GIZ na Benki ya Dunia. Utekelezaji ulianza Septemba 2009 kama majaribio. Inatarajiwa kuwa mfumo huu utakapokamilika na kukiwa na 100% ya uhiari wa kulipa kodi, Halmashauri itakusanya Kodi ya Majengo kutoka Tshs. 15 – 20 millioni hadi Tsh. 200 million kwa mwaka. Ili kufikia malengo yaliyopangwa mbinu zifuatazo ziliwekwa;

(i) **Kujenga uelewa wa wamiliki wa majengo.** Mikutano na warsha nyingi za kuelimisha wamiliki wa majengo ziliandaliwa katika ngazi za Kata na Mitaa ili kujenga uelewa kuhusu mfumo huu mpya wa ukusanyaji kodi.

(ii) **Kubadilisha Ramani na Mipaka ya vitalu kuwa ya Digitali**. Eneo lote la Halmashauri lilitengenezewa ramani ya digitali. Ramani zote za juu na za chini zilikuwa muhimu katika zaezi la kutengeneza ramani za digitali. Picha za majengo na wamiliki zilichukuliwa ili kuhifadhiwa kwa malengo ya rejea. Chuo cha Utafiti cha Naliendele kilichangia kwenye zoezi la kutengeneza ramani za dijitali kwa kutumia Technologia ya GPS. Kila nyumba ilipitiwa na kupimwa kwa ushirikiano na VETA. Matumizi ya wataalamu toka nje ya Halmashauri kukadiria majengo yalilenga kupunguza upendeleo; hivyo walitumika wanafunzi wa VETA.

(iii) **Ukaguzi na Uthamini wa majengo.** Zoezi la kuthaminisha Majengo lilifanywa na wataalamu wa uthamini kuainisha thamani halisi katika soko ya kila jengo kama msingi wa kukadiria kodi ya jengo. Angalia picha 2. Matokeo yakawa viwango tofauti kulingana na sifa za jengo, mahali lilipo, ukubwa, matumizi na aina ya jengo.


(iv) **Uanzishaji wa mfumo wa Cadastrali.** Kwa kutumia kompyuta, (FCDS/CAMA) mfumo wa Cadastrali ulianzishwa (angalia jedwali 3.1.). Wataalamu wa Technolojia ya Habari na Mawasiliano kutoka Chuo Kikuu cha Dar es –Salaam walisaidia sana zoezi hili.

(v) **Uhakiki wa mbinu za kukusanya taarifa.** Mfumo huu ulihakikiwa kwa kufanyiwa majaribio na maboresho yakafanyika kwenye baadhi ya vipengele vyake kabla ya kuingiza taarifa za majengo na wamiliki (angalia jedwali 3.1).

(vi) **Kuingiza Taarifa.** Baada ya kuthibitisha mfumo wa CAMA, taarifa ziliingizwa kuanzia hatua (ii) na (iii) hapo juu kieletroniki na kwa kuandika. Kulingana na mahali na sifa ya jengo, mfumo huu uliweza kukadiria kiasi cha kodi ya jengo anayotakiwa kulipa mmiliki (hati ya madai), Picha 3.2.

(vii) **Kutenga Madaraja na Kubandika Alama za Majengo**. Zoezi la kuweka alama katika majengo lilifanyika kwa kubandika namba za utambulisho wa jengo kwa kila nyumba. Majengo yamegawanywa kwa umiliki yaani binafsi au umma, (yale ya mashirika ya dini na taasisi za serikali) kwa Makazi au kwa malengo ya Biashara. Angalia picha 3.2. na jedwali 3.1.

(viii) **Muundo wa kitaasisi wa mfumo wa Cadastrali.** Muundo wa kitaasisi wa FCDS/CAMA umeelezewa kwenye mchoro 3.1. na gharama za uanzishaji zimewekwa kwenye jedwali 3.2. Muundo unaonyesha kuwa Chuo Kikuu cha Dar –es – Saalam kupitia kituo cha kompyuta (UCC) hutoa ushauri wa kitaaalamu kwa wataalamu wa CAMA waliopo kwenye sehemu ya mapato ya Manispaa ya Mtwara. Wataalamu hawa wanahusika na kuendesha mfumo na kuboresha taarifa zinazotoka kwa Watendaji wa Kata. Wataalamu hawa huandaa na kutoa hati za madai za mwaka na kuzipeleka kwa Watendaji wa Kata. Watendaji wa Kata huzipeleka kwa Watendaji wa Mitaa ili kuzigawa kwa wamiliki. Wamiliki hulipa kodi zao katika ofisi za Kata. Kila Ijumaa Mtendaji wa Kata hupeleka makusanyo ya kodi za majengo Makao Makuu ya Manispaa na hupewa asilimia 10 ya makusanyo kama motisha. Kuna Idara ya Sheria ambayo husimamia utekelezaji wa sheria ndogo ya kodi ya majengo. Idara ya Mipango Miji ni muhimu katika kuhakikisha majengo yote mapya yanaingizwa kwenye Mpango Mkuu (Master Plan) wa matumizi ya Ardhi wa Manispaa.




**Mchoro.3.1:Muundo wa Kitaasisi wa Mfumo wa Cadastrali**

## 5.0 RASILIMALI ZILIZOTUMIKA

Raslimali zilizotumika katika utekelezaji wa mpango huu zinatoka katika vyanzo vikuu muhimu yaani mapato ya ndani na fedha za wafadhhili kama inavyooneshwa kwenye jedwali 3.2. Fedha kutoka GIZ ndio mchango mkubwa (90.3%) katika gharama zote na fedha hizi zilitumika kwenye mafunzo, ada za ushauri, magari,usafiri, kompyuta na mifumo ya kompyuta. Fedha kutoka Programu ya Maendeleo ya Miji inayofadhiliwa na Benki ya Dunia zilitumika kwenye mafunzo, kuhamasisha jamii na kuendesha semina za kuongeza utayari/uhiari wa kulipa kodi za majengo kwa viongozi wa ngazi za chini. Chuo cha utafiti cha Naliendele kulichangia vifaa vya kutengeneza ramani za digitali kupitia teknolojia ya GPS. Mchango wa Manispaa (9.7%) ulitumika katika kulipa posho, mishahara na gharama nyingine za Wataalam Washauri.

## 6.0 MATOKEO NA MAFANIKIO

Mfumo kompyuta wa kuendeshea utaratibu huu mpya ulitengenezwa na unafanya kazi vizuri. Manispaa iliweza kutengeneza Ramani za Dijitali za Manispaa nzima kwa mafanikio na kurahisha utambuzi wa majengo (angalia mchoro 3). Mchakato wa dijitali ulisaidia kukusanya na kuingiza kwenye kompyuta asilimia 75 ya nyumba zote na kubandika alama kwenye milango ya nyumba zote zilizokaguliwa. Halmashauri pia imefanikiwa kufanya zoezi la kutambua thamani kwa nyumba zote kwa uhakika wa hali ya juu na kwa kuzingatia usawa. Kupitia mfumo huu kumekuwa na uwazi zaidi wa thamani ya madai ya kodi ya majengo kama inayoonekana kwenye alama ya jengo (mchoro 2) hapo chini, utambulisho wa Halmashauri unaanza kwanza ikimaanisha mfumo huu unaweza kuigwa na Halmashauri nyingine. Utambulisho wa Mtwara MCC HQ ni 0905, iliyopo kwenye Kata namba 052, Mtaa namba 534, na jengo katika eneo hili lipo kwenye daraja la 01 yaani eneo muhimu, na utambulisho wa ofisini wa jengo ni namba 0082 ikirejea kwenye jengo namba 01.

Tangu Desemba 2011 mfumo unafanyakazi na hati za madai zinatolewa kwa mfumo huu FCDS/CAMA na kugawanywa kwa Watendaji wa Kata na Mitaa. Malipo ya Majengo yanafanyika katika ofisi za Kata. Wakati Manispaa inasubiri mapitio na ulinganishi wa sheria ndogo ya fedha, Halmashauri imeendelea na mfumo wa kodi moja kwa majengo yote yaani, shs 10,000/=, 20,000/= na 30,000/= kwa majengo ya makazi na shs. 20,000/=, 40,000/=, na 60,000/= kwa majengo ya biashara. Karibu majengo 12,000 kati ya 16,000 yameshatambuliwa. Majengo yote yameandikishwa kutumia rejea ya GPS ambayo ni ya kudumu. Watumishi toka Idara za Fedha na Ardhi walifundishwa juu ya FCDS/CAMA. Taarifa zote zilizokusanywa na mfumo wa Cadastrali zinatumiwa na Idara nyingine pia kutambua kodi za ardhi, ushuru wa hotel na ada za huduma.





**Mchoro 3.3 Namba ya Utambulisho wa Jengo**

**Boksi 3.1: Maoni ya Wadau**

Meya Mhe. Selemani Mtalika:
Kulingana na Mhe. Meya Selemani Mtalika, Wazo la Kutumia mfumo wa Cadastrali umekua kutoka kipindi cha maboresho ya Serikali za Mitaa awamu ya kwanza (mwaka 2002/03). "Mfumo huu ni mzuri kuliko ule wa kodi inayofanana; huu unaangalia thamani ya soko na usawa, ingawa unahitaji ufuatiliaji wa karibu na maafisa Watendaji wa Kata ili kuona na kuongeza mabadiliko ya majengo haraka iwezekanavyo . Watakapokuwa umehamasishwa vya kutosha walipaji watalipa kwa ridhaa yao bila kulazimishwa. Pia mfumo huu unaweza kutumiwa kwa malengo kama kukadiria ushuru wa hoteli"

Afisa Mtendaji wa Kata ya Chikongoli Bwana Justini Mkwara anasema "mfumo huu ni fanisi kwa sababu majengo yote yametambuliwa, yamesajiliwa, yamethaminiwa na yamewekwa alama. Ofisi zote za Kata ni vituo vya kulipia kodi ya majengo. Kila Ijumaa tunapeleka makusanyo ya wiki na katibu asilimia 10 inatakiwa irudi kwenye ofisi ya Kata kama sehemu ya motisha".

Kiambatanisho (Jedwali 1) pamoja na Chati iliyopo hapa chini vinaonyesha mtiririko wa mapato ya ndani kutoka vyanzo vikubwa vya Manispaa ya Mtwara-Mikindani kwa kipindi cha miaka minne iliyopita. Mtiririko huu unaonyesha kodi ya majengo ni ya pili baada ya ada za huduma hata kabla ya viwango vipya kuanzishwa (rejea mchoro hapo chini). Ni pato la uhakika kwa miaka yote na chanzo cha kutegemewa kwani mali za kudumu huwa na tabia ya kuongeza thamani kuliko kupungua. Majengo mengi yanaendelea kujengwa kila siku na maendeo ya thamani za juu kadri biashara inavyokua.




**NB: Series 1=2009data; Series 2 =2010data; Series 3 =2011data; Series 4= 2012data**

**Chanzo: Uchambuzi wa taarifa za fedha za MMC 2012**

## 7.0 CHANGAMOTO

### (i) Upungufu wa watumishi

Mfumo huu bado upo kwenye majaribio. Kwa sasa hakuna idadi ya kutosha ya watumishi wa kuendesha mfumo huu kama inavyooneshwa kwenye jedwali 3.3.

**Jedwali 3.3. Makisio ya Watumishi kwa ajili ya mfumo wa FCDS**

| Utaalam | Makisio | Waliopo |
|---|---|---|
| Mipango Miji | 35 | 8 |
| Huduma za Sheria | 5 | 2 |
| ICT /FCDS/CAMA | | 4 |

**Chanzo: Mtwara-Mikindani 2011**

### (II) Majengo yanayokadiriwa Kodi

Katika mfumo, ukusanyaji wa taarifa hujumuisha taarifa kutoka majengo ambayo yamesamehewa na sheria za sasa. (kama majengo ya serikali na yale ya taasisi za kidini). Hili ni muhimu kwa mabadiliko ya sheria siku za mbele kuhusu majengo yanayokadiriwa kodi. Majengo ambayo leo hayatozwi kodi yanaweza kulazimika kulipa kesho.

### (iii) Mapitio na uoanishaji wa sheria ndogo

Ingawa FCDS inatumika kuna mapungufu mengi ya kisheria hayajashughulikiwa. Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa inataka kuwa katika kukadiria kodi za majengo unaweza kutumia viwango vya soko au thamani ya badiliko la jengo ili kupata tozo la kodi. Hapo awali, Manispaa ya Mtwara ilitumia viwango sawa ambapo mfumo wa sasa unahitaji kutumia viwango vya soko na thamani ya badiliko la jengo. Badiliko hili linahitaji marekebisho ya sheria ndogo kabla ya kutekelezwa moja kwa moja.

## 8.0 UENDELEVU WA MFUMO

Uendelevu hutegemea uwepo wa watumishi wenye dhamira na utashi wa kisiasa wa uongozi pamoja na watumishi wa Manispaa. Kazi hii inahitaji wataalumu waliobobea na kujikita katika eneo la Tecknolojia ya Habari na Mawasiliano, Fedha, Mipango Miji na Sheria mpaka ngazi za chini kabisa. Pia kuna hofu ya kupungua kwa watumishi kutokana na kuhamishwa na kuhudhuria masomo ya muda mrefu. Manispaa itaendelea kupata ushauri toka Chuo Kikuuu cha Ardhi na kitengo cha Komputa cha UCC ili kufanya mfumo huu uendelee kufanya kazi. Halmashauri itaendelea kuongeza uelewa wa walipa kodi, kufuatilia na kupima utendaji wa mfumo huu. Mafanikio ya jaribio hili yatapelekea kuanzishwa kwa mfumo huu katika Halmashauri nyingine. Halmashauri zote zinakaribishwa kuja kujifunza mfumo huu katika Manispaa ya Mtwara-Mikindani.

## 9.0 SIRI YA MAFANIKIO NA MASUALA YA KUIGWA

Siri za mafanikio Manispaa ya Mtwara-Mikindani zimejificha kwenye haya yafuatayo;

(i) Uhiari wa Halmashauri kutumia mbinu mpya ya FCDS/CAMA ni suala la kwanza kabisa. Gharama za mwanzo ni kubwa lakini faida zitakazopatikana zitadumu kwa miaka mingi. Inashauriwa kwa wale watakaoiga mfumo huu kuainisha gharama za mwanzo na matokeo yake katika bajeti ya Halmashauri. Pia wanatakiwa kuchunguza uwezo wa Technolojia ya Habari na Mawasiliano iliyopo eneo hilo.

(ii) Kesi ya Manispaa ya Mtwara ni ya kipekee kwani asilimia 93 ya gharama zote ni msaada toka GIZ. Halmashauri zenye fedha chache lakini zinataka kuiga mfumo huu wanatakiwa kutafuta washirika wa maendeleo. Hata hivyo kiasi cha fedha za kuanzishia mfumo huu kiko ndani ya uwezo wa Halmashauri nyingi za Tanzania. Kinachotakiwa ni uwekaji kipaumbele wa miradi na utafutaji changamfu wa washirika na misaada kutoka vyanzo mbalimbali.

(iii) Dhamira ya Halmashauri kutambua, kusajili na kubandika alama katika majengo, viwanja na mitaa ndani ya manispaa hata bila mfumo wa kompyuta. Inahitaji dhamira kuingia katika zoezi gumu kama hili ikizingatiwa kuwa kodi ya majengo ni eneo ambalo halijatumiwa vizuri na halmashauri zote, Halmashauri zinashauriwa kuongeza kodi za majengo.

(iv) Ushiriki thabiti wa wadau. Kwa mfano, GIZ, Idara ya Ardhi, Idara ya Fedha, Chuo cha Utafiti, Chuo Kikuu cha Ardhi, na UCC wote walikuwa muhimu katika kufanikiwa kwa FCDS/CAMA.

(v) Mabadiliko ya sheria ndogo ni ya lazima ili kwenda pamoja na sheria za fedha za nchi. Kabla Halmashauri haijaiga mfumo huu ni lazima kufanya mapitio ya sheria za fedha za Halmashauri. Halmashauri nyingi zinatumia viwango vinavyofanana kwenye kodi za majengo lakini mfumo wa CAMA hutumia viwango vinavyoshabihiana na thamani za majengo za Soko. Viwango hivi vina haki na usawa na huboresha ari ya walipakodi.

(vi) Kama Halmashauri zitaamua kuiga mfumo huu, kuna haja ya kutenganisha ukusanyaji wa taarifa za majengo na zoezi la uthaminishaji ili kupunguza tofauti za kimaslahi. Shughuli hizi mbili hazitakiwi kufanyika pamoja.

(vii) Ili kuongeza ufanisi na utendaji ni vyema kutumia kampuni binafsi kufanya ukusanyaji wa takwimu.

(viii) FCDC ni muhimu katika kukusanya takwimu muhimu kwa idara nyingine za Halmashauri. Zinaweza kutumiwa kukadiria ushuru wa mahoteli na nyumba za kulala wageni.

(ix) Inaweza kutumika kukusanya taarifa za Jiografia kama umri, jinsi, kazi na idadi ya wakazi katika nyumba.

(x) Inaweza kutumika kufanya uchambuzi wa hali ya uchumi wa kanda tofauti za Jiji au Manispaa.

(xi) Mfumo ni muhimu kwenye ushughulikiaji wa majanga kama kujikinga na moto kwa sababu misingi yake ni Mipango Miji ya jumla. Inarahisisha kuacha nafasi ya kutosha kati ya majengo ili magari ya zimamoto yaweze kupenya bila ucheleweshwaji.

(xii) Mfumo huu una umuhimu katika kuhifadhi mazingira. Unahakikisha ukuaji wa mji safi.

(xiii) Ni kitendeakazi muhimu katika Mipango Miji katika Majiji na Miji.

**Jedwali 3.2: Gharama za Kuanzisha Mfumo wa Cadastrali**

| Kipengele | GIZ TAS. | M-M MC TAS. |
|---|---|---|
| Ukarabati wa Ofisi (samani, viyoyozi n.k) | | 9,000,000 |
| Kutayarisha Ramani na Mipaka ya vitalu kuwa ya Digitali. | 1,190,000 | 1,800,000 |
| Kutayarisha Ramani na Mipaka ya vitalu kuwa ya Digitali. | 500,000 | |
| Kutayarisha Ramani na Mipaka ya vitalu kuwa ya Digitali. | 3,345,000 | |
| Vifaa vya Utafiti (Data Sheet, Stickers, Measurement | 260,000 | 2,400,000 |
| Ukusanyaji wa Takwimu | 31,000,000 | |
| Posho | | 600,000 |
| Usimamizi na udhibiti wa ubora | 2,650,000 | |
| Usafiri | 450,000 | 400,000 |
| Vitendea kazi (Kompyuta, Printa, Mtandao, Kamera) | 19,875,000 | |
| Mafunzo na Uhuishaji wa mfumo | - | - |
| Jumla Ndogo | 59,270,000 | 14,200,000 |
| Kujenga Mfumo na kuingiza Takwimu | 25,850,000 | |
| Ukaguzi na Uthamini wa Majengo | 70,800,000 | |
| Jumla | 155,920,000 | 15,200,000 |
| Asilimia | 90.3 | 9.7 |

Chanzo: Mtwara-Mikindani Municipal Council 2011

# Rate Assessment: Current and Proposed



| | | |
|---|---|---|
| Prop. Ref. No (PRN) + Bld No: | 0905-052-516-001-0002 | 1 |
| Rateable/Non-Rateable: | RATEABLE | |

**LAND CHARACTERISTICS**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Land Use | Residential | Location Adj. Zone | AO |
| Road Access | Earth Road | Electricity | No |
| Water Supply | Metered / Main | Land Plot Area | 0 |
| Sanitation | Septic Tank | | |
| Perimeter Fence Type | None | Total Fence Length (M) | 0 |
| Fence Condition | None | Avg. Fence Height (M) | 0 |

Location Adjustment Rate: 0.89

**BUILDING CONSTRUCTION CHARACTERISTICS**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Building Type | Detached House | Number of Floors | 1 |
| Structure Type | Cement Brick | | |
| Exterior Wall Type | Brick-Plastered | Roof Type | Metal Sheet |
| Floor Finish Type | Cement | Ceiling Finish Type | None |
| Construction Year | 2008 | Gen. Ext. Condition | Good |
| Reconstruction Year | 0 | Gen. Int. Condition | Good |
| | | Total Bld. Area (M2) | 41 |

| | | |
|---|---|---|
| Base Construction Cost per M2 (TSh) | | 350,000 |
| Base Flat Rate per M2 (TSh) @ | 0.05% | 175 |

| EWT | FFT | RFT | CFT | Product |
|---|---|---|---|---|
| 1.00 | 1.00 | 1.00 | 0.90 | 0.90 |

| | | |
|---|---|---|
| Adj. Construction Cost per M2 (TSh) | | 315,000 |
| Depreciated Adj. Cons. Cost @ | 10% | 283,500 |
| Estimated Property Fiscal Value (TSh) | | 10,300,000 |
| New Tot. Flat Rates Liability @ | 0.05% | 5,000 |
| Current Property Flat Rates Liability | | 10,000 |

Figure 3.2: Rate Assessment

Chanzo: Mtwara-Mikindani Municipal Council 2011

## Schedule1: Property Rate Data Sheet

### PROPERTY RATE DATA SHEET
Mtwara-Mikindani Municipal Council

Doc. Ref. No. (Year / Bundle No. / Page No.)

☐ New Record ☐ New Sales ☐ Update Rec. ☐ Delete Ppty ☐ Delete Bld

Prop. Ref. No.: 0 9 0 5 (LGA / Ward / Mtaa / Rate Block / Object No / Shared / Building No.)

Shared PRN: 0 9 0 5 (LGA / Ward / Mtaa / Rate Block / Object No) — Non-Rateable ☐

**PROPERTY LOCATION**

| Street + Location: | Plot No: | Geo Code: | Existing Property Reference Number: |
|---|---|---|---|
| | | | |

**1 OWNER / 2 OCCUPIER / 3 BENEFICIARY** — TIN:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1 Individual | First Name: | Middle Name: | Last Name: | Cell Phone No: |
| 2 Legal Entity | Full Company Name | | | Main Land Line Phone No: |
| Street + Location: | | | Plot No: | P.O. Box: |
| Municipality: | | Ward: | Mtaa: | Email Address: |

**LAND CHARACTERISTICS**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Tenure: 1 Leasehold 2 Untitled 3 Other | Land Use: 1 Residential 2 Business/ Commerce 3 Industry/ Factory 4 Institutional 5 Agriculture 6 Other | | Electricity Connection: 1 Yes 2 No |
| Perimeter Fence Type: 1 Steel Rod/Bar 2 Brick Wall 3 Metal Sheet 4 Iron Mesh 5 Timber 6 Plant 7 Other 8 None | Road Access: 1 Tarmac Rd 2 Murram/ Gravel Rd 3 Earth Rd 4 Foot Path 5 Other 6 None | Water Supply: 1 Metered/ Flat Rate 2 Communal Stand Tap 3 Borehole 4 River/ Stream 5 Rain 6 Other/ None | Sanitation: 1 Sewer 2 Septic Tank 3 Pit Latrine 4 Other 5 None |
| General Perimeter Fence Condition: 1 Very Good 2 Good 3 Fair 4 Poor | Total Fence Length (M): / Avg. Fence Height (M): | Plot Area (M2): | Loc. Adj. Code: |

**BUILDING CONSTRUCTION CHARACTERISTICS** ☐ Under Construction

| | | | |
|---|---|---|---|
| Building Type/Use: Commercial/Industrial C: 1 Shopping Mall/Dept. Store 2 Shop/ Rest./Bar 3 Office/ Bank 4 Hotel 5 Petrol Station 6 Factory/ Warehouse 7 Storage Tank 8 Other | Building Type/Use: Institutional I: 1 School 2 Sport/ Recreation 3 Clinic/ Hospital 4 Worship 5 Government 6 Other | Building Type/Use: Residential R: 1 Detached House 2 Semi Detached 3 Apart./ Condo 4 Hut 5 Other | Structure Type: 1 Steel 2 Concrete 3 Cement Block 4 Claysoil Brick 5 Timber 6 Other |
| General Exterior Condition: 1 Very Good 2 Good 3 Fair 4 Poor | Roof Type: 1 Concrete 2 Corr. Alum./ Metal Sheet 3 Tiles 4 Asbestor 5 Grass/Palm 6 Other 7 None | Exterior Wall Type: 1 Concrete 2 Glass 3 Metal Sheet 4 Brick - Plastered 5 Brick - Cladded 6 Timber 7 Mud 8 Other 9 None | Construction Year: / Reconstruction Year: / Number of Floors: / Elevator/Escalator (Y/N): |

**ADDITIONAL BUILDING CHARACTERISTICS**

| | | | |
|---|---|---|---|
| General Interior Condition: 1 Very Good 2 Good 3 Fair 4 Poor | Floor Finish Type: 1 Marble/ Granite 2 Stone 3 Terazzo 4 Tiles 5 Timber/ Wooden 6 Cement 7 Earth 8 Other | Ceiling Finish Type: 1 Concrete 2 Gypsum 3 Timber 4 Softboard/ Hardboard 5 Chipboard 6 Other 7 None | Floor Number: / Number of Rooms: |
| Total Building Floor Area (M2): (see calc. in the back page) | | | Number of Full Baths: / Number of Toilets: |


**SIGNATURES**

The information registered on this form is true and accurate to the best of my knowledge. Need Re-Survey? ☐ Issue New Bill? ☐

| | | | |
|---|---|---|---|
| Date: | Date: | Date: | Data Entry Initial/ Date: |
| 1 Owner 2 Occupier 3 Beneficiary | Enumerator/ Surveyor ID | Supervisor ID | |

FORM DM-09/001 (2/19/2010 11:05 AM)

Figure 3.4 Ramani ya Digitali ya Manispaa ya  Mtwara- Mikindani




**Chanzo: Mtwara – Mikindani MC 2011**

Kiambatisho: Jedwali 1:  Mtiririko wa ukusanyaji mapato toka vyanzo vikuu

| Vyanzo Vikuu | Mwaka | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **2008/09** | **2009/10** | **2010/11** | **2011/12** |
| Ushuru wa Huduma | 163044826 | 154630701 | 189986323 | 275423156 |
| Kodi ya Majengo* | 53307904 | 49203004 | 37841974 | 45229918 |
| Ushuru wa Korosho | 14325862 | 15202600 | 31459880 | 100552480 |
| Leseni ya Uvuvi | 13801700 | 19434600 | 20656000 | 2699300 |
| Ushuru wa Soko | 21132900 | 24837200 | 24098800 | 45339470 |
| Kodi ya pango | 5489485 | 18093687 | 28121409 | 27263370 |
| Ushuru wa ramani ya jengo | 16572580 | 1872600 | 10374010 | 8889907 |
| Mfuko wa Elimu | 15174892 | 55605207 | 30459148 | 15145279 |
| Ushuru wa Nyumba za Kulala Wageni | 18228751 | 27733400 | 29223267 | 25560800 |

**Chanzo: Mtwara Mikindani MC 2012**

*NB: when in full operation new property tax system will provide stable income of over 200 million TAS annually.

# HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA

## UBORESHAJI WA MAPATO KWA NJIA YA UJASIRIAMALI




*MBEYA CC: KITUO CHA MIKUTANO CHA MKAPA*

## 1.0 UTANGULIZI

Jiji la Mbeya lipo katika Wilaya ya Mbeya na ni moja ya Wilaya nane za Mkoa wa Mbeya. Wilaya ipo kwenye latitudo 7 na 9 kusini mwa Ikweta na kati ya longitudo 33 na 35 Mashariki mwa Greenwich. Inapakana na Wilaya ya Mbarali kwa Mashariki, Rungwe na Ileje kwa Kusini, Mbozi kwa Magharibi na Chunya kwa Kaskazini Magharibi. Hali ya hewa ya Jiji la Mbeya ni ya baridi ikiwa wastani wa nyuzi joto kati ya 11c hadi 25c. Jiji lina huduma nzuri za mawasilano, yaani kuwa na uwanja wa ndege mzuri, reli ya Tazara, na barabara kuu ya TANZAM. Pia ni Jiji la kibiashara kwa maeneo ya nyanda za juu kusini na limetekeleza miradi mbalimbali kwa kutumia fedha toka Serikali Kuu, vyanzo vya ndani, wafadhili na michango ya jamii.

## 2.0 HISTORIA

Toka waka 1996/1997 Serikali ya Tanzania ilianza kutekeleza uamuzi wake wa kurekebisha Tawala za Mikoa na kuimarisha Serikali za Mitaa ambazo zinafanya kazi vizuri katika kuleta maendeleo na kutoa huduma za kiuchumi na kijamii kwa watu. Katika ukweli huu, kifaa muhimu cha kazi ni raslimali fedha. Pia Serikali za Mitaa zinahitaji vitendea kazi na miundombinu sahihi kwa ajili ya utoaji huduma. Ingawa majukumu ya Serikali za Mitaa yanaongezeka kila mwaka, fedha zinazotoka Serikali Kuu hazilingani na shughuli zinazokuwa zimepangwa. Hali hii huleta mzigo mkubwa kwa Serikali za Mitaa wa kutafuta mapato katika vyanzo vya ndani.

Manispaa ya Mbeya (Sasa Jiji) ni moja ya Halmashauri ambazo zilipata shida kutokana na kupata fedha kidogo toka Serikali Kuu na mapato madogo kutoka vyanzo vya ndani. Ili kupambana na hali hii, Halmashauri iliamua kujenga ukumbi wa kisasa wa mikutano na bweni ili kuongeza mapato, kitendo cha uvumbuzi ambacho kinastahili kuigwa na Halmashauri nyingine. Ni kwa kigezo hiki TOA iliamua kuchagua kesi hii ya Mbeya kuwa ya mfano kwenye eneo la kuboresha mapato.

## 3.0 TATIZO LILILOKUWEPO KABLA YA UBORESHAJI WA MAPATO

Jiji la mbeya lilikuwa likikabiliwa na tatizo la mapato ya chini kutoka kwenye vyanzo vya ndani. Kwa mfano, mwaka 2004 Halmashauri ilikusanya Tsh. 604,991,257 tu. Halmashauri haikuwa na huduma za ukumbi wa mikutano kuweza kuendesha mikutano ya kitaifa na kimataifa na kujipatia mapato.

## 2. LENGO

Lengo la jiji likawa ni kuongeza mapato ya ndani ili kujihakikishia upatikanaji wa huduma bora za kijamii na kiuchumi kwa wakazi wa Jiji.

## 3.0 MIKAKATI NA SHUGHULI ZA UTEKELEZAJI

Mwaka 2003 Baraza la Madiwani ambalo ndilo chombo cha juu kabisa cha maamuzi na upitishaji wa matumizi ya fedha liliamua ufanyike ujenzi wa kituo cha kisasa cha mikutano ambacho kitakuwa mojawapo ya vyanzo vya mapato ya ndani. Ili kufikia lengo hili yafuatayo yalifanyika;

(i) **Kuainisha eneo.** Ilikubalika kujenga kituo cha kisasa cha mikutano kwenye eneo la kituo cha zamani cha jamii. Eneo limekaa kimkakati zaidi kwani lipo katika eneo la kati la kibiashara (CBD) la Jiji la Mbeya ambako kuna shughuli nyingi za kijamii. Pia pamezungukwa na huduma mbalimbali za nyumba za kulala wageni, maduka na taasisi za dini. Bweni la Halmashauri lipo mahali muhimu, zamani paliitwa uzunguni chini ya milima mizuri ya Loleza.

(ii) **Upembuzi yakinifu.** Baada ya kuchagua eneo, upembuzi yakinifu ulifanyika ili kujiridhisha na matokeo ya mradi kijamii, kiuchumi kijinsia na kimazingira. Zoezi hili lilifuatiwa na uchoraji mchoro wa kituo na hatimaye kupitishwa na Baraza la Madiwani.

(iii) **Utafutaji wa fedha.** Fedha kwa ajili ya mradi huu zilitoka kwenye mapato ya ndani na Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB). Bodi hii ni taasisi ya fedha ambayo hutumika kama chanzo cha mitaji kwa Halmashauri kwa ajili ya uwekezaji. Uwekezaji huu unalenga katika ukuaji wa uchumi kwa kusaidia utekelezaji miradi ya kiuchumi ili kuongeza uwezo wa Serikali za Mitaa kimapato. Pia bodi hii hutoa misaada ya kifedha kupitia ruzuku, dhamana na kadhalika. Bodi pia inatoa huduma kwa niaba ya Serikali za Mitaa hivyo bodi ilikuwa ni chanzo stahili kwa mradi huu.

(iv) **Ujenzi.** Taratibu za kawaida za kupata mkandarasi zilifanyika na mzabuni aliyeshinda alipewa mkataba. Mshauri na Mhandisi Mkazi walisimamia ujenzi hadi kukamilika.

(v) **Umaliziaji wa kazi.** Mradi ulimalizika kwa kuhakikisha kuwa una vifaa vyote na huduma zinatolewa. Bustani, wigo na eneo la kuegesha magari vilitengenezwa. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwaka 2003 na kukamilika 2004.

## 4.0 KIASI NA AINA YA RASILIMALI ZILIZOTUMIKA

Jumla ya gharama za kujenga kituo cha mikutano ilikuwa shs 450 milioni. Jiji lilidiriki kukopa shs 400 millioni kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa na shs 50 million zilitoka ndani. Jedwali 3.5 linaonyesha gharama za mradi.

**Jedwali 3.4: Gharama za Ujenzi za Kituo cha Mikutano cha Mkapa**

| Hatua za Utekelezaji | Jumla ya Shilingi |
|---|---|
| 1.Upembuzi | 10,000,000/= |
| 2.Ujenzi wa wigo | 40,000,000/= |
| 3.Ujenzi wa Ukumbi | 340,000,000/= |
| 4.Bustani | 20,000,000/= |
| 5.Umaliziaji | 40,000,000/= |
| **Jumla** | **450,000,000/=** |

**Chanzo: MCC 2011**


## 5.0 MATOKEO NA MAFANIKIO

Kutokana na mradi huu wa kivumbuzi, kwanza ukumbi wenyewe unavutia ukiitwa “Kituo cha Mikutano cha Mkapa” kwa heshima ya Rais Mstaafu. Kituo kina kumbi nne, tatu kati ya hizi zinatumika kibiashara na mmoja unatumika kama kituo cha jamii kwa wakazi wa Jiji. Angalia picha hapa chini.




*Kituo cha Mikutano cha Mkapa*

Matokeo ya mradi huu ni kuwa wakazi wa Jiji la Mbeya wana sehemu ya kufanyia shughuli za mapumziko pamoja na matukio mbalimbali ya kijamii kama harusi, muziki, matamasha, mikutano na shughuli za kutangaza bidhaa na huduma. Pia kituo kinatoa huduma za mikutano na warsha kwa ubora wa kitaifa na kimataifa kibiashara. Mchoro No. 2 unaonyesha ongezeko la ukusanyaj mapato kuanzia mwaka 2006/2007. Faida kutoka kwenye chanzo hiki huchangia kwa kiasi kikubwa kwenye mapato ya ndani ya Halmashauri, rejea jedwali 3.5. Ongezeko la mapato ya ndani limepelekea utoaji wa huduma bora kama ujenzi wa zahanati, madarasa, huduma za maji na usafi wa barabara kwa jamii ya Jiji.




**Mchoro 3.4: Mtiririko wa Mapato**
**Chanzo: MCC 2011**

**Jedwali 3.5: Mapato ya Ndani**

| **Mwaka wa fedha** | **Mapato (shs)** |
|---|---|
| 2004/05 | 604,991,257 |
| 2005/06 | 721,777,973 |
| 2006/07 | 1,460,000,000 |
| 2008/09 | 2,200,000,000 |
| 2009/10 | 3,500,000,000 |
| 2010/11 | 7,300,000,000 |
| **Total** | **15,786,769,230** |

**Chanzo: MCC 2011**

**Bweni la Halmashauri**

Vyote, Kituo cha Mikutano na Bweni vimejengwa ili kuboresha utoaji wa huduma ndani ya Jiji. Kituo cha mikutano huenda sambamba na huduma za Bweni. Katika kutambua hili Jiji lilianzisha mradi wa bweni. Bweni lina vyumba 42 ambavyo vina huduma zote ndani na vyumba viwili vya watu mashuhuri. Jumla ya gharama za miradi ni shs 876 million. Chanzo cha fedha hizi ni mkopo mwingine toka bodi ya mikopo ya serikali za mitaa (Sh. 650 million) na mapato ya ndani ya Halmashauri (Sh. 226 million). Mradi upo katika hatua za mwisho na utaanza kutoa huduma kuanzia robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2011/2012. Angalia picha hapa chini.



***Bweni -Mbeya CC***

**Matarajio ya Mapato toka kwenye Bweni**

Inatarajiwa kuwa bweni litazalisha jumla ya Shs., 691,200,000 kwa mwaka endapo litatumika kikamilifu na gharama za uendeshaji kulipwa kama matumizi ya kawaida ya Halmashauri kama inavyoonyesha kwenye jedwali 3.6. makadirio haya yanazingatia uhitaji wa mabweni uliopo Jijini Mbeya. Kama Bweni litatumika kwa asilimia 50% mradi utahitaji miaka miwili kurejesha mtaji.

**Jedwali 3.6: Makisio ya Mapato ya Mradi**

| Aina ya Chumba | no | Kiasi kwa siku | Mapato |
|---|---|---|---|
| Suites | 2 | 120 000 x 360 days | 86,400,000 |
| Self contained | 42 | 40 000 x 360 days | 604,800,000 |
| **Jumla** | **44** | **Kiasi** | **691,200,000** |

**Chanzo: MCC 2011**

**6.0 CHANGAMOTO**

Changamoto kuu wakati wa utekelezaji wa mradi ilikuwa mfumuko wa bei. Kulikuwa na ongezeko la bei kwenye vifaa vya ujenzi lillilopelekea Halmashauri kutenga fedha (Sh. 50,000,000.) kutoka kwenye mapato ya ndani ili kumalizia mradi wakati wa ujenzi wa Kituo cha Mikutano cha Mkapa.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Ili kuendeleza ongezeko la mapato Halmashauri iliamua kukodisha baadhi ya vyanzo vya mapato ili kuongeza ukusanyaji na kujihakikishia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati.

Uendeshaji wa majengo. Ili kusimamia utendaji wa mradi, Halmashauri iliunda timu ya menejimenti ili kusimamia shughuli za kila siku na kuboresha utoaji wa huduma. Timu hii imepewa madaraka ya kuanzisha miradi midogo midogo ambayo itasaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa mradi, kwa mfano kwa kuanzisha duka la shajala na huduma za mtandao.

Jiji linajisifu kwa kusimamia sheria ndogo za fedha kwa lengo la kuongeza mapato. Pia Halmashauri itaboresha miundo mbinu inayoelekea kwenye eneo la mradi ili kuvutia na kuongeza wateja.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO NA MASUALA YA KUIGWA**

Mafanikio ya mradi huu wa Jiji la Mbeya yalitokana na;

(i) Ubunifu katika kuongeza mapato. Wazo la kituo cha mikutano na bweni ni wazo la kivumbuzi kwa ngazi ya Halmashauri linalistahili kuigwa na Halmashauri nyingine. Bwana Kabwe, Mkurugenzi wa Jiji aliyekuwepo alikuwa ndio mwanzilishi wa wazo la miradi ya Kituo cha Mikutano na Bweni. Inahitaji watu wabunifu kuanzisha miradi mipya ya kuongeza vyanzo vya pato katika Halmashauri. Pia unahitajika uongozi wenye stadi za ujasiriamali na uthubutu ili kuanzisha miradi iongezayo pato.

(ii) Baadhi ya taasisi huhofia kuchukua mikopo lakini Jiji la Mbeya lilikuwa na ujasiri wa kutoogopa hatari na kuchukua kiasi tosha cha fedha/mkopo na kuwekeza kwenye miradi ya uhakika ya Kituo cha Mikutano na Bweni. Kwa sababu kuna taasisi za fedha na mikopo ikisubiri ubunifu tu wa maendeleo, ni vyema Halmashauri zikatumia fursa hizi kwa kuandika mapendekezo na mipango ya kibiashara ili kuzivutia taasisi za mikopo.

(iii) Timu ya Menejimenti ya Halmashauri (CMT) imeonyesha uwezo wa hali juu ya ushawishi kwa kuweza kuwashawishi Madiwani kukubali kuingia kwenye uwekezaji huu wa muda mrefu.

(iv) Uendeshaji wa miradi hii miwili unafanywa na kamati maalum. Kiongozi wa kamati hii anateuliwa kutoka ndani ya Halmashauri. Timu hii imepewa madaraka ya kuhakikisha kuwa Halmashauri inapata mapato ya kutosha kwa kubuni miradi midogo midogo kuzunguka maeneo ya miradi hii miwili. Pia timu imepewa madaraka ya kufanya kazi na sekta binafsi ili kuhakikisha miradi ina ushindani na mvuto kwa wateja.

# Sura ya Nne: Ushirikishwaji wa Jamii katika Utoaji wa Huduma

Kupanga mipango kwa njia shirikishi ni hatua ya mwanzo kabisa katika kutoa huduma kwa jamii. Kupanga mipango ni mchakato endelevu wa kuweka malengo, kutambua fursa au rasilimali na uwezo uliopo wa kutekeleza miradi hadi kufikia malengo, katika muda muafaka uliowekwa na Taasisi, Serikali, Idara au Kitengo cha Utawala. Kupanga mipango kunasaidia sana katika kutekeleza miradi kwa utaratibu wenye mantiki na kufikia malengo yaliyowekwa, kufuatilia matumizi ya rasilimali na kutatua vikwazo. Katika mazingira halisi ya Serikali za Mitaa, mipango husaidia kuanisha maeneo yanayohitaji kuwekewa mkazo na vipaumbele vya jamii vinavyohitaji kushughulikiwa kwa kutumia rasilimali zilizopo. Mipango husaidia katika kugawanya rasilimali na utekelezaji wa kila shughuli iliyopo kwenye mpango. Mpango shirikishi ni zana ya kuusadia uongozi wa taasisi ili uweze kusimamia shughuli za maendeleo na kutoa huduma kwenye Serikali za Mitaa.

Mipango shirikishi humaanisha kwamba wadau, walengwa, wataalamu, washitiri wa maendeleo, watunga sera hukaa kikao/vikao vya pamoja kuchambua, kujadiliana, kukubaliana na kuweka mkakati au mpango wa pamoja. Kwenye ngazi za msingi za Serikali za Mitaa kama vile Kijiji katika Tanzania, mipango shirikishi inahusisha Kamati ya Kijiji, Maafisa Ugani wote wa Kijiji, wanakijiji, na marafiki wa maendeleo. Wadau wote hawa, hujaribu kuchambua hali halisi iliyopo, kukubaliana juu ya hali njema tarajiwa, kukubaliana juu ya hatua muafaka za kuchukua ili kufikia hali njema tarajiwa, mikakati ya utekelezaji, kujadili na kukubaliana kuhusu mgawanyo wa majukumu, muda hadi mradi kukamilika, na vipindi vya utekelezaji.

Azma ya mpango shirikishi jamii ni kujenga uhusika halisi na wa haki wa kila mdau katika maamuzi ya rasilimali, matumizi mazuri ya raslimali za asili, kufikia muafaka na makubaliano juu ya mustakabali wa maisha ya jamii husika, kuhakikisha maoni na mahitaji ya makundi mbali mbali ya kijamii yamezingatiwa ndani ya mpango, jamii kumiliki mchakato, uwekezaji na uendelevu wa mradi hata baada ya muda wa utekelezaji kuisha.

Katika sura hii, visa mkasa vinne kuhusu ushirikishwaji wa jamii katika utoaji wa huduma vimewasilishwa. Halmashauri ya Ileje ina kisa mkasa kuhusu mipango shirikishi jamii, uwekaji vipaumbele, utekelezaji wa miradi shirikishi jamii inayogusa mahitaji halisi ya jamii, tena kwa kutumia rasilimali zilizopo ndani ya jamii, uzoefu na ujuzi wa jamii yenyewe. Ni mfano halisi wa maendeleo ya jamii asilia kwa kutekeleza mradi wa ujenzi wa daraja la mawe ili kutatua tatizo la vivuko.

Jiji la Mwanza ni kisa mkasa kuhusu uzoaji taka shirikishi, Jiji limetumia ushitiri wa sekta ya umma na sekta binafsi. Linahusisha ubunifu wa kufanya uskauti wa kukagua usafi kwa kutumia kampuni binafsi (Sherifu) kukamata wakiukaji na kwa kutumia kamera za siri. Halmashauri ya Nzega ina kisa mkasa kuhusu usafi wa mazingira kwenye Kata ya Mambali ambacho kilipelekea jamii kubadili fikra, hali, tabia , utamaduni na desturi potofu za kutotumia vyoo na kuanza kuchimba na kutumia vyoo kwenye Vijiji vinne. Mwisho, Halmashauri ya Igunga ina kisa mkasa kinacholenga usimamizi imara wa Mfuko wa Afya ya Jamii kwenye huduma za afya kama njia mbadala ya kupata fedha za kutoa huduma za afya kwa jamii, kwani bajeti yake siku zote haitoshelezi mahitaji.

Masomo makuu tunayojifunza kutokana na visa mkasa vilivyopo kwenye sura hii yanaonesha kwamba:

- Maendeleo ya watu yataletwa na watu wenyewe. Kwa mantiki hiyo Tanzania haipaswi kuendelea kutegemea misaada na rasilimali za kutoka nje, bali kuna haja ya kutekeleza maendeleo asilia kwa njia shirikishi.
- Kama ikitumika njia muafaka katika kuwashirikisha watu, jamii ya Watanzania imekwishaamka ili kujiletea maendeleo yao.
- Tanzania bado hatujatumia rasilimali zetu za asili inavyopasa. Bado zipo rasilimali nyingi zinazohitaji ubunifu tu na kuanza kuzitumia. Tanzania haipaswi kuendelea kufikiri kwamba taka siku zote ni kitu kibaya na kisicho na faida, ni muhimu kuzichukulia taka kama rasilimali kwa kuanza kuzitenga taka kwenye makundi mbalimbali tangu zinakozalishwa, na kurudisha baadhi kwenye matumizi mbadala mfano plastiki, chupa, vyuma na kuzalisha gesi kutokana na taka.
- Ufanisi katika huduma za kuzoa na kutupa taka huenda sambamba na upangaji mzuri wa Mipango Miji; utungaji na utekelezaji wa sheria ndogo, kanuni, makubaliano na maelewano ili kujenga utii wa sheria bila shuruti.
- Ushitiri kati ya sekta binafsi na sekta ya Umma maarufu kama PPP ni wa muhimu sana kwenye huduma shirikishi jamii. Sekta binafsi, vikundi vya kiraia lazima vihusike ipasavyo katika kuboresha utoaji wa huduma.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA ILEJE

## UJENZI WA MADARAJA YA MAWE YENYE GHARAMA NAFUU



*Timu ya Halmashauri ya ujenzi wa madaraja ya mawe ikitoa maelezo juu ya ufanisi na umadhabuti wa madaraja ya mawe*



## 1.0 UTANGULIZI

Andiko hili ni juhudi ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango kazi ulioandaliwa na watumishi wa Serikali za Mitaa waliopata mafunzo Osaka nchini Japani. Mafunzo haya yaliandaliwa chini ya makubaliano ya pande mbili yaani Serikali ya Tanzania na Serikali ya Japani. Halmashauri ya Wilaya ya Ileje ni moja wa Halmashauri zinazotekeleza mpango ulioandaliwa baada ya mafunzo ya Osaka. Umoja wa Wakurugenzi waliosoma Osaka yaani (TOA) uliichagua Halmashauri ya Wilaya ya Ileje kama kisa mkasa kinachofaa kuonyesha jinsi ambavyo mahitaji halisi na vipaumbele vya jamii vinaweza kushughulikiwa kwa ufanisi kwa kutumia rasilimali zilizopo ndani ya jamii yenyewe na kupitia kujifunza kunakotokana na uzoefu upatikanao katika kutekeleza miradi ya jamii. Ni kisa mkasa cha kipekee kinachowakilisha maendeleo ya jamii asilia yanayoletwa na watu wenyewe, na inawakilisha miradi ya maendeleo inayomilikiwa na kutekelezwa na watu wenyewe.

Japokuwa Halmashauri ya Ileje haijafanikiwa kuchakata mchakato wa fursa na vikwazo kwa maendeleo ya Jamii yaani (O&OD), bado waliweza kubaini vipaumbele vya jamii katika kila Kijiji kwa kutumia mbinu shirikishi. Vipaumbele hivi hufanyiwa mapitio na kuhuishwa kila mwaka.

Tatizo la vivuko kwenye mito inayofurika wakati wa masika lilijitokeza kuwa tatizo la kipaumbele katika mojawapo ya Vijiji vya Halmashauri ya Wilaya ya Ileje. Katika ushirikishwaji, wananchi waliainisha makaravati ya mawe na madaraja ya mawe kuwa ndiyo njia muafaka ya kutatua tatizo la vivuko kwenye mito inayofurika wakati wa masika. Ileje ni mfano wa kuigwa siyo tu kwenye madaraja ya mawe, bali hata kwenye miradi mingine shirikishi ya maendeleo ya jamii. Kwa mfano wananchi wameshiriki kujenga barabara za Vijijini, Zahanati, miradi ya umwagiliaji, miradi ya maji safi na salama na soko la kimataifa la mahindi. Halmashauri ya Wilaya ya Ileje ni mfano mzuri kuhusu matumizi ya fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Viongozi wa kisiasa na watendaji wao husisitiza matumizi ya rasilimali za asili, thamani ya fedha kwenye miradi inayotekelezwa inaonekana bayana. Kutokana na matumizi mazuri ya rasilimali, Halmashauri imekuwa ikipata hati safi isiyo na mashaka toka kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Hata hivyo, katika andiko hili tutajikita kwenye madaraja ya mawe ambayo ni teknolojia muafaka na ya asilia kwa kutatua kero za vivuko nchini.

Halmashauri ya Ileje ni moja ya Hamashauri za Mkoa wa Mbeya uliopo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania. Ni moja ya Halmashauri za pembezoni, Kusini inapakana na nchi ya Malawi, Wilaya ya Kyela upande wa Mashariki, Wilaya ya Rungwe upande wa Kaskazini Mashariki, Mbeya Vijijini upande wa Kaskazini, na Wilaya ya Mbozi upande wa Magharibi. Kiutawala Wilaya hii imegawanyika katika Tarafa mbili, Kata 18 na Vijiji 71. Hali ya mwiinuko wa ardhi inaweza kugawanyika kwenye kanda kuu mbili nazo ni ukanda wa juu wa milima ya Undali hususan Tarafa ya Handali na ukanda wa chini

mabondeni Tarafa ya Bulambya. Milima ya Undali ni maarafu kwa kilimo hai, na uzalishaji wa kahawa ya daraja la "A", migomba, iliki, mbao na mazao yatokanayo na ngombe wa maziwa. Hali ya hewa ya maeneo haya ni ya ubaridi. Kuhusu utalii, kwenye milima ya Undali anapatikana aina adimu ya Mbega mweupe. Milima hii ndiyo chanzo cha mito mingi inayomwaga maji yake kwenye mto mkuu Songwe, ambao humwaga maji yake kwenye ziwa Nyasa. Kutokana na wingi wa mito hii, hasa wakati wa masika, uvukaji kutoka upande mmoja kwenda upande mwingine ni changamoto kubwa inayowakabili wananchi wanaoishi maeneo hayo, na kwa Halmashauri ya Ileje. Kwenye milima hii pia kuna utajiri mkubwa wa mkaa wa mawe kiasi cha tani milioni 100 zimelala kwenye mlima Kaguru zamani ukiitwa mradi wa makaa ya mawe Kiwira. Yapo maanguko kadhaa ya maji ambayo yanatosha kuzalisha umeme wa maji wa kiwango cha kati au cha chini. Maarufu kati ya maanguko haya ni yale ya Ruswisi na Isoko. Wamisionari wa Kimoravia wanazalisha umeme kutokana na maanguko ya Isoko na kutoa huduma ya umeme kwa Vijiji na taasisi zinazozunguka eneo hili.

Ukanda wa chini ni eneo lote la Tarafa ya Bulambya, hupatikana Kusini na Kusini Magharibi na ni maarufu kwa kilimo cha mahindi, maharage, alizeti na biashara ya mpakani kati ya Malawi na Tanzania. Kutokana na ukweli kwamba Wilaya hii ni miongoni mwa Wilaya za pembezoni, Ileje imebaki nyuma kimaendeleo hususan kwenye miundombinu, fursa za biashara na viwanda vya kuongeza thamani ya mazao. Matokeo yake, Ileje ni miongoni mwa Wilaya fukara sana mkoani Mbeya na nchini kwa ujumla.

Kulingana na kauli ya Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo Mh. Mohamed Mwala, Ileje iko pembezoni na ina hali mbaya ya kiuchumi. Kwa kutambua hili, wananchi wa Ileje walilazimika kuwa wabunifu na ving'ang'anizi katika kufukuzia fursa za maendeleo. Kwa kutambua fursa walizo nazo, wananchi walitekeleza kwa ushirikiano miradi kadhaa ya maendeleo ili kukidhi haja za wananchi. Mfano wamejenga Zahati, barabara za Vijijini ambazo haziko chini ya Wakala wa Barabara nchini (TANROAD) ili kuhakikisha Vijiji vinafikika. Wamejenga barabara za Ibaba, Malangali, Luswisi na Mbege. Halmashauri imeweza kuvutia mradi wa Soko la Kimataifa pale Isongole mpakani na Malawi. Soko hili hutoa fursa kwa wakulima wa mahindi wa Ileje, Wilaya za karibu na Wilaya ya Chitipa nchini Malawi. Soko hili limekaa ki-mkakati kwani hutumiwa pia na Wakala wa hifadhi ya chakula nchini (SGR). Mahindi yanayouzwa hapa yanasafirishwa kwenda DRC Kongo na Zambia. Kupitia soko hili Halmashauri hupata ushuru wa mazao, idadi kadhaa ya wananchi wanapata ajira na bishara ndogondogo zimeshamiri. Hata hivyo, miundombinu ya barabara na madaraja ni changamoto kubwa, na ndiyo maana madaraja ya mawe yanayojengwa na jamii ni ya muhimu sana.

## 2.0 TATIZO LILILOKUWEPO KABLA YA UJENZI WA MADARAJA YA MAWE

Kama ilivyoelezwa kwenye utangulizi, hali ya nchi ya Halmashauri ya Ileje ni milima, mabonde na makorongo marefu ambayo husabisha matatizo mengi katika uvukaji wa mito wakati wa masika kutoka Kijiji kimoja kwenda kingine. Mfano Vijiji vya Kikota na Ibeta viko kwenye Kata ya Ikinga na vimetengwa na mto Shija. Kabla ya mwaka 2010,

watu wa Vijiji hivi walikuwa wanapata matatizo makubwa kuvuka mto Shija. Ilikuwa vigumu kupata huduma za kijamii na kiuchumi na usafirishaji wa bidhaa za ndizi, maharage na mbao. Pia ilikuwa shida kufikia huduma za Soko, Shule, Vituo vya Afya na Zahati. Matukio mawili ya vifo yaliwahi kutokea wakati watu wakijaribu kuvuka mto uliofurika. Ama kwa hakika, tatizo hili halikuwa kero kwa Vijiji hivi viwili pekee, bali kwa Halmashauri nzima, kwani hakukuwa na njia mbadala ya kuvuka mto Shija. Changamoto hii iliwasukuma wananchi kukusanya nguvu zao na kuzielekeza kwenye kuweka vipaumbele na kisha wakaazimia kujenga vivuko vya kudumu.


**3.0 LENGO**

Lengo la wananchi lilikuwa kujikwamua na tatizo la mawasilano ya vivuko kati ya Kijiji cha Kikota na Ibeta pamoja na Kata zinazovizunguka kwa kujenga daraja la kudumu la mawe.

## Kisanduku 4.1: Daraja la mawe ni nini?

- Kwa karne nyingi, madaraja ya mawe yamekuwepo kwa asili kutokana na maji kumomonyoa miamba laini iliyo chini ya mito, kuacha miamba migumu juu na kutengeneza daraja la asili mfano wa upinde. Warumi wa zamani kwa kuona hili waliasili teknolojia hii ya asilia zaidi ya miaka elfu mbili iliyopita.
- Madaraja ya mawe yenye sura ya upinde yanapendelewa zaidi duniani kwa sababu yana uwezo mkubwa wa kuhimili uzito , ni madhubuti na yanadumu kwa muda mrefu ukilinganisha na madaraja ya mlazo yanayojengwa kwa nondo. Madaraja ya namna hii yaliyojengwa mamia ya miaka iliyopita bado yamesimama na yanatumika sehemu mbalimbali duniani. Ni rahisi kulitambua daraja la aina hii kwani lina nguzo zake zilizosimikwa kwenye mwamba mgumu kila upande, lina sura ya upinde na halijajengwa kwa nondo wala zege.
- Madaraja haya hujengwa kwa mawe, mchanga na sementi nyingi kuliko kawaida. Kutokana na sura ya upinde, mzigo unapopitishwa juu ya daraja hili, uzito haubonyezi katikati kama ilivyo madaraja ya mlazo, bali uzito hugawanyika mara mbili na kuhamia kwenye kuta za pembeni na kuishia kwenye mwamba mgumu ulioko chini ya mto husika ona  mchoro 4.1.Katika ujenzi, mafanikio hutegemea na ustadi wa kuliweka jiwe kuu la katikati angalia mchoro na  4.2.






Mchoro 4.1: Daraja la mawe mfano wa upinde kuonesha kuta na uwekaji wa jiwe kuu. Mchoro 4.2: uwekaji wa Jiwe kuu la kati ili kulipa daraja uhimili unaotakiwa.

**Kisanduku 4.2: Kwa nini daraja la mawe lina sura ya upinde?**

Watu wa Ileje waliamua kujenga madaraja ya mawe yenye sura ya upinde kwani ndiyo teknolojia muafaka kwao kutokana na mambo yafuatayo:

- **Lina Nguvu**: kutokana na uzoefu uliopatikana baada ya ujenzi wa madaraja madogo ya aina hii yaliyojengwa na kasisi wa Kanisa Katoliki miaka ya 1970, yamedhihirisha kwamba yana nguvu sana na yanahimili uzito mkubwa ikilinganishwa na madraja mlazo yanayojengwa kwa nondo na zege.
- **Kudumu muda mrefu**: ushahidi uliopo duniani unaonyesha kwamba madaraja haya yanadumu muda mrefu.
- **Ujenzi rahisi**: madaraja ya mawe sura ya upinde hayahitaji ujuzi mkubwa wala utaalamu wa kutoka nje.
- **Gharama ndogo**: Ni ya bei nafuu na hupunguza gharama kwa 50% kuliko madaraja ya zege na nondo
- **Matumizi ya rasilimali za asili**: hujengwa kwa kutumia rasilimali zilizopo eneo husika kama vile mawe, mchanga, sementi na rasilimali watu.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Kwanza iliandaliwa mikutano ya uhamasishaji kati ya wananchi wa Vijiji vya Kikota na Ibeta, wataalamu na viongozi wa Halmashauri. Lengo la mikutano hii ilikuwa ni kujadili namna ya kutatua tatizo la vivuko. Matokeo ni kwamba baada ya kubadilishana mawazo, kwa pamoja jamii waliamua kujenga madaraja ya mawe ya kudumu yenye sura ya upinde badala ya yale ya muda ya kuning'inia yaliyojengwa kwa kamba.

**Ushiriki wa wadau**

Eneo la kujengwa kwa daraja kwenye mto Shija lilichaguliwa kwa ushirikiano kati ya wataalamu wa DANIDA chini ya mpango wa DADPs. Jamii iliamua kukusanya mchanga na mawe. Halmashauri ilitoa usafiri na mafundi mchundo kutoka miongoni mwa Vijiji husika walifanya kazi za uashi. Wataalamu wa Halmashauri walikuwa na jukumu la kusimamia shughuli za ujenzi wa daraja. Katika mchakato wa ujenzi mafundi mchundo walijenga stadi za ujenzi wa madaraja ya mawe, yenye sura ya upinde. Vifaa vya ujenzi vilitolewa na walengwa wa mradi huu, huku misaada ya kifedha kununua vifaa ambavyo havipatikani kwenye jamii husika mfano sementi ikitolewa na Halmasahuri na DANIDA. Jambo lililosisitizwa hapa ni ushirikiano wa wadau wa ndani na wadau wa nje mfano Kaya, Serikali za Vijiji, Halmashauri, DANIDA na DASP.

**Kutambua na kutumia rasilimali za asili zilizopo kwenye jamii na uwezo wa utendaji**

Kutokana na kuwa pembezoni, Halmasahuri ya Ileje ililazimika kuutumia vizuri uwezo na ujuzi wa wahandisi wazalendo walio kwenye Halmashauri na mafundi mchundo toka Vijijini. Katika

kutekeleza azma hii, Halmashauri ilivitambua rasmi vikundi vitatu vya mafundi mchundo tayari kwa usajili. Hivi ni vikundi vilivyoundwa na mafundi wenyewe kwa ridhaa na uwezo wao wa kujipanga na vimekaa kimkakati ili kutekeleza kazi ndogondogo ambazo haziwavutii makandarasi wakubwa; na mafundi hawa wamedhihirisha kwamba wanaweza. Kikundi kimojawapo kwa jina la SHITUPOKA ikimaanisha "yetu kwa pamoja" kilipewa kazi ya kumalizia ujenzi wa nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa zilizokuwa zimetelekezwa na makandarasi. Vikundi hivi pia vinapewa kazi ya kukarabati sehemu zilizoharibika za barabara za Halmashauri kwa nia ya maendeleo asilia. Dhana ya kutambua hivi vikundi vya mafundi mchundo inakwenda kulingana na mkakati wa Bodi ya usajili ya Makandarasi nchini(CRB). Kwa mujibu wa miongozo ya CRB, vikundi vya mafundi mchundo vitasajiliwa tu pale vitakapohakikisha kwamba kuna angalau mmoja wao mwenye cheti cha fundi mchundo yaani *Full Technician Certificate (FTC)* kutoka vyuo vya ufundi vinavyotambulika.

## 5.0 RASILIMALI ZILIZOTUMIKA

Mchango wa kila mdau umeoneshwa kwenye jedwali 1. Jamii ilichanga 9% kwa kuthaminisha vifaa na nguvu kazi mfano (nguvu kazi, mawe, mbao na mchanga). Halmashauri ilichanga 56% kwa kulipa mishahara, fedha za kujikimu, sementi, kokoto na misumari, waya na usafiri. Msaada kutoka nje wa DANIDA ni sawa na 35%, na hii ilijumuisha gharama za mafunzo na uhamasishaji kama ilivyo kwenye Jedwali 4.1.

**Jedwali 4.1: Mchango wa wadau mbalimbali**

| MCHANGO WA WADAU | KIASI TZS | % |
|---|---|---|
| DADPs/DANIDA | 7,328,000/= | 35 |
| Jamii/Walengwa | 1,832,000/= | 9 |
| Halmashauri ya Ileje | 11,598,600/= | 56 |
| JUMLA | **20,758,000/=** | 100 |

**Chanzo: Halmashauri ya Wilaya ya Ileje 2011**

## 6.0 MATOKEO

Mwaka 2010 daraja la mawe la bei nafuu na lenye sura ya upinde lilijengwa kukatiza mto Shija na kuunganisha Vijiji vya Kikota na Ibeta. Watu wa pande zote mbili 3,010 kutoka Kikota na 1,070 toka Ibeta sasa wanaweza kukatiza na kuuza bidhaa zao za kilimo mwaka nzima bila hofu. Uwepo wa daraja hili ni mwanzo wa kufufua shughuli za kiuchumi kwenye Kata ya Ikinga hususani Vijiji vya Kikota na Ibeta. Daraja hili linaweka mawasiliano ya uhakika kwa mtandao wa barabara kwenda Wilaya za jirani mfano (Kyela na Rungwe) na kuziendea huduma za afya kwenye Hospitali teule ya Isoko, Shule ya sekondari Kafule na kwenye minada. Inategemewa katika siku za mbeleni litainua uchumi na elimu, kupunguza umaskini na kisha kuinua kiwango cha umri wa watu kuishi uwe zaidi miaka 51 ya sasa.

Bei ya daraja hili imedhihirika kwamba ni ya chini kuliko madaraja ya zege na nondo. Kwa mfano daraja la mita 18 la Kikota liligharimu TZS. 20,758,000 in sawa na (40.7%) chini kuliko

daraja la mita chache ( 8 tu) la zege na nondo la Kata ya Luswisi kukatiza mto Makoga lililogharimu TZS.35,000,000/=. Kutokana na unafuu huu, Halmashauri imejenga madaraja mengine ya namna hii kama ilivyo kwenye Jedwali 4.2.

**Jedwali 4.2: Ileje- Idadi ya madaraja ya mawe yaliyojengwa tangu 2005**

| Kata | Idadi ya madaraja |
|---|---|
| Ikinga | 1 |
| Kalembo | 1 |
| Chitete | 2 |
| Itumba | 1 |
| Jumla | 5 |

**Chanzo: Halmashauri ya Wilaya ya Ileje, 2011**

Mafundi mchundo, wahandisi wazalendo na mafundi wengine waliohusika katika ujenzi huu wamefaidika sana kwa kupata uzoefu na stadi za kujenga madaraja ya mawe katika utekelezaji wa mradi huu. Sasa hawa ni rasilmali ya Taifa na wataweza kutumika kwenye halmashauri nyingine nchini ambazo zitahitaji ujuzi na uzoefu wao.

**Kisanduku 4.3: Maoni ya wadau**

**Mwenyekiti wa Halmashauri, Mh. Mohamed Mwala** ..“aina hii ya madaraja ni muafaka kwa mazingira yetu, na kwa kweli natamani kama ningelikuwa na uwezo basi yangejengwa sehemu zote yanakohitajika hapa Halmasahuri ya Ileje. Ni ya bei nafuu, yanadumu na ni rahisi kuyajenga…”

**Fundi Mchundo Bwn. Lusubiro Swila …** “madaraja haya yana nguvu sana na pengine yanafaa sana kujengwa ya urefu mfupi yaani kwenye (mito miembamba)..”

## 7.0 CHANGAMOTO ZA MADARAJA YA MAWE SURA YA UPINDE

Ujenzi wa madaraja ya mawe sura ya upinde yanahitaji usimamizi wa karibu sana. Pale chini kwenye msingi ambapo uzito wa daraja utalalia ni lazima pachaguliwe kwa uangalifu na lazima pawe na mwamba mgumu. Ujenzi ukishaanza, ni lazima uendelee hadi umalizike bila kukoma; na hii inamaanisha kwamba rasilimali zote na vifaa vya ujenzi lazima vikusanywe mapema. Madaraja haya yanahitaji idadi kubwa ya mawe yenye ukubwa na sura ya kufanana. Pale ambapo mawe hayapatikani karibu, gharama inaweza kuongezeka kwa sababu ya usafiri. Panahitajika mafundi waashi wanne kwa wakati mmoja, mmoja kila kona ya daraja. Kwa vile hakuna nondo, mchangayiko wa mchanga utahitaji kiwango cha sementi nyingi kuliko ile ya kawaida.

## 8.0 MIKAKATI YA UENDELEVU

Halmashauri ya Wilaya ya Ileje imetenga fedha ya ukarabati wa mara kwa mara wa madaraja haya. Uongozi na jamii husika umeonesha dalili za umiliki wa mradi na wako tayari kuyalinda madaraja haya. Halmashauri imekuwa ikijenga uwezo wa wadau ngazi mbalimbali kama ilivyooneshwa hapo juu. Kwa sasa, kuna watumishi wanne kwenye Halmashauri wenye stashahada ya juu ya Mipango Miji, mafundi mchundo watano kwenye Idara za Maji, Umwagiliaji na Ujenzi. Kuna mafundi mchundo saba waliobobea kwenye ujenzi wa madaraja ya mawe na vikundi vitatu vimeundwa tayari kutambuliwa na bodi ya makandarasi. Kiasi cha 59% ya Kata zote zina Maafisa Ugani wa Kilimo, Mifugo, Maendeleo ya Jamii, Misitu ambao hufanya shughuli mtambuka katika ngazi za msingi.

## 9.0 SIRI YA MAFANIKIO NA MAMBO YANAYOFAA KUIGWA

Kwa mujibu wa maelezo ya Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ileje, siri ya mafanikio ni ubunifu wa wananchi wenyewe. Baada ya kujitambua kwamba wanakabiliwa na madhara ya kuwa pembezoni mwa nchi, jamii ilijizatiti kushughulikia kero za msingi na kuweka vipaumbele kwa kuzingatia uhalisia. Kulikuwepo na uongozi shupavu katika kila ngazi iliyohusika. Zaidi ya yote kulikuwa na mahusiano ya amani baina ya jamii, kaya na miradi ya maendeleo. Ushirikiano wa dhati kati ya Idara mbalimbali za Maendeleo ya Jamii, Mipango, Kilimo na Mifugo, ulisaidia sana kwenye mafanikio yanayoonekana:

(i) Ushirikiano wa jamii, asasi za kiraia, watumishi wa Halmashauri, ulikuwa imara sana. Pia kulikuwa na ushirikiano na programu za maendeleo kama vile DADPS, TASAF na vikundi vya kujitolea kama vile kikundi vya mafundi mchundo.

(ii) Kushirikiana kwa Idara za Halmashauri kama Maendeleo ya Jamii na Ofisi ya Mhandisi wa Wilaya kulikuwa ni kwa muhimu kwani wakati mwingine ililazimu kuchangiana rasilimali kama vile usafiri.

(iii) Kamati ya Menejimenti yaani CMT ilidhamiria kuona shughuli za maendeleo zinaendelea vizuri na walikuwa na motisha toka ndani yao wenyewe kutaka kufikia malengo.

(iv) CMT ya Ileje ilitumia vyema rasilimali zilizopo, uzoefu wa watu wao, na stadi ili kujiletea maendeleo yao wenyewe. Ushirikishwaji wa mafundi mchundo kwenye kazi ndogondogo ulisaidia kuleta ushiriki wa kweli na haki wa jamii.

(v) Halmashauri ya Ileje imepata kujifunza maarifa, ujuzi na uzoefu utokanao na kutekeleza miradi ya jamii. Kwa sasa wana kundi la wazoefu wa kujenga madaraja ya mawe. Halmashauri nyingine nchini zinaweza kuwatumia wazoefu hawa kuwajengea madaraja ya mawe sura ya upinde na pia ingefaa Halmashauri nyingine zifanye ziara ya mafunzo kujifunza maendeleo kwa kutumia rasilimali zilizoko kwenye jamii asilia.

(vi) Mwisho ni mwitikio na ushiriki wa dhati wa jamii, asasi za kiraia, asasi za dini, Halmashauri, DADPS, na TASAF. Nguvu hii ya pamoja ilikuwa na inaendelea kuwa msingi wa mafanikio katika ushirikishwaji wa jamii katika utoaji wa huduma.

# HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

## UKUSANYAJI NA UDHIBITI BORA WA TAKA NGUMU




*CHASAMA- WAKALA WA KUKUSANYA TAKA NGUMU*

## 1.0 UTANGULIZI

Jiji la Mwanza lipo kusini mwa fukwe za Ziwa Victoria, Kaskazini-Magharibi mwa Tanzania. Jiji hili lina ukubwa wa $Km^2$1,325 kati ya hizo $Km^2$ 900 zimefunikwa na maji na zilizobaki $km^2$ 425 ni nchi kavu. Wastani wa $Km^2$ 86.8 ni eneo la mji na zilizobaki zimefunikwa na misitu, mabonde, mashamba yanayolimwa, ukanda wa nyasi na milolongo ya vichuguu vya mawe na majabali.

Kiutawala, Mamlaka ya Jiji imegawanyika kwenye Wilaya mbili nazo ni Nyamagana na Ilemela. Jiji lina kata 21 kati ya hizo 12 ziko Nyamagana na kata 9 ziko Ilemela. Kulingana na matokeo ya sensa ya taifa kuhusu watu na makazi ya 2002, Jiji la Mwanza lilikuwa na watu 476,646 kati yao 210,735 wanaishi Wilaya ya Nyamagana na 265,911 wanaishi Wilaya ya Ilemela. Kwa sasa inakadiriwa kwamba Jiji la Mwanza lina jumla ya watu wapatao 800,000 na kasi ya kukua kwa idadi ya watu ni 3.2%. Jiji linapata wahamiaji wengi toka Vijijini kwa kiasi cha 8% kila mwaka. Wingi wa watu kwa eneo ni watu 134 kwa kilomita ya mraba, ikiwa ndilo Jiji la pili lenye ujazo mkubwa wa watu kwa eneo baada ya Jiji la Dar es Salaam.

Kwa kuwa Jiji la Mwanza lina idadi kubwa ya watu kwa eneo, vivyo hivyo huzalisha taka ngumu na maji taka kwa wingi. Mandhari ya Jiji hili lililojaa vichuguu vya mawe na majabali husababisha ugumu katika zoezi zima la Mipango Miji na mifumo ya kukusanya na kutupa takataka. Ikumbukwe kwamba, kwa mujibu wa kanuni za uhifadhi mazingira, Ziwa Victoria linapaswa kuwa safi na bila mazingira yake kutoharibiwa kwa namna yoyote ile. Ili kuhifadhi uasilia wa ziwa hili na makazi ya viumbe waliomo, basi kazi ya kukusanya na kutupa taka ndani ya Jiji inapaswa kufanyika kwa tahadhari kubwa.

Kwa kuwa hii ndiyo hali halisi, Jiji la Mwanza lina Idara inayoshughulikia masuala ya Afya na Mazingira ikijumuisha vitengo vya: Afya ya Jamii, Hifadhi ya mazingira; na Kitengo cha Kukusanya na kutupa taka. Vitengo vyote vinasimamiwa na watumishi wenye utaalamu na stadi za kutosha, kufuatilia shughuli za kila siku na kuwawajibisha wadau mbalimbali wanye wajibu wa kuhakikisha kwamba Jiji liko safi, na bustani zake zinavutia. Ili kuhakisha kwamba mitaa yote ya Jiji inakuwa safi na inakuwa na bustani nzuri na za kupendeza, Jiji linawahusisha kaya, sekta isiyo rasmi ya wafanyabiashara ndogondogo, makampuni kwenye sekta binafsi, taasisi za umma, asasi za kiraia na kampuni ya “Sherifu”. Sherifu ni kikosi cha wadau toka makampuni binafsi wanaozunguka Jijini kukagua, kuwavizia, kuwakamata na kuwawajibisha wanaochafua Jiji.

## 2.0 TATIZO LILILOKUWEPO KABLA YA UDHIBITI BORA WA TAKA NGUMU

Kati ya miaka ya 1990 na 2000, idadi ya watu kwenye Jiji la Mwanza iliongezeka kwa kasi kubwa. Ilipofika mwaka 2000 Jiji la Mwanza lilishuhudia kuongezeka kwa watu waliovamia na kuishi kwenye makazi yasiyopimwa hususan kwenye vilima na majabali yanayozunguka Jiji, ambamo kuna mamia ya kaya. Vilima vilivyoko Jijini Mwanza vinahifadhi idadi kubwa ya wakazi wanaoishi kwenye ardhi isiyopimwa na ambayo kwa kweli siyo viwanja rasmi. Wakati huo huo eneo na idadi ya watu washio kwenye makazi yaliyopimwa rasmi imeongezeka mara dufu. Ongezeko kubwa la watu waishio na wale wanaoingia na kutoka kila siku limesababishwa na




vivutio vingi vya kiuchumi vilivyoko Jijini Mwanza kama vile uvuvi, madini, biashara za jumla na rejareja. Ongezeko kubwa la taka zinazozalishwa kila siku ni matokeo ya kukua kwa shughuli za kiuchumi kama vile viwanda, mahoteli, taasisi za mafunzo, taasisi za umma, biashara za watu binafsi na sekta isiyo rasmi katika kipindi hicho kifupi.

Ongezeko la watu na shughuli hizi za kiuchumi kwenye miaka ya 2000 limepelekea ongezeko la uzalishaji wa taka ngumu kwa kiasi cha tani 220 kwa siku. Kwa bahati mbaya, ongezeko hili la taka halikwenda sambamba na uwezo Jiji wa kukusanya na kusafirisha na kuzihifadhi taka kwenye maeneo ya dampo. Kiasi cha taka ngumu kiliongezeka hadi kufikia tani 72 kwa siku. Kwa maneno mengine, hata zile taka ngumu zilizozalishwa kwa siku kwenye Wilaya ya kibiashara katikati ya Jiji, ilikuwa ni vigumu sana kuzikusanya na kusafirisha zote. Maeneo mengi ya Jiji yalijaa marundo ya takataka hasa kwenye vituo vya kukusanya taka. Masalia ya taka zilizooza, taka za plastiki na mifuko ya plastiki zilizagaa kila mahali.

Kwa upande mwingine Jiji lilikuwa halijatunga sheria ndogo zenye makali ya kudhibiti uzalishaji, uchambuzi, kukusanya, kusafirisha na kutupa taka ngumu. Idara husika ya Afya na Maziningira ilikuwa na watumishi wachache sana, yaani watumishi 58 tu na hii ilijumuisha Maafisa na watumishi wengine wanaohusika kudhibiti usafi na ukusanyaji taka kwenye Jiji lote na viunga vyake. Mwisho, Idara hii ilikuwa na malori matatu tu ya kusomba taka, vifaa chakavu; zaidi ya yote, jamii, kaya na wafanyabiashara na wenye viwanda walikuwa hawana habari kwamba wanapaswa kuwajibika ipasavyo kwa taka walizozalisha wenyewe na kuliweka Jiji safi na la kuvutia. Ndiyo maana haikushangaza kwamba hadi kufikia mwaka 2000, Jiji la Mwanza lilikuwa chafu sana na lilikuwa halivutii hata kidogo.

**3.0 MALENGO**

Ilipofika mwaka 2000, Menejimenti ya Jiji ilibaini tatizo hili la taka na kuamua kuweka dira/malengo mapana yaliyosomeka kama ifuatavyo; Jiji la Mwanza litakuwa“Jiji safi na la kuvutia kupitia uwepo wa mfumo dhabiti wa ukusanyaji na utupaji taka”. Malengo mahsusi yalikuwa kwamba, ili kuweka Jiji safi na la kuvutia ni lazima (i) Kutunga na kutekeleza sheria ndogo kuhusu huduma za ukusanyaji, usafirishaji na kutupa taka (ii) Kuongeza kiasi cha taka kinachokusanywa na kutupwa na (iii) kuongeza uelewa wa jamii kuhusu masuala yanayohusu ukusanyaji, usafirishaji na utupaji taka ngumu.

**4.0 MIKAKATI YAUTEKELEZAJI**


Menejimenti ya Jiji iliandaa programu kabambe yenye kuainisha kwa undani na bayana shughuli zitakazo tekelezwa ili kufikia malengo ya kuweka Jiji safi na la kuvutia.  Shughuli ya kwanza ilikuwa ni kutunga sheria ndogo kuhusu ukusanyaji na utupaji taka na kuhakikisha kwamba

inatekelezwa ipasavyo. Kuhusu jambo hili, ilipofika mwaka 2000 Halmashauri ya Jiji la Mwanza ilitunga na kuanza kutekeleza sheria ndogo kuhusu ukusanyaji na utupaji taka. Sheria hii ndogo iliingiza kipengele cha ushiriki wa jamii na sekta binafsi kama suluhisho la kuleta ufanisi katika zoezi zima la ukusanyaji na utupaji taka. Kabla ya kutekeleza sheria hii ndogo, palifanyika mashauriano na mikutano mingi ya pamoja ili kuimarisha utayari wa jamii kulipia gharama za huduma za kuzoa na kutupa taka inayotolewa katika Kata zote mjini. Mwishowe ilikubalika kwamba gharama itakayotozwa kwa kaya kwa ajili ya huduma hii ni TZS 800 kwa mwezi. Hata hivyo, sheria ndogo ya mwaka 2000 haikugusia vya kutosha kuhusu ushiriki wa sekta ya viwanda mbayo inakua kwa kasi, biashara za jumla na taasisi za umma kwenye uzalishaji, ukusanyaji na kutupa taka.

Mwaka 2007, Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza alihudhuria mafunzo kule Osaka Japani na aliporudi akaanda warsha ya mafunzo hapa Mkoani ili kutoa mrejesho kuhusu mambo mapya aliyojifunza na yanayofaa kuigwa kutokana na mafunzo ya Osaka. Kati ya mambo yaliyofaa kuigwa na kuwekwa kwenye mpango kazi wa Jiji la Mwanza uliosomeka “Uboreshaji na uhifadhi wa mazingira” yalikuwa ni uboreshaji wa mazingira uliolenga usafi, unadhifu huku uhifadhi wa mazingira ukilenga kulinda na kutunza mazingira ya Jiji.

Mpango kazi huu uliotokana na mafunzo ya Osaka uliharakisha kutungwa na kutekelezwa kwa sheria ndogo mpya ya mwaka 2010 kuhusu ukusanyaji na utupaji taka. Sheria ndogo mpya iliruhusu kutoza faini ya papo kwa hapo ya TZS 50,000 kwa mtu yeyote, kaya, jengo la biashara au taasisi au asasi itakayekamatwa kwa kushindwa kuwajibika na sheria ya kukusanya na kutupa taka ngumu. Sheria hii iliruhusu uanzishwaji wa kitengo cha kushughulikia kesi zinazohusu usafi na mazingira ndani ya Idara ya Afya na Mazingira. Pia iliruhusu kuwepo kwa Sherifu, ambaye wajibu wake ni kudhibiti utupaji taka usiozingatia sheria na kukamata wachafuzi wa mazingira. Sherifu ana wajibu wa kukusanya faini kutoka kwa wale wanakiuka sheria ya usafi na mazingira.

Halmashauri ya Jiji ilihakikisha kwamba Jiji linapata zana na vifaa vya kutosha na kuaminika vya kuzoa taka, watendaji wenye ujuzi na muundo muafaka wa utendaji kazi. Mfano mwaka 2002, Halmashauri ilichukua jukumu la kuihusisha sekta binafsi katika zoezi la kukusanya na kusafirisha taka; pia ilinunua malori mapya na kufanya Jiji kuwa na jumla ya malori 5 ya kuzoa taka..




*Baadhi ya malori ya kuzoa taka na mtambo wa kupakia taka ngumu*

Ili kazi ya usafi ifanyike kwa ufanisi, Jiji liligawanywa kwenye kanda tatu za kuzolea taka ambazo ni kanda ‘A’, ‘B’ na ‘C’. Kanda ‘A’ inajumuisha Kata 6 zilizoko kwenye “Wilaya ya Kibiashara ya Katikati ya Jiji” (CBD) nazo ni: Pamba, Nyamagana, Isamilo, Mirongo, Mbugani na Kirumba. Kanda hii hupata huduma toka kwa makampuni binafsi (Sherifu) ambayo husafisha, hufagia barabara zilizopo, kuondoa maji yaliyotuama, kusomba taka ngumu na kuzipeleka dampo bila ruzuku ya Serikali. Makampuni haya (Sherifu) hufidia gharama zao kwa kutoza kodi ya huduma kwa wale wanaofaidi huduma hizo na faini zinazotozwa kwa wanaokiuka sheria ndogo kuhusu usafi na mazingira.




**OFISI YA SHERRIF KATA ILIYOKO BARABARA YA PAMBA**

Kanda ‘B’ inajumuisha Kata 4 yaani Kitangiri, Nyamanoro, Pasiansi na Nyakato. Mawakala katika kanda hii ni asasi za kiraia (CBOs). Wanawajibika kusafisha na kuchukua taka toka zinapozalishwa na kuzikusanya kwenye vituo maalumu vilivyotengwa. Kutoka kwenye vituo hivi, malori ya Jiji hupakia taka ngumu na kuzisafirisha hadi kwenye dampo zinakofukiwa. Asasi hizi za kiraia hulipwa ruzuku kwa mwezi kulingana na ukubwa wa eneo wanalohudumia kila siku.

Kanda 'C' hujumuisha kata 8 za pembezoni mwa Jiji ambazo ni Igogo, Mkuyuni, Butimba, Mkolani, Buhongwa, Ilemela, Mahina na Igoma. Katika kata hizi, mawakala hukusanya taka ngumu kutoka majumbani na toka kwa wazalishaji wengine na kuzirundika kwenye vituo maalumu vilivyotengwa kwa ajili ya kukusanyia taka. Mawakala hawa hulipwa ruzuku ya kila mwezi kutokana na ada za huduma zinazolipwa na walengwa wa majumbani na wale wa kwenye maeneo ya wazi na ya biashara.



*Picha hii inawaonesha wanachama wa Asasi ya Kiraia Nyakato wakiwa kazini*

**Jedwali 4.3: Orodha ya mawakala na maeneo wanayohudumia**

| Na | KAMPUNI/ CBO | ENEO LA KAZI/KATA |
|---|---|---|
| **1.** | CHASAMA | PAMBA, MIRONGO NA ISAMILO |
| **2.** | ALLY-AKRABI ENTERPRISES | NYAMAGANA NA MBUGANI |
| **3.** | MEMCO | KIRUMBA |
| **4.** | MAENDELEO MBUGANI | MKOLANI NA BUHONGWA |
| **5.** | BORESHA MAZINGIRA | BUTIMBA |
| **6.** | HIMAJA | MKUYUNI |
| **7.** | KENYAGESI IGOGO | IGOGO |
| **8.** | TUFUMA | NYAKATO 'B' |
| **9.** | UZOTA | NYAKATO 'A' |
| **10.** | MKUWA | IGOMA |
| **11** | MUFAJUS | MAHINA |
| **12.** | CHARITY ORGANIZATION | KITANGIRI |
| **13.** | WAJANE | NYAMANORO 'A' |
| **14.** | MAENDELEO MKUDI | NYAMANORO 'B' |
| **15.** | PATUMA | PASIANSI |
| **16.** | GILGAL | ILEMELA |

**Chanzo:Halmashauri ya Jiji la Mwanza, 2011**

Kama tulivyoona hapo juu, huduma za kuzoa taka kwenye kanda B na C, hufanywa na makampuni binafsi yakishirikiana na asasi za kiraia kama ilivyo kwenye jedwali hapo juu, na hawa huzirundika taka kwenye vituo maalumu 32. Hadi kufikia Julai 2012 Jiji lilikuwa na mapipa 250 ya kutupa taka yakiwa yamepangwa kwenye mitaa (Street) mbalimbali ili kuzuia raia wasitupe taka ovyo na kuchafua Jiji.




***Mapipa ya taka mtaani na Vidampa (skip bucket) vya kukusanyia***

**Jedwali 4.4: Vituo vya kukusanyia taka**

| Na | Vituo vya kukusanyia taka kwa kila kanda | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Kanda A** | | **Kanda B** | | **Kanda C** | |
| | **KITUO** | **KATA** | **KITUO** | **KATA** | **KITUO** | **KATA** |
| **1.** | Soko kuu | Pamba | Kwa Msuka | Nyamanoro | Igogo sokoni | Igogo |
| **2.** | Mission | | Ghana quarters | | Mchafukoge | |
| **3.** | Bugarika | | Soko la Kitangiri | Kitangiri | Mkuyuni | Mkuyuni |
| **4.** | Makoroboi | Nyamagana | Pasiansi | Pasiansi | Mkuyuni sokoni | |
| **5.** | Custom | | Buzuruga | Nyakato | Butimba corner | Butimba |
| **6.** | Capri point | | Soko la Mwendesha | Mahina | Nyegezi corner | |
| **7.** | Zimamoto | | Nyakato nundu | Nyakato | Nyegezi bus terminal | |
| **8.** | Seth Benjamin | Mbugani | | | Mkolani | Mkolani |
| **9.** | Mabatini sokoni | | | | SAUT (University) | |
| **10.** | Mlango mmoja | | | | Buhongwa market | Buhongwa |
| **11.** | Community center | Mirongo | | | Ilemela | Ilemela |
| **12** | Furahisha | Kirumba | | | Sabasaba market | |
| | | | | | Igoma | Igoma |

**Chanzo:Halmashauri ya Jiji la Mwanza, 2011**

Kwa sasa, usafirishaji taka toka vituo vyote 32 vya kukusanya hufanyika kwa kutumia malori 8 ya Jiji na mengine 8 ya mawakala binafsi kama ilivyooneshwa kwenye jedwali hapo juu. Taka hizi hupelekwa kwenye dampo lililopo Buhongwa na kufukiwa huko. Kazi nyingine muhimu inayofanywa na Halmashauri ya Jiji ni kupunguza taka kwa njia ya kuchambua, kutenga na kurudisha baadhi ya taka kwenye matumizi mengine na kuangamiza zile ambazo hazihitajiki.
Mchakato huu unafanyika kama ifuatavyo;

(i) Kupunguza taka hatarishi zitokanazo na Vituo vya Afya kwa njia ya kuziangamiza kwa moto hadi kuwa majivu kwenye matanuru 42 yaliyoko kwenye vituo Vyote vya Afya. Njia hii huweza kupunguza taka toka Vituo vya Afya kwa 80%.

(ii) Kila siku kiasi cha tani 1.5 ya taka za plastiki hukusanywa na kurudishwa kwenye matumizi. Wapo watu binafsi wamejiajiri kukusanya taka za plastiki na kuziuza kwa wanunuzi wakuu watatu waliopo ambao huzisafirisha kwenda kwenye viwanda vilivyoko Mwanza, Morogoro, Dar es Salaam na Mombasa kutengenza bidhaa nyingine.

(iii) Kiasi cha tani mbili za chuma chakavu hukusanywa kila siku na kupelekwa kwenye kiwanda cha Nyakato steel Mill Mwanza na kile cha Sayona steel Mill kilichoko Wilaya ya Misungwi.

Kazi ya mwisho ni kufukia taka zinazooza kwenye udongo. Kwa sasa kisi cha tani 296 kati ya tani 518 za taka ngumu zinazozalishwa kwa siku husafirishwa kwa malori ya Halmashauri na yale ya mawakala binafsi hadi dampo la Buhongwa lililoko km 15 kusini mwa Jiji, kandakando ya barabara ya Shinyanga ona Jedwali 4.4.

**Jedwali 4.4: Uzalishaji wa taka ngumu (tani) kwa siku ikilinganishwa na uwezo wa kuzikusanya**

| Aina ya taka ngumu | Kiasi kinacho zalishwa | Kiasi kinacho kusanywa |
|---|---|---|
| Taka za majumbani | 330 | 240 |
| Taka toka maeneo ya biashara na taasisi | 132 | |
| Taka za viwandani | 56 | 56 |
| Jumla | 518 | 296 |

**Chanzo:Halmashauri ya Jiji la Mwanza, 2011**

Eneo la dampo la Buhongwa lina ukubwa wa hekta 99. Mbinu inayotumika kufukia ile ya kufukia taka mchanganyiko kama zilivyo, kwani hakuna uchambuaji wa kina wa taka kwenye makundi kama vile taka za jikoni, taka za asili ya mimea, taka nyepesi(isiyo chuma) na taka ngumu(asili ya vyuma na bati). Hata huo ufukiaji wenyewe siyo wa hakika na wakati mwingine hawafukii kwani mitambo inayotumika ya *wheel loader* na *bulldozer* haviaminiki kutokana na uchakavu na kuharibika mara kwa mara. Kwa sababu wanazamika kukodisha mitambo ya kufukia kila baada ya miezi mitatu.




*Mtambo wa kukodi wa wheel loader ukiwa kazini*

Kwa sasa ni fahari kwamba Jiji la Mwanza ndilo Jiji linaloongoza kwa usafi na lenye mandhari ya kuvutia kuliko miji yote nchini Tanzania. Kwa miaka mitano mfululizo, Jiji hili limekuwa likipata vikombe vya ushindi wa kwanza katika mashindano ya Majiji, yanayoandaliwa na Jumuia ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (ALAT), kwa vigezo vya usafi, unadhifu na uzuri wa madhari zake. Shughuli hizo hapo juu siyo pekee zinazofanya Jiji kuwa safi. Halmashauri ya Jiji la Mwanza imeanzisha mikataba kadhaa ya maelewano/maafikiano (MOUs) na taasisi mbalimbali zinazolenga kuweka Jiji safi na nadhifu. Kwa sheria ndogo iliyopo na kwa mujibu wa maelewano

haya ni kosa kwa mwendelezaji ardhi yeyote ndani ya Jiji kutokuweka mazingira yanayomzunguka kiwe kiwanda, nyumba au biashara yake katika hali ya usafi na kuzungushia bustani za maua na kupanda miti. Kwa kuzingatia haya, imesaidia sana kulifanya Jiji la Mwanza kuwa na mandhari nzuri ya kuvutia.

Maeneo ya wazi kama vile kwenye mizunguko ya barabara (*roundabouts*) na bustani za Jiiji zinatunzwa kwa ushirikiano na sekta binafsi na taasisi za umma. Jiji limewekeana mikataba mahsusi ya maelewano na baadhi ya taasisi yanayotaka taasisi hizo kuziweka safi na kuzitunza bustani za Jiji. Kwa mfano taasisi kama Benki kuu na Coca Cola hutumia rasilimali zao kusafisha na kutunza bustani na mizunguko iliyopo kwenye Jiji bila kuzuia umma wa Watanzania kutumia huduma hizi. Taasisi hizi huingia mikataba hii kwa ajili ya kutangaza biashara zao kwenye bustani hizi na pia kutimiza wajibu wao wa kutoa mchango wao kwa jamii bila kudai malipo yoyote.

Jambo jingine la kihistoria ambalo Jiji la Mwanza limefanya ili kudhibiti mrundikano wa taka ngumu na uchafuzi wa mazingira ni kwa njia ya kufunga kamera zinazochukua picha za ufuatiliaji kwa siri katika mitaa ya Jiji hususannkatika Wilaya ya kibiashara ya katikati ya Jiji (CBD). Kwa ushirikiano na askari wa Jiji, Mitaa yote iliyo katikati ya Jiji, vituo vya kukusanya taka na mapipa ya takataka yanaonekana na kufuatiliwa kwa karibu kutokea ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji na ile ya Mkuu wa Idara ya Afya na Mazingira. Kamera hizi zinasaidia kuchukua hatua za haraka inapotokea mrundikano wa taka, utupaji taka ovyo na utupaji haramu wa taka.

## 5.0 RASILIMALI ZILIZOTUMIKA KWA MIAKA MITATU

Ukusanyaji taka na kuziangamiza ni jambo la muhimu mno katika kuboresha maisha, lakini ni shughuli inayohitaji fedha nyingi angalia jedwali 4.5. Kwa miaka mitatu iliyopita Jiji la Mwanza limetumia jumla TZS 1,680,168,906.00 kwa ajili ya huduma ya taka ngumu kama inavyoonekana kwenye Jedwali hapo chini.

**Jedwali 4.5: Gharama za kuzoa taka (2009 – 2012)**

| Chanzo cha fedha | 2009/2010 | 2010/2011 | 2011/2012 |
|---|---|---|---|
| **Basket fund** | 39,208,500 | 61,221,750 | 64,203,756 |
| **Block grant** | 110,205,200 | 130,353,200 | 1,967,000 |
| **Vyanzo vya ndani** | - | 474,887,000 | 508,375,700 |
| **Capital Development Grant** | 289,746,800 | - | - |
| Jumla | **439,160,500** | **666,461,950** | **574,546,456** |

**Chanzo:Halmashauri ya Jiji la Mwanza, 2011**

**Jedwali 4.6: Malipo kwa Asasi za kiraia (CBOs)zinatoa huduma**

| JINA/ KAMPUNI/ CBO | RUZUKU YA MWEZI |
|---|---|
| **MAENDELEO MBUGANI** | 1, 084,000.00 |
| **BORESHA MAZINGIRA** | 1, 035,090.00 |
| **HIMAJA** | 775,000.00 |
| **KENYAGESI IGOGO** | 862,000.00 |
| **TUFUMA** | 1, 152,800.00 |
| **UZOTA** | 831,500.00 |
| **MKUWA** | 666,000.00 |
| **MUFAJUS** | 936,000.00 |
| **CHARITY ORGANIZATION** | 959,000.00 |
| **WAJANE** | 1, 022,000.00 |
| **MAENDELEO MKUDI** | 846, 000,00 |
| **PATUMA** | 722,000.00 |
| **GILGAL** | 1, 111,500.00 |
| **TOTAL** | **12, 002,890.00** |

**Chanzo:Halmashauri ya Jiji la Mwanza, 2011**

## 6.0 MATOKEO NA MAFANIKIO

Jiji la Mwanza lina historia ndefu ya ukusanyaji taka ngumu. Maamuzi ya mwaka 2002 na sheria ndogo ya mwaka ya 2010 pamoja na utaratibu wa sasa wa kuzoa na kutupa taka ngumu imepelekea mafanikio kadhaa; moja likiwa ni ;"Jiji safi la mfano, Jiji nadhifu na lenye mandhari ya kuvutia hususani katikati ya Jiji" Mafanikio mengine ni ;

- Ukusanyaji taka umeongezeka kutoka tani 72 (32%)kwa siku mwaka 2000 hadi tani 296 (57.14%) mwaka 2012.
- Kwa kupitia ushitiri na makampuni binafsi mfano (makampuni binafsi 3 na asasi 3 za kiraia) Halmashauri imefanikiwa kusafisha barabara za lami zenye urefu wa km 62 , eneo la wazi lenye ukubwa wa $m^2$120,000 na kuzibua mifereji ya maji ya mvua km 96 kila siku.




**OFISI YA SHERIFU KATA YA IGOMA**

- Sekta binafsi inashiriki kikamilifu kutoa huduma za kuzoa na kutupa taka.
- Ile Kanuni ya mchafuzi wa mazingira kulipa faini ya papo kwa papo, imeleta nidhamu kwa wageni wanaotembea Jiji la Mwanza.
- Idadi ya rasilimali watu wa Idara ya Afya na mazingira imeongezeka kutoka 58 mwaka 2000 hadi 320 mwaka 2012. Ongezeko hili ni ongezeko kwenye makampuni binafsi (siyo ongezeko kwa waajiriwa wa Jiji)
- Idadi ya vifaa vya kuzolea taka, malori, zana za kazi na mapipa ya taka yameongezeka sana pia yanatumika vizuri. Malori ya taka yaliongezeka kutoka 5 mwaka 2002 hadi 16 mwaka 2012 (8 kati ya hayo ni mali ya Jiji na 8 ya sekta binafsi)
- Jiji la Mwanza limekuwa likishinda tuzo ya Jiji safi kuliko yote nchini kwa miaka saba mfululizo sasa.




*Tuzo/vikombe vya ushindi Mwanza Jiji safi kuliko yote nchini*

- Jiji la Mwanza limefanikiwa kuepuka magonjwa ya kuambukiza haraka kama vile kipindupindu, kwa miaka 10 sasa; ikumbukwe kwamba bado kipindipindu ni tatizo kubwa kwa baadhi ya Miji nchini.

**7.0 CHANGAMOTO**

Halmashauri ya Jiji la Mwanza katika kufikia mafanikio yanayoonekana kuhusu uzoaji na utupaji taka hadi kupata hadhi ya Jiji safi na nadhifu imekutana na changamoto kadhaa. Nazo ni;

- Kwa kiasi fulani kulikosekana utayari wa jamii kulipia ada za huduma ya kuzoa uchafu waliozalisha wenyewe.
- Bado sekta binafsi na asasi za kiraia zina uwezo mdogo wa nguvukazi, vifaa na mitambo ya kuzoa taka ngumu.
- Uhaba wa mitambo ya kufukia taka na uwezo mdogo wa Jiji kukarabati.
- Kukosekana kwa mizani ya kupima kiasi cha taka kinachofukiwa
- Kutokuwepo kwa uzio kuzunguka eneo la dampo kuzuia waokota taka wasio na vibali kuvamia eneo la dampo.
- Pamekuwepo na majaribio ya wanasiasa kutaka kuingilia juhudi za Jiji ili kuingiza wadau wa kila aina wanaowataka wao katika huduma za kuzoa na kutupa taka.

**8.0 MIKAKATI YA KUPAMBANA NA CHANGAMOTO**

Jiji la Mwanza limeendelea kuweka msisitizo wa kubakia kuwa safi na nadhifu kupitia mikakati ifuatayo;

- Uhamasishaji endelevu na programu za kupanua uelewa kwa jamii ya Mwanza ili kuijengea tabia ya usafi na kuacha kutupa taka ovyo.
- Kukazia utekelezaji wa sheria ndogo kwa ushirikiano na ofisi ya kampuni binafsi ya Sherifu na askari wa Jiji.
- Kutangaza shughuli za kuzoa na kutupa taka ili kampuni na asasi za kiraia zenye uwezo waombe kazi hizi.
- Ununuzi wa mitambo miwili ya kupakia taka kutokana na mapato ya ndani ya Jiji
- Kukarabati mtambo wa kufukia taka na kushindilia taka uliokuwa haufanyi kazi
- Kuwashawishi washirika wa maendeleo na wadau wengine wawekeze katika biashara ya kuzoa taka na kusimamia dampo hususan mradi unaojulikana kama *“Clean Development Mechanism Project”.*
- Kuomba misaada ya kiufundi, vifaa na mitambo inayohusiana na taka ngumu kutoka mradi wa Tanzania Strategic Cities Project (TSCP).

**9.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Jiji la Mwanza ni moja miongoni mwa Majiji kadhaa ya Tanzania na hutoa huduma kwenye mazingira halisi kama Majiji mengine. Swali moja ni hili, ipi siri ya mafanikio kwenye uzoaji taka na kuwa Jiji safi na nadhifu? Baadhi ya siri hizo ni pamoja na mambo yafuatayo;

- Mambo mazuri yaliyoshuhudiwa kutoka mafunzo ya Osaka kuhusu tabia ya watu kupenda usafi, kukusanya, kutenganisha na kurudisha baadhi ya taka kwenye matumizi mbadala. Mafunzo ya Osaka yalituwekea msingi na ndiyo yalikuwa kichocheo kwenye timu ya Menejimenti ya Jiji kutaka kuyaiga mambo mazuri yahusuyo uzoaji na utupaji taka waliyoyaona Japani na kuyaingiza kwenye Jiji la Mwanza, kama ilivyo kwenye mpango kazi ulioandaliwa baada ya kutoka Osaka mwaka 2007.
- Timu ya Menejimenti ya Jiji (CMT) kufanya kazi kama timu moja, Idara ya Afya na Mazingira husůsan kitengo cha kuzoa na kutupa taka kilikuwa kikifanya mikutano ya mara kwa mara na wadau mbalimbali kushughulikia masuala mbalimbali kuhusu udhibiti wa taka kwa kujituma.
- Maandalizi ya mpango thabiti na muundo wa kufanya kazi kwa ushirikiano na asasi za kiraia na kuzilipa ruzuku; Kutenga Jiji kwenye kanda mbalimbali kuliongeza ufanisi kwenye zoezi la uzoaji taka.
- Utekelezaji thabiti wa sheria ndogo kupitia kwa kampuni binafsi (Sherifu), kuwepo kwa kitengo cha sheria cha kuhukumu masuala ya usafi na mazingira, faini ya papo kwa papo kwa wakiukaji wa sheria ya usafi na mazingira, na matumizi ya kamera za siri. Mafaniko ya Mwanza yametokana na ushirikishwaji wa wadau mbalimbali.
- Dhamira ya kweli ya Halmashauri ya Jiji iliyodhihirika kwa kutumia rasilimali zake toka vyanzo vya ndani kwenye masuala ya kukusanya na kutupa taka ngumu.
- Kutumia fursa ile ya sekta binafsi ya kutaka kujitengenezea jina zuri na kuakisi taswira njema kwa jamii; kuwashinikiza waendelezaji wenye viwanda, nyumba, bohari na taasisi mbalimbali katika kufanya usafi na kutunza mazingira ili kupendezesha Jiji. Makubaliano kwamba wawekezaji wote wenye (viwanda, taasisi mbalimbali, bohari) ni lazima kuweka mazingira yao safi na kutengeneza mandhari za kupendeza ikihusisha bustani zenye mvuto na mfumo wa maji mithili ya chemichemi. Hii ni kwa sababu walio wengi wako usoni au pembeni mwa mitaa na barabara kuu za Jiji. Kwa kusafisha mazingira na kuhudumia bustani za Jiji sekta binafsi na taasisi hujijengea jina zuri na taswira njema machoni pa Wananchi.
- Jiji la Mwanza limezungukwa na mawe na majabali. Mawe na majabali yana kawaida ya kupendezesha Mji kwa asili. Kwa mantiki hii, Halmashauri ya Jiji la Mwanza inatumia rasilimali zote zilizopo. Kwa mfano, Jiji linatumia mawe yaliyopo kutengeneza barabara za mawe za kipekee.
- Kuna kamera za siri (CCTV) zimefungwa katika mitaa ya Wilaya ya kibiashara ya katikati ya Jiji na kuunganishwa moja kwa moja na ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji. Kupitia kamera hizi, Mkurugenzi anaweza wakati wowote kuona kurundikana kwa taka, anaweza kuwaona wanaokiuka sheria ya usafi na mazingira, na pia kama kuna msongamano wa magari anaweza kuchukua hatua za haraka maana msongamano wa magari ni sehemu ya uchafuzi wa Jiji. Katika hili, Halmashauri ya Jiji inashirikiana na sekta binafsi kupitia kampuni ya BARMEDA. Kupitia mfumo huu wa kamera, askari wa usalama barabarani wanaweza kuwashauri madereva kubadili uelekeo au barabara kwa njia ya radio ya FM inayomilikiwa na Jiji. Kupitia mfumo wa kamera Mkurgenzi anaweza kumpigia simu Sherifu aliyepo kwenye mtaa husika ili kumkamata mchafuzi wa mazingira au mvunjaji wa sheria ndogo ya Jiji. Kwa wale wanaojua kamera hizi zinavyofanya kazi, wanaogopa sana kutupa taka ovyo na hii imesaidia kuweka Jiji katika hali ya usafi.

- Uhamasishaji wa uhakika uliofanywa na Halmashauri ili kuamsha ari ya jamii; matumizi ya kampuni binafsi ya Sherifu na kufanya kazi kwa karibu na asasi za kiraia ilivutia uwajibikaji wa jamii kujitoa na kutekeleza sheria ndogo bila kushurutishwa. Jamii kuzingatia kanuni za Jiji kwa kupeleka takataka za majumbani kwao kwenye vituo vilivyotengwa rasmi kwa kazi hiyo. Kwa hiyo kila kaya ina wajibu wa kuwa na kifaa cha kuwekea taka na mara kwa mara kuzipeleka taka kwenye kituo ili kurahisisha ubebaji na kuzipeleka kwenye dampo kwa malori.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA

## MRADI WA AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA KATA YA MAMBALI



*SAMPULI NA 1 YA CHOO CHA MAMBALI*



*SAMPULI NA 3 YA CHOO CHA MAMBALI*

## 1.0 UTANGULIZI NA TATIZO LILILOKUWEPO

Kata ya MambalI ipo kwenye Halmashauri ya Nzega na ina Vijiji vinne na Kaya 2,469. Mwaka 2008 utafiti uliofanyika katika Kijiji cha Mambali ulibaini kwamba idadi kubwa ya watu walikuwa wakiishi kwenye mazingira machafu yanayozunguka kaya zao. Wengi wao hawakuwa na vyoo hata vile vya shimo hivyo walikuwa wanajisaidia vichakani. Tabia hizi zilisababisha harufu mbaya kwenye kaya na vyanzo vya maji navyo vilichafuliwa vilevile. Utafiti huo ulibaini kwamba jamii ya Mambali walikuwa na hali tabia hasi kuhusu usafi wa mazingira na matumizi ya vyoo iliyotokana na mila potofu. Baadhi ya mila hizi ni zile zilitoa maoni kwamba (i) wazee hawapaswi kuonwa au kujulikana waziwazi kwamba wanakwenda chooni (ii) wanawake hawapaswi kutumia choo kimoja na wazazi au wakwe zao (iii) familia nzima haipaswi kushiriki choo yaani shimo la pamoja.

Utafiti uligundua kwamba kati ya Kaya 620 zilizotembelewa kwenye Kijiji cha Mambali ni Kaya 365 tu ndizo zilizokuwa na vyoo na hii ni sawa na 59%. Kati ya hizo 365 zenye vyoo, ni kaya 5 tu zilizokuwa na vyoo bora ambavyo vinaweza kufanyiwa usafi.

Matokeo ya tabia hizi za uchafu ni ongezeko la magonjwa ya minyoo kutokana na kukosekana matumizi mazuri ya choo kwenye 59% ya kaya zote. Hata hivyo, kiasi cha 98% ya kaya zenye vyoo walikiri kutokuwepo matumizi sahihi ya vyoo kutokana na baadhi ya wanafamilia kutozingatia na wengine kung'ang'ania mila potofu kuhusu matumizi ya vyoo.

## 2 MALENGO YA MRADI

Mwaka 2006, Halmashauri ya Nzega ilishiriki kwenye warsha za mafunzo za mikoa za ufuatiliaji za Wakurugenzi walioshiriki mafunzo ya Osaka Japani. Mpango kazi wa Halmashauri ulioibuka kutokana ya warsha hii ulikuwa na kipengele kinachohusu usafi wa mazingira. Na ikumbukwe kwamba utafiti ule wa Mambali wa 2008 ulipendekeza mradi wenye lengo la kuboresha usafi wa mazingira, ili kupunguza magonjwa yatokanayo na mazingira machafu. Halmashauri ya Nzega iliandaa mpango mkakati kufikia lengo hili, kwa kuanzia na Kijiji cha Mambali ambacho kingetumika hapa Nzega kama Kijiji cha mfano na baadaye kueneza mafanikio ya mradi huo kwenye Vijiji vingine ndani ya Kata na kwenye Halmashauri yote.

## 3.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

Katika utekelezaji wa mradi huu, ililazimu Halmashauri kumpeleka mtaalamu wa afya ya jamii kwenye Kijiji cha ya Mambali ambaye alifanya kazi kwa karibu kabisa na jamii pamoja na serikali ya Kijiji cha Mambali. Wadau wengine ni Kituo cha Afya, Shule ya Msingi yaani wanafunzi na walimu. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na ;

(i) Kutoa elimu muafaka kuhusu umuhimu wa kuwa na mazingira safi kuzunguka kaya. Hii ilifanyika 2008 katika Vijiji vinne vya Mambali, Kikonoka, Mbutu na Nkindu.

(ii) Kuamsha ari ya jamii, kuhamasisha jamii ili kubadili mtizamo, hali tabia na kuachana na mila potofu zinazokinzana na kanuni za afya ya mtu binafsi na ya jamii nzima, kushirikiana matumizi ya vyoo, na usafi wa mazingira. Uhamasishaji huu

ulitekelezwa kwa ushirikiano na asasi isiyo ya kiserikali ya SEMA kutoka Singida. Katika zoezi hili mbinu bunifu ambayo ni shirikishi ijulikanayo kama "Mtumba" ilitumika. Tofauti yake na mbinu ya PRA ni kwamba hii ni PRA iliyofanyiwa mabadiliko, hutumia siku chache zaidi lakini husaidia kupanua eneo linalofikiwa na zoezi la uhamasishaji.

(iii) Mbinu shirikishi zilitumika katika mafunzo ya vitendo kwenye ujenzi wa vyoo bora kwenye jamii ya Mambali. Zoezi la mafunzo lilianza na watu wachache waliojitolea, hawa baada ya kufuzu walisadia kueneza elimu hii kwa wengine na kwenye Vijiji vingine.

(iv) Kupashana habari na maarifa kwenye Kata ya Mambali kuhusu umuhimu wa usafi wa mtu binafsi na usafi wa mazingira ya Kaya. Maarifa haya yalihusisha mbinu za usafi wa Kaya na mazingira yake.

(v) Mafunzo kwa ajili mafundi mchundo 16 wa mwanzo, ambao walitengeneza timu ya wataalamu wa jamii wa ujenzi wa aina mbalimbali za vyoo. Mafunzo yalihusu aina za vyoo, gharama zake, vifaa vya ujenzi na stadi za ujenzi wenyewe. Wakati huo huo, jumla ya waraghibishi 24 waliandaliwa mafunzo maalum ya mbinu bora za kuamsha ari na kuhamasisha jamii katika ujenzi wa vyoo bora na matumizi yake. Mpango wa mafunzo uliwafikia wale walioitwa "marafiki wa afya" mia mbili katika Vijiji vinne. Mafunzo kwa jamii yalifanyika kwa njia ya mikutano ya Vijiji, mashairi, ngonjera, maigizo na nyimbo.

(vi) Ujenzi wa aina tofauti za vyoo 12 vya mfano ulifanyika katika kijiji cha Mambali kupitia mradi wa vyoo na usafi wa mzingira. Mradi uliandaa vipeperushi vyenye maelezo ya kila aina ya choo na kuvibandika kwenye ukuta wa kila choo husika il wageni wavisome.



*Aina mojawapo ya vyoo na kipeperushi kutani*

(vii) Kuendesha mafunzo ya ujasiriamali kwa kile kiundi cha mafundi mchundo 16 kutoka Vijiji vinne. Mafunzo yalilenga kwenye kuwawezesha kuzalisha fedha na kuziwekeza kwenye biashara ndogodogo na nyingine wajengee kituo cha mafunzo ya afya na usafi wa mazingira.

**(viii)** Kuendesha mafunzo kwa wanafunzi wa Shule za Msingi yaliyojulikana kama mafunzo ya "mtoto kwa mtoto" kwenye shule 10 za msingi. Mafunzo haya yalilenga kubadili tabia za watoto ambao ndio wazee wa baadaye kwa kuona na kufurahia ujenzi wa vyoo bora na kuvitumia. Mafunzo haya yalilenga pia kuvunjilia mbali zile mila potofu kabla watoto hawajazirithi.

**4.0 MATOKEO YA MRADI**

Mradi wa Usafi na Mazingira wa Mambali ulipata mafanikio halisi yafuatayo;

(i) Kuanzishwa kwa kituo cha mafunzo kwa vitendo kuhusu ujenzi wa vyoo bora. Kituo hiki kina aina 12 za vyoo vya shimo kama ilivyo kwenye picha. Vifaa vilivyo vingi vya ujenzi huu hupatikana katika eneo hili; navyo ni majani, miti, nguzo na matofali.

(ii) Kuanzishwa kwa kikundi kilichojipanga vizuri cha mafundi mchundo wajenzi wa vyoo bora kutoka miongoni mwa jamii ambao ndio wanaokitunza kituo cha mafunzo , ndio wanaoendesha mafunzo kwa wanavijiji wenzao, ndio wanaotoa maelezo kwa wageni na kutunza fedha za kituo. Kikundi kina mfuko ambao hadi Julai 2012 ulikuwa na TZS 590,000.80. Mfuko hutumika kwa mzunguko kwa kununua vifaa vya ujenzi na kuwalipa mafundi na hupata fedha kutokana na malipo mbalimbali ya huduma zinazotolewa na kikundi.

(iii) Mpango huu umekwishafikia Kaya 3,757 yaani( 87%) kati ya Kaya 4,317 na hivi ni vyoo vile vilivyojengwa Kijiji cha Mambali peke yake. Mradi umefanikiwa kubadilisha tabia za watu wa Mambali na kuasili tabia ya kimaendeleo. Ujenzi wa vyoo bora na vya kisasa kabisa umefanyika kwenye kaya 1,906 ambazo ni sawa na 44% ya Kaya zenye vyoo bora, huku kaya 1,851 zikiwa zimejenga vyoo vyenye ubora wa chini, na hawa ni sawa na 43% ya Kaya zote zenye vyoo.



*Choo maalum cha kukaa kwa wazee na wasiojiweza*



*Sampuli ya Choo, Namba 4*

(iv) Kuna badiliko kubwa kwenye jamii ya Mambali kwani wananchi walio wengi wamekubali kuanza maisha mapya kwa kujenga na kutumia vyoo.

(v) Magonjwa ya minyoo yamepungua kwa kiasi kikubwa katika miaka minne iliyopita. Jedwali 4.7 linaonesha kupungua kwa magonjwa manne yanayotokana na uchafu.

**Jedwali 4.7: Kupungua kwa magonjwa**

| | 2008 | | 2009 | | 2010 | | 2011 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ugonjwa | **Chini ya miaka 5** | **Zaidi ya 5** | **Chini ya miaka 5** | **Zaidi ya 5** | **Chini ya miaka 5** | **Zaidi ya 5** | **Chini ya miaka 5** | **Zaidi ya 5** |
| Kuharisha | 671 | 141 | 530 | 394 | 112 | 74 | 52 | 6 |
| Minyoo ya tumboni | 36 | 89 | 205 | 264 | 42 | 102 | 17 | 61 |
| Magonjwa ngozi | 143 | 77 | 198 | 114 | 122 | 141 | 88 | 90 |
| Kichocho | 8 | 113 | 0 | 61 | 0 | 0 | 4 | 20 |

**Chanzo: Kituo cha Afya Mambali 2011**

(vi) Ujenzi wa vyoo umekuwa ni biashara inayovutia kwa kile kituo na mafundi mchundo. Ujenzi wa vyoo vya aina za Mambali umeenea kwenye Kata nyingine kwenye Wilaya za Nzega, Tabora na Singida.

(vii) Halmashauri ya Nzega imesambaza elimu ya usafi wa mazingira kwa kuanzisha vituo vingine viwili ambavyo vina uongozi na staili ya usimamizi kama ule wa Mambali.

(viii) Watu wa Kata ya Mambali wameasili tabia ya ustaarabu na usafi kwani sasa wananawa mikono kabla ya kula na baada ya kutoka chooni, pia sasa wanaweka maji ya kunawa kwenye vyoo vyao (kibuyu chirizi).

(ix) Kata ya Mambali hupokea wageni wengi, wakiwa mmojammoja na hata vikundi wenye hamu ya kujifunza kuhusu ujenzi wa vyoo. Mfano Halmashauri ya Chamwino ilileta Madiwani mwaka 2012. Wengine ni Kikundi cha EYEWASH, Watendaji wa Halmashauri ya Iramba na watumishi wa NGOs kadhaa kutoka Kenya na Uganda walifika 2011.

(x) Kikundi cha mafundi mchundo hutoka kwenda kueneza ujuzi wa ujenzi wa vyoo hivi kwenye maeneo mengine nchini. Mfano hivi karibuni kikundi hiki kilikaribishwa kwenda Halmashauri ya wilaya ya SIHA kwenda kutoa mafunzo ya ujenzi wa vyoo.

## 4.0 RASILIMALI ZILIZOTUMIKA

Mradi huu wa Kata ya Mambali ulitekelezwa na Halmashauri kwa ushirikiano na asasi zisizo za kiserikali na jamii yenyewe. Mtaji wa mwanzo ulihusisha TZS 27 milioni kati ya hizo (water aid) walichanga TZS 24 milioni na wananchi wa Mambali walichanga TZS 3 milioni. Mradi wa ujenzi wa vyoo vya mfano ulikamilika ndani ya siku 45.

## 5.0 CHANGAMOTO

Mradi wa usafi wa mazingira wa Mambali ni mradi wenye mafanikio makubwa kwa jamii za Vijijini hapa Tanzania. Hii inatokana na ukweli kwamba jamiii za Vijijini si wepesi kubadilika na kuachana na mila na desturi zao. Hata hivyo mafanikio haya yalikumbana na changanoto zifuatazo:

(i) Vifaa vya ujenzi vilipatikana kwa shida kwani Kata ya Mambali ipo mbali tena porini sana toka Nzega mjini kunakouzwa vifaa hivi.

(ii) Umaskini wa kipato wa kaya ndio umechangia mradi usiweze kufikia malengo ya kwa 100% . Baadhi ya kaya zilishindwa hata kuchangia gharama za hata kile choo cha bei nafuu kuliko vyote.

(iii) Timu za uraghibishi hazikuwa na usafiri wa kuaminika ili wafanye safari za mara kwa mara kwenye kaya ili kuimarisha mchakato wa mabadiliko. Pia timu hizi hazikuwa na motisha ya kutosha kwa minajili ya kuhamasisha na kuamsha ari ya jamii kujenga vyoo.

(iv) Baadhi ya kaya zinaishi kwenye maeneo ya udongo chepechepe ambao haustahimili kuchimbwa vyoo vya shimo. Sehemu nyingine ardhi yao ina maji karibu sana kiasi cha mita 2 chini ya ardhi na kufanya vyoo vinavyojengwa visidumu na uimara wake kuwa mashakani.

(v) Kata ya Mambali ina baadhi ya wakazi wake ambao kwa asili ni wafugaji. Hawa huhamahama kutafuta maji na malisho. Kwa hiyo ilikuwa vigumu kuwafikia hawa ili wabadilishe tabia. Hata wale waliofikiwa, wachache wao bado wanarudi kwenye mila na mazoea yao.

## 6.0 MIKAKATI YA UENDEVU

Kituo cha mradi wa usafi na mazingira Kata ya Mambali kimekwishaainisha changamoto na kimeweka mikakati ya kujinasua nazo. Baadhi yake ni pamoja na;

(i) Kuendelea na zoezi la uhamasishaji kuamsha ari kupitia timu za uraghibishi. Hii itahusisha pia ufuatiliaji wa mbadiliko ya tabia za jamii kuhusu ujenzi na matumizi ya vyoo bora.

(ii) Halmashauri ya Nzega itatoa motisha kwa timu ya waraghibishi na timu ya mafundi mchundo ili wasichoke kuendeleza harakati za kujenga na kutumia huduma za choo.

(iii) Halmashauri ya Nzega itatenga kiasi cha TZS 7.2 millioni kila mwaka ili kuimarisha shughuli za mradi huu muhimu. Hizi zitatumika kuendesha mafunzo ya mara kwa mara ya wajenzi wa vyoo wapya ili kuondoa uhaba wa mafundi na kufanya gharama za ujenzi zisipande na kukwamisha zoezi.

(iv) Halmashauri ya Nzega inakusudia kuhakikisha Vijiji vyote vinapata ujuzi wa ujenzi na ukarabati wa vyoo ili ziwe ni shughuli za kawaida kwenye kaya.

## 7.0 SIRI YA MAFANIKIO

Ni kweli kabisa kwamba Mkurugenzi wa Halmashauri (Bwana Kyuza Kitundu) na timu yake ya CMT walidhamiria kufanya mabadiliko ya tabia na mila zilizopitwa na wakati zilizokataza matumizi ya vyoo. Kwa kutumia mbinu shirikishi ya Mtumba, CMT haikutumia fedha nyingi. Mbinu hii iliasiliwa kutoka mradi wa Water Aid (2007) na mtindo huu ndio ulikuwa siri kubwa ya mafanikio. Hatua mbalimbali katika mchakato huu ni hizi zifuatazo;

(i) Kamati ya afya na mazingira ; kamati hii ndiyo kama dereva na ilihakikisha kila kaya inatoa vifaa vilivyohitajika kwa usafi wa mazingira na kwa mantiki hii kaya zilitoa vifaa vya kujenga vyoo vya kisasa na kuhakikisha hakuna anayejisaidia tena vichakani.

(ii) **Kufyatua/kufyatuka** ambako kulikusudia jamii yenyewe ianze kuchukua hatua baada ya kuwafumbua macho na kuona vitendo vya aibu na vyenye madhara kwao vinavyotokana na kujisaidia vichakani na madhara yake kwa afya zao. Mtindo wa "Mtumba" umeboreshwa kidogo kulingana na mahitaji na unatumika kama ifuatavyo:

**(iii)** **Kufanya uchambuzi na kuchora ramani ya hali ya usafi wa mazingira;** hii ni njia ya kuhakikisha jamii yenyewe inashiriki katika zoezi la kuchambua hali yao halisi ya maisha kwa kuzitambua kaya na taasisi ambazo hazina vyoo bora na kuyatambua maeneo ambayo watu wanajisaidia ovyo mfano mabondeni, vichakani na karibu na vyanzo vya maji.

(iv) **Kataa ya njia/matembezi ya afya.** Zana hii hutumika kuhakiki yale yaliyochorwa kwenye ramani ya usafi na mazingira kama ndivyo ilivyo kweli.

(v) **Waraghibishi wa masuala ya usafi na mazingira.** Zoezi la kupandisha ari ya mabadiliko kwa jamii hufanywa na waraghibishi waliobobea, na hii ni kanuni moja muhimu sana katika uhamasishaji wa masuala ya usafi na mazingira.

(vi) **Mafundi mchundo wa usafi na mazingira.** Mafundi mchundo ni watu miongoni mwa wanajamii ambao hufundishwa ili kupambana na changamoto tajwa hapo juu. Mafundi mchundo hupata mafunzo kwa vitendo yenye lengo la kuinua viwango vyao vya ujasiriamali na mbinu za masoko na kunadi huduma zao. Hawa ndio hufuatilia kwa karibu utekelezaji wa shughuli za mradi.

**(vii)** **Vituo vya mafunzo ya usafi na mazingira.** Hivi ni vituo mahsusi kwa ajili ya maonesho ya aina mbalimbali za vyoo ambazo wateja wanaweza kufanya uchaguzi kulingana na utashi na uwezo wao.

**(viii)** **Stadi za ushawishi na utetezi ngazi ya Kata na sekta binafsi.** Ushawishi hufanyika kutafuta uungwaji mkono toka Halmashauri, Kata, na sekta binafsi katika kuendeleza masuala ya usafi na mazingira. Vikundi vya mafundi mchundo vitahitaji kuwa na akaunti benki, hivyo vinahitaji uwezeshwaji wa ngazi ya Kata na Halmashauri. Mchango wa sekta binafsi ni wa muhimu ili kutuhakikishia upatikanaji wa malighafi zinazohitajika kwa masuala ya afya na mazingira.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA

## UTEKELEZAJI BORA WA MFUKO WA AFYA YA JAMII



*KAYA INAYOFAIDIKA NA MFUKO WA CHF*

## 1.0 UTANGULIZI

Tangu uhuru, Serikali ya Tanzania imekuwa ikipambana na maradhi katika jamii kama moja ya maadui watatu wa Taifa. Juhudi za Serikali na wadau wengine zimejikita katika kuimarisha mifumo, sera na jitihada mbalimbali ili kuwafaidisha maskini ambao ndio wengi na wote waliopo katika mazingia hatarishi. Mfuko wa Afya ya Jamii ni mkakati mojawapo wa kuhamasisha jamii kushiriki katika huduma za afya.

Mfuko wa Afya ya Jamii ni mpango wa hiari uliopo kwenye Halmashauri na ulianzishwa chini ya Sheria Na. 1 ya mwaka 2001 ambayo inaruhusu ukusanyaji wa fedha kutoka kwa jamii kwa lengo la kutoa huduma za afya kwa wanachama wake. Mfuko huu huhitaji malipo ya ada za huduma kwa ajili huduma za afya. Pia kuna mbinu zilizowekwa za kusamehe maskini na makundi yasiyojiweza. Punguzo hutolewa kwa wagonjwa ambao hawaingii moja kwa moja kwenye msamaha wa kisheria lakini wanahitaji kufikiriwa, hawa wanaitwa “hawana uwezo wa kulipa“. Mpango huu unaendeshwa kwa ushirikiano kati ya jamii na Serikali. Serikali Kuu huchangia kiasi kulingana na mchango wa jamii kwa Halmashauri husika na jamii hutoa michango yao wakati wa mavuno na kufurahia huduma mwaka mzima. Jamii za kilimo hutegemea mauzo kutoka katika mazao yao ambayo hupatikana kwa msimu. Kamati za Afya za Jamii hukusanya na kusimamia matumizi ya fedha; hata hivyo mfuko huu haujalenga kuchukua nafasi ya Serikali kulipia huduma za afya.

Mfuko huu wa Afya ya Jamii hutoa huduma bora na rahisi kupitia mbinu bora na endelevu za kifedha. Unaboresha usimamizi wa huduma za afya kwenye jamii kupitia Ugatuaji. Una hakikisha uwepo wa madawa na vifaa kwenye Zahanati na Vituo vyote vya Afya. Mfuko huu huongeza ubora wa huduma za afya zinazotolewa kwa kuhakikisha uwepo wa watoa huduma wa kutosha, wenye sifa na ari; na zaidi ya hayo mfuko unaimarisha ushiriki wa jamii.

Wilaya ya Igunga ni moja kati ya Wilaya sita za Mkoa wa Tabora. Wilaya ipo kati ya latitudo 30 na 40 kusini mwa Ikweta na longitudo 30 na 32 Mashariki mwa Greenwich. Kutokana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002 Wilaya inakadiriwa kuwa na watu 324,094; kati yao 118,817 ni wanaume na 165,277 ni wanawake. Makadirio ya sasa ya idadi ya watu ni 452,278; ambapo 223,502 ni wanaume na 228,776 ni wanawake, katika Kaya 59,012. Wilaya ina tarafa 4, Kata 26 na Vijiji 98. Kuna taasisi za afya 54 ambazo 2 ni Hospitali, moja ya Serikali na nyingine inaendeshwa na Shirika la Dini, Vituo vitano vya Afya ambapo vinne ni vya Serikali na kimoja kinaendeshwa na Shirika la Dini, kuna Zahanati 47, kati ya hizi 45 ni za Serikali na mbili ni za Mashirika ya Dini.

Kwa Halmashauri ya Igunga mfuko huu ulitokana na utafiti ambao ulifanywa kitaifa toka mwaka 1990 hadi 1992 ambao ulionyesha kuwa watu wengi wanaoishia Vijijini na Mijini wako tayari kuchangia ili kuondokana na tatizo la ukosefu wa madawa na vifaa vya afya kwenye taasisi za afya. Toka kuanzishwa kwake Igunga, mfuko huu umekuwa ukijiendesha vizuri sana hadi kufikia TOA kuchagua kesi hii kama mbinu bora ya kulipia huduma za afya hapa Tanzania ambapo Halmashauri nyingine zinaweza kwenda kupata uzoefu.

Mfuko wa Afya ya Jamii uliundwa mwaka 1995 na washauri wa Kitanzania na ukafanyiwa majaribio Wilayani Igunga. Utafiti uliofanyika mwaka 1996 ulibaini kuwa watu 21,046 kati ya 26,308 walikubali kuchangia mfuko. Kabla ya utekelezaji wa mfuko huu kila taasisi ya afya ilipata madawa muhimu kupitia mfumo wa "push" yenye thamani ya shs. 150,000 kwa kifurushi, mgawanyo huu ulitosheleza asilimia 45 tu ya mahitaji ya taasisi zote za afya. Fedha zinazopatikana zinatengeneza daraja kati ya mahitaji ya huduma za afya na upungufu wa raslimali katika huduma hizi. Mfuko wa Afya ya Jamii ni namna ya kukusanya raslimali katika jamii kuziba pengo kwenye utoaji wa huduma za afya.

Katika kusimamia utekelezaji wa mfuko, Halmashauri ilitunga sheria ndogo mwaka 2002 na Kuanzisha Bodi ya Mfuko wa Afya ya Jamii chini ya kifungu 86A cha Sheria za Serikali za Mitaa za Wilaya Namba 7 ya 1982.

## 2.0 TATIZO LILILOKUWEPO KABLA YA UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII

Kabla ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Afya ya Jamii mwaka 1996, ubora wa huduma za afya ulikuwa chini na mazingira halisi ya utoaji huduma yalikuwa duni. Sera ya Taifa ya Afya inahitaji kila Kijiji kiwe na Zahanati na kila Kata iwe na Kituo cha Afya. Kwa hiyo mahitaji yalikuwa Zahanati 96 na Vituo vya Afya 26. Jedwali 4.8 linaonyesha hali ilivyokuwa.

**Jedwali 4.8: Taasisi za afya za Halmashauri ya Igunga**

| Tasisi | Binafsi/dini | Serikali | Jumla | Mahitaji | Pungufu |
|---|---|---|---|---|---|
| Hospitali | 1 | 1 | 2 | 1 | +1 |
| Vituo vya afya | - | 4 | 4 | 26 | 22 |
| Zahanati | 2 | 18 | 20 | 96 | 76 |
| Jumla | 3 | 23 | 26 | | |

**Source: Igunga DC 2011**

Kabla ya utekelezaji wa mfuko huu hali ilikuwa mbaya sana. Taasisi zote za afya zilikuwa zikitoa huduma kwa watu 203,341 ambao ni juu kabisa ya uwezo. Wagonjwa walilazimika kutembea umbali mrefu kati ya kilometa 15 – 20 kufuata huduma za afya ilihali kilometa zinazoshauriwa ni mbili. Katika taasisi za afya kulikuwa na ukosefu wa kutisha wa madawa na vifaa vingine muhimu. Kipato kidogo cha wanajamii pia kiliongeza ugumu kuweza gharama za huduma za afya na hivyo kutegemea uganga wa kienyeji kama kimbilio. Hatimaye vifo vya wanawake vikaongezeka na kufikia 362/100,000 wakati vifo vya watoto wachanga viliongezeka hadi 99/1000. Ushiriki mdogo wa jamii katika maamuzi na michango kwenye Masuala yanayoathiri afya zao hasa wanawake na watoto chini ya miaka mitano ilichangia zaidi hali hii.

## 3.0 MALENGO

Wadau wa Afya wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga waliamua kubadili hali mbaya ya huduma za afya kwa kulenga yafuatayo;

(i) Kuboresha usimamizi wa huduma za afya kupitia Ugatuaji na kuwapa uwezo wanajamii kufanya maamuzi na kuchangia kwenye Masuala yanayohusu afya.

(ii) Kukusanya raslimali fedha kutoka kwa jamii ili kuweza kutoa huduma za afya kwa wanajamii na kupunguza dharura kupitia mbinu ya malipo kabla.

(iii) Kutoa huduma za afya zilizo bora na rahisi kupitia mbinu za fedha endelevu


(iv) Kuongeza ufanisi, usawa, ubora na uhakika wa fedha katika kulipia na kutoa huduma za afya.

## 4.0 MKAKATI WA UTEKELEZAJI

### (i) Kuandikishwa kwa Wanachama wa mfuko


Kama ilivyotajwa hapo mwanzo, uanachama kwenye mfuko huu ni wa hiari na kila nyumba katika Halmashauri huchangia kiasi kinachofanana cha ada ya uanachama kama walivyokubaliana wanajamii wenyewe na kadi ya afya hutolewa kama kitambulisho. Walioandikishwa na michango yao inaonekana kwenye mchoro Na 4.5 na kitambatanisho 4.1. Takwimu zinaonyesha kuwa idadi ya wafaidika, michango ya jamii na ada zimekuwa zikiongezeka kila mwaka. Kinyume chake, fedha toka Serikalini (linganifu na michango ya jamii) hazikuja kwa baadhi ya miaka. Kwa mfano mwaka 1996, 1997, 1999, 2003, 2005 na 2008 Serikali haikuingiza fedha kwenye mfuko. Rejea mchoro Na. 4.5 na kiambatisho 4.1.

**Mchoro 4.5: Mtiririko wa Kaya Kujiunga na Mfuko**




**Chanzo: Igunga DC 2011**

**Mchoro 4.6: Mtiririko wa Fedha toka Serikali Kuu linganifu na Michango ya Jamii**




**Chanzo: Zimekokotolewa toka Igunga 2011**

**(ii) Kuanzishwa kwa Bodi ya Halmashauri ya Huduma za Afya**

Bodi ya Halmashauri ilianzishwa ikiwa na wajumbe wanne kutoka jamii zinazofaidika na huduma za afya, kati yao wawili ni wanawake, mmoja toka asasi zisizo za kibiashara na mmoja toka watoa huduma za afya binafsi. Wengine ni Afisa Mipango wa Halmashauri, Mganga Mkuu wa Halmashauri ambaye ni Katibu, mjumbe anayewakilisha Hospitali ya Wilaya na mwakilishi wa Timu ya Menejimenti ya Afya ya Mkoa. Mwenyekiti huchaguliwa na wajumbe wa bodi hii.

**(iii) Kuanzisha Kamati za Afya za Kata**

Kamati za Afya za Kata zilianzishwa zikiundwa na Diwani wa Kata husika, Afisa Mtendaji wa Kata, Mwalimu mmoja toka Shule ya Msingi iliyopo ndani ya Kata husika (kwa kubadilishana) na huteuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata, wanachama wawili kutoka katika jamii ambao mmoja lazima awe Mwanamke na Mfawidhi wa Taasisi ya Afya katika Kata ambaye ndiye Katibu, mjumbe mmoja anayeteuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata na mwakilishi mmoja toka asasi za kijamii anayeteuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata.

**(iv) Kuimarisha Bodi ya Halmashauri ya Huduma za Afya na Kamati za Afya za Kata**

Bodi na Kamati hizi zimekuwa mstari wa mbele katika kusukuma utekelezaji wa mfuko. Maeneo ambayo vyombo hivi vimetoa msaada mkubwa ili kuongeza ubora wa huduma za afya ni kuandaa mipango, kuendesha kampeni za uhamasishaji, usimamizi na ufuatiliaji wa siku hadi siku wa maendeleo ya mfuko. Uelewa wa kutosha wa kaya juu ya mfuko huu huongeza utayari wa kulipa na uwezo wa kujiunga na mfuko. Ufuatiliaji na upimaji wa mfuko na kutafuta mikakati sahihi ya kuendelea na wanachama waliopo na kuongeza kiasi cha uandikishaji.

**(v) Kusambaza Madawa ya ziada kwenye Taasisi za Afya**

Ili kukabiliana na mahitaji ya jamii ilibidi kununua baadhi ya madawa kujazia pengo lililopo kwenye mgawo wa kawaida wa madawa wa Wizara ya Afya. Jedwali 4.9. linaonyesha mtiririko wa matumizi ya kununulia madawa ya ziada kutumia mfuko wa CHF. Kwa miaka mitatu, gharama za madawa ya ziada zilifikia Sh. 52,680,000/=; mtiririko huu unaonyesha kupanda na kushuka kwa mgawo wa madawa wa kawaida ikidhihirisha kuwa mgawo huu hauwezi kukidhi mahitaji ya mfuko wa madawa na vifaa vya afya. Mtiririko unaopungua unaashiria kuna ongezeko la mgawo wa madawa toka Serikali, ndio maana manunuzi toka sehemu nyingine yanapungua.

**Jedwali 4.9: Madawa yaliyonunuliwa na CHF (2009-2011)**

| Mwaka | Thamani TZS |
|---|---|
| 2009 | 17,738,000.00 |
| 2010 | 19,350,000.00 |
| 2011 | 15,592,000.00 |
| **Total** | **52,680,000.00** |

**Chanzo: Igunga DC 2011**

**(vi) Ukarabati wa Taasisi za Afya**

Kati ya mwaka 1998 na 2005, mfuko wa CHF ulitumika kukarabati taasisi 20 zilizopo Nsimbo, Nanga, Ziba na Choma ambazo ni Vituo vya Afya; na Buhekela, Uswaya, Igumo, Mwisi, Mizanza, Ulaya, Mwamashimba, Itunduru, Isakamaliwa, Kininginila, Itumba, Mwalala, Mwamashingo, Bukoko, Igurubi ambazo ni Zahanati. Angalia picha hapa chini.



*Kituo cha Afya cha Igurubi kilikarabatiwa kwa gharama za CHF*

**(vii) Kuhamasisha Jamii**

Jamii pia inatakiwa kujishirikisha katika mchakato huu wa kupata taarifa za maendeleo ya mfuko. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Igunga kuna mikutano ya mfuko ya mara kwa mara yenye lengo la kuhakikisha jamii ina uelewa wa kutosha kuhusu mfuko huu. Kuzitembelea jamii katika makazi husaidia kuongeza uandikishwaji na utambuzi wa kaya zisizojiweza ili kuziingiza kwenye orodha ya wanaostahili kupunguziwa malipo ili kuwalinda maskini.

**(viii) Kununua Samani**
Samani ni mojawapo ya mahitaji muhimu katika mfuko huu ili kuhakikisha kuna mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Halmashauri ya Igunga imenunua samani kwa ajili ya Zahanati sita za Mwenzugi, Mwabulele, Mwanyangula, Bukama, Majengo na Igunga zenye thamani ya shs. 11,197,000/=

**(ix) Kufanya Usimamizi, Ufuatilialiaji na Marejeo ya Utekelezaji wa Mfuko**
Kipengele muhimu cha mfuko huu ni ufuatiliaji kuanzia ngazi za chini. Kuna mbinu mbalimbali ambazo zingeweza kuliimarisha hili. Mbinu rahisi imekuwa kuamuru Vituo vya Afya na Zahanati kuleta taarifa za mwezi, robo mwaka na mwaka juu ya shughuli za mfuko kwenye Halmashauri ili kusaidia wadau kupata uelewa wa shughuli za mfuko.

**(x) Kuanzisha mfumo wa Rufaa kwenda Hopitali ya Nkinga**
Kuna matatizo ya kiafya ambayo hayawezi kumalizwa katika Zahanati au hata Vituo vya Afya, haya hupewa rufaa za kwenda Hospitali ya Wilaya.

**(xi) Kupatikana kwa ajira ya muda kwa watumishi wa Afya**
Katika Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati huwa kuna upungufu wa watumishi mara nyingi ambao hulazimu menejimenti ya mfuko kuajiri watumishi wa muda mfupi. Karibu watumishi sita wa muda mfupi walipewa mikataba ya kufanya kazi katika Zahanati 5 na Kituo cha Afya kimoja.

## 5.0 KIASI NA AINA ZA RASLIMALI ZILIZOTUMIKA

### Fedha
Makusanyo ya Mfuko wa CHF toka 1996 yalikuwa shs 936,163,550 kwa miaka 16. Vyanzo vya fedha vinahusisha fedha za Serikali Kuu (linganifu na za mfuko), michango ya wanachama na ada za watumia huduma za afya. Angalia jedwali 4.10. Mwaka 2008 shs 3,935,650 zilitumika kwa ajili ya rufaa za wagonjwa 277 katika Hospitali ya Nkinga na mwaka 2011 shs 6,000,000 zilitumika kwa ajili ya rufaa 184 za wanachama wa mfuko wa CHF. Takribani shs 131,896,550 zilitumika kununulia gari la mfuko.

**Jedwali 4.10: makusanyo ya CHF kwa miaka 16 toka1996**

| **Wachangiaji** | **Kiasi TZS** | **%** |
|---|---|---|
| Ada ya Wanachama | 136,950,310.00 | 15 |
| Michango ya Jamii | 436,375,000.00 | 47 |
| Fedha linganifu | 359,838,270.00 | 38 |
| **Jumla** | **936,163,580.00** | **100** |

**Chanzo: Igunga DC 2011**

**Raslimali Watu**

Mfuko wa CHF unasimamiwa na kuendeshwa na Madiwani, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Bodi ya Halmashauri ya Huduma za Afya, Mhasibu wa CHF, Kamati za Afya za Kata pamoja na Kamati za Vituo vya kutolea Huduma za Afya. Pia kuna watumishi sita wa muda wanaofanya kazi kwenye Zahanati za Vijijini.

**Raslimali nyingine**

Huduma za mfuko wa CHF zinafanyika katika ofisi ya chumba kimoja ndani ya Hospitali ya Wilaya. Halmashauri imenunua gari moja. Gari hili (landacruiser hardtop) linatumika kusambaza madawa na mahitaji mengine kwenda kwenye taasisi za afya, kufanya usimamizi ufuatiliaji na kuhamasisha jamii.

**6.0 MAFANIKIO YA CHF WILAYANI IGUNGA**

**Ubora wa huduma umeongezeka**

Utendaji wa mfuko huu kwa Halmashauri ya Igunga unavutia. Ubora wa huduma umeongezeka sana katika kupatikana na kufikika. Upatikanaji wa uhakika wa dawa muhimu umeongezeka toka 45% mwaka 1996 hadi 80% mwaka 2011 na upatikanaji wa vifaa vingine vya afya umeongezeka toka 35% hadi 75% kwa kipindi hicho hicho. Mwaka 1996 ilipoanzishwa CHF, waliandikishwa wanachama 2,448, lakini mpaka mwisho wa mwaka 2011 wanachama waliongezeka hadi kufikia 7,856. Hata hivyo hii ni 30% tu ya walengwa ambao ni Kaya 26,260. Halmashauri imeweza kuajiri watumishi wa afya sita kupitia mfuko huu. Halmashauri ya Igunga hulipa 5% ya makusanyo yote ya mfuko kwa watoa huduma za CHF kama motisha.

Toka kuanza kwa mfuko huu, umbali kutoka kaya kwenda kwenye taasisi za afya umepungua na kufikia wastani wa km 10 – 15. Vifo vya akina mama vimepungua toka 362/100,000 mwaka 1996 hadi 145/100,000 mwaka 2011, na vifo vya watoto wachanga vimepungua toka 98/1000 hadi 56/1000 mwaka 2011.

**Uboreshaji wa Miundombinu ya Afya**

Mfuko umelipia ujenzi wa Zahanati mpya za Vijiji vya Akimbo, Nyandekwa, Mwashiku, Ikunguipiana, Kidalu, Mwanshoma, Ntobo, Igumu, Ibole, na Kagongwa kulingana na sera ya taifa ya kila Kijiji kuwa na Zahanati. (Angalia picha chini). Taasisi sita za afya zimeunganishwa na umeme wa Gridi ya Taifa na gharama zinalipwa na mfuko. Taasisi zilizounganishwa ni Vituo vya Afya vya Nanga na Choma na Zahanati za Ndembezi, Mwisi, Igunga na Ziba.



*Zahanati ya Igumo iliyojengwa kwa fedha za CHF*

**Mfumo bora wa Rufaa**

Halmashauri imefanikiwa kuanzisha mfumo wa rufaa kwa wanachama kwenda Hospitali ya Wilaya. Mfuko umenunua gari ili kuboresha utoaji huduma, usimamizi, ufuatiliaji,uhamasishaji na ugawaji wa dawa na vifaa vingine vya afya mpaka maeneo ya Vijijini angalia picha chini.



*Gari la Mfuko wa CHF la Wilaya*

**Matokeo mengine/ya ziada**

Halmashauri ya Igunga imekuwa ya mfano katika utekelezaji wa CHF tangu 1996. Kati ya Halmashauri 133 za Tanzania Bara, jumla ya Halmashauri 102 zimetembelea Igunga kupata uzoefu juu ya utekelezaji bora wa mfuko wa CHF. Kati ya hizo ni Halmashauri za Nzega, Urambo, Kiteto, Sikonge, Rorya, Rufiji na Misenyi. Mfano huu mzuri si kwa Tanzania tu bali na nje ya mipaka pia. Mwaka 2008 chini ya ufadhili wa GTZ walifika wageni toka Msumbiji kujifunza Igunga. Mwaka 2010 Halmashauri ya Igunga ilikuwa mojawapo ya Halmashauri zilizotekeleza vizuri CHF na mwaka 2012 Igunga ilipata kombe la ushindi na zawadi ya sh. 150,000 (angalia picha chini).



*Mkurugenzi wa Halmashauri akionyesha tuzo ya utendaji mzuri wa CHF, 2012*

**Ushirikishaji wa wadau**

Kwa kawaida kuna umuhimu wa kuwashirikisha wadau katika mazingira ya Vijiji kusaidia jitihada za mfuko; kwa mfano taasisi za dini, vyama vya ushirika na makundi mengine ya kijamii yalishirikishwa. Mfumo wa CHF wa Igunga umekuwa na ubunifu wa kushirikiana na wadau wakuu ndani ya Wilaya. Mashirika matatu yasiyo ya kiserikali (NGO'S) na vyama vingine vya msingi vya ushirika vilichangia jumla ya sh. 5,450,000/= ili kutunisha mfuko wa CHF kama inavyoonyesha kwenye jedwali 4.11

**Jedwali 4.11: Michango ya washirika wa CHF, 2011**

| Asasi | Ruzuku TZS | Idadi ya wanufaika |
|---|---|---|
| YADEC | 500,000 | 100 |
| JIDA | 900,000 | 180 |
| TDTF | 250,000 | 50 |
| Jumla Ndogo | 1,650,000 | 330 |
| Partner Cooperative society | | |
| Mwamashimba | 2,000,000 | 400 |
| Kinungu | 800,000 | 160 |
| Itunduru | 600,000 | 120 |
| Bukama | 400,000 | 80 |
| Jumla Ndogo | 3,800,000 | 760 |
| Jumla Kuu | 5,450,000 | 1090 |

**Chanzo: Igunga DC 2011**

## 7.0 CHANGAMOTO WAKATI WA UTEKELEZAI

Changamoto za kitaasisi na menejimenti zinazokumba utekelezaji wa mfuko zinajumuisha upungufu wa watumishi, upungufu wa taasisi za afya, upotevu wa fedha kutokana na misamaha/ punguzo na idadi ndogo ya nyumba za watumishi wa afya Vijijini.

**Upungufu wa Watumishi.** Mahitaji ya watumishi wa afya kwa Wilaya nzima ni watumishi 565 wa kudumu wa kada mbalimbali. Kwa sasa kuna watumishi 314 tu, kati yao 140 ni wataalam na 174 si wataalam kamilifu. Kuna upungufu wa watumishi wa afya 251 ambao ni sawa na asilimia 44 ya mahitaji.

**Upungufu wa taasisi za afya.** Kuna taasisi 4 tu za afya katika Mji mdogo wa Igunga. Vijiji 46 (47%) havina taasisi zozote za afya.

**Sera Pana ya misamaha.** Sera ya msamaha iliondoa makundi yote ya wasiojiweza na inatoa msamaha kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano, wanawake wajawazito, watoto yatima, wazee na wengine wasioweza kulipa. Sera hii inapelekea uchangiaji mdogo kutoka kaya zenye makundi haya. Karibu 90% ya wakazi wanategemea kilimo hivyo pato la kaya ni la msimu. Kutotabirika kwa mvua na mabadiliko ya hali ya hewa kunaleta mazao machache na hivyo kaya kushindwa kulipia michango yao kwenye mfuko na kulazimisha mfuko kutumia ada za watumiaji kujazia mfuko.

**Upungufu wa nyumba za watumishi wa afya**. Watumishi katika taasisi 37 za afya (sawa 742) wanaishi kwenye nyumba za muda tu ambazo zina ubora wa chini na zipo maeneo ya pembeni kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali 4.12.

**Jedwali 4.12: Nyumba za watumishi wa afya Igunga Desemba 2011**

| Aina ya Taasisi | Mahitaji | Zilizopo | upungufu |
|---|---|---|---|
| Zahanati | 90 | 12 | 78 |
| Vituo vya Afya | 40 | 23 | 17 |
| Jumla | 130 | 35 | 95 |

**Chanzo: Igunga DC 2011**

## 8.0 MIKAKATI YA KUPUNGUZA CHANGAMOTO

Kila mwaka kuna ajira mpya za kuongeza watumishi wa huduma za afya. Kulingana na mahitaji, mfuko hutumika kuajiri watumishi wa muda wa afya. Kwa mwaka 2012/2013, kwa kutumia bajeti ya ndani, Halmashauri ya Igunga inatarajia kuajiri watumishi 97 wa afya.

Halmashauri ya Igunga inakusanya fedha kutoka kwa jamii ili kukamilisha ujenzi wa majengo ya vituo vya huduma za afya katika Vijiji na Kata kulingana na maelekezo ya Serikali. Pia Halmashauri itaendelea kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuchangia mfuko wa CHF ili kuboresha hudhuma za afya. Ili kupunguza pengo linalotokana na misamaha, mbinu mbadala

zinatafutwa. Kwa mfano taasisi za dini na vyama vya ushirika huombwa kuchangia gharama hizo.

## 9.0 MIKAKATI KWA AJILI YA UENDELEVU

Halmashauri ya Igunga itaendelea kuimarisha uwezo wa Bodi, Kamati za Kata, Timu ya Menejimenti ya Afya ya Wilaya pamoja na watoaji wa huduma kwa kuwapatia stadi zinazofaa na taarifa juu ya faida na gharama za CHF. Pia Halmashauri ina Mpango wa kuanzisha safari za masomo kwenda kwenye taasisi ambazo zimefanya vizuri kwenye uendeshaji wa mfuko wa CHF ndani na nje ya nchi.

Kwa mwaka 2012/2013 Halmashauri imetenga shs 165,000,000/= kukamilisha ujenzi wa nyumba 10 kwenye Zahanati 10 za Vijiji na shs 42,632,833 kumalizia ujenzi wa Zahanati mpya nane.

Pia inakadiriwa kuwa mpaka mwaka 2015 takribani 45% ya kaya zote za Halmashauri zitakuwa zimesajiliwa kama wanachama wa CHF. Kiwango cha mchango wa uanachama umeongezwa kutoka sh 5,000/= mwaka 1996 hadi sh. 10,000/= Agosti 2011 kwa mwaka. Halmashauri inaandaa mpango wa madaktari warukao kwa ndege kutoka Taasisi ya CCBRT na Hospitali ya rufaa ya KCMC ili kuboresha huduma za afya. Hii itaboresha huduma na kupunguza matukio ya rufaa.

## 10.0 SIRI YA MAFANIKIO

(i) Dhamira thabiti ya Timu ya Menejimenti ya Halmashauri kuhakikisha kuwa mfuko wa CHF unafanya kazi vizuri. Wajumbe wote wanafanya kazi kama timu kuhakikisha CHF inafaulu.
(ii) Wakuu wa Idara wenye dhamira thabiti. Kwa mfano ndoto ya kununua gari maalumu kwa ajili ya shughuli za CHF inaonyesha dhamira yao ya kuhakikisha uwepo wa huduma bora toka CHF.
(iii) Uvumbuzi wa kuunda Kamati za Usimamizi wa mfuko kuanzia ngazi ya Halmashauri hadi Kijiji. Kuna kitengo cha uratibu katika ngazi ya Halmashauri ambacho kinaratibu shughuli zote za CHF na kuhamasisha jamii kuchangia kwenye mfuko. Muundo huu unafanya kazi vizuri na ni muhimu katika udhibiti.
(iv) Ushirikishwaji wa wadau ndio siri kuu ya mafanikio. Kulikuwa na ushirikiano kati ya Kaya na Serikali za Vijiji na watumishi wa CHF katika Zahanati, Kata na Halmashauri. Halmashauri ilishirikiana vizuri na Serikali Kuu hivyo kukawa na mtiririko mzuri wa mahitaji ya afya. Chama cha Ushirika na taasisi za dini zilishiriki kikamilifu. Kwa mfano Hospitali ya rufaa ya Wilaya ya Igunga (Nkinga) inamilikiwa na taasisi ya dini. Zaidi ya hayo ushiriki wa jamii ulikuwa muhimu sana kuleta mafanikio ya mpango huu katika Halmashauri ya Igunga ikilinganishwa na Halmashauri nyingine Tanzania.

(v) Mwisho, mfuko wa CHF umekuwa mfumo uliopangika wa rufaa. Kesi ngumu hupewa rufaa kwenda Hospitali ya Rufaa (Wilaya) ya Nkinga. Ikilinganishwa na mifumo mingine ya rufaa ambako wagonjwa wanatakiwa kujihudumia wenyewa kwenye Hospitali za Rufaa, CHF ya Igunga hulipa sh. 30,000/= kwa kila mgonjwa anayepelekwa rufaa ili kumpunguzia gharama za rufaa. Pia mfuko una mpango wa kulipia gharama za usafiri kwa wanachama wanaopewa rufaa za kwenda Hospitali za Rufaa za Bugando na Muhimbili.

# Sura ya Tano: Maendeleo ya Jamii Kiuchumi

Sura ya Tano inahusisha visa mkasa vinne vinavyohusu juhudi za maendeleo ya jamii kiuchumi kwa asilia hususan matumizi ya dhana mpya inayojulikana kama vuguvugu la "**Zao moja kwa Kijiji kimoja**" kwa kifupi *OVOP* ikimaanisha jamii asilia kwa ujumla kuchagua na kuendeleza bidhaa au mazao machache yanayoonekana kama msingi wa kiuchumi yanayoweza kukwamua wananchi wa eneo husika. Dhana hii imejengwa juu ya nadharia ijulikanayo kama "maendeleo ya jamii asilia kulingana na mazingira yaliyopo" ambayo husisitiza kuchagua na kuendeleza bidhaa chache za kipekee zinazopatikana eneo husika tu; mfano zao la Vanila ni zao adimu la bei kubwa na halipatikani kila mahali, hushamiri vizuri mikoa ya Kagera na Morogoro, kwa hiyo ni fursa yao kubwa kiuchumi. Mfano mwingine ni Tangawizi ambayo Halmashauri ya Wilaya ya Same kwa kuasili vuguvugu la OVOP imeamua kuelekeza nguvu zao katika kuendeleza zao hili na kuliingiza katika mpango wa mnyororo wa ongezeko la thamani na imesaidia sana kupata faida kubwa, kuongeza kipato cha kaya na kuboresha maisha ya wakulima husika. Halmashauri ya Chamwino ni modeli nyingine ya kuigwa kwa jinsi walivyoweza kuamsha ari na kukusanya wakulima za zabibu kwenye vikundi vya ushirika kuunganisha nguvu zao kuzalisha zao la zabibu, linalohitaji mtaji mkubwa lakini ni zao la kibiashara mkoani Dodoma. Kutokana na uamuzi wao wa kuasili vuguvugu la OVOP wamepata faida lukuki za ongezeko la kipato cha kaya, kijamii na kiuchumi kuliko mazao mengine yaliyokuwa yanalimwa kimazoea tu. Kesi ya Halmashauri ya Wilaya ya Iramba imejikita katika kuongeza thamani ya mbegu za Alizeti, kupitia jitihada za ushirikiano na sekta binafsi (PPP) na huduma bora za kilimo kwa wakulima.

Dhana ya OVOP asili yake ni Wilaya ya Oita nchini Japani kwenye miaka ya 1970, na ilitumika kufufua uchumi wa Wilaya hiyo ambayo kabla ya hapo ilikuwa miongoni mwa Wilaya fukara sana nchini humo. Wazo la asili lililenga kila Kijiji cha Oita kuchagua bidhaa moja ya kipekee kisha kuiendeleza kibiashara na kuipigia debe au kuitangaza nchini kote na nje ya Japani kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika kimataifa.

Lengo kuu la vuguvugu la OVOP ni kufufua maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Wilaya na Mikoa husika kwa njia ya kuamsha ari ya wananchi kufufua uchumi wao bila kushurutishwa. Kabla ya vuguvugu la OVOP huko Oita, waanzilishi walijikita kuunganisha mitaji ya kijamii kupitia michezo (soft ball tournament) pamoja na mahusiano na Miji dada rafiki nje ya nchi. Mkakati huu pia ulilenga kuwaleta pamoja wananchi fukara na kuwapa fursa ya kubadilishana mawazo, uzoefu na ikawa mwanya wa kupenyeza sera mbadala ya uchumi wa jamii kwa kuongeza thamani na kujenga mshikamano. Hatimaye walianza kuweka miundo mbinu ya kuendeleza bidhaa zao ambazo si za kawaida na kuziongeza thamani. Hii ilihusisha kuanzisha viwanda vya kuchakata na kusindika mazao yao na kuendeleza vivutio vya utalii hasa utalii wa ndani ya nchi na jinsi jamii inavyoweza kupanua upeo na kutambua uwezo wao.

Vuguvugu la OVOP linatakiwa kujengwa kwenye misingi ya "mtaji wa kijamii". Pia, halitakiwi kutafsiriwa kuwa Kijiji kinalazimika kuchagua zao moja tu bali jamii ina uhuru wa kuchagua bidhaa moja hadi tatu ambazo jamii itafaidika zaidi kwa vigezo vya uzalishaji, hali ya hewa, ardhi, maliasili, upatikanikaji wa mali ghafi, uzoefu, stadi, maarifa na masoko. Pia, Vuguvugu la OVOP siyo la maelekezo ya mamlaka za juu kwenda chini, bali huhitaji ushawishi wa kina wa wanufaika. Jamii ikifanya maamuzi, hujikita kwenye uzalishaji wa bidhaa pekee zenye tija katika eneo husika. Mamlaka za serikali za Mitaa zinawajibika kusaidia jitihada za jamii kupitia huduma za ugani, uchakataji/usindikaji, utambulishaji na utangazaji wa bidha na utafutaji wa masoko. Hii inajumuisha kuendeleza uzalishaji wa ndani kwa matumizi ya ndani. Walaji wenyeji na utalii wa ndani vinatakiwa kuwa soko la awali kabla ya kufikiria masoko ya nje.

Vuguvugu la "zao moja kijiji kimoja" ni njia ya kuendeleza stadi za jamii za ujasiriamali kwa kutumia rasilimali zinazopatikana katika eneo husika, ujuzi asilia na uzoefu uliopo katika jamii ili kuziongezea thamani na kuzipa bidhaa hizo utambulisho na umiliki wa jamii. Kimsingi, vuguvugu la OVOP ni matumizi ya maarifa kuhusu rasilimali-ardhi na rasilimali nyingine yanayozingatia uhifadhi wa mazingira na huu ndio msingi wa nadharia ya maendeleo ya jamii asilia. Wale walioasisi vuguvugu la OVOP wana kauli-mbiu isemayo "fikiri kimataifa, tekeleza kulingana na mazingira asilia " yaani "*think globally, act locally*".

**Kisanduku 5.1. Fikiri kimataifa, tekeleza kulingana na mazingira asilia**

Kauli-mbiu hii imetumika kwenye sekta mbalimbali hasa Mipango Miji, Elimu na Mazingira. Kauli-mbiu hii inawataka watu wote kuzingatia usalama na afya ya dunia nzima na kuchukua hatua katika mazingira yao, jamii na miji inayowazunguka. Kabla Serikali hazijaanza kutekeleza sheria za uhifadhi wa mazingira, watu binafsi walianza kujipanga kwa pamoja kulinda makazi na viumbe mbalimbali wanaoishi ndani yake. Jitihada hizi ni za kijamii zaidi. Vuguvugu hili lilianzia ngazi za msingi, hata hivyo kwa sasa limekuwa ni dhana yenye umuhimu mkubwa kimataifa. Dhana hii inasistiza kufanya biashara kulingana na mahitaji ya ndani na ya kimataifa.

Vipengele muhimu vinavyotokana na kesi zilizowasilishwa kwenye sura hii:

- OVOP siyo mfumo wa maelekezo kutoka juu kwenda ngazi za msingi, kwa hiyo, ili Halmashauri zifanikiwe katika maendeleo ya jamii kiuchumi, kunatakiwa kuwe na jitihada za wataalam na viongozi ya kufanya maandalizi ya kutosha ya jamii. Maandalizi ya kijamii yafanyike kwanza kwa kuamsha ari ya walengwa yaani jamii asilia(kaya,kijiji,uongozi,soko,taasisi) watambue fursa walizo nazo, kuandaa na kuziimarisha asasi za kijamii zitakazosimamia shughuli za uzalishaji , kutengeneza sharia na kanuni zitakazotumika kama mwongozo wa matumizi na usimamizi wa rasilimali za jamii, na kuweka mtandao madhubuti wa kuunganisha vikundi vya uzalishaji na masoko

pamoja na taasisi za fedha. Hii inatakiwa kuwa sehemu ya mchakato wa kukuza vikundi mpaka vitakapofuzu/kukomaa.

- Masoko ya bidhaa na mbinu za kuuza kwa faida ndiyo changamoto kubwa inayozikabili Halmashauri nyingi chini. Kukiwepo na masoko ya uhakika na bei yenye tija, wazalishaji wataitikia na kuzalisha kwa wingi. Ni wajibu wa maafisa ugani kutafuta na kuwapa wazalishaji taarifa za masoko na mabadiliko ya bei na kuwaunganisha kwenye masoko ya bidhaa.
- Utaratibu wa kuzipa bidhaa utambulisho na umiliki (*branding)* ni mkakati muhimu sana wa kuteka soko la bidhaa. Kwa bahati mbaya au kwa kutotambua hapa Tanzania tunazo bidhaa chache sana zenye utambulisho na umiliki mfano "Matombo sweet" ni machungwa makubwa na matamu sana yanayozalishwa Matombo. "Dodoma wine" ni mvinyo maarufu unaozalishwa Dodoma, "Same ginger" ni Tangawizi kutoka Wilaya Same, "Morogoro Vanilla" ni vanila inayo zalishwa Morogoro vijijini; "Kula na Bwana" ,"shingo ya mwali" ni aina maalumu za mpunga wa Morogoro, "liquid gold" ni mafuta ya alizeti toka Singida "Itigi honey" ni asali maarufu inayozalishwa Manyoni kutokana na maua miti inayojulikana kama Itigi-Sumbu thicket na ambayo haipatikani popote pengine duniani. Huenda tunazo bidhaa nyingi maarufu lakini hapajakuwepo na juhudi ya kuzitambua, kuzipa utambulisho na umiliki.
- Uwezeshaji madhubuti ndiyo injini ya mafanikio kwa juhudi zinazotekelezwa kwa kutumia vuguvugu la OVOP. Wawezeshaji (maafisa ugani) ndio kiungo kati ya wazalishaji na taasisi mbalimbali kama za vituo vya utafiti wa teknolojia bora ya uzalishaji,vyuo vikuu kwa ajili ya maarifa katika fani fulani mahsusi, masoko ya bidhaa kwa ajili ya taarifa za soko na bei, vyombo vya fedha kwa ajili ya huduma za fedha, walaji na wateja kwa ajili ya kutambua soko linapenda bidhaa zenye ladha na sifa zipi na kubadilisha uzoefu kupitia ziara za mafunzo. Kwa mantiki hii uwezo na sifa za wawezeshaji ndizo zitakazosababisha mafanikio. Ndiyo maana ni muhimu sana kwa Halmashauri kuhakikisha kwamba inawapa maafisa ugani mafunzo ya mara kwa mara wapate maarifa yanayokwenda na wakati, kuwajengea stadi na kuwabadilisha halitabia ziendane na lengo la kufikia maendeleo ya jamii kiuchumi. Kwa hiyo, idadi na ubora wa wawezeshaji ni mambo ya muhimu katika kufanikisha miradi kwa vuguvugu la OVOP.
- Viongozi wenye maono na wapenda maendeleo ni hazina muhimu katika mafanikio ya OVOP. Inapendekezwa kwamba iwapo kiongozi kama vile Mkurugenzi au kiongozi yeyote ameanzisha shughuli za uzalishaji kwa kutumia vuguvugu la OVOP, apewe muda wa kutosha atoe usimamizi elekezi na kufikia malengo tarajiwa kabla ya kuhamishwa. Hii ni kwa sababu hakuna uhakika kwamba mrithi wake atakuwa na nia ya kuendeleza juhudi zilizokwishaanza. Kama hakuna uendelevu, huo ndio mwanzo wa kuwakatisha wakulima na wazalishaji wengine tamaa na watachoka kwani hawaoni mwisho na matunda ya juhudi zao.

- Suala la kuongeza thamani kwa bidhaa zote ni la muhimu na ni wajibu wa wadau wote kusisitiza hili. Ni lazima kuwa na vifungashio vinavyowavutia wateja, kuzipa bidhaa vibandiko vya majina mazuri kulingana na kanuni za soko kimataifa. Wazalishaji wajizuie kuuza mali ghafi, kwa hiyo wadau wavisaidie vikundi vya wazalishaji kuongeza thamani ya bidhaa zao kupitia mnyororo wa kuongeza thamani.
- Mnyororo wa ongezeko la thamani kwa bidhaa za wakulima ndiyo jibu kwa suala uzalishaji duni na kutokuwa na uhakika wa chakula katika kaya. Hata hivyo lazima pawepo na uratibu mzuri katika kila hatua ya kuongeza thamani. Vuguvugu la OVOP linapaswa kuongozwa na mahitaji ya soko la jamii husika, kitaifa na kimataifa. Soko hili lisibanwe na kuwa la mazao ya kilimo pekee. Zipo maliasili za aina nyingi kama vile maporomoko ya maji, mapango, chemichemi za maji moto, miamba /majabali ya kipekee, miti, vyakula vya asili, nyumba za asili vinavyoweza kutumika kama mtaji na hivyo “Tanzania yenye neema haijafikiwa”.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO

## UENDELEZAJI WA MAZAO YASIYOTHAMINIWA




*Vanila ya Morogoro*

*Tangawizi ya Morogoro*

## 1.0 UTANGULIZI

Miaka ya hivi karibuni, vuguvugu la zao moja kwa kijiji kimoja (OVOP) limeenea nchi za jirani na mataifa yanayoendelea yakiwepo yale ya Afrika na Amerika ya kusini. Hapa nyumbani Tanzania dhana hii inaenezwa na watendaji na viongozi wa Serikali za Mitaa waliopata mafunzo nchini Japan, na bado iko katika hatua za mwanzo sana. Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ni miongoni mwa Halmashauri chache ambazo zimekwisha asili dhana hii. Kwa bahati nzuri Halmashauri hii imejaaliwa kuwa na mifumo mbalimbali ya mazingira ya uzalishaji na kilimo ambako kunapatikana aina mbalimbali za mazao, mboga hususan yale mazao ya thamani kubwa kama vile vanilla, mdalasini, tangawizi, matunda na pilipili manga. Kuna juhudi za makusudi kuendeleza mazao ya thamani kubwa na wakulima wamehamasishwa kupanua uzalishaji na kuongeza thamani. Juhudi zilizofanywa na uongozi wa Halmashauiri kuendeleza mazao yasiyozoeleka ndizo zilizowasukuma uongozi wa Umoja wa Wakurugenzi waliosoma Osaka Japani (TOA) kuchagua Halmashauri ya Wilaya Morogoro kuwa kesi ya mfano na mahali ambapo Halmashauri nyingine nchini zinaweza kujifunza. Mkurugenzi Mtendaji Bw. Munisi (aliyekuwepo) ndiye aliyekuwa mwanzilishi wa dhana hii hapa Morogoro. Ubunifu wa Mkurugenzi huyu haukuwa tu kwenye OVOP, bali alifanikiwa sana katika mbinu bunifu za kuwavutia wafanyakazi(waalimu, waganga, wakunga) na kuwafanya wapende kufanya kazi maeneo magumu ya milima ya Uluguru ambako watumishi wengi hupakimbia na hawataki kufanya kazi huko.

Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ni miongoni mwa Halmashauri sita za Mkoa wa Morogogo ambazo zina fursa kubwa ya maendeleo ya kiuchumi na kuboresha maisha ya jamii. Kuna hali nzuri ya hewa na mvua za kutosha kwa ajili ya kilimo na uwekezaji wa aina mbalimbali. Halmashauri hii ipo Kaskazini- Mashariki mwa Mkoa wa Morogoro, kati ya Latitudo 6º00' na 8º00' Kusini mwa Ikweta na kati ya Longitudo 36º00' na 38º Mashariki mwa Greenwich. Imepakana na Wilaya za Bagamoyo na Kisarawe (Mkoa wa Pwani) kwa upande wa Mashariki, Kilombero upande wa Kusini na Mvomero upande wa Kaskazini Magharibi. Halmashauri hii ina eneo la ukubwa wa km² 11,925 sawa na 16.34% ya eneo lote la Mkoa wa Morogoro lenye km² 72,973. Kulingana na ripoti ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002, idadi ya wakazi kwa mwaka 2011 ilikadiriwa kuwa 304,019. Jedwali 5.1 linaonesha mgawanyo wa ngazi za utawala.

Jedwali 5.I: Mgawanyiko wa ngazi mbambali za utawala

| Na. | Tarafa | Kata | Vijiji | Vitongoji |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Bwakira | 5 | 20 | 121 |
| 2 | Mvuha | 5 | 26 | 154 |
| 3 | Mikese | 3 | 11 | 54 |
| 4 | Mkuyuni | 4 | 23 | 118 |
| 5 | Matombo | 7 | 38 | 170 |
| 6 | Ngerengere | 5 | 23 | 99 |
| **JUMLA** | | **29** | **141** | **716** |

***Chanzo: Taarifa za Kiuchumi na Kijamii Wilaya ya Morogoro, 2010***

Kwa wastani kiwango cha joto huanzia 20$^0$C hadi 30$^0$C. Wastani wa mvua ni mm 600 -3000 kwa mwaka. Halmashauri hii hupata mvua za kutosha na kuna misimu miwili ya mvua za vuli na masika. Mvua za vuli hunyesha kati ya mwezi Oktoba –Desemba, mvua za masika hunyesha kuanzia mwezi Machi hadi Mei na kuna kipindi kifupi cha ukame kati ya Januari na Febuari. Mwezi Agosti mpaka Novemba kwa kawaida ni kipindi cha ukame na joto kali. Halmashauri imejaliwa kuwa na ardhi ya kutosha yenye rutuba. Kuna udongo wa kichanga, udongo wa mfinyanzi; na udongo mchanganyiko wa kichanga na mfinyanzi. Eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta 75,321 na linafaa kwa mazao mbalimbali mchanganyiko.

Halmashauri iko kwenye kanda mbalimbali za miinuko: Ukanda wa juu milimani ni 25% ya eneo lote la Wilaya na liko juu ya milima ya Uluguru m 1200 juu ya usawa wa bahari. Hupokea mvua kiasi cha mm 1000 – 3000 kwa mwaka. Eneo hili linafaa kwa kilimo cha maharage, iliki, kahawa, chai, mboga na matunda. Ukanda wa pili ni ukanda wa chini ya milima na umechukua 20% ya eneo lote. Ukanda huu upo kati ya m 600 hadi 1200 juu ya usawa wa bahari. Kiwango cha mvua kwa wastani ni kati ya mm 1000 – 2000 kwa mwaka na kiwango cha juu cha joto ni 29$^0$C. Udongo uliopo katika eneo hili ni wa kichanga na eneo hili linafaa sana kwa kilimo cha mahindi, mihogo na ulezi. Eneo hili linafaa pia kwa ufugaji. Ukanda wa tatu ni ukanda wa chini kwenye uwanda wa Savanna na unachukua 55% ya eneo lote la Wilaya. Ukanda huu unapatikana kati ya m 600 hadi 800 kutoka usawa wa bahari. Kwa wastani hupata mvua kati ya mm 900 hadi 1200 kwa mwaka. Eneo hili limejaaliwa kuwa na mito mingi inayotoka kwenye kanda za miinuko nayo ni mto Mgeta, Kafa, Ruvu, Wami, Msongozi, Mbulumi, na Ngerengere. Mito hii ndiyo chanzo cha uhai kwa wananchi waishio kanda za chini. Udongo wa maeneo haya ni ule ulioletwa na maji ya mito kwenye mabonde na unafaa kwa kilimo cha mahindi, mboga, matunda , mpunga. Kilimo cha umwagiliaji kimeshamiri sana na shughuli za uvuvi ni fursa nyingine muhimu kwenye ukanda huu.

Uchumi wa Halmashauiri ya Morogoro hutegemea kilimo kwa kiasi kikubwa na 82% ya wakazi watu wazima hupata riziki zao kutokana na kilimo cha kujikimu, 6% ni wafanya biashara, 6% wamejiajiri, 4% watumishi maofisini ,1.3% kutokana na ufugaji. Mazao makuu ya chakula ni mahindi, mpunga, mhogo na mtama. Mazao ya biashara ni pamba na mkonge. Pia wanalima aina mbalimbali za mboga, viungo na matunda ya kitropiki.

## 2.0 TATIZO LILILOKUWEPO KABLA YA UENDELEZAJI WA MAZAO YASIYOTHAMINIWA

Japokuwa Halmashauri hii ina uwezo mkubwa wa kuzalisha mazao mbalimbali mchanganyiko, fursa hii inakwamishwa na kilimo cha mazoea na cha kizamani. Wakulima wengi hawafuati kanuni za kilimo bora. Bado wakulima wengi hutumia mbegu za kizamani ambazo hazitoi mazao mengi. Bado wakulima wengi hawajaasili mbegu na teknolojia ya kisasa. Wadudu na magonjwa vimechangia sana katika uzalishaji duni. Pia, mabadiliko ya tabia nchi yamepelekea kutokutabirika kwa kiasi na mtawanyiko wa mvua. Hata mazao machache yaliyovunwa yaliuzwa kama mali ghafi kwa bei za chini kwani hayakuwa na ongezeko la thamani. Kwa hiyo, kaya, hasa zile zinazoishi ukanda wa chini zimekuwa zikikumbwa na uhaba mikubwa wa chakula. Baadhi ya Vijiji kama vile Kijiji cha Mkono wa Mara kwenye kata ya Mkambarani viliwahi kulazimika kuomba chakula cha msaada, jambo ambalo si la kawaida na linaonekana

kama ni aibu. Tatizo la Mkono wa Mara lilizidishwa na ukataji miti wa kukithiri wakati wa kilimo cha tumbaku miaka ya 1970-1980 na hii ilichangia uhaba wa mvua na mvua za mtawanyiko.

## 3.0 MALENGO

Lengo kuu lilikuwa kueneza vuguvugu la kijiji kimoja zao moja (OVOP) ili kuifanya Halmashauri hii kuwa ukanda wa uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula na biashara. Malengo mahsusi yalikuwa :

(i) Kuendeleza mazao yale yenye uwezekano mkubwa wa kustawi vizuri kulingana hali ya hewa na aina za udongo uliopo.
(ii) Kuanzisha kilimo cha mazao ya thamani kubwa.
(iii) Kuongeza thamani kwenye mazao ya wakulima.
(iv) Kuanzisha kilimo kinachozingatia uhifadhi ardhi.
(v) Kuanzisha vituo vya masoko na mfumo wa kukusanya na kupashana taarifa za masoko.

## 4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

**(i) Kupendekeza mazao kulingana na mfumo wa kilimo uliopo**

Kama ilivyoelezwa hapo juu, lengo la OVOP ni kufikia uzalishaji wa hali ya juu wa mazao kwa kuendeleza uzalishaji kulingana na mifumo bora ya kilimo iliyopo. Vigezo kama vile aina na rutuba za udongo, mabadiliko ya tabia nchi vinapaswa kuzingatiwa. Kwa kuanzia na zao la mahindi, hili ni zao la chakula na biashara linalostawi vizuri kwenye uwanda wa chini wa savanna na kwenye mabonde ya mito. Uzalishaji wake hutegemea mtawanyiko wa mvua. Mahindi mabichi ya kuchoma na kuchemsha huuzwa maeneo ya mjini, mahindi makavu huuzwa na kusagwa unga ambao ndiyo chakula kikuu kwa Watanzania. Mtama unastawi vyema ukanda wa chini ya milima Uluguru kwenye mvua za mtawanyiko na zao hili huchukuliwa kama kinga ya njaa. Zao la mhogo hustawi kwenye ukanda wa chini milimani na kwenye uwanda wa savanna na zao hili pia huchukuliwa kama kinga ya njaa. Zao la mhogo huuzwa kwa bei nzuri hususan wakati wa mfungo wa Ramadhani. Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ni ngome muhimu ya kilimo cha mkonge mkoani Morogoro na hulimwa kibiashara maeneo ya Kidugalo na Ngerengere. Halmashauri ina udongo unaofaa kwa kilimo cha pamba kwenye maeneo ya Kisaki, Mvuha, Ngerengere na Dutumi. Kwa bahati mbaya bado bidhaa za pamba zina ushindani mkubwa kutokana na bidhaa za pamba zinazotoka nje mfano Taiwan, Korea kusini na China ambazo ni bora zaidi na zinauzwa kwa bei za chini.

Ufuta ni zao jingine la kibiashara la Halmashauri hii na hustawi vizuri maeneo ya Ngerengere, Bwakira, na Mvuha. Ufuta ni moja ya mazao ya thamani kubwa ambayo yana uwezekano wa kumkwamua mkulima lakini soko lake lina ukiritimba wa walanguzi wa kati ambao nao huwauzia wafanyabiashara wa Kihindi kule Dar es Salaam. Mbegu za ufuta zipo za rangi mbalimbali mfano rangi ya kahawaia, nyekundu, nyeusi, ya njano na maziwa; inaaminika kwamba zile zenye rangi ya giza zina ladha nzuri zaidi. Bado matumizi ya mbegu za ufuta siyo mengi hapa nchini na hali hii inasababisha ufuta kusafirishwa kwa wingi nje ya nchi kuliko linavyoliwa hapa nchini, tena bila kuongezwa thamani. Zao la alizeti hustawi vyema ukanda wa chini milimani na uwanda wa savanna. Ni zao muhimu mno kwa biashara na matumizi ya

chakula kwenye kaya kwani hukamuliwa mafuta ambayo yanafaa sana kiafya, kwani hayana lehemu. Mashudu ya alizeti ni kiungo mojawapo kwenye vyakula vya mifugo na yana soko mjini Morogoro.

Miaka ya karibuni Watanzania walio wengi wameanza kujali afya zao na ili kuepuka magonjwa ya moyo wamebadili tabia na kula zaidi mafuta yatokanayo na mimea kama vile alizeti. Mahitaji ya mafuta ya kula ni makubwa na kiasi kikubwa 55% huagizwa toka nje. Mpunga wa umwagiliaji mabondeni hulimwa kwenye skimu za Kiroka, Mlilingwa, Matuli, Tulo, Kongwa, Bonye na Magogoni ambako kuna uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya umwagiliaji. Ikumbukwe kwamba mchele ndiyo chakula kikuu namba mbili baada ya mahindi nchini, na Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ina uwezo mkubwa wa kutumia kutoka skimu nyingi za umwagiliaji zilizoanzishwa kuzalisha mpunga kwa wingi na wenye ubora wa hali ya juu.

**(ii) Kuanzisha kilimo cha mazao yenye thamani kubwa**

Mazao ya thamani kubwa ambayo yameshaanza kulimwa ni pamoja na vanilla, iliki,pilipili manga, karafuu,tangawizi, binzari;mazao ya mafuta hususani alizeti na ufuta. Matunda ya thamani kubwa kama vile machungwa, maembe, mananasi, mzeituni, na ndizi. Haya ndiyo mazao ambayo Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ina upendeleo wa asili wa kustawi vizuri. Kwa mfano machungwa brandi ya Matombo huzalishwa eneo la Matombo. Zao la vanilla ni brandi nyingine ya Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro na pia kuna aina ya matunda yenye ladha za pekee kama vile ndizi, tangawizi na binzari. Tazama picha hapo chini.



*Mmea wa tangawizi*



*Mmea wa binzari*





***Mmea wa alizeti*** ***Mmea wa Ufuta***

**(iii) Kituo cha kuchakata na kusindika Vanila**

Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro imewajengea wakulima wa vanilla jengo litakalotumika kuchakata na kufungasha vanilla kwenye viwanja vya nanenane ndani ya uwanja wa maonesho ya kilimo cha kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Vanila ni zao lenye thamani kubwa na kilo moja ya vanilla inaweza kufikia TZS 75,000/=.



*Kituo cha kuchakata/kusindika vanila*

(iv**) Kugawa mbegu za kisasa za mazao mbalimbali**

Ili kuongeza uzalishaji kwa mazao ya biashara yenye viwango, Halmashauri iligawa mbegu bora, zinazozaa kwa wingi, zinazokomaa mapema na zinazovumilia magonjwa kama zinavyoonekana hapa chini kisanduku 2.

**Kitufe 2: Aina za mbegu za mazao**
Ufuta (aina ya Lindi),
Mhogo (aina ya kiroba),
Mtama (aina ya Macia, KARI-1, Kari-2 ),
Mananasi (aina ya Smooth cayan variety ),
Machungwa (aina ya Matombo sweet).
Mpunga (aina ya Nerica-1),

**(iv) Kuimarisha miundombinu kwenye maeneo ya OVOP**

Miundombinu ni ya muhimu kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi. Bahati nzuri Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro inahudumiwa na barabara kuu ya Tanzania-Zambia (TANZAM),

barabara kuu ya Dar es Salaam- Dodoma, reli ya TAZARA na ile ya kati ambazo ni muhimu kusafirisha mazao kwenda sokoni. Halmashauri ina mtandao wa barabara za vijijini ili kufikia masoko ya pembejeo na bidhaa za kilimo. Halmashauri imejenga Benki mazao kule Gomera, Kisaki na Milengwelengwe. Masoko mawili ya wakulima yamejegwa kule Kinole na Toweri. Maeneo haya ni maarufu kwa uzalishaji wa mazao ya bustani na hutumika na wakulima kama sehemu ya kukusanya mazao yao ili kuyauza kwa ushirika. Halmashauri imewekeza kwenye umwagiliaji kule Kiroka, Mlilingwa, Matuli, Tulo /Kongwa**,** Bonye na Magogoni. Uwagiliaji husaidia wakulima kutotegemea sana mvua.

(v) **Kugawanya mitambo na zana za kilimo**

Ili kujinasua na matatizo ya kulima, usafirishaji mazao, na kuongeza thamani, Halmashauri ya Morogoro iligawa bure matrekta madogo aina ya *power tillers* kwa vikundi vya wakulima kwenye Vijiji vya Mbalagwe (2) Kiroka (1) na Tulo (1). Hii ni kwa sababu taifa limeamua uwezeshaji wa vikundi kuliko mtu mmoja mmoja kwani ndio uwezeshaji wenye tija. Halmashauri pia imegawa mashine za kusaga nafaka Kiroka na Gomelo; mashine ya kukoboa mpunga kwenye Kijiji cha Lubasazi. Kwa ushirikiano na mashirika kama WOPATA, Halmashauri ilijenga mitambo ya kukamua mafuta ya alizeti kwenye Vijiji vya Mikese na Kikundi.

**(vi) Mafunzo kwa wakulima**

Mafunzo endelevu ni sehemu muhimu katika kuasili dhana ya OVOP. Hii huwawezesha wakulima kupata stadi na uzoefu, mawazo na teknolojia mpya. Halmashauri iliandaa ziara za mafunzo kwa ajili ya wakulima na maafisa ugani ili kubadilishana uzoefu. Wakulima wa Twanduseni walienda Bukoba kubadilishana uzoefu juu ya kilimo cha migomba. Chuo cha Kilimo cha Ilonga hutoa mafunzo ya uzalishaji mpunga kwa mtindo wa kupokezana yaani mhitimu kumfundisha mkulima mwenzie. Chuo hufundisha wakulima wa mfano 16 na kila mmoja wao huenda kufundisha wenzake 5, na hawa nao kila mmoja hufundisha wengine wawili. rejea modeli hii kisanduku 3.

**Kisanduku 3:Modeli ya mafunzo kwa kupokezana**

Angalia mtiririko wa mafunzo. Kundi la washiriki wa mwanzo 16 " wakulima wa mfano" (16x1=16). Kila mmoja kati ya hao 16 huenda kufundisha wakulima wengine watano (16x5=80). Kila mmoja wa hao 80 hufudisha wakulima 2 (80x2=160). Hatimaye jumla ya wakulima 256 wamefikiwa. Ni njia ya bei nafuu ya mafunzo.

"wakulima wa mfano ni wale wepesi kupokea mawazo mapya na kuasili teknolojia mpya.

**(vi) Kilimo kinachozingatia hifadhi ya ardhi**

Kwa ushirikiano na shirika la CARE International, Halmashauri ilianzisha vituo vya habari kwa wakulima maarufu kama *resource centre* kwenye Kijiji cha Kolelo mahsusi kwa ajili ya mafunzo ya wakulima kuhusu kilimo kinachozingatia hifadhi ya ardhi kwa kutumia makinga maji, kulima mazao yanayofunika ardhi, kutifua mara mbili ili kuendana na ile kauli mbiu ya "fikiri kimataifa, tenda kulingana na mazingira asilia".

**(Viii) Ushitiri baina ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP)**

Halmashauri ilijenga ushitiri baina yake na shirika la *Tanzania Agriculture Partnership*(TAP) ili kujenga maghala kwa ajili ya benki mazao na kumpa mafunzo Meneja wa ghala katika Kijiji cha Milengwelengwe. TAP iliandaa ziara za mafunzo na ushiriki wa wakulima katika maonesho kwa ajili ya wakulima. Pia Halmashauri inafanya kazi kwa karibu na Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) ambao ni muhimu sana katika kuunganisha wakulima kimtandao, ushawishi na utetezi kwa ajili ya maslahi ya wakulima na matokeo yake vituo viwili kwa ajili ya masoko ya wakulima vimejengwa kule Kinole na Toweri.

**(iX) Mnyororo wa ongezeko la thamani:**

Halmashauri hutilia mkazo zoezi la kuongeza thamani ya mazao kwa sababu ni mkakati wa kuongeza faida kwa mkulima. Ongezeko la thamani hufanyika kwa njia ya kusaga vanilla, kufungasha na kuzipa majina ya vibandiko muafaka. Mahindi husagwa kuwa unga na kusafirishwa kwenye masoko nje ya Halmashauri, alizeti hukamuliwa mafuta kwenye viwanda vilivyopo kwenye Vijiji vya Mikese na Kikundi. Hata hivyo haitoshi, kuna mengi yanayoweza kufanyika katika kuongeza thamani ya mazao ya mkulima.

**(X) Kuwapanga wataalamu wa ugani kimkakati**

Kama ilivyo sehemu nyingi za Tanzania, Halmashauri ya Wilaya Morogoro ina upungufu mkubwa wa wataalamu wa ugani. Wataalam wa Ugani huwekwa hasa kwenye ngazi ya Kata wakihudumia kati ya Vijiji viwili na vitatu. Kwa sasa tuna wagani wa kilimo wapatao 98 tu ambayo ni sawa ya 70% ya mahitaji ya wagani 141 kulingana na muundo uliopo. Ili kupambana na upungufu huu, Halmashauri huweka wagani wengi zaidi pale penye shughuli nyingi za kiuchumi. Wamezingatia kwamba katika kila Kata yenye shughuli za kiuchumi lazima awepo Afisa Ugani mmoja mwenye walau Stashahada au Cheti katika fani za Kilimo, Mifugo, Kilimo cha mboga na Matunda. Maafisa Ugani ni wawezeshaji/waraghibishi jamii wa mstari wa muhimu.

## 4.0 RASILIMALI

Halmashauri inamiliki pikipiki 39 zinazotumiwa na Maafisa Ugani na zimenunuliwa kwa thamani ya TZS.234,000,000/= ikimaanisha kwamba nusu ya Maafisa Ugani wamepatiwa usafiri wa pikipiki. Kiasi cha matrekta ya mkono yaani power tillers 49 zilinunuliwa kwa TZS 268,000,000/=. Afisa kilimo na mifugo wa wilaya (DALDO) anatumia gari moja chakavu. Kiasi cha TZS billioni 1.7 zilitumika kujenga skimu za umwagiliaji kama ilivyo kwenye Jedwali 5.2.

**Jedwali 5.2: Ujenzi wa skimu za umwagiliaji na gharama zake**

| No | Skimu | TZS |
|---|---|---|
| 1 | Kiroka | 548, 985, 000 |
| 2 | Mbalangwe | 630, 000, 000 |
| 3 | Tulo/Kongwa | 530, 000, 000 |
| | Jumla | 1, 708, 985, 000 |

***Chanzo:Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, 2010***

Mitambo mitano ya kusaga mahindi ilinunuliwa kwa TZS 9,910,000/= na kusambazwa kwenye Vijiji vya Kisaki station (2), Nyarutanga (1) na Lubasazi (2). Halmashauri imekarabati ghala la mazao la Vijiji vya Nyarutanga na Gomelo kwa ushirikiano wa wadau TAP walitoa TZS 9,000,000/= na DADPs TZS 16,000,000/=

Kiasi cha TZS 8,260,000/= zilitumika kununua pembejeo na vifaa vya mafunzo kwa ajili ya mashamba darasa (FFS) ya mahindi, mpunga, mtama ona kisanduku 5.4. Wazalishaji wa vanilla walipewa mafunzo ya mbinu za kisasa za uzalishaji na usindikaji kwa gharama ya TZS 2,048,000/=.

**Kisanduku 5.4: Mashamba darasa ni mchakato unaozingatia maarifa**
Mbinu ya Shamba Darasa huweka wazi kwamba maarifa na habari ndiyo nguzo muhimu na za msingi katika kujasirisha jamii za wakulima vijijini ili waweze kujikimu katika kupata riziki na mahitaji muhimu ya maisha (kupunguza umaskini, uhakika wa chakula kwenye kaya) na kutoa msukumo stahili kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Zaidi ya yote Halmashauri imejenga jengo la kiwanda cha kuchakata vanila kwa gharama ya TZS 43, 318,450/= na jumla ya Maafisa ugani kilimo 40 (toka Wilayani, Kata na Vijijini) walipatiwa mafunzo kuhusu kanuni za kuendesha mashamba darasa ambayo yaligharimu TZS 12,400,000/= kwa wiki mbili. Jumla ya TZS 3,500,000/= zilitumika kuandaa ziara za mafunzo kuhusu kilimo cha mahindi wilayani Kongwa.

## 5.0 MAFANIKIO NA MATOKEO

Mafanikio kadhaa yamefikiwa:

**(i) Wakulima wameasili mbinu za kisasa za kilimo**

Wakulima wamekwisha asili kanuni ya kupanda kwa mistari, kwa nafasi inayopendekezwa, kutumia mbegu bora kulingana na miinuko na kanda za kilimo.

(ii)**Kuasili mazao ya thamani kubwa**

Kuna idadi nzuri ya mazao ya thamani kubwa imeanza kulimwa kwenye mifumo ya kilimo stahili kama vile Vanilla Kijiji cha Twandoseni Kata ya Makuyuni, ambako kilo moja inauzwa kwa TZS 75,000/=; karafuu imeanza kulimwa Kondo na Kibogwa na

huuzwa kwa TZS 15,000 – 20,000 kwa kilo; Mbegu bora za alizeti zimeingizwa Kiloka na Ngerengere; pilipili manga, tangawizi na binzari zimeshaanza kulimwa Kinole.

**(iii)Mnyororo wa ongezeko la thamani**

Kuna juhudi japo siyo za kutosha kuongeza thamani ya mazao kwa njia ya kusindika nafaka na kufungasha. Kwa mfano kukamua na kuchuja mafuta kwenye Vijiji vya Kikundi na Mikese; Usindikaji wa Vanilla kwenye Kijiji cha Twandoseni Kata ya Makuyuni na pia wamejengewa jengo la kiwanda kwenye viwanja vya maonesho ya kilimo vya Mwalimu Nyerere, Manispaa ya Morogoro.

(iv)**Ongezeko la mavuno kwa ekari**

Kuna ongezeko kubwa la mavuno ya mazao ya thamani kubwa na yale yaliyozoeleka. Mavuno ya mahindi kutoka magunia 3-5 zamani na kufikia 15-16 kwa ekari; Mpunga gunia 5-8 hadi 30-38 kwa ekari; mazao ya mananasi yameongeka sana baada ya kuanza kulima mbegu mpya aina ya smooth cayan.

**(v)Vijiji jirani vimeanza kuiga**

Vijiji vya jirani vimeshaanza kuiga, kuchukua na kuasili teknolojia ya kisasa mfano Vijiji vya Kibungo juu, Kinole na Kiswilla wameasili kilimo cha kisasa cha mananasi kutoka kwa majirani zao wa ukanda wa chini.

(**vi)Ongezeko kipato cha kaya**

Kipato cha kaya kimeongezeka na ushahidi ni kwamba wakulima wameanza kujenga nyumba za kisasa za matofali na kuezeka bati katika Kijiji cha Mkono wa Mara.

(**vii)Uhakika wa chakula katika kaya umeimarika**

Kwa mfano Kijiji cha Mkono wa mara tangu 2010 hakuna upungufu wa chakula tena baada ya kuasili teknolojia ya zao la mtama. Haya ni matunda ya mwanzo ya OVOP inayosisitiza jamii kula mazao wanayolima wenyewe.

(viii**) Kuanzishwa kwa mpango chakula mashuleni**

Wakulima wa Kijiji cha Mkono wa Mara sasa wanaweza kuchangia kilo 10 za nafaka kwa mtoto kwa ajili ya mpango wa chakula mashuleni, matokeo yake ni kwamba utoro mashuleni umepungua kwa kiasi kubwa na kiwango cha idadi ya wanaojua kusoma na kuandika kuongezeka.

(ix) **Ushiriki wa jamii umeongezeka**

Kuna mwamko mkubwa wa jamii kushiriki katika shughuli zao za maendeleo. Kwa mfano katika Kijiji cha Mkono wa Mara wananchi wamejenga kwa nguvu zao barabara ya kijijini ya km saba ambayo zamani isingewezekana kwani wananchi wengi walikuwa na njaa na hivyo waliishia kuhemea vyakula.

## 7.0 CHANGAMOTO

Shughuli za OVOP katika Halmashauri zimejikita zaidi kwenye mazao ya kilimo. Hapajakuwepo na juhudi za kutosha kuendeleza shughuli ambazo si za kilimo mfano utalii, kazi za mikono na kuchonga vinyago. Ikumbukwe kwamba kuna vivutio vingi vya utalii mfano upandaji mlima, ngoma za Waluguru n.k. Matokeo yake ni mmomonyoko wa ardhi na ukataji miti ovyo kuanzisha mashamba hivyo ni tatizo kubwa kwenye ukanda wa juu milimani.

Mawasiliano na usafiri ni tatizo kubwa huko milimani kutokana na hali ya miinuko ya nchi ilivyo. Maeneo ya milimani hayafikiki kirahisi mfano kuna Vijiji vya Mkono wa Mara na Dimilo ambavyo hufikika kwa njia ya mguu tu. Pikipiki ni usafiri wa muhimu ukanda wa chini lakini haziwezi kubeba kiasi kikubwa cha mizigo. Kuna upungufu wa pikipiki 107 kwa ajili ya maafisa ugani kuhudumia maeneo haya.

Kuna upungufu wa Maafisa Ugani 64 wanaotakiwa kuwezesha vikundi vya wazalishaji. Bahati mbaya idadi ya maafisa ugani hupangwa na Ofisi ya Utumishi makao makuu na vibali vya ajira haviruhusu kujaza pengo hili katika muda mfupi ujao.

Mabadiliko ya mara kwa mara ya bei kwa baadhi ya mazao kama vile ufuta hukatisha wakulima tama kwa sababu wakulima hufuata ile modeli ya utando wa buibui (cobweb model) inayosema kwamba maamuzi ya kilimo msimu ujao hutokana na bei za mazao za msimu huu.

Wadudu na magonjwa ni kikwazo kingine kwa ushamiri wa mazao. Kuna mashambulizi makubwa ya ndege kwenye mashamba ya mtama hasa wakati wa kuchanua mbegu zinapoanza kujaza.

Katika kupambana na changamoto hizi, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro inasistiza sana kuwa na kilimo cha mkataba. Hii itasaidia kuwa na soko la uhakika hasa kwa mazao ya thamani kubwa. Halmashauri inasisitiza kilimo chenye tija cha eneo dogo lakini mazao mengi kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Ziara za mafunzo zinaandaliwa ili wakulima wabadilishane uzoefu na wenzao wa maeneo mengine. Halmashauri pia inajaribu iwezavyo kueneza mbegu kinzani kwa magonjwa na wadudu waharibifu.

## 8.0 MIKAKATI YA UENDELEVU

Ili kuhakikisha kwamba shughuli za OVOP zinaendelea kwa muda mrefu ujao, Halmashauri inakusudia kujenga vituo vya masoko ya mazao ya wakulima katika Vijiji vya Ngerengere na Mtamba. Juhudi zinafanyika ili kuvutia wadau wengine katika harakati hizi. Kwa mfano Mamlaka ya Uendelezaji Bonde la Rufiji (RUBADA) wameonyesha nia ya kusaidia ujenzi wa benki mazao kwa ajili ya kuhifadhi nafaka na kudhibiti kudorora kwa bei kwa Vijiji vilivyo katika eneo la mamlaka hiyo, pia wanaunga mkono makambi ya vijana kwa lengo la kuwavutia vijana wengi katika shughuli za kilimo.

## 9.0 SIRI YA MAFANIKIO NA MAMBO YANAYOFAA KUIGWA

(i)**Ushirikiano wa dhati wa wadau mbalimbali**

Kuna idadi nzuri ya wadau waliounga mkono shughuli za maendeleo katika Halmashauri ya wilaya ya Morogoro. Kwa mfano MVIWATA, TANRICE, na Tanzania Agricultural Partnership; WOPATA, CARE International,Chuo kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Chuo cha Kilimo - MATI Ilonga, na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Mikocheni. Pia upo ushirikiano wa karibu baina ya Kaya, Serikali za Vijiji, Halmashauri na Asasi Zisizo za Kiserikali. Ushirikiano huu ni wa muhimu sana kwani kila mmoja ana mchango wake katika maendeleo ya mpango huu.

(ii) **Eneo la uzalishaji limekaa kimkakati**

Halmashauri imeunganishwa na masoko ya pembejeo na yale ya bidhaa kwa njia ya barabara na reli. Halmashauri imezungukwa na taasisi za elimu ya juu na utafiti, vyuo vikuu vinne, idadi kubwa ya mahoteli na migahawa ambayo hununua bidhaa za wakulima, kuna kumbi mbalimbali za mikutano na semina zinazowavutia wateja kutoka nje ya Morogoro, wote hawa ni walaji wa mazao ya mkulima. Kuna idadi kubwa ya masoko ya pembezoni mwa barabara kuu ambayo yanasaidia sana kuzitangaza na kuuza bidhaa za wakulima kwa wasafiri.

(iii) **Uwezeshaji wenye tija**

Uwezeshaji ni jambo la muhimu katika vuguvugu la OVOP kwani wakulima ni lazima watengenezewe mtandao wa kuzifikia huduma za teknolojia ya kisasa, masoko na mafunzo. Halmashauri ilifanya kwa makusudi kuwaweka Maafisa Ugani wengi kwenye maeneo yenye shughuli nyingi za kiuchumi. Halmashauri imebahatika kuwa na Wagani wanaojituma. Kwa mfano kuna bibi shamba wa mfano wa kuigwa , Anna Basil ambaye ni Afisa Ugani wa Kata (WAEO) Kata ya Mkambarani rejea kisanduku 5. Katika ngazi ya Kata Maafisa Ugani wanajitahidi kulingana na maarifa na ujuzi mdogo walio nao. Wangeweza kufanya vizuri zaidi kama wangekuwa wamepata mafunzo stahili ya uraghibishi na kuamsha ari ya jamii kujiendeleza.

> Kisanduku .5. Bi. Anna Basil ni Bibi shamba wa mfano wa kuigwa
> "Bi. Anna Basil, Afisa Ugani wa kilimo wa Kata ya Mkambarani ni bibi shamba wa mfano wa kuigwa anayejituma na anayeipenda kazi yake. Wakati wa njaa hapa kijijini kwetu tulikuwa wagumu kumwelewa lakini alijitahidi kwa nguvu zote kuwaamsha wakulima kuondokana na kilimo cha mazoea. Alijitolea rasilimali zake binafsi ilipolazimika kufanya hivyo. Aliwezesha kwa mfano na siyo maneno matupu. Kwa mfano tulipokuwa wagumu kupokea kilimo cha mtama na mhogo, yeye alilima shamba lake la mfano akapanda mbegu za kisasa za mtama na mhogo na wakulima tulipoona mafanikio na kutamani akatugawia mbegu zake bure. Matokeo ya juhudi zake ni kwamba wananchi wa Kijiji cha Mkono wa Mara tumeasili mazao yanayofaa kwenye eneo letu kulingana na mfumo wa kilimo uliopo yaani Mtama na Mhogo. Njaa sasa ni historia kwenye kijiji hiki. Bahati mbaya anakaribia kustaafu na kwa kweli wawezeshaji wa aina yake ni nadra kuwakuta siku hizi". Hivi ndivyo alivyolalama mmoja wa wanakijiji cha Mkono wa Mara.

(iv) **Uongozi shupavu**

Viongozi wenye maono na utashi wa kisiasa ni mambo ya msingi sana kwa ajili ya kuinua shughuli za kiuchumi kwa kupitia dhana ya OVOP. Aliyekuwa Mkurugenzi Bw. Munisi alikuwa kiongozi mpenda maendeleo na eliendeleza sana shughuli za kiuchumi na kijamii. Kwa upande mwingine Mkuu wa Mkoa naye aliwahi kununua na kusambaza bure mbegu za mhogo. Viongozi wote wa Serikali za Mitaa (DED, DALDO, WAEOs and VAEOs) walishiriki kwa bidii kushughulikia kero za wananchi.

**Mambo mengine ya kuigwa:**

(v) Uwezo wa Halmashauri kushawishi ngazi za msingi zishiriki kwenye mchakato, kwa mfano kile kitendo cha kutoa usafiri wa pikipiki kwa Maafisa Ugani na kuwatengenezea mazingira muafaka ya kafanyia kazi kiliwachochea ari ya kufanya kazi. Viongozi wa Wilayani wanawathamini sana Maafisa Ugani wa Vijiji.

(vi) Huduma ya kulea miradi michanga na juhudi za wananchi mfano miradi midogo na ile ya kati maarufu kama (SMEs). Tumetangulia kusema kwamba Halmashauri ilijenga kituo maalum kwa ajili ya wazalishaji wa Vanilla wakitumie kuchakata na kufungasha mazao yatokanayo na Vanilla. Ili dhana ya OVOP ifanikiwe, inahitaji mikakati mizuri ya masoko na fursa za kuuzia bidhaa. Mkulima mmojammoja hawezi kufikia soko zuri lenye faida. Halmashauri ni lazima ifanye utaratibu wa shughuli, usimamizi elekezi, kufuatilia na kuvijengea vikundi uwezo hatua kwa hatua hadi wafike mahali pa kuhitimu.

(vii) Ongezeko la thamani ni kivutio tosha katika ushamiri na uendelevu wa juhudi za wananchi. Halmashauri ya Morogoro wanajitahidi kuhakikisha mazao ya kilimo yanaongezwa thamani kwa kusindika, kufungasha na kuzipa majina na vibandiko vya maelezo.

(viii) Kutambulisha na kumiliki bidhaa yaani kutengeneza brandi ni jambo la muhimu sana katika mikakati ya masoko. Halmashauri ya Morogoro inajivunia brandi yao "Matombo sweet" ambayo ni aina ya kipekee ya machungwa yanayolimwa matombo na ukiyaona utapenda ukubwa, muonekano, rangi halisi ya chungwa na ladha tamu haina kifani na kwa sababu hiyo chungwa hili linaweza kushindana vyema na machungwa mengine sokoni.

(ix) Maandalizi sahihi ya kijamii ni hatua muhimu kabla ya kujaribu kuendeleza shughuli za kiuchumi kwa kutumia dhana hii ya OVOP. Shughuli za OVOP hufanyika kwa njia ya vikundi yaani kulima mashamba ya binafsi, lakini **mauzo yote hufanyika kwa pamoja** ili kuwa na nguvu ya soko kuwakabili walanguzi na kumhakikishia mzalishaji faida ya kutosha. Mauzo ya mazao na manunuzi ya pembejeo ya pamoja yanahitaji maelewano mazuri baina ya wanachama, ushirikiano badala ya ushindani, kupongezana badala ya kuoneana wivu miongoni mwa wanachama, hiyo ndiyo OVOP.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME

## UZALISHAJI WA TANGAWIZI NA MNYORORO WA ONGEZEKO LA THAMANI



**1.0 UTANGULIZI**



*ZAO LA TANGAWIZI*

Wilaya ya Same ni miongoni mwa Halmashauri kongwe za Mkoa wa Kilimanjaro. Ina Tarafa 6, Kata 31, Vijiji 91 na Vitongoji 471. Kulingana na matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka ya 2002 kulikuwa na watu 222,149, na idadi ya watu kwa eneo ni watu 41 kwa kilomita moja ya mraba. Kipato cha mtu kwa mwaka ni Tshs 149,300, hii ni kulinga na takwimu za mwaka 2000. Wilaya ya Same ina kanda tatu. Ukanda wa juu, wa kati na wa chini. Ukanda wajuu uko milimani na ndio wenye watu wengi zaidi (250 kwa kilomita moja ya mraba) na hupata mvua nyingi ya kutosha kuliko ukanda wa chini ambao ni kame sana. Ukanda wa juu na ule wa kati ndizo zinazofaa zaidi kwa kilimo na mazao makuu ni pamoja na Kahawa, Miti ya mbao, Ndizi, Mahindi, Maharage, na Tangawizi.

**2.0 TATIZO LILILOKUWEPO KABLA YA UBORESHAJI WA ZAO LA TANGAWIZI**

Idadi ya watu kwenye Halmashauri ya Same imekuwa ikiongezeka kwa kasi kubwa na kusababisha msongamano mkubwa watu katika ukanda wa juu na wa kati, hali Iliyopelekea uharibifu mkubwa wa mazingira, kupungua kwa mvua na kiasi cha maji kinachohitajika kwa umwagiliaji kwenye maeneo ya bondeni ambayo ni kame lakini maarufu sana kwa kilimo cha mpunga na mboga. Iwapo wadau mbalimbali wasingelifanya juhudi za makusudi kunusuru hali hii, wananchi wa Same wangelikuwa wanapata mazao kidogo sana na kipato duni cha kaya. Hii ingelipelekea matatizo mengine ya kijamii kama vile utoro mashuleni, kushindwa kulipa karo za shule, ongezeko la vifo kutokana na lishe duni, kipato duni na umaskini kwa ujumla.



*KILIMO CHA TANGAWIZI KWENYE MATUTA YA NGAZI*

**3.0 MALENGO**

Licha ya ukweli kwamba wananchi

wa maeneo ya Kata za Myamba, Mpinyi na Bwambo walianza kulima zao la tangawizi miaka ya 1980, mchango wa Halmashauri haukuwa mkubwa katika kuendeleza zao hili hadi ilipofilkia 2006 yaani wakati wa semina za mrejesho za Wakurugenzi waliosoma Osaka Japan kutoka Kanda ya Kaskazini. Baada ya semina, viongozi wa Wilaya yaani Mkuu wa Wilaya, Afisa Tawala wa Wilaya, Mkurugenzi wa Halmashauri na Wakuu wa Idara waliamua kuboresha kilimo kwa kuzingatia zaidi mazao machache yanayoelekea kuwakwamua wananchi kwenye maskini na yanayostawi vizuri kulingana na ukanda kijiografia na mfumo wa kilimo uliopo, msisitizo uwekwe kwenye kilimo hai yaani kilimo kisichotumia kwa wingi madawa na mbolea za viwandani. Malengo makuu ya mkakati huu wa kilimo yalikuwa ni matumizi mazuri ya rasilimali ardhi, kuongeza uzalishaji kwa eneo, kuongeza kipato, na kupunguza viwango vya umaskni miongoni mwa wananchii wa Wilaya ya Same.

Ikumbukwe kwamba kabla ya mkakati huu, huko nyuma miaka ya 2000 Halmashauri ya Same ilishaanza kuzalisha tangawizi kwenye yale maeneo ambayo inastawi vizuri zaidi chini ya programu ya kuendeleza mfumo wa masoko ya bidhaa za kilimo maarufu kama *AMSDP*. Kwa kuzingatia haya, mwaka 2008 Halmashauri ya Same iliweka malengo mahususi ikiwa ni pamoja na:

i. Kuongeza, uchakataji, na ufungashaji wa zao la tangawizi ili kuongeza thamani.
ii. Kuanzisha vikundi vya wakulima wazalishaji wa Tangawizi, ushirika wa wazalishaji tangawizi na vyama vya ushirika vya msingi.
iii. Kuboresha matumizi na usimamizi wa rasimali za pamoja, mfano rasilimali ardhi na rasilimali maji
iv. Kusaka na kujiunga na masoko ya kuaminika ya tangawizi hapa nchini na nje ya nchi.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Shughuli za uzalishaji za kilimo zinahitaji maandalizi ya kutosha yaani mpango mzima na utaalamu utakaohitajika. Ili kufikia malengo ya kuendeleza zao la tangawizi liweze kuongeza kipato cha wananchi, Halmashauri iliazimia kutekeleza shughuli mbalimbali pamoja na hizi zifuatazo;

(i) Kuanzisha ushitiri na shirika la "Faida Mali" (kama wakala) chini ya programu uendelezaji masoko yaani AMSDP.
(ii) Kufanya utafiti wa masoko kwa kuhusisha Maafisa masoko, Ushirika wa wakulima wa tangawizi, Maafisa kilimo na Wanasiasa.
(iii) Kuanzisha chama cha msingi cha wazalishaji tangawizi cha Mamba yaani *Mamba Ginger Growers Rural Cooperative Society.* Chama hiki kilikuwa na wanachama 350 kutoka Kata za Myamba, Mpinji na Bwambo kwa kusudi la kuongeza uzalishaji, uchakataji, na ufungashaji wa tangawizi, kuongeza ajira, na kuinua kipato cha kaya.
(iv) Kuwashawishi waheshimiwa Madiwani juu ya fursa iliyopo kwenye kilimo cha tangawizi katika kuongeza kipato cha kaya. Hili lilipelekea kikao cha Baraza la Madiwani cha 2009 kupitisha azimio kwamba tangwizi litakuwa ndio zao kuu la biashara kwa wananchi waishio ukanda wa juu na ule wa kati wa milimani. Kikao

hiki pia kiliagiza juhudi za ziada zitumike katika kuweka mifumo, miundo na taasisi muafaka kwa ajili ya usimamamizi wa uzalishaji na uendelezaji wa zao la tangawizi.




(v) Kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa njia ya ziara za mafunzo ikihusisha wakulima wa mfano. Wakulima wa mfano waliwezeshwa kutembelea wenzao wa Kenya na kujionea uzalishaji, uchakataji tangawizi na taasisi za mauzo, ambazo masoko yao makuu yapo Kenya kwenyewe, Uganda na Uholanzi.

(vi) Uandishi wa andiko la kitaalamu la mpango wa biashara kuhusu ujenzi wa ghala, kiwanda cha uchakataji na ufungashaji. Kiwanda tarajiwa chenye uwezo wa kuchakata kwa uchache tani 10 za tangawizi kwa siku.

(vii) Kuamsha ari ya wakulima kujiunga kwenye vikundi na ushirika wa wakulima wa tangawizi, matumizi yenye tija ya rasilimali ardhi na maji, matumizi ya samadi na kujitolea katika ujenzi wa kiwanda cha kuchakata tangawizi.

(viii) Kusimamia na kuhakikisha kwamba wakulima wa tangawizi wanafanya chaguzi za kidemokrasia, mikutano ya kikatiba, kuzingatia kanuni za mikutano na mahusiano yenye tija kati yao na watendaji wa vyama vya ushirika, kiwanda cha kuchakata tangawizi na Halmashauri yao.

(ix) Ukarabati wa barabara za vijijini ili kuharakisha usafirishaji wa tangawizi na mazao mengine toka kwa mkulima hadi sokoni.

(x) Kuamsha ari na kutoa usimamizi elekezi kwenye ujenzi wa maghala, majengo ya masoko kwa ajili ya uhifadhi na uchakataji endelevu wa tangawizi.

(xi) Ujenzi na ukarabati wa kudumu wa miundombinu ya umwagiliaji kama vile mito midogo, mabwawa kwa mbinu ya kuziba mito maarufu kama (ndiva) na miferejei ya umwagiliaji na hivi vyote vikifadhiliwa kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo Wilaya (DADPs)

(xii) Kuanzisha na kuboresha utendaji kazi wa mfumo wa stakabadhi ghalani ili kudhibiti kuporomoka kwa bei za mazao.

(xiii) Kuanzisha mfumo wa upashanaji habari baina na miongoni mwa wazalishaji wa tangawizi, vyama vya ushirika, washitiri wa maendeleo maarufu kama (PPP), Halmashauri ya Wilaya na Serikali Kuu.

**Sanduku 1: Mkakati maalum: Mnyororo wa kuongeza thamani ya tangawizi**

- *Mnyororo wa kuongeza thamani ya zao la tangawizi unapendekezwa na Halmashauri ya Same kama mbinu mojawapo ya kuinua vipato vya kaya, kuboresha hali za maisha ya watu na kuongeza mapato kwa Halmashauri.*
- *Halmashauri ya Same iliweza kuanzisha Mnyororo wa kuongeza thamani ya tangawizi kwa njia shirikishi ya kuchambua hali halisi ya mazingira yaliyopo kupitia mbinu ya PRA, mikutano ya Madiwani, uchambuzi wa kitaalamu, na maamuzi sahihi ya Timu ya Menejimenti ya Halmashauri.*
- *Halmashauri ya Same iliendesha zoezi la kuchambua faida tarajiwa kwa kipande cha ardhi(hekta) na kuanisha ni zao gani ambalo lina faida kubwa kwa kila hekta. Ilibainika kwamba mkulima wa tangawizi anaweza kununua tani 8.2 za mahindi kwa kutumia faida yake kabla haijakatwa kodi. Kipande cha ardhi cha hekta 1 kilizalisha faida ghafi (kabla ya kodi) ya tani 1.4.*
- *Katika zoezi la PRA iligundulika kwamba mazao mengi yanayolimwa na wakulima kimazoea yana faida kidogo saa kwa kila hekta moja ikilinganishwa na tangawizi.*
- *Baada ya matokeo ya utafiti huu wa kisayansi kuhusu faida itokanayo na Tangawizi kwa ekari, Kamati ya Kudumu ya Huduma za Uchumi ilipendekeza kwamba mpango wa mnyororo wa ongezeko la thamani uingizwe kwenye agenda ili ujadiliwe na Baraza la Madiwani. Pendekezo lilipitishwa na kutekelezwa*

## 5.0. RASILIMALI ZILIZOTUMIKA

Ili kufikia malengo ya uzalishaji endelevu na kuchakata tangawizi kwa faida, Halmashauri ilitenga rasimali mbalimbali kwa ajili ya shughuli hii. Kwa upande wa rasilimali watu ilihusisha viongozi wa kuchaguliwa na wa kuteuliwa ambao walifanya kazi kubwa sana. Wadau mbalimbali pia walihusika kwa namna moja au nyingine. Jedwali 5.3 linaonesha mchango wa kila mdau.

**Jedwali 5.3: Wadau muhimu na michango yao**

| TAASISI | MCHANGO WAO |
|---|---|
| **Faida Mali** | - Kuamsha ari na ufahamu wa wakulima wa tangawizi kuhusu uuzaji na udhibiti wa bei ya tangawizi.<br>- Kufanya tathimini ya masoko na bei na kuwaunganisha wazalishaji na masoko. |
| **SIDO** | - Kujenga na kuendelea kukarabati mtambo wa kuchakata tangawizi.<br>- Kuwajengea wakulima stadi za uzalishaji, kuhifadhi na kuchakata tangawizi. |
| **SARI- Tengeru** | - Kutafiti kuhusu tangawizi na mbegu zake.<br>- Mafunzo kwa wakulima na Maafisa Ugani kuhusu mbinu muafaka za uzalishaji tangawizi.<br>- Mafunzo kwa wakulima kuhusu kilimo kwa ujumla, kuhifadhi na kuchakata tangawizi.<br>- Mafunzo ya wakulima kuhusu upangaji wa madaraja ya tangawizi.<br>- Usambazaji wa mbegu bora za tangawizi. |

| | |
|---|---|
| **MVIARF** | - Kupambana na wadudu na magonjwa ya tangawizi.<br>- Kuendeleza na kukarabati miundombinu ya masoko na barabara za vijijini kwenye maeneo yanayozalisha tangawizi.<br>- Kuhamasisha jamii ili kuongeza uzalishaji wa tangawizi.<br>- Kuhakikisha uwepo wa amani, utulivu na maelewano. |

**Chanzo: Halmashauri ya Wilaya ya Same 2011**

Kuhusu rasilimali fedha, Halmashauri ya Wilaya ya Same imetumia kiasi kikubwa cha fedha kuwalipa Maafisa Ugani, gharama za kujikimu, gharama za usafiri, kulipia matumizi mbalimbali na yale ya kiutawala zinazohusiana na uzalishaji wa tangawizi.

Kuanzia miaka ya mwishoni mwa 1950 hadi leo Halmashauri imetumia kiasi kikubwa cha fedha kujenga ndiva (mabwawa yanayojegwa kwa kuziba mto), mifereji, miundombinu ya masoko na ukarabati wa masoko mambo ambayo kimkakati yamesaidia sana ushamiri wa zao la tangawizi. Mwisho, Halmashauri imetumia kiasi kikubwa cha fedha kutoka kwenye programu kama vile AMSDP, DADPs na mchango kwa wazalishaji ili kufikia lengo la kuzalisha, kuchakata na kuuza tangawizi ndani na nje ya nchi.

## 6.0 MATOKEO

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Same uzalishaji umepanuka haraka na kwa kiasi kikubwa na kuboresha hali za maisha kijamii na kiuchumi wa wananchi kwenye zaidi ya Kata 12. Matokeo dhahiri yameoredheshwa hapa chini.

(i) Wakulima wa tangawizi wameamshwa ari na kuanzisha vikundi vya uzalishaji na ushirika wa wakulima wa tangawizi ambao umesaidia sana katika kudhibiti mauzo na kudorora kwa bei ya tangawizi.




*Duka la Mkulima*



*Tangawizi ya Unga iliyofungashwa*

(ii) Kipato cha kaya cha mkulima wa tangawizi kimeongezeka. Hili limedhirishwa na ujenzi wa nyumba bora, kupanuka kwa uwezo wa kulipa karo kwa watoto na wanafunzi wa vyuo vikuu, kupanuka kwa uhakika wa chakula wa kaya, kupungua vifo vya mama na watoto na wakulima kununua na kutumia usafiri wa pikipiki kuliko hapo mwanzo.

*(iii)* Kukamilika kwa kiwanda cha kuchakata Tangawizi ambacho tayari kinazalisha unga wa tangawizi na tangawizi ya vipande maarufu kama *chips*. Kiwanda kinamilikwa na chama cha ushirika cha Myamba yaani *Myamba Ginger Growers Rural Cooperative Society Ltd.*







*Mtambo* *Vipande/chipsi* *Unga*

(iv) Wakulima wa tangawizi wamekwisha-asili mbinu za kisasa za kilimo endelevu kwa zao la tangawizi husunan stadi za umwagiliaji, jinsi ya kupanda, hifadhi ya ardhi, matumizi ya samadi.

(v) Uzalishaji wa zao la tangawizi kwa mwaka umeongezeka kutoka tani 7,000 mwaka 2008 hadi tani 12,000 mwaka 2011.

(vi) Kata zinazolima tangawizi zimeongezeka kutoka Kata 3 mwaka 2008 hadi kufikia kata 12 kwa sasa.

(vii) Mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Same yamepanda kutokana na ushuru wa mazao unaolipwa na wanunuzi binafsi wanaosafirisha tangawizi kutoka katika Kata zinazozalisha kwenda penginepo hapa Tanzania au kusafirisha nje ya nchi.

(viii) Kukamilika kwa utafiti ulioshirikisha Halmashauri na FAIDA MALI ulisaidia kubaini fursa za masoko ya Tangawizi nazo ni;

a. Tanzania Zanzibar Organic Products (TAZOP). TAZOP hununua kiasi cha tani 40 za tangawizi vipande (chips) kwa mwezi
b. Tanzania Tea Packers (TATEPA). TATEPA hununua kiasi cha tani 158 za unga wa tangawizi kwa mwezi.
c. Jambo Factory in Nairobi. Kiwanda hiki huagiza tani 1.5 za unga wa tangawizi kwa mwezi

d. Unifine Co Ltd, kampuni ya Ufaransa ambayo hununua kiasi cha tani 25 chips za tangawizi kwa mwezi.
e. Baadhi ya maduka makubwa maarufu kama *supermarkets* huko Arusha, Moshi na Dar es salaam hununua tani 13 za unga uliofungashwa kenye chupa kwa mwezi.

**7.0 CHANGAMOTO**

Uzalishaji wa tangawizi katika Halmashauri ya Same umekuwa ukiongezeka kwa miaka 10 iliyopita kwa maana ya eneo linalolimwa na kiasi kinachozalishwa. Jamii ya wakulima wanaohusika wameshudia faida za kijamii na ongezeko la kipato. Hata hivyo biashara hii ina kumbana na vikwazo mbalimbali vinavyohitaji kuzingatiwa kwa makini.

Halmashauri ya Same imeendelea kukumbwa na vipindi virefu vya ukame katika miaka ya karibuni. Hali hii inapelekea wazalishaji kugombea maji ya umwagiliaji kwa ajili ya uzalishaji wa tangawizi na mazao mengine. Uzalishaji wa mazao ya chakula umepungua na gharama za kuzalisha tangawizi zimeongezeka kwani sasa panahitajika umwagiliaji wenye ufanisi na wa kisasa zaidi. Kwa hakika uhaba wa mvua umesababishwa na uharibufu mkubwa wa mazingira unaotokana na vitendo viovu vya binadamu hasa kukata miti kwa wingi kwa ajili ya kufungua mashamba zaidi na uzalishaji wa mbao na kilimo holela kinachosababisha mmomonyoko wa udongo.

Miundo mbinu ya barabara za Vijiji haijaendelezwa vya kutosha. Barabara nyingi hazijawekewa changarawe kwani ziko kwenye miinuko na kutokana na miinuko, barabara hizi humomonyoka mwaka hadi mwaka. Hali hii husabibisha usafirishaji wa tangawizi kuwa wa ghali na wa shida. Miundo mbinu ya soko na ile ya umwagiliaji bado haitoshelezi.

Ushirika wa wakulima wa tangawizi bado hauna uongozi mzuri hasa kutokana na kiwango kidogo cha elimu kwa viongozi wake. Kukosekana kwa mikopo na taasisi za fedha Same Vijijini hudumaza ule uwezo wa kukua kwa ushirika wa wazalishaji na vyama vya ushirika. Wazalishaji bado hawana stadi za kutosha za kuzalisha, kuvuna, kuchakata, kuuza, na kufikia muafaka wa bei hasa inapowahusisha wanunuzi binafsi, vyama vya ushirika na wadau wengine.

Wazalishaji pia wanakumbana na tatizo la upatikanaji wa pembejeo kama vile mbolea na mbegu zinazofaa. Uhaba wa ardhi umesababisha ongezeko la bei ya kusafirisha samadi kutoka uwanda wa chini kwenda ukanda wa juu na kwa mantiki hiyo gharama za kuzalisha tangawizi kwa hekta moja au kilo moja imepanda sana, huku bei za kuuza zikiwa hazitabiriki kabisa.

## 8.0 MIKAKATI YA UENDELEVU

Ili kupambana na changamoto hizo hapo juu, Halmashauri inayo mikakati mingi. Mkakati wa kwanza ni ushirikishwaji wa wananchi katika hifadhi ya mazingira, kuhifadhi misitu, kukarabati barabara na ujenzi wa miundo mbinu ya masoko. Jamii imekuwa ikihusishwa kwenye mikutano yenye lengo la kuchangia kwa hali, mali na fedha.

Mbili, kuwatumia Wabunge, Madiwani na Mkuu wa Wilaya imesaidia kuamsha ari kwa viongozi wa Serikali za Mitaa na kuzifanya jamii kushiriki vyema katika shughuli za maendeleo yao katika maeneo wanayoishi na hii imesaidia sana kupunguza baadhi ya changamoto.

Tatu, wananchi wa Same ni wachapakazi na wamehamasika sana na shughuli zinazolenga kuwaongezea kipato. Kwa mantiki hiyo, shughuli za tangawizi zinapata msukumo wa jamii kutokana na kivutio cha ongezeko la kipato tarajiwa.

Mwisho, juhudi endelevu na utoaji huduma unayofanywa na Maafisa Ugani wa Halmashauri ambao hujituma sana katika kuwashawishi wakulima kutumia mbinu za kisasa za kilimo, Vyama vya ushirika na ushiriki wa jamii vimesaidia sana kupunguza changamoto zilizopo.

## 9.0 SIRI YA MAFANIKIO NA MAMBO YANAYOFAA KUIGWA

- Uongozi wa Halmashauri ya Same ulikuwa muhimu sana katika kufanikisha kesi hii. Nafasi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Bw. Joseph Mkude na Timu ya Menejimenti ya Halmashauri ulisaidia sana kuleta ushitiri baina ya watendaji na wanasiasa ulioifanya jamii ya wakulima ielekeze nguvu katika kilimo cha tangawizi kama zao mbadala la biashara. Mchango wa Mbunge Mh. Anne Kilango Malecela ni mfano wa kuigwa katika kuhamasisha uzalishaji, kuongeza thamani na kuongoza hafla za kuchangisha fedha kwa ajili ya mambo mbalimbali. Ki-mkakati anaunganisha vikundi vya wakulima na masoko ya nje ya Wilaya.

- Kuna mahusiano mazuri kati ya wanasiasa na watendaji wa Halmashauri ya Same. Wapo watumishi wenye ubunifu mkubwa na kujituma kwa hali ya juu ambao hufanya kazi kama timu moja. Hili limewezekana kwa sababu ya uongozi changamfu wa Mkurugenzi wa Halmashauri na Timu ya Menejimenti.

- Halmashauri inaheshimu juhudi na vipaumbele vya wananchi. Hata kama Halmashauri ilikuwa na sababu za kupendelea zao jingine kama vile kahawa, lakini walilazimika kuelekeza nguvu kwenye kipaumbele cha wananchi ambacho ni mnyororo wa thamani wa zao la tangawizi. Ili kufikia azma hii, kampeni zenye mvuto ilibidi zifanyike kuamsha ari ya jamii ya kuendeleza zao la tangawizi.

- Kwa ushirikiano na kituo cha utafiti wa Kilimo cha SARI Tengeru, Halmashauri iliweza kufikia matumizi mazuri ya teknolojia ya kisasa ya kilimo.

- Licha ya ushitiri baina sekta ya umma na sekta binafsi ambao ulisaidia sana katika suala zima la masoko na uuzaji, Halmashauri iliutumia vyema mtandao na wadau wengine ndani na nje ya Wilaya. Hii inajumuisha matumizi mazuri ya programu ya Serikali Kuu ya kuendeleza masoko (AMSDP).

- Katika juhudi za kudhibiti bei katika soko, wakulima walitumia mbinu ya kuchelewa kuvuna. Kwa maana nyingine ni kuhifadhi tangawizi ardhini. Pale bei zinapokuwa za kuridhisha uvunaji hufanyika mara moja, lakini ikitokea bei ziko chini, tangawizi hubaki ardhini kama njia ya kutengeneza uhaba na ambayo ni kichocheo cha kupanda kwa bei. Ikumbukwe tangawizi haiharibiki kirahisi ikiwa ardhini.

- Siri kubwa ya mafanikio hapa na ambayo Halmashauri nyingine nchini hawana budi kuiga ni mbinu ya kupambana na wachuuzi hasa walanguzi wa kati kuhusu bei. Jamii ya wazalishaji tangawizi iliweka sheria ndogo inayomzuia mzalishaji mmoja mmoja kupatana bei na mlanguzi. Mapatano yote ya bei hufanyika ki-jumuia na hushirikisha chama cha ushirika kwa kuwakilisha maslahi ya wazalishaji.

- Mwisho, ushiriki wa jamii ulikuwa wa kutia moyo. Hii inatokana na mbinu sahihi za kuraghibisha jamii zilizotumiwa na Maafisa Ugani wa kilimo ambao nao walikuwa wanajituma sana.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO

***UENDELEZAJI WA KILIMO CHA ZABIBU***



## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino ni moja kati ya Wilaya za mkoa wa Dodoma. Halmashauri hii ilitokana na iliyokuwa Halmashauri ya Dodoma Vijijini. Wilaya hii ina ukubwa wa eneo la kilomita za mraba 8,056. Sehemu kubwa ina tabia nchi ya Savana, na kwa ujumla ni eneo kame likiwa na uelekeo wa nusu-jangwa. Chamwino kama zilivyo Wilaya nyingine za Dodoma hupata mvua za wastani wa mm 500 kwa mwaka na 85% ya mvua hizi hunyesha kati ya Desemba na Machi. Mvua hazina uhakika na mtawanyiko wake hautabiriki na hivyo kupelekea mavuno kidogo sana hususan mahindi, mtama na uwele na hivyo kupelekea uhaba wa chakula wa mara kwa mara na umaskini uliokithiri. Jedwali 5.4.

Vijiji kama vile Buigiri na Chinangali II vilivyopo pembezoni mwa barabara kuu itokayo Dodoma-Morogoro huonyesha ufukara uliokithiri kwa kigezo cha makazi. Zaidi ya nusu ya nyumba zimejengwa kwa udongo na kuezekwa kwa udongo yaani "tembe". Ifikapo Febuari na Machi kila mwaka; Vijiji hivi huzungukwa na mashamba ya mahindi, mtama na uwele yakionekana kukauka kabisa na hukatisha tamaa kwamba hayatazalisha chakula cha kutosha na kipato kwa ajili ya mahitaji mengine kama ada za watoto shuleni, sare za wanafunzi na madaftari.

**Jedwali 5.4: Kiwango na mtawanyiko wa mvua**

| Miezi | Nov | Des | Jan | Feb | Machi | Apr |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kiwango cha Mvua (mm)** | 23.74 | 136.70 | 77.84 | 51.30 | 70.30 | 14.14 |
| **Siku za kunyesha** | 4 | 10 | 4 | 3 | 4 | 1 |

**Chanzo: Halmashauri ya Chamwino 2011**

Mwaka 2008 Kikao cha Kamati ya Ushauri Mkoa (RCC) kilielekeza Halmashauri zote kuchukua hatua madhubuti na za dhati ili kuongeza kipato cha jamii zao. Ilipendekezwa kila Halmashauri kubuni na kuandaa mbinu zitakazopelekea wananchi kufanya kazi kwa pamoja katika shughuli za uzalishaji mali ili kuvuna matunda yatokanayo na umoja kwa njia ya vikundi, ushirika na vyama vya msingi. Halmashauri ya Chamwino iliidhinisha mapendekezo hayo na ikauunganisha moja kwa moja na jitihada ya Serikali Kuu maarufu kama "Kilimo Kwanza".

Kwa mantiki hiyo Halmashauri ya Chamwino iliamua kujikwamua kwa kukazania kilimo cha zabibu kwa njia ya ushirika wa wanavijiji na Halmashauri ikawezesha mchakato kuelekea kuundwa kwa chama cha ushirika chenye nguvu. Lakini msingi wa wazo hili unatokana na watendaji wa Halmashauri hii kuielewa vyema na kuikubali dhana ya kijiji kimoja- zao moja maarufu kama OVOP. Dhana hii inasisitiza matumizi ya rasilimali za asili zipatikanazo katika eneo kuzalisha kipato na kuboresha maisha ya jamii husika. Ikumbukwe kuwa Mkurugenzi wa Chamwino Bw. Daudi Mayeji aliwahi kwenda Japan na kujifunza dhana hii naye alikuwa na haya ya kusema kuhusu dhana ya zao moja kwa kijiji kimoja yaani OVOP.

***"…… Nilibahatika kutembelea Oyama nchini Japani. Nilifurahishwa sana na maneno ya hekima ya Bw. Yahata aliyewaambia watu wake wa Oyama mwaka 1961, kwa nini waajiriwa wa miji mikubwa hupata Bonasi kila mwaka na nyongeza ya kila mwaka juu ya mishara yao halisi, ili hali sisi wakulima tunafurukuta ili angalao tuishi mwaka hadi mwaka; Kwa nini na sisi tusiweze kuchukua likizo na kwenda kustarehe America kwenye miji ya starehe kama vile Hawaii? Ni liwaza kwa undani juu ya mantiki iliyoko kwenye ujumbe huu na kuamini kwa dhati kwamba watu wa Halmshauri ya Chamwino wana rasilimali ardhi na hali ya tabia nchi inayoweza kubadili maisha ya wanavijiji. Niliamua kuchukua hatua katika uzalishaji wa zabibu ……."***

Madiwani waliafiki maagizo ya RCC na uamuzi wa CMT kuendeleza kilimo cha zabibu na kuridhia utekelezaji ufanyike kwa mfumo wa mradi. Mradi unawahusu wakulima 300; kati ya hao 250 wametoka Vijiji vya Chamwino, Buigiri, Chinangali II, Mlebe, Manchali na Makoja. Wakulima 50 ni vijana waliovutiwa na mradi baada ya kuona juhudi za pamoja zilizoanzishwa na Halmashauri. Masharti ya mradi yanamtaka kila mkulima amiliki ploti katika eneo la mradi, afyeke na kuchimba mitaro ya zabibu na kushiriki vikao vya maamuzi. Ili kuwezesha maandalizi ya ardhi ya kupanda zabibu Halmashauri iliwseshesha upatikanaji wa mkopo toka Benki ya CRDB na kutoa dhamana kwa wakulima 250. Wale wakulima 50 waliojiunga baadaye walitumia rasilimali zao wenyewe kuandaa ploti zao tayari kwa upandaji zabibu.

## 2.0 TATIZO LILILOKUWEPO KABLA YA UENDELEZAJI WA KILIMO CHA ZABIBU

Wananchi wa Halmashauri ya Chamwino kwa miaka mingi wamekuwa wakivuna mazao kidogo sana kutokana na uhaba wa mvua, kupungua kwa rutuba kwenye udongo. Hali hii ilipelekea kipato duni cha kaya na hali duni ya maisha inayojidhihirisha kwenye nyumba ambazo si bora kwa maisha, utoro wa watoto shuleni na kushindwa kulipa kodi na michango mbalimbali. Kipato duni na maisha mabaya ya vijijini yanasababisha watu kukimbilia mijini kutafuta vibarua na biashara ndogondogo kwenye sekta isiyo rasmi ili kujinusuru kimaisha. Jedwali 5.5.

**Jedwali 5.5: Idadi ya vijana waliovihama vijiji vyao**

| Vijiji | 2006/2007 | 2007/2008 | 2008/2009 |
|---|---|---|---|
| **Chamwino** | 182 | 120 | 20 |
| **Buigiri** | 60 | 34 | 8 |
| **Chinangali II** | 104 | 42 | 13 |
| **Mlebe** | 34 | 16 | 9 |
| **Manchali** | 62 | 18 | 2 |
| **Makoja** | 41 | 12 | 6 |

**Chanzo: Halmashauri ya Chamwino 2011**

Wahitimu wa shule za Sekondari na Vyuo vya Ufundi ambao wangetegemewa wabaki Vijijini na kushiriki katika shughuli za kilimo na kuzalisha mali nao walivikimbia Vijiji vyao. Kwa bahati mbaya mfumo wa elimu wa Tanzania bado hauandai moja kwa moja wahitimu wa Sekondari na Vyuo vya Ufundi waweze kujiajiri na kuwa wajasiriamali kwenye maeneo ya Vijijini. Wahitimu wa Chamwino nao wanategemea sana sekta ya ajira ya umma ambayo haina uhakika na hivyo uamuzi wa vijana ni kukimbilia maeneo ya mijini, hususan mjini Dodoma.

Kilimo cha zabibu kimekuwepo Wilaya ya Chamwino kwa miaka mingi na wakulima hawakuweza kujihusisha na kilimo hiki kwa sababu ya ukosefu wa mitaji, uwezo duni wa kujipanga katika vikundi vya ushirika, ufahamu duni wa mbinu za kilimo cha kisasa, ukosefu wa stadi na teknolojia sahihi za uzalishaji wa zabibu. Licha ya ufugaji wa mbuzi na ng'ombe ambao mara kwa mara hushambuliwa na magonjwa na wakati mwingine kuibiwa, wakazi wa Chamwino huishi kwa kilimo cha jembe la mkono kinachotegemea mvua ambayo ni kudra ya Mwenyenzi Mungu. Kwa ujumla maisha ya wakazi wa Chamwino ni ya kimaskini mno.

**3.0 MALENGO**

Kama ilivyoonyeshwa kwenye utangulizi, RCC na Halmashauri ya Chamwino zilibaini tatizo la kushuka kwa hali ya maisha ya watu na wakaamua kushughulikia tatizo hili. Malengo mahsusi katika kufanya kilimo cha zabibu kuwa cha kisasa yalikuwa ni;

- Kupunguza uhaba wa chakula, kuinua hali za maisha ya watu na kupunguza umaskini.
- Kuongeza ajira kwa kuwekeza kwenye kilimo cha zabibu na kuvutia vijana wakae Vijijini .
- Kuongeza kipato cha kaya ili kuboresha hali ya maisha kuhusu uhakika wa chakula, huduma za afya na fursa za elimu.
- Kuzalisha maarifa, teknolojia na stadi mpya za uzalishaji zabibu .
- Kuimarisha juhudi za pamoja za uzalishaji mali za wanavijiji kupitia vikundi na vyama vya ushirika.

**4.0 UTEKELEZAJI**

Kuna usemi usemao " waza kimataifa, tekeleza kulingana na mazingira asilia", *Think globally act locally* . kwa kuzingatia usemi huu Halmashauri iliamua kuendeleza zao la zabibu ambalo ni fursa kwa wananchi wa Chamwino. Utekelezaji wa mradi huu haukuwa rahisi na ulihitaji umakini mkubwa kwani ulihusisha wanavijiji wa Vijiji vitano na wadau wengine mbalimbali. Shughuli ya kwanza ilikuwa kuraghibisha na kuhakikisha walengwa wanaelewa vyema makusudio ya mradi wa uzalishaji zabibu utakaoongeza kipato cha kaya, uhakika wa chakula wa kaya na kuboresha hali za maisha ya watu. Kwa maneno mengine

Halmashauri ilikuwa inawashawishi wakulima wabadilike kutoka kilimo cha kizamani cha zabibu na kuanza kilimo cha kisasa.

Pili Halmashauri iliwashawishi wanavijiji ili wajiunge kwenye vikundi au vyama vya ushirika. Ikumbukwe hapa Tanzania Vijiji vingi vilianzishwa kwa nguvu ili watu waishi na kuzalisha kwa pamoja. Kati ya mwaka 1970 na 1980 baadhi ya Vijiji vilikuwa na mashamba na maduka ya Vijiji ambayo yaliendeshwa kwa njia ya ushirika, hata hivyo juhudi zote hizi hazikuweza kuleta mafanikio tarajiwa. Kwa vile bado kumbukumbu hizi bado zipo kwenye fahamu za wanavijiji wetu, siyo rahisi sana kuwashawishi wanajamii wa Vijijini kuunda na kujiunga na ushirika . Hata hivyo Halmashauri ya Chamwino iliweza kushawishi wanavijiji kuunda na kujiunga na ushirika wa kuweka na kukopa (SACCOs) na ushirika wa masoko ya bidhaa za kilimo (AMCOs).



MKUTANO WA WANAKIJIJI CHA BUIGIRI

Tatu, Halmashauri iliandaaa andiko la kitaalamu la mradi wa kibiashara ili kushawishi vyombo vya fedha kwamba mradi wa uzalishaji zabibu ungekuwa na faida. Andiko hili lilisaidia kupata mkopo wa kilimo kutoka CRDB. Andiko liliainisha jinsi mradi ungeweza kurudisha mkopo ndani ya muda wa mkopo na kwamba zaidi ya kulipa mkopo ungekuwa na faida nyingine lukuki; mfano wakulima kulipa mikopo yao, kuboresha kipato cha kaya na kuinua hali ya maisha ya watu.

Nne, Halmashauri iliweza kutafiti na kupata ardhi inayofaa na ya kuwatosha wanachama wote wa ushirika wa wakulima wa zabibu. Ardhi hii iligawanywa kwa wanachama ili waiendeleze. Hata hivyo bado ni 30% yaani ekari 300 zimetumika mpaka sasa. Hii ni fursa kwa Halmashauri kuunda ushirika mwingine wa wakulima wa zabibu katika eneo hili.

Tano, Halmashauri iliainisha vyanzo vya uhakika vya maji. Mwanzoni kuliwa na visima virefu vitatu vilivyochimbwa kwa msaada wa Serikali ya watu wa Bulgaria na vikaingizwa kwenye mradi. Kwa kutumia fedha za Halmashauri bwawa kubwa la kuhifadhi maji ya kumwagilia lenye ujazo wa lita 21,000,000 lilichimbwa. Hili lilikuwa ni muhihu kwani maji ambayo yanatoka kwenye visima hivyo vitatu yanakusumuwa na kuhifadhi kabla ya kumwagilia bustani za zabibu kwa njia ya matone.




Sita, Halmashauri ilitafuta teknolojia sahihi ya umwagiliaji. Taasisi mbalimbali za umwagiliaji, wakulima wakubwa wa zabibu, vituo vya mafunzo ya kilimo na watengenezaji wakubwa wa zana za umwagiliaji walitembelewa. Halmashauri illipata ushauri wa kitaalamu kutoka ARI Makutopora na Ofisi ya Kanda ya Umwagiliaji kabla ya kutoa tenda kwa kampuni ya BALTON Tanzania LTD ili kujenga bwawa, kusimika pampu na kujenga nyumba ya pampu za kusukuma maji. Kampuni hii ilisaidia kupata teknolojia muafaka ya umwagilijai zabibu kwa njia ya matone na yenye uwezo wa kumwagilia ekari 30 kwa wakati mmoja kwa masaa manne kila siku.



*Pampu ya umwagiliaji kwa njia ya matone na mabomba ya chini ya ardhi*

**4.0 RASILIMALI ZILIZOTUMIKA**

Juhudi za Halmashauri ya Chamwino za kuinua kipato na hali za maisha ya wakazi zilihusisha shughuli zilizoko kwenye sehemu ya nne hapo juu. Shughuli hizi zilihitaji rasilimali mbalimbali zikiwepo rasilimali watu, fedha na vitu halisi. Kuhusu rasilimali watu Madiwani wote na Watendaji wa Halmashauri walihusika kuhakikisha mradi unaaza kama ulivyopangwa. Pia shamba pamoja na mitambo ya umwagiliaji vinasimamiwa na Meneja wa

shamba, Maafisa ugani watano, mtaalamu mmoja mstaafu aliyebobea katika zabibu na wataalamu wanne toka ARI Makutopora.

Rasilimali nyingine ni pamoja na ekari 300 (120Ha) za ardhi zikiwa kamili na mfumo wa umwagiliaji wenye uwezo wa kumwagilia hadi ekari 1000 (400Ha), bwawa la maji, visima 3, miundo mbinu ya barabara na Bajaji ya kuwasafirisha walinzi na wahudumu wa pampu.

Mradi ulitumia mtaji wa mwanzo wa Tshs 97 Millioni kutoka mchango wa wakulima, Tshs 1.3 Billion za ASDP (hizi ni kwa makubaliano na Madiwani kuahirisha miradi mingine na kutoa kipaumbele kwa mradi wa zabibu) na Tshs 1.5 Billioni, ni mkopo toka CRDB.

**6.0 MAFANIKIO**

Japokuwa zabibu huchukuwa miaka kadhaa hadi kutoa mazao, mradi wa Chamwino umeanza kuonesha matokeo kadhaa chanya. Moja ni kwamba mradi unamilikiwa na kusimamiwa na wakulima wenyewe. Hili ni jambo la muhimu sana katika uendelevu wa mradi. Wakulima hukutana na kupanga mipango kupitia SACCOS yao bila kuingiliwa kusiko kwa lazima na uongozi wa Halmashauri au wadau wengine.

Jambo la pili, tayari kwa kiasi fulani mradi umepanua uwezo wa wakulima wa kuzalisha zabibu kwani wamehusika katika hatua zote za kuandaa shamba, kuanzisha kitalu cha miche, kuhamisha miche na kupanda kwa nafasi, kutumia viuatilifu, umwagiliaji kwa mzunguko na stadi nyingine muhimu kwenye kilimo cha bustani za zabibu.

Tatu, kuna faida hata nje ya mradi kwani sasa mradi huu umegeuka kuwa shamba darasa kwa wadau wa ndani na nje ya Wilaya.

Nne, mradi umeshaanza kuwafurahisha kundi la vijana na kuwashawishi kubaki Vijijini kwani mradi wa zabibu una hakika ya kuzalisha tani 6-15 kwa mwaka na kipato cha uhakika kwa miaka 50 mbele.



*Shamba la Mizabibu - Chinangali*

Japokuwa bado hazijaanza kuzaa kama inavyotakiwa kwa uwezo kamili wa mmea, wakulima

wameshavuna mara mbili kwa msimu wa 2011/12 na kipato kutokana na zabibu kinazidi kwa mbali kipato kutokana na shughuli nyigine za kilimo. Wakulima kupitia mwenyekiti wao wa SACCOS wameonesha furaha yao kama ilivyonukuliwa hapa chini.



*Matunda ya Zabibu*

***….Tumevuna mara moja… na huu ni msimu mdogo…..lakini tumepata pesa, wengine tumenunua mahindi kwa chakula nyumbani, wengine tumelipa karo za wanafunzi wa Sekondari, wengine tumeendelea kuweka huku shambani… tunategemea mazao yenyewe mwezi wa nane na wa tisa.... naweza kukuhakikishia kwamba tutakuwa na furaha kubwa kila mtu atakuwa na fedha ya kutosha na kuwaza kujenga nyumba bora au kununua pikipiki….”***

**7.0 CHANGAMOTO**

Mradi wa zabibu wa Chamwino ulioko eneo la Buigiri and Chinangali II pembeni mwa baraba kuu ya Dodoma-Morogoro umebadili kanda kame hii kuwa eneo la kijani likifunikwa na mashamba ya zabibu. Mradi huu wa aina yake una faida za kijamii na kiuchumi kwa jamii ya wakulima na Halmashauri yenyewe. Hata hivyo mradi umekutana na changamoto kadhaa ambazo hazina budi kutatuliwa kwa ajili ya uendelevu wa mradi.

**Usalama wa miundombinu na mazao shambani.** Kuna watu kutoka jamii zinazozunguka mradi huvamia na kuiba vifaa vya umwagiliaji na mazao mashambani. Hii inaashiria ushirikishwaji duni wa jamii kuhusu ulinzi shirikishi na usalama wa shamba lao. Ipo haja ya wanavijiji wote kutambua umuhimu na thamani ya mradi huu kwa jamii nzima na kuwajibika kiusalama na kuripoti kwa uongozi wa Kijiji au uongozi wa SACCOs tabia za kutiliwa mashaka na zisizovumilika katika mradi.

**Viwango vya kujizatiti na uwajibikaji wa walengwa pia vinatofautiana.** Wakati wakulima wengine wanafanyakazi kwa bidii kuhakikisha mashamba yao ni masafi, wengine ni wavivu

na hawajishughulishi na hivyo kupelekea mashamba yao kutopaliliwa vizuri na matumizi mabaya ya maji na hivyo kupungua mazao. Kwa hali hii ipo haja ya chama cha Ushirika kuweka sheria ndogo ili kuwapiga faini wale wote wasidhihirisha uwajibikaji wa kutosha kwa mradi.

**Kuanzisha uzalishaji wa zabibu ni gharama kubwa.** Pembejeo za zabibu kama vile mbolea na viuatilifu ni ghali hazipo miongoni mwa zile zinazopewa ruzuku na Serikali Kuu. Hii inasabaisha kutotumia pembejeo zote stahili kwenye zabibu na hivyo kupungua kwa mazao. Umwagiliaji hutegemea pampu zinazoendeshwa kwa za umeme na bei za umeme zinapanda karibia mara nne kwa mwaka. Huu nao ni mzigo na unakula sehemu kubwa ya faida kwa mkulima.

**8.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Uzalishaji wa zabibu Chamwino unakusudia kupunguza umaskini kwa kuinua kipato cha kaya kwa wakulima waishio vijiji vilivyo katika eneo la mradi. Ili kufikia lengo kwa uendelevu, Halmashauri imeandaa programmu ya kuwajengea wakulima uwezo kila wakati kwa kukitumia kituo cha ARI Makutupora na Maafisa kilimo wa wilaya. Shughuli za SACCOS zitapata usimamizi elekezi wa Maafisa Ushirika wa Wilaya.

Kwa ushirikiano na wadau wengine kuna haja ya kuomba Serikali Kuu itengeneze bodi ya zao la zabibu itayokuwa na jukumu la kusimamia uzalishaji na shughuli za masoko. Halmashauri pia inakusudia kuiomba Serikali iingize pembejeo za zabibu kwenye orodha ya zile zinazopewa ruzuku na Serikali kama mazao mengine.

Halmashauri inaendelea na mkakati wa kuhamasisha jamii iachane na kilimo cha kizamani na kuelekeza nguvu zao katika zabibu. Maafisa Maendeleo wa Jamii hukutana na wakulima kujadili uzalishaji na mabadiliko tarajiwa katika kubadili hali ya maisha ya jamii.

Halmashauri pia inaendeleza mazungumzo na wasindikaji wa juisi na mvinyo, kuwa na maelewano (MoU) kuhusu bei za uhakika kwa zabibu za Chamwino. Lengo la muda mrefu ni kuwasadia wakulima waweze kuongeza thamani ya mazao yao kwa kuchakata na kufungasha bidhaa za zabibu kwa njia ya kuanzisha viwanda vidogo. Hii itahusisha pia kuanzishwa mtandao wa wakulima wa masoko na teknolojia ya zabibu.

Ili kuwa na umiliki wa kweli wa mradi, kila mkulima atachanga gharama za uendeshaji na matengenezo ya of TZS 150,000/= kwa mwaka kwa ekari. Hii itaondoa utegemezi usioisha wa miradi mingi ya jamii hapa nchini kutegemea sana misaada ya Serikali hata baada ya kukabidhiwa kwa jamii.

**9.0 SIRI YA MAFANIKIO**

(i) Uongozi wa Halmashauri ulikuwa ndiyo ufunguo wa mafanikio haya; ulikuwa na mawazo mapya kwa vile walishapata mwanga juu ya wazo mbadala na mbinu mpya. Hasa aliyekuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Chamwino (Bw. Daudi Mayeji) ndiye Gwiji la uanzishaji wa mradi huu. Baada ya kutembelea Oyama Japani wanakotekeleza dhana ya OVOP, alivutiwa na kile alichokiona hivyo akaazimia kuleta mabadiliko ndani ya Halmashauri. Yeye ndiye aliyeleta wazo la kilimo cha ushirika wa zabibu Chamwino[11]. Bahati mbaya alihamishwa kabla ya kuona ndoto zake zikitimia. Alikuwa makini kuteua viongozi makini wa jamii na mafundi mchundo walioko katika jamii.

(ii) Uwezeshaji: wakulima walihamasishwa kuanzisha ushirika wa wakulima wa zabibu ambao ndiyo kitakuwa chombo cha wananchi kusimami mradi.

(iii) Vipaumbele: Kulikuwa na uamuzi wa makusudi wa Baraza la Madiwani wa kuahirisha miradi mingine ya maendeleo na kuelekeza nguvu kwenye zabibu uliohitaji uwekezaji mkubwa kwa mategemeo makubwa ya mapato ya muda mrefu.

(iv) Utashi wa kisiasa wa Madiwani ulikuwa wa muhimu sana katika kuanzisha mradi huu. Katika hatua za kulea na kuutunza mradi huu mchanga Halmashauri iliendelea kulipa bili za umeme. Malezi ya miradi ni jambo muhimu mno kwa hatua za mwazo za miradi hasa katika vipindi vya mpito.

(v) Halmashauri kuwa mdhamini wa mikopo: Halmashauri ilikuwa ndiye mdhamini wa mikopo ya wakulima 250 kutoka CRDB. Ili kuhakikisha matumizi mazuri ya mikopo hiyo, fedha iliekezwa kwenye chama cha ushirika ambacho ndiye wakala wa utekelezaji mradi.

(vi) Ushirikiano na mashauriano baina ya wadau wote muhimu wa mradi ilikuwa siri nyingine ya mafanikio. Utendaji kazi kama timu moja chini ya Mkurugenzi lilikuwa jambo la maana sana.

(vii) Mitandao: Halmashauri ilifanya utafiti kisha kuwaunganisha wakulima kwa kampuni ya BALTON Tanzania ambao ndio walipata tenda ya miundombinu ya umwagiliaji kwa njia ya matone, Waliunganishwa na kituo cha utafiti wa zabibu na kupata mbegu stahili.

(viii) Ujasiri wa kujiingiza kwenye teknolojia muafaka ya umwagiliaji kwa matone kwa kuchimba bwawa, ulikuwa uamuzi wa kijasiri ili kuzalisha zao la thamani kubwa na la muda mrefu. Halmashauri za Tanzania zinashauriwa kuwekeza kwa nguvu zote kwenye miradi ya thamani kubwa kulinga na bidhaa zisizo za kawaida zinazopatikana katika Halmashauri zao.Kilimo cha eneo dogo mazao mengi, ni muhimu Halmashauri nyingine zikaiga kwa Chamwino.

(ix) Mwisho wakulima walionyesha ushirikiano wa kutosha; waliunda chombo madhubuti yaani chama cha ushirika na endapo wataendelea kuwa na viongozi

[11] Kwa sasa Bwana Daudi Mayeji amehamishiwa Halmashauri ya Kilindi Mradi ukiwa mchanga kabisa

imara wapenda maendeleo, modeli hii ya Chamwino ina uwezekano mkubwa wa kuendelea vizuri. Katika modeli hii shughuli zote za mradi husimamiwa na uongozi wa ushirika.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA

**UZALISHAJI WA ALIZETI NA MNYORORO WA ONGEZEKO LA THAMANI**



***ALIZETI YA IRAMBA***

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ipo ndani ya Mkoa wa Singida, Mji wa Kiomboi ndio makao yake makuu na uko umbali wa kilomita 100 toka Makao Makuu ya Mkoa. Halmashauri hii inapatikana kati ya Latitudo 4º hadi 4º.3º Kusini mwa Ikweta na Longitudo 34º hadi 35° Mashariki mwa mstari wa Greenwich. Ina uwanda mpana ulio kati ya mita 1,000 na 1,500 juu ya usawa wa bahari. Imepakana na Wilaya za Meatu na Mbulu upande wa Kaskazini, Hanang' upande wa Mashariki, Singida upande wa Kusini, Shinyanga upande wa Magharibi, Maswa na Meatu upande wa Kaskazini-Magharibi.

Wilaya hii ina katika Tarafa saba, Kata 31, Vijiji 135 na Vitongoji 676. Ina Madiwani 42, kati yao 15 ni Wanawake na 27 ni Wanaume. Halmashauri ina jumla ya watumishi wapatao 2,118. Kulingana na matokeo ya sensa ya watu na makazi ya 2002 Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ilikuwa na watu 367,036, kati yao 178,297 ni Wanaume na 188,739 ni Wanawake.

Wilaya hii hupata wastani wa milimita 500 mpaka 850 za mvua kwa mwaka ambazo hunyesha kati ya Novemba na Mei. Kuna utajiri mkubwa wa uoto wa asili ikihusisha miti ya miombo, migunga na uwanda wa majani. Eneo la ardhi ni kilomita za mraba 7,900 zilizogawanyika kulingana na matumizi. Ardhi ya kilimo ni kilomita za mraba 3,500 sawa na (44.3%) ya ardhi yote. Hata hivyo ardhi inayotumika kwa sasa ni kati ya kilomita za mraba 1,500 to 2,000 sawa na (19% - 25%) ya ardhi yote. Eneo la malisho ni kilomita za mraba 3,370 (42.7% ) ya ardhi lote. Misitu huchukua kilomita za mraba 734.7 (9.3%) ya ardhi yote. Kiasi cha kilomita za mraba 294 zimefunikwa na maji na miamba.

Takriban 85.2% ya wakazi wote hujishughulisha na kilimo. Shughuli nyingine za kiuchumi ni pamoja na ufugaji, utunzaji wa nyuki na urinaji asali, uchimbaji mdogo wa madini na uvuvi . Shughuli hizi huipatia Halmashauri mapato kama inavyoonekana kwenye jedwali na 5.6 hapa chini.

**Jedwali 5.6: Mtiririko wa mapato toka vyanzo vya ndani**

| Mwaka | Makusanyo(Tshs) |
|---|---|
| 2004/05 | 439,345,736.70 |
| 2005/06 | 60,083,420.87 |
| 2006/07 | 97,817,785.26 |
| 2007/08 | 117,101,647.16 |
| 2008/09 | 184,950,904.47 |
| 2009/10 | 205,444,436.52 |
| 2010/11 | 223,066,117.07 |

**Chanzo: Halmashauri ya Wilaya Iramba 2011**

Kati ya mwaka 2004-2005 kiasi kikubwa cha mapato kilitokana na kodi ya kichwa, kodi ya mazao na mifugo ambazo zilifutwa mwaka 2005 kwa kile kilichoitwa "kodi zenye kero". Hata hivyo kati ya 2006 – 2012 kuna ongezeko la mapato kutokana na vyanzo vipya

hususan kodi itokanayo na alizeti ambayo iliongezeka toka Tshs 500 hadi 1,000 kwa gunia moja. Vyanzo vingine ni kodi za minara ya mawasiliano, masoko, minada na uvuvi kwenye Ziwa Kitangiri.

## 2.0 TATIZO LILILOKUWEPO KABLA YA UBORESHAJI WA ZAO LA ALIZETI

Kabla ya juhudi za kuhamasisha zao la alizeti, Halmashauri ilikuwa ina changamoto ya ongezeko la watu ambalo haliendani na ongezeko la kipato cha kaya. Hali hii ilichangiwa na uhaba wa mvua kwa miaka kadhaa mfululizo. Yale mazao yaliyozoeleka kulimwa kienyeji kama vile mtama hayakuweza kukidhi mahitaji ya msingi kama vile chakula na ziada ya kuuza ili kujenga nyumba za kisasa za bati. Uzalishaji ulikuwa mdogo; mfano mwaka 2008/09 hekta nzima ya alizeti ilizalisha kiasi cha tani 1.0 tu. Hali hii ilitokana na matumizi ya zana duni, mbinu duni, mbegu hafifu, teknolojia zilizopitwa na wakati na matumizi duni ya pembejeo kama vile mbolea, samadi na viuatilifu.

Licha ya kwamba wananchi walishaanza kulima zao la alizeti kwa muongo mmoja uliopita, uzalishaji ulikuwa mdogo na kilimo hiki hakikuweza kuboresha kipato cha kaya wala hali ya maisha ya watu kwa sababu hapakuwa na mbinu za kuongeza thamani ya zao hili. Mfano hadi 2008/2009 kulikuwa na mashine 27 tu za kukamulia mafuta ya alizeti Wilaya nzima. Upotevu wa mazao baada ya kuvuna ulikuwa mkubwa sana kutokana na njia duni za kuhifadhi nafaka, ucheleweshwaji wa kusindika, masoko yasiyo na uhakika, mabadiliko ya bei za mazao na upatikanaji usioaminika wa pembejeo kama vile mbegu bora na pembejeo nyingine.

## 3.0 MALENGO

Mwaka 2006 watumishi wa Halmashauri walishiriki katika mafunzo ya Mkoa wa Singida yaliyohusisha mrejesho wa mambo mapya yaliyotokana na mafunzo ya Wakurugenzi waliokwenda Osaka Japani. Baada ya mafunzo ya Osaka kila Halmashauri ilitakiwa kuandaa mpango kazi wa kutekeleza kwa yale masuala mazuri na mafunzo mapya waliyojifunza Japani. Halmashauri ya Iramba ilizingatia na kuazimia kuendeleza zao la alizeti ili kuinua kipato cha kaya na kuboresha hali ya maisha ya wananchi. Maazimio haya ya jumla yaliwekewa malengo mahsusi kama ifuatavyo:.

I. Kuhamasisha wananchi ili kuongeza uzalishaji wa zao la alizeti kibiashara.
II. Kuwezesha wakulima waongeze uzalishaji wa alizeti kutoka wastani wa tani 1.0 /ha 2008/2009 hadi tani 2.0 /ha mwaka 2011/12.
III. Kukazania kilimo cha kisasa ikihusisha zana za kisasa za kilimo, mbinu za kisasa kwa ajili ya uzalishaji bora wa alizeti.
IV. Kuivutia sekta binafsi iwekeze katika uzalishaji mbegu bora, kuziandaa, kufungasha, kusafirisha na kusambaza mbegu.
V. Kuanzisha mfumo wa stakabadhi ghalani ili kudhibiti bei ya alizeti
VI. Kuhamasisha wakulima wajiunge na SACCOs, kuongeza idadi ya SACCOs toka 13 hadi 29 na kutoa usimamizi elekezi wa jinsi ya kuendesha SACCOs ili kukidhi

matakwa ya Utawala Bora na ziweze kuwafaidisha wanachama na wakulima kwa ujumla.

**4.0 MKAKATI WA UTEKELEZAJI**

Uhamasishaji kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa alizeti katika Halmashauri ya Iramba haukuwa rahisi. Kazi kubwa ilikuwa ni kubadili mitazamo ya wakulima ili waweze kuondokana na kilimo cha mazoea, mbinu za kilimo cha kizamani na wakubali badiliko la kuanza kutumia mbinu za kisasa na kwa wengine kuanza kulima zao mbadala la alizeti. Juhudi hizi zilizaa matunda na pakawepo na ongezeko la wakulima wazalishaji wa zao la alizeti. Sasa kazi ikawa ni jinsi gani Halmashauri iwasaidie wakulima waongeze uzalishaji kwa kila hekta na wapate faida kutokana na uzalishaji huu. Ili kufanikisha haya mambo yafuatayo yalifanyika;

I. Kununua matrekta ya mkono ya aina ya *power tillers* 49 (29 kutoka DADPs, 7 kutoka World Vision Tanzania na 13 zilinunuliwa na watu binafsi). Matrekta haya yalikuwa muhimu ili kuongeza maeneo yanayolimwa na kila kaya na pia kulima kwa wakati na kupanda kwa wakati muafaka.
II. Ujenzi wa vituo vya kujifunzia vya Kata 3 maarufu kama *Ward Resource Centers* (Luono 2009, Gumanga 2010 na Mwanga mwaka 2011). Vituo hivi vya Kata ni vya muhimu katika kusambaza mbinu za kisasa za kilimo, kusambaza mbegu za kisasa, kuangamiza wadudu na wanyama waharibifu, kutoa ushauri kuhusu matumizi ya mbolea za viwandani na ushauri elekezi wa papo kwa papo kuhusu kilimo cha Alizeti.
III. Kuendesha mafunzo kwa wakulima 297,695 kuhusu mbinu bora za kilimo hususan muda sahihi wa kulima, aina za mbegu, aina na kiasi cha mbolea inayofaa kutumiwa, aina za viuatilifu, uchanganyaji wa mazao kwa ajili ya matumizi endelevu ya ardhi.
IV. Uzalishaji wa mbegu bora zilizothibitishwa (*Quality Declared Sunflower Seeds(QDS)*. Hii ilifanyika kwa ushirikiano na mashirika ya ICRISAT, HOPE, Songela Investment and RLDC. Mbegu hizi za kisasa zinavumilia ukame, hutoa mazao mengi kwa ekari na hutoa mafuta mengi kuliko mbegu nyingine.
V. Kuanzisha mashamba darasa. Haya huwapa wakulima fursa ya kujifunza kwa vitendo, kupokea uzoefu na kuona kwa macho mbinu bora za kilimo na matokeo yake.
VI. Kuwatia moyo wauzaji wa pembejeo za kilimo kusambaza pembejeo na kushauriana nao ili watoe mikopo ya kilimo kwa wakulima wasioweza kulipa wakati wa msimu wa kilimo. Utaratibu huandaliwa kwa wakulima kukopa pembejeo wanazohitaji na kulipa wakati wa mavuno.
VII. Kuwezesha wawekezaji binafsi kujenga mashine za kukamua mafuta na kununua mbegu za alizeti kutoka kwa wakulima. Lengo la mkakati huu ni kuongeza usindikaji wa alizeti, kutoa ajira kwa vijana na kuwapa wakulima fursa ya kuongeza thamani ya mazao yao na kuongeza kipato.

VIII. Kuanzisha mfumo wa stakabadhi ghalani kweye Vijiji vya Iambi na Msai ili kukusanya na kuhifadhi alizeti wakati wa msimu; mkakati huu unalenga kuimarisha na kudhibiti bei. Wakulima hulipwa malipo ya awali ili kukidhi mahitaji yao ya lazima kabla mazao yao kuuzwa kwa bei nzuri. Mfumo huu husaidia kuondoa ukiritimba wa sekta binafsi na kuwaumiza wakulima kwa kuwalipa bei za chini ambazo hazikidhi gharama za uzalishaji.

## 5.0 RASILIMALI ZILIZOTUMIKA

Kwa kuwa Halmashauri ya Iramba ilikuwa imedhamiria kufanya Alizeti kuwa zao la biashara litakalosaidia kuongeza kipato cha kaya na hali njema ya maisha kwa wakazi wake palihitajika kujitoa kwa dhati kifedha na rasilimali-watu kwa maana ya utaalamu. Kwa kipindi cha miaka mitatu kiasi cha Tshs 622,000,000 zilitumika katika kutekeleza shughuli zilizoainishwa hapo juu kama ifuatavyo:

I. Ununzi wa matrekta 49 ya mkono (29 toka mfuko wa DADPs, 7 kutokana na fedha za World Vision Tanzania na 13 toka watu binafsi) Jedwali 5.7

**Jedwali 5.7: Idadi ya matrekta ya mkono zilizonunuliwa**

| Mwaka | Idadi ya matrekta toka (DADPs) | Gharama |
|---|---|---|
| 2008/09 | 1 | 6,650,000 |
| 2009/10 | 22 | 154,000,000 |
| 2010/11 | 6 | 42,000,000 |
| 2011/12 | 20 (World Vision na watu binafsi) | 91,350,000 |
| | | 294,000,000 |

**Chanzo: Halmashauri ya Iramba 2011**

II. Ujenzi wa vituo vya kujifunzia vya Kata kwa gharama ya Tshs 194,000,000 yaani (Luono Tshs 15,000,000 mwaka 2009, Gumanga Tshs 94,000,000 mwaka 2010 na Mwanga Tshs 85,000,000 mwaka 2011).

III. Uanzishwaji wa mashamba darasa ulitumia jumla ya Tshs 7,000,000

IV. Uzalishaji wa mbegu daraja la kuazimia iligharimu jumla ya Tshs 10,000,000

V. Ujenzi wa viwanda 43 binafsi vya kusindika mafuta na SACCOS; Kijiji cha Kinampanda (viwanda 6), kijiji cha Kyengege (viwanda 2 ) , Kijiji cha Ulemo (viwanda 3), Kijiji cha Tumuli (kiwanda1), Kijiji cha Iguguno (viwanda 6), Kijiji cha Nkungi ( viwanda 4), Kijiji cha Shelui ( viwanda 6 ), Kijiji cha Ndago (viwanda 4), Kijiji cha Misigiri (viwanda 3), Kijiji cha Kiomboi (viwanda 6), Kijiji cha Kinambeu (viwanda 10 ) na Kijiji cha Maluga (kiwanda 1) jedwali 5.8.



**Alizeti ikiwa katika ngazi mbalimbali za usindikaji (kukusanya, kuchagua/kusafisha, kukamua na kuchuja)**

**Jedwali 5.8: Idadi ya viwanda vya kusindika mafuta ya alizeti vilivyojengwa**

| Mwaka | Idadi |
|---|---|
| 2008/09 | 27 |
| 2009/10 | 38 |
| 2010/11 | 43 |

**Chanzo: Halmashauri ya Iramba 2011**

VI. Shughuli ya kuweka mfumo wa stakabadhi ghalani katika Kijiji cha Iambi mwaka 2009 uligharimu Tshs 59,000,000 na katika Kijiji cha Msai mwaka 2010 kwa gharama ya Tshs 49,000,000.

## 6.0 MATOKEO YA UTEKELEZAJI

Halmashauri ya Iramba imepata mafanikio kadhaa katika kuhamasisha na kuongeza thamani ya zao la Alizeti. Moja ya matokeo mazuri ni ongezeko la maeneo yanayolimwa kutoka hekta 40,688 mwaka 2008 hadi hekta 69,940 mwaka 2011. Uzalishaji kwa hekta umeongezeka kutoka tani 0.8 mwaka 2008 hadi tani 1.8 kwa hekta mwaka 2011. Kuna ongezeko kwa hekta na ni lengo la Halmashauri kuwasaidia wakulima kuzalisha tani 2.0 kwa hekta ifikapo 2015.



***Shehena ya mbegu za alizeti iliyotayari kuongezwa thamani***

Uzalishaji wa mbegu bora za alizeti zilizothibitishwa umeongezeka kutoka kilo sifuri mwaka 2007 hadi kilo 11,146.5 mwaka 2011 na kupelekea ongezeko la uzalishaji wa tani kwa ekari kwa mwaka. Angalia jedwali 5.9.

**Jedwali 5.9:uzalishaji wa mbegu daraja la kuazimia kutoka 2009-2011**

| Mwaka | Uzalishaji kwa Tani/ha | Hekta | uzalishaji kwa Tani/ha |
|---|---|---|---|
| 2008/09 | 1.0 | 36,750 | 40,688 |
| 2009/10 | 1.5 | 41,300 | 45,165 |
| 2010/11 | 1.8 | 59,100 | 62,784 |

**Chanzo: Halmashauri ya Iramba 2011**

Halmashauri imefanikiwa kuanzisha mashamba darasa yapatayo 105 kwenye Vijiji vinavyozalisha Alizeti. Halmashauri ilikuwa na mashamba darasa 28 mwaka 2009, 98 mwaka 2010 na 105 mwaka 2011/12. Mashamba darasa yamesaidia sana wakulima kupata elimu ya nadharia na elimu kwa vitendo kupitia maonesho ya mbinu za kilimo za kisasa. Wakulima wamepata ujuzi wa matumizi ya matrekta ya mkono na jinsi ya kuyafanyia matengenezo na ukarabati. Wakulima pia wamejifunza njia sahihi za upandaji kwa nafasi, matumizi ya mbegu bora, kutambua magonjwa na wadudu waharibifu, mbinu za kisasa za palizi na kuvuna alizeti kutokana na mashamba darasa. (Picha hapa chini inamwonesha Afisa Ugani Kijiji cha Kidarafa akifundisha namna ya kuzalisha mbegu bora za alizeti zilizothibitishwa (*QDS)*



***Afisa ugani kwenye Shamba darasa la alizeti***

Jumla ya SACCOS 29 zimeanzishwa kutokana na hatua ya Halmashauri kuunganisha juhudi za wakulima kujiunga katika vikundi na kisha kivitunza na kuvilea vikundi hadi vinapofikia usajili kuwa SACCOS kamili. Juhudi hizi pia zimesaidia katika upatikanaji wa mikopo, utafiti wa masoko, ushawishi wa mashirika na sekta binafsi, wanunuzi wa alizeti, wamiliki wa viwanda vya usindikaji alizeti na kupelekea kuwa na bei zisizobadilika sana. Hizi SACCOS zimesaidia sana kujenga uwezo wa wakulima kujipanga na kujipangia mustakabali wa maisha yao, kujihami na mifumo katili ya bei hodhi ya sekta binafsi, na kupata uhakika wa bei na fursa za mikopo.

Licha ya ongezeko la SACCOS Halmashauri imeshuhudia ongezeko la mawakala wa pembejeo za kilimo wanaotoa huduma mbalimbali pamoja na mikopo kwa wakulima, uuzaji wa vifaa na zana za kilimo, uchakataji na usindikaji wa mbegu za alizeti, kufungasha na kutafuta masoko ya nje. Angalia jedwali 5.10

**Jedwali 5.10: Ongezeko la wakala wa pembejeo za kilimo**

| Mwaka | Idadi ya wakala |
|---|---|
| **2009/10** | 7 |
| **2010/11** | 19 |
| **2011/12** | 57 |

**Chanzo: Halmashauri ya Iramba 2011**

Kuna ongezeko la kuridhisha katika kipato cha kaya na maboresho katika hali za maisha ya wakulima kwenye Halmashauri ya Iramba. Baadhi ya wakulima wamejenga nyumba bora kwa kutumia matofali ya kuchoma na kuezeka kwa bati ikilinganishwa na miaka mitano iliyopita. Kama inavyonekana kwenye picha hapa chini katika Kijiji cha Ulemo wakulima wengi waliishi kwenye tembe lakini sasa wameboresha hali ya nyumba zao.



***Nyumba ya kizamani***

Mabadiliko ya maisha ni dhahiri hasa ukitazama kwa wale wanaotumia barabara kuu toka Mwanza hadi Dar es salaam, utaona mafuta ya alizeti yaliyofungashwa yakiuzwa kwenye masoko ya pembezoni mwa barabara. Bei ya lita moja hutegemea msimu; ni kati ya Tshs 3000 wakati wa mavuno na zaidi ya Tshs 6000 kati ya Desemba na Aprili. Idadi ya vijana wauza mafuta kwenye masoko ya pembezoni mwa barabara inazidi kuongezeka ikitafsriwa kuwa ni ongezeko la ajira na ukuaji uchumi.

Miradi ya matofali ya kuchoma ni shughuli nyingine muhimu na fursa ya kiuchumi nyingine inayotokana na kukua kwa kilimo cha alizeti. Wanunuzi wa matofali ni wakulima wa alizeti

wenye fedha na wanapenda kujenga nyumba bora za matofali ya kuchoma. Nyumba za wakulima zinapendeza na zote zina michoro inayofanana. Tazama mfano kwenye picha hapa chini.



*Utengenezaji wa matofali ya kuchoma*



*Nyumba bora ya Mkulima inaendelea kujengwa*

Mafanikio mengine ni pamoja na ongezeko la vijana wanaoandikishwa kwenda shule za Sekodari na kupungua kwa utoro mashuleni. Kwa sasa wakulima wana uwezo wa kulipa karo na mahitaji mengine muhimu kwa ajili ya watoto wao. Hii yote inatokana na ongezeko la kipato kutokana na mauzo ya alizeti na mauzo yatokanayo na alizeti kama anavyokiri mmoja wa wakulima wa Alizeti.

***"….Zao hili limetupa ujasiri na fahari… tulikuwa na shida sana kwenye Kijiji hiki….watoto walikuwa hawaendi shule kwani tulikuwa hatuwezi kulipa ada… vijana wa kiume walikimbilia mjini kutafuta vibarua… tuliishi kwenye nyumba mbovu… lakini hivi ninavyooongea…. hebu tazama nyumba yangu nzuri… watazame watoto wangu… wako shuleni… mmoja yuko shule ya bweni Arusha mjini… na ninaweza kulipa… kwa sababu… Nimejaza magunia ya alizeti ndani ya nyumba na ina magudulia ya mafuta yanauzwa huko kwenye masoko pembeni mwa barabara… napata fedha kila siku… Hapa kwetu Alizeti inaitwa BATI kwani imewezesha wakulima kujenga nyumba bora zilizoezekwa kwa bati"***

Matokeo mazuri yasiyotarajiwa kutokana na ongezeko zao la alizeti ni mengi. Hali ya maisha kwenye vijiji kando ya barabara kuu ya Dar es salaam inazidi kuwa ya kimji kuliko ilivyo ya Kijijini. Kuna ongezeko la biashara za rejareja na za jumla, ulaji wa bidhaa mbalimbali za vyakula na vinywaji umeongezeka. Umiliki wa nyumba na vyombo vya usafiri kama magari na pikipiki nao umeongezeka ghafla.

**7.0 CHANGAMOTO**

Licha ya ukweli kwamba mafanikio haya yametokana na watumishi wenye moyo wa kujitolea na utashi wa wanasiasa na tabia ya wenyeji wa Iramba ya kujituma katika kazi bado kulikuwa na vikwazo kadhaa. Changamoto kubwa ni mvua ambazo hazitabiriki. Imekuwa ni vigumu kutabiri mvua za mwanzo, kiasi cha mvua na zitadumu kwa muda gani. Wakati mwingine zinanyesha lakini zinaisha kabla ya mazao kukomaa. Hali hii inamaliza mtaji wa wakulima waliowekeza kwenye kulima, palizi na pembejeo. Katika muongo mmoja uliopita kumekuwa na badiliko kubwa la hali ya mvua za mwaka.

Changamoto ya pili ni kuyumba kwa bei za zao la alizeti, mafuta na mazao mengine yatokanayo na alizeti. Ongezeko la bei haliendani na thamani ya shilingi ambayo imekuwa ikishuka mwaka hadi mwaka na kusababisha gharama kubwa za pembejeo ilihali bei ya Alizeti na bidhaa zake ikiendelea kushuka. Angalia Jedwali 5.11 na 5.12.

**Jedwali 5.11: Ongezeko la bei ya mavuno ya alizeti kwa miaka mitatu mfululizo**

| Mwaka | (Tshs)/Kg |
|---|---|
| **2009** | 460 |
| **2010** | 600 |
| **2011** | 750 |

**Chanzo: Halmashauri ya Iramba 2011**

**Jedwali 5.12: Badiliko kubwa la bei za mbegu za alizeti kwa miaka mitatu mfululizo**

| Mwaka | Ina ya Mbegu | (Tshs)/Kg |
|---|---|---|
| **2009** | Kenya Feather | 2800 |
| **2010** | Kenya Feather | 3500 |
| **2011** | Kenya Feather | 4250 |

**Chanzo: Halmashauri ya Iramba 2011**

Changamoto ya miundo mbinu duni hususan usafiri wa Vijijini bado ni kikwazo kikubwa kwenye maeneo ya Vijiji vinayolima alizeti. Barabara nyingi za Vijijini hazina matunzo na ukarabati wa mara kwa mara kiasi kwamba mvua za msimu husababisha uharibifu mkubwa kwa barabara yenyewe na madaraja. Hali hii huathiri sana usafirishaji wa mazao kutoka mashambani kwenda viwandani na sehemu za mauzo.

Upatikanaji wa mitaji ni shida kubwa kwenye Halmashauri ya Iramba DC. wazalishaji walio wengi hawapati mikopo ya kutosha, pia chini ya mfumo wa soko huria hakuna mamlaka yenye mamlaka ya kudhibiti bei za mazao, kukoseka kwa chama cha ushirikia cha wakulima wa alizeti, kukosekana kwa mfumo rasmi unaratibiwa kukusaya taarifa za masoko na bei, Kukosekana kwa njia ya kuunganisha wakulima na masoko ya nje na ushindani katika soko la alizeti kutokana ka kuibuka kwa mazao mengine ya mafuta ya mimea.

**8.0 MIKAKATI ENDELEVU**

Kwanza ni uwajibikaji wa hali ya juu wa Timu ya Mejimenti ya Halmashauri ili kuhakikisha zao la alizeti linashamiri katika Halmashauri ya Iramba. Hii inadhihirishwa na mikakati iliyowekwa kuleta uendelevu wa zao hili. Mkakati wa kudhibiti kuyumba kwa bei kwa njia ya kujenga mfumo wa stakabadhi ghalani kwenye Vijiji vya Iambi na Msai utasaidia kuhifadhi alizeti ghalani kwa pamoja hadi bei zipande kiasi cha kumpa mkulima faida baada ya kuondoa gharama za uzalishaji, usafiri na kuhifadhi.

Mkakati wa pili ni ule wa SACCOS 16 za Ndago, Shelui, Mzawangeza, Nduguti, Ulemo, Nkungi na Iguguno. SACCOS zitafanya kazi kwa pamoja na mfumo wa stakabadhi ghalani, lakini SACCOS zitahusika kutoa mikopo ya masharti nafuu na kuwa dhamana kwa wanachamana wake wanaokopa kwenye vyombo vya fedha. Hii itaondoa ukosefu wa mitaji wakati wa msimu wa kilimo.

Ipo mikakati kadhaa kuhakikisha uendelevu wa kuzalisha zao hili, kuchakata na kuuza mazao yatokanayo na alizeti ikihusisha;

I. Kuhimiza wakulima waendelee kushirikiana na wachakataji wa bidhaa za kilimo na mawakala wanaohusika na mfumo wa masoko ili kuimarisha mnyororo wa thamani kutoka ngazi ya uzalishaji na makoso na kuunganisha wakulima na wachakataji wa mazao ya alizeti

II. Kuwezesha mitandao ya wakulima ndani na nje ya Wilaya ili kujenga mahusiano imara ya kibiashara yatakayowezesha kubadilishana mawazo kuhusu mikakati ya soko, teknolojia za kisasa na uzalishaji wenye tija.

III. Kuimarisha vyombo vya fedha Vijijini mfano (SACCOS) ili wakulima waweze kupata mikopo yenye masharti nafuu.

IV. Kukigeuza kilimo cha mkulima mdogo kuwa kilimo cha soko ili kuharakisha kasi ya ukuaji wake na kuongeza uzalishaji.

**9.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Halmashauri ya Iramba imefanya mapinduzi makubwa katika uzalishaji wa zao la alizeti na mnyororo wa ongezeko la thamani kutokana na mambo yafuatayo;

(i) Siri kubwa ni uwezo wa Timu ya Menejimenti ya Halmashauri kufikiri na kuchukua hatua za makusudi na haraka ili kuteka fursa iliyojitokeza miaka ya karibuni kwa Watanzania kubadilika kitabia na kupendelea zaidi mafuta ya mimea na kuachana na mafuta ya wanyama yaliyojaa lehemu ili kunusuru afya zao. Badiliko hili la tabia ndio hasa chanzo cha msukumo katika kufunguka kwa soko la alizeti na mazao yake kiasi kwamba Mkoani Singida kwa sasa mafuta ya alizeti yanajulikana kama "dhahabu maji". Badiliko la tabia za walaji limesababisha mahitaji makubwa ya bidhaa za alizeti hapa nchini. Jambo la kujifunza kwa Halmashauri ya Iramba ni uwezo wa kuchambua hali halisi ya soko na kuwapa wananchi taarifa kuhusu mabadiliko ya soko wachukue hatua muafaka.

(ii) Mashudu ya alizeti ni moja ya mazao yatokanayo na alizeti. Mahitaji ya mashudu nayo ni makubwa kwani hutumika kwa ajili ya kulisha wanyama. Katika kuendeleza uzalishaji wa alizeti, Halmashauri ya Iramba imehamasisha pia uzalishaji wa bidhaa za wanyama kama vile ufugaji wa nguruwe, kuku, ngombe wa maziwa na wanyama wadogo kama vile sungura.

(iii) Halmashauri ya Iramba imetumia kwa ufanisi mkubwa fedha kutoka programu za Serikali Kuu kama vile DADPs, ASDP, na taasisi za utafiti katika hatua za mwanzo za kuwajengea uwezo wazalishaji. Mfano taasisi hizi zilitumika kuanzisha mashamba darasa, kuhamasisha sekta binafsi wawekeze kwenye uzalishaji wa mbegu za alizeti na kuanzisha viwanda vya kuchakata alizeti. Matokeo yake Halmashauri ya Iramba ndiyo nyenye viwanda vingi vya kuchakata alizeti kuliko Wilaya nyingine nchini.

(iv) Halmashauri hii ilikuwa na Timu ya Menejimenti hodari na thabiti, inayojiwajibika vizuri ambayo ilijikita katika utendaji kazi wa pamoja kwa ajili ya shughuli zote za Maendeleo ya Wilaya.

(v) Halmashauri ya Iramba ilitumia fursa ya ushirikiano wa sekta binafsi na sekta ya Umma yaani dhana ya (PPP). Mfano RLDC ilikuwa mshirika wao wa kimkakati kwani RLDC ni huhamasisha dhana ya mnyororo wa thamani ambayo ni ya muhimu sana kwa kazi kama hii ili wakulima wapate faida kutokana na uzalishaji wao.

(vi) Ushiriki thabiti wa wakulima katika hatua mbali mbali za mmnyororo wa ongezeko la thamani ilikuwa ndiyo msingi wa mchakato mzima. Wakulima wamejikita kwenye uzalishaji na kidogo kwenye kukusanya mazao kungoja bei nzuri. Baadhi ya wakulima wanamiliki mashine za kukamua alizeti za ukubwa mbalimbali na wengine wameweza kufungasha mafuta kwenye vifungashio vya ukubwa tofauti. Wenye viwanda kazi yao ni kuchakata, watafiti kuhakiki mbegu bora na mafunzo.

(vii) Mafinikio yanayoonekana yametokana na uwezeshaji bora wa Maafisa Ugani, watafiti na uraghibishi uliofanywa na viongozi wa kisiasa na wa kuteuliwa.

# Marejeo

Braathen, et all. (2005) Local governance, finances and service delivery in Tanzania. Joint Report.

Haman, et all. (2005). Local governance as a complex system: lessons from mining in South Africa, Mali and Zambia. *The Journal of Corporate Citizenship*.

PMO-RALG, (2004-2007) Regional Post Osaka Training Reports

PO-RALG, (1998) Local Government Reform Policy Paper

Van Klinken, R. (2003). Operationalising local governance in Kilimanjaro. **Development in Practice, 13**(1).